# TOP SCHOOLS KISWAHILI TRIALS

## (QUESTIONS &MARKING SCHEMES)

# 2019 SET OF MOCK EXAMS

## ALLIANCE BOYS HIGH SCHOOL

K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM

Julai 2019

KISWAHILI

**Karatasi ya 1 (Insha)**

101/1
Karatasi ya 1
(insha)
***MAAGIZO*** :

(a) Andika insha mbili. Insha ya kwanza ni ya lazima.

(b) Kisha chagua insha nyingine moja kati ya hizo tatu zilizobaki.

(c) Kila insha isipungue maneno 400.

(d) Kila insha ina alama 20.

(e) Kila insha iandikwe kwa lugha ya Kiswahili

MASWALI

1. Wewe ni mwanahabari wa kituo cha runinga cha mwelekezi. Andika mahojiano kati yako na mtaalamu wa maadili kuhusu hali ya maadili katika jamii ya sasa.

2. Suala la utovu wa usalama ni changamoto kubwa katika jamii. Jadili.

3. Tunga kisa kitakachodhihirisha ukweli wa methali .Mchumia juani hulia kivulini.

4. Tunga kisa kitakacho malizika kwa .Nilifurahi sana kwamba niliweza kupata ufanisi wa kiwango hicho.

# ALLIANCE BOYS HIGH SCHOOL

## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM

## Julai 2019

## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

***UFAHAMU***

***Soma kifungu kasha ujibu maswali.***

Dawa za kulevya ni donda ndugu katika taifa letu. Ni zimwi linalotesa na kufisha wazee kwa vijana. Halichagui jinsia, tabaka, rangi wala umri. Uraibu wa dawa hizi hauna faida yoyote. Wanaotumia dawa za kulevya huzitia mwili kwa kunusa, kuvuta, kumeza na kujidunga sindano. Zinapoingia katika miili ya watu madhara huwa mengi .

Kuna wale wanaokosa hamu ya kula, wengine huambukizwa maradhi kama vile ukimwi wanapotumia sindano zilizotumiwa na watu wenye virusi vya maradhi hayo kujidunga sindano na kutia dawa mwilini.

Mihadarati pia inaweza kufanya mtu awe mwendawazimu. Vifo pia hutokea ikiwa uraibu utazidi na mtu akose kupata matibabu. Mtu anayetumia dawa za kulevya huathirika akili. Yeye huwa hana uamuzi wenye hekima katika maisha yake . Wengi wao hushiriki katika vitendo vya uhayawani. Wao hukosa fikra za utu. Baadhi yao wamebaka kina mama na watoto wadogo na wengine wamezua vita katika familia na kusababisha madhara makubwa katika jamii zao kwa sababu ya ulevi.

Familia za wanaotumia mihadarati hazina amani. Jamaa zao hutumia hela nyingi kuwalipia ada ya hospitali ili wapate matibabu baada ya kuzidiwa na uraibu. Mali hufujwa na watu wenye uraibu wa dawa hizo pale wanapohakikisha hawazikosi kila siku. Mzazi kwa
mfano anaweza kutumia hela kununua dawa za kulevya badala ya kumlipia mwanawe karo. Kuna wale wanaowaibia majirani na marafiki ili wakidhi mahitaji yao.

Ajali barabarani pia husababishwa na madereva walevi. Dereva yeyote awe wa matatu au gari la kibinafsi anapoendesha gari akiwa mlevi huwa anahatarisha maisha yake mwenyewe, abiria na wananchi wanaopiga miguu barabarani .Uchumi

wa taifa huzorota baada ya wananchi kutumia mihadarati. Watu wenye uraibu hukaa mbumbumbu bila kufanya lolote hasa kutokana na kudhoofika kwa afya yao au ulegevu unaosababishwa na ulevi. Watu wa aina hiyo huwa wanamchango haba katika ukuzi wa uchumi wa taifa.

Dawa hizi zimesambaa kila mahali utapata zinauzwa masokoni, shuleni, njiani na hata pahali popote pale penye watu. Dawa za kulevya haziuzwi hadharani nchini Kenya kwa sababu serikali imepiga marufuku uuzaji wa bidhaa hiyo. Waja wanaoziuza hufanya hivyo kisiri. Walanguzi wa mihadarati aghalabu hutumia watu wengine kuuza kwa niaba yao. Kuna wale wanaotumia watoto , wanaorandaranda almaarufu chokoraa na wengine hutumia vijana katika shule za misingi, upili na vyuo vikuu kama **mawakala**.

Vijana hasa wamejipata katika mtego huu kwa kuwafanyia walanguzi biashara hii haramu hili waweze kupata hela za kukidhi matakwa yao ukweli ni kuwa pesa wanazopatiwa na waajiri wao ni chache mno na hatimaye wao hutumia dawa zile na kuishia kuwa na uraibu unaosababisha wao wenyewe kuwa wateja wa mabwenyenye hao wasio na utu.

Watu maarufu kama vile wafanyabiashara, wanamuziki na wanasiasa wametuhumiwa kushiriki katika biashara hii. Washukiwa hawa mara nyingi hukosa kufikishwa mahakamani kwa sababu jamii hukosa ushahidi wa kutosha dhidi ya tabia hiyo. Ni nani hasa muhusika katika kuingiza sumu hii katika nchi yetu ? Hakuna mtu anayeweza kusimama **kandamnasi** na kusema hiyo ndiyo kazi yake. Mbona tushiriki katika biashara tusiyoweza kujivunia?

Ni mwito wangu kwa kila mwananchi mzalendo kuungana na wenzake ili kupinga biashara hii haramu. Tuhubiri makanisani, shuleni misikitini, hekaluni na mahali popote pale. Tukemee adui huyu wa afya na mali. **Washauri nasaha** washike usukani wawashauri wazee kwa vijana, wakubwa kwa wadogo, weusi kwa weupe tuizike mihadarati katika kaburi la sahau.

Maswali (al.15)

1. Yape makala haya anwani mwafaka. (al.1
2. Mwandishi anamaanisha nini anaposema kuwa dawa za kulevya ni dondandugu katika taifa letu. (al.2)
3. Taja namna ambavyo dawa za kulevya zinavyotumiwa. (al.4)
4. Eleza athari ya dawa za kulevya kwa familia za wanaotumia . (al.2)
5. Kuna changamoto gani katika kupiga vita matumizi ya mihadararati. (al.1)
6. Eleza sera ya serikali kuhusu dawa za kulevya. (al.2)
7. Msamiati ufuatao umetumika kumaanisha nini kwa mjibu wa taarifa. (al.3)

(i) mawakala

(ii) kadamnasi

(iii) washauri nasaha

***UFUPISHO***

***<u>Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali.</u>***

Kila msanii anacho kifaa chake ambacho anakitumia, ambacho kinakuwa alama ya usanii wake. Mchoraji anategemea sana kalamu au rangi zake na mchongaji anao ubao au mti wake.

Vivyo hivyo mwanafasihi naye anategemea lugha katika usanii wake. Matumizi ya lugha ni miongoni mwa mambo muhimu yanayotofautisha kazi ya fasihi na kazi isiyo ya fasihi. Jinsi ambavyo mwandishi anavyoitumia lugha yake na kiwango cha usanii anachofurahia ndivyo alama muhimu inayomtofautisha na mwandishi mwingine wa fasihi.

Katika uhakiki wa kazi za fasihi za hivi karibuni, hasa katika Kiswahili, kumekuwa na msisitizo mkubwa katika maudhui ya kazi hizo au kwa lugha rahisi, ujumbe unaotolewa na mwandishi. Hivyo maswali yanayoulizwa ni kama kazi hii ina umuhimu gani katika jamii ya leo? Inajengaje tabia, mwenendo na mwelekeo wa jamii? Ina maadili gani?

Mara nyingi, wahakiki hawaulizi mwandishi alivyofaulu kisanaa isipokuwa kama jambo la ziada tu mwishoni uhakiki wa namna hii hasa umehusu kazi za fasihi zisizo za ushauri kwa sababu imekubalika kwa muda mrefu kuwa mshauri lazima aitawale lugha yake vizuri ndipo aweze kuleta ule mvuto maalum unaotakiwa na kufikia viwango vinavyokubalika katika fani hii.

Haiwezekani kutenganisha maudhui na usanii katika kazi yoyote ile ya fasihi ujumbe unaoletwa katika kazi ya fasihi unaweza kutolewa na mtu mwingine yeyote kwa njia nyingine. Ujumbe huo unaweza kutolewa kwa njia ya hotuba, vitabu au maongezi ya kawaida.

Katika isimu ya lugha , tunaposema ya kwamba mwanadamu anajua lugha yake, tuna maana kuwa “amemeza” mfumo wa lugha yake wa matamshi, muundo wa maneno, muundo wa sentensi na maana zinazokusudiwa. Ujuzi alio nao mwanadamu huyu ni sawa, na ujuzi walionao wanadamu wengine wa jamii yake wanaozungumza lugha moja. Hivyo tukisema kuwa mwanadamu aongee lugha hatuna maana tu ya kule kumeza mfumo wake wa lugha bali ni uwezo wake wa kuitumia katika mahusiano yake na wanajamii wengine. Katika lugha yoyote ile kuna mitindo mingi inayotumika kutegemea kile kinachozungumziwa.Hivyo, tunaweza kuwa na mtindo wa siasa, sheria dini na kadhalalika pia upo mtindo wa kawaida unaotumika.

Katika mawasiliano ya kila siku ya wanajamii moja Katika mtindo huu kuna matumizi ya aina mbalimbali kihusiana na nyanja tofauti za maisha. Matumizi haya

yanaitwa rejesta kwa lugha ya kitaalam. Rejesta yoyote ile inategemea nani anazungumza nini na nani, wapi kuhusu nini na kwa sababu gani.

Mtu anayejua lugha yake vizuri tunategemea aweze kuitumia katika mitindo

iliyobadilika na aweze kujua mazingira anayopaswa kutumia mtindo mmoja badala ya mwingine katika mahusiano ya kawaida, mtumiaji wa lugha anapaswa kujua ni rejesta gani anapaswa kutumia kila wakati. Mwandishi wa habari lazima awe "amefuzu" kuliko kuweka haya matumizi tofauti ya lugha.

Mwandishi huyu anatakiwa kuwa mtafiti ili ajue Yale matumizi ambayo yeye hana haja nayo katika mahusiano yake ya kawaida na huyo aweze kuchora jamii yake
inayostahili katika kazi yake. Sababu kubwa ya kumtaka mwanafasihi kuyajua kinaganaga matumizi tofauti ni ule ukweli kuwa kazi ya fasihi haina mpaka na utumizi wa lugha.

Maswali.

(a) Eleza vipengele muhimu vya lugha katika uwasilishaji wa fasihi (maneno 70-80)
(al.8)

(b) Fupisha aya **tatu** za mwisho(maneno 75-85)
(al.7)

**MATUMIZI YA LUGHA.**

(a) Andika sifa za sauti zifuatazo. (al.2)
(i) /o/
(ii) /i/
(iii) /m/
(iv) /gh/

(b) Huku ukitoa mifano eleza maana ya silabi funge na silabi wazi.
(al.2)

(c) Tunga sentensi kudhihirisha dhana **tatu** za kiimbo.
(al.3)

(d) Ainisha viambishi katika maneno yafuatayo. (al.2)

(i) wimbo
(ii) muundo
(iii) pazuri
(iv) darasani

(e) Tunga sentensi kwa kutumia aina zifuatazo za maneno.
(al.2)
i) nomino ambatani
ii) nomino ya kitenzi jina

(f) Tumia kiwakilishi kiashiria cha mbali badala ya maneno yaliyopigiwa mstari.
(al.2)

(g) Eleza matumizi moja ya viakifishi vifuatavyo
(al.2)
i) Koma
ii) Mshazari

iii) Ritifaa

iv) Vifungo

(h) Onyesha miundo miwili ya nomino katika ngeli ya (KI- VI.) (al.2)

(i) Kanusha sentensi zifuatazo (al.2)
i) Angesoma kwa bidii angeenda chuo kikuu.
ii) Nimeenda Nairobi kununua gari.

(j) Andika sentensi ifuatayo upya kwa kubadilisha maneno yaliyopigiwa mstari kuwa kinyume.
(al.2)
Mwendawazimu alitembea haraka alipokumbuka alipotoka.

(k) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya udogo umoja. (al.2
Ngoma hizo zao ziliibwa na wezi wale.

(l) Andika katika usemi wa taarifa. (al.3)
"Jichunge, " alimkemea Kamau, "Mienendo yako itakuonyesha cha mtema kuni"

(m) Andika katika hali ya kufanyia.
(al.2)
Yesu alikufa kwa dhambi zetu.

(n) Tunga sentensi moja kudhihirisha maana ya vitate vifuatavyo. (al.1)
gesi/kesi

(o) Changanua kwa kutumia jedwali. (al.4)
Baba yake amemnunulia baiskeli aliyomwahidi mwaka jana.

(p) Tunga sentensi mbili kuonyesha matumizi yafuatayo ya (ku)
(al.2)
i) Kikanushi cha wakati uliopita.
ii) Nafsi ya pili umoja.

(q) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao.
(al.2)
KN (W+RV) + KT (T+RE)

(r) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo.
(al.3)
Mgema aliyesifiwa kwa kuwagemea wakazi tembo nzuri kwa nazi amenaswa.

***ISIMU JAMII*** ***(AL.10)***

***Soma makala haya kisha ujibu maswali.***

Kwani mnauza salamu? Sina *time ya kuwaste hapa*. *Am a busy person* leta *order* yako haraka... Nimesema samaki wa kupaka. Mimi ng'ombe na *chicken*.

(a) Tambua sajili hii. (al.1)
(b) Fafanua sifa **tisa** za sajili hii. (al.9)

# ALLIANCE BOYS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

**Swali la lazima.**

1. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Hapo zamani za kale paliishi sungura na ndovu. Wanyama hawa waliishi baharini.Maulana alikuwa amewatunukia mapenzi si haba.Makazi yao yalikuwa yamepambwa yakapambika. Walitegemea matunda mbalimbali yaliyokuwa baharini kama mapera, matomoko, matikitimaji na kadhalika.

Siku moja usiku wa manane, maji yakaanza kupwa. Ndovu aliathirika zaidi.Alijaribu kuinama majini lakini hakuweza.Alimwita sungura amsaidie lakini sungura alikuwa ametoweka.

Ndovu aliamua kwenda kumtafuta sungura.Alimtafuta hadi msituni lakini hakumpata.Alihofia kurudi baharini na hadi wa leo yumo msituni.

***Maswali***

(a) Tambua utanzu na kijipera chake. (al.2)
(b) Taja fomyula zingine mbili za kutanguliza kifungu hiki. (al.2)
(c) Eleza umuhimu wa kijipera hiki. (al.5)
(d) Eleza sifa za kifungu hiki. (al.5)
(e) Eleza umuhimu wa fomyula:
(i) Kutanguliza (al.3)
(ii) Kuhitimisha (al.3)

***<u>TAMTHILIA ; KIGOGO NA TIMOTHY AREGE</u>***

2. Tulipoanza safari hii matangazo yalikuwa bayana, dhahiri shahiri babu!
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al.4)
(b) Tambua mbinu za uandishi zilizotumika katika kifungu hiki. (al.4)
(c) Eleza matatizo yanayoikumba safari inayorejelewa. (al.12)

3. Eleza nafasi ya mwanamke katika jamii ya kigogo. (al.20)

***RIWAYA YA CHOZI LA HERI NA ASHUMTA K. MATEI***

4. Matatizo mengi yanayowakumba wahusika wengi katika riwaya hii ni mwiba wa kujidunga. Jadili (al.20)
5. Kwa kurejelea riwaya hii, fafanua mbinu zifuatazo. (al.20)
(i) Kinaya
(ii) Mbinu rejeshi
(iii) Sadfa
(iv) Jazanda

**HADITHI FUPI : TUMBO LISILISHIBA.**

6. Kwa kurejelea hadithi ya *Mapenzi ya kifaurongo* na *shogake dada ana ndevu* fafanua changamoto zinazowakumba vijana. (al.20)

7. ***Mame Bakari***
"Una nini ? Umeshtuka mwanangu ! Unaogopa? Unaogopa nini?"
(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (al.4)

(b) Tambua mbinu **mbili** za lugha zilizotumika katika dondoo. (al.2)

(c) Eleza sifa za mrejelewa. (al.6)

(d) Eleza umuhimu wa msemaji. (al.4)

(e) Tambua maudhui yanayojitokeza katika kifungu hiki. (al.1)

(f) Fafanua maudhui katika swali la (***e)*** kwa kurejelea hadithi nzima. (al.3)

8. ***USHAIRI.***
**Soma shairi hili kisha ujibu maswali.**

Sinusubuwe akili, nakusihi e mwandani
Afiya yangu dhahili, mno nataka amani
Nawe umenikabili, nenende sipitalini
Sisi tokea azali, twende zetu mizimuni
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani
Tuna dawa za asili, hupati sipitalini
Kwa nguvu ya kirijali, mkuyati uamini
Kaafuri pia kali, dawa ya ndwele fulani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani.

Mtu akiwa halali, tumbo lina walakini
Dawa yake ni subili, au zogo huauni
Zabadi pia sahali, kwa maradhi yalo ndani
Au kwenda wasaili, wenyewe walo pangani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Mtu kwenda sipitali, nikutojuwa yakini.
Daktari kona mwili, tanena kansa tumboni
Visu vitiwe makali, tayari kwa pirisheni
Ukatwe kama figili, tumbo nyangwe na maini
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Japo maradhi dhahili, kuteguliwa tegoni,
Yakifika sipitali, huwa hayana kifani
Waambiwa damu, kalili ndugu msaidieni

Watu wakitamali, kumbe ndio buriani
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani

Mizimu wakupa kweli, wakueleze undani
Maradhiyo ni ajali, yataka vitu dhamani
Ulete kuku wawili, wamajano na wa kijani
Matunda pia asali, vitu vyae chanoni
Nifwateni sipitali, na dawa zi mlangoni?

***Maswali.***

1. Lipe shairi hii anwani mwafaka. (al.1)
2. Toa sababu zinazofanya mshairi kutaka kwenda hospitali. (al.3)
3. Andika ubeti wanne kwa lugha ya nathari/ tutumbi. (al.4)
4. Taja bahari **mbili** zilizotumika katika shairi hili. (al.2)
5. Tambua nafsineni katika shairi hili. (al.1)
6. Tambua toni ya shairi hili. (al.1)
7. Eleza muundo wa shairi hili. (al.4)
8. Fafanua uhuru wa mshairi unavyojitokeza katika shairi hili. (al.2)
9. Andika maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi hili.

   (al.2)
   (i) dhalili
   (ii) azali

# KAPSABET BOYS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

1. Ndugu yako ameamua kuasi ukapera. Andika ratiba itakayotumiwa siku ya arusi yake.
2. Eleza mikakati ambayo serikali ya Kenya imeweka kukabiliana na mashambulizi ya mara kwa mara ya Kigaidi nchini.
3. Andika insha kuonyesha busara iliyomo katika methali "Mchelea mwana kulia hulia mwenyewe".

4. Andika insha itakayomalizika kwa maneno haya:
   ……………Nilikumbuka ushauri niliopewa na mama mazazi mara kwa mara. Uchungu usiomithilika ulinichoma moyoni, laiti ningalijua.

# KAPSABET BOYS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

1. **UFAHAMU**

   ***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

   Je wajua kwamba Kiswahili ni lugha ya sita ulimwenguni na inatumiwa na watu zaidi ya milioni sita? Kiswahili hivi sasa kimewanda na kunawiri kila pembe ya dunia licha ya vizingiti vinavyoiumba katika usambazaji wake.

   Mbali na lugha za wageni, lugha ya Kiswahili ndiyo ya kipekee ambayo chimbuko lake ni janibu ya pwani ya Afrika, Mashariki Kenya. Ni bayana kuwa lugha hii imevuka mipaka ya Afrika na inaenziwa na waja wa ughaibuni.

   Lugha ya kigeni hasa Kiingereza ndiyo ilitumika kama lugha ya mawasiliano nchini Kenya kabla na baada ya uhuru. Walowezi walipuuza lugha ya Kiswahili na kuhimiza Kiingereza. Baada ya uhuru, baadhi ya viongozi walioshika hatamu ya uongozi walipigia debe Kiingereza na kuweka Kiswahili kapuni. Walidai eti Kiswahili ni lugha ya watu wasio na elimu na ustaarabu.

   Mwasisi wa taifa la Kenya hayati Mzee Jomo Kenyatta anastahili mkono wa tahania kwa kuhimiza viongozi kuhutubia wananchi kwa lugha sanifu ya Kiswahili. Yeye mwenyewe
   hakuachwa nyuma, kwani hotuba zake nyingi ziliendelezwa kwa Kiswahili; ili kukuza na na kuendeleza Kiswahili miongoni mwa wakenya. Serikali iliteua tume ya kuchunguza na kupendekeza mikakati ya kuimarisha elimu nchini. Tume hii iliongozwa na msomi Ominde mwaka 1964. Baada ya utafiti, tume hii ilipendekeza kuwa lugha ya Kiswahili iwe somo la lazima katika shule za msingi nchini. Viongozi mbalimbali tangu wakati huo wametoa maoni kabambe kuhusu kukuza na kuendeleza Kiswahili, lakini vitendo vimekuwa haba mno. Watunga mitaala na sera za Wizara ya Elimu tangu uhuru, wamekuwa na mikatani ya kuyumbayumba kuhusu somo la Kiswahili katika viwango vyote vya elimu.

Mathalani, somo la Kiswahili lilikuwa likifunzwa katika viwango vya shule za msingi bila kutahiniwa. Vipindi vya lugha hii vilikuwa, na hata sasa, vichache vikilinganishwa na Kiingereza ambacho kimekuwa somo la lazima katika viwango vyote vya elimu na utahiniwa.

Chama cha KANU kilichokuwa uongozini wakati huo kilitoa mawazo mema kuhusu Kiswahili. Kwa mfano, mnamo 1969 azimio lilitolewa kuwa Kiswahili kiwe lugha ya taifa, kwa hiyo ilizizititizwa kitumiwe bungeni. Hali hii ndiyo ilipelekea sharti la wabunge kumaizi Kiswahili kabla kuteuliwa kuwania ubunge. Ilipendekezwa na katibu wa chama cha KANU kuwa ifikiapo mwaka 1974, Kiswahili kingekuwa lugha zote mbili zitumiwe kwa pamoja.

Rais mtaafu Daniel arap Moi, alijaribu mno kukuza na kuendeleza lugha hii. Mikutano yake mingi iliendelezwa kwa Kiswahili. Kwa upande mwingine, nchi ya uongozi wake, sera mbalimbali kuhusu Kiswahili ziliibuka Kiswahili kilifunzwa na kutahiniwa katika viwango vya shule za msingi na za upili. Ni somo la lazima katika viwango vya shule za msingi na za upili. Ni jambo la kutia moyo kwani Kiswahili kinafunzwa katika vyuo na shahada mbalimbali hutolewa.

Licha ya kuwa na vyombo vya habari vingi nchini, vipindi vingi hasa katika runinga na redio huendelezwa kwa Kiingereza. Magazeti ya Kiswahili ni haba mno. Hali hii hurudisha maenezi ya Kiswahili nyuma. "Mgalla mue na haki umpe" chambilecho wenye busara. Baadhi ya vyombo vya habari kama kipindi cha kamusi ya changamka" katika redio ya Nation ni kielelezo bora cha kukuza lugha hii tukufu.

Mpaka leo, Kiswahili ni lugha ya wananchi wengi wa Kenya hata imevuka mipaka. Ni wazi kuwa ni lugha ya taifa na kimataifa na hivi karibuni kulingana na kielezo bora cha katiba, itakuwa au imekuwa lugha rasmi, licha ya kutopewa hadhi inayostahili. Kiingereza bado ni lugha rasmi inayotumika katika shughuli mbalimbali. Tatizo kubwa linalokumba uenezaji wa Kiswahili nchini ni wingi wa viongozi ambao wamekua na kulelewa katika mazingira ya kigeni. Baadhi yao hufanya juu chini kutukuza Kiingereza. Huu ni ukengeushi usiofaa. Lugha ya mtaani kwa jina maarafu "sheng| inafukuza badala ya kutukuza Kiswahili.

Iwapo lugha ya Kiswahili inaenziwa na wageni kama mashirika ya utangazaji kama BBC, sauti ya Amerika na sauti ya China, seuze sisi Wakenya? Ni muhimu kuelewa kuwa mwacha mila ni mtumwa. Lugha hii ni yangu, yako na yetu. Ni chombo cha pekee cha

kukuza na kuimarisha umoja wa kitaifa. Taifa lisilo na lugha ni sawa na mtoto asiye na mzazi. Tuvute pamoja tuhifadhi utamaduni wetu wa lugha.

***Maswali***

(a) Eleza njia **nne** zilizotumiwa na waasisi wa taifa la Kenya kukuza na kuendeleza Kiswahili. (Alama 3)

(b) Thibitisha ukitoa ushahidi kuwa Kiswahili ni lugha ya kimataifa. (Alama2)

(c) Kuna vizingiti gani katika maenezi ya Kiswahili nchini Kenya.

(Alama4)

(d) Mwandishi wa makala haya anatoa mfano upi wa kutoa matumaini ya kuendeleza

Kiswahili nchini Kenya. (Alama2)

(e) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika kwenye habari. (Alama 4)

(i) inaenziwa

(ii) sera

(iii) mikakati

(iv) ughaibuni

**2. UFUPISHO**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswahi yanaofuata.***

Uwezo wa mtu kudanganya huonekana mapema zaidi na katika dunia yenye watu wakazi tofauti uwezo huu huonekana katika kila aina ya watu duniani kwa kipindi cha mapema zaidi.

Saikolojia ya nadharia ya uwongo ambapo mtu anaweza au kuufinyanga anavyotaka nikidi ambapo mtu ana miaka minne, lakini si nchini ya hapo.

Watoto hujifunza kutokana na uzoefu na kama wakigundua kwamba wanaposema uwongo wanaadhibiwa huacha kusema uwongo mpaka pale ambapo wanajua namna ya kuunga uwongo wao na kuacha maswali ambayo hayawezi kujibika.

Watoto wanapokuwa wameshajua namna ya kuujenga uwongo mpaka ukakubalika wanakuwa hatari zaidi kwani wanakuwa wameshatoka katika maadili ya kawaida ya ubaya wa kudanganya.

Watoto hawa huweza kujifunza kudanganya baada ya kuona kwa miaka mingi watu wanavyodanganya. Wengine hudanganya kwa bahati mbaya na wengine huwa na tabia mbaya.

Wanaodanganya kwa bahati mbaya mara nyingi hubadilika wanapokuwa watu wazima, lakini pia hata wale wanatengeneza tabia hubadiliki baadaye lakini si sana.

Wakati fulani wapo watu wanaofikiri kwamba watoto hudanganya zaidi kuliko watu wazima.

Uwongo wa watu wazima huwa mbaya zaidi na wenye utata mkubwa kuutambua na hii hutegemea zaidi mbinu za udanganyifu, mazingira na tabia nyingine za watu wazima. Na wapo watu wazima wenye tabia ya kudanganya au kwa lugha ya kitaalamu, pseudolojia fantastika.

Wanafalsafa kama Mkakatifu Augustine, na pia Thomas Aquinas na Immanuel Kant, wanalaani aina zote za udanganyifu. Kwa mujibu wa watu hao watatu hakuna sababu ya aina yoyote ile ya kudanganya.

Ni vyema mtu akauawa, kuteseka au kupata magumu kuliko kudanganya hata kama njia moja pekee iliyobaki ya kujihami ikiwa ni hiyo. Wanafalsafa hao

wanasema kwamba kudanganya kunaharibu uwezo wa mtu kuaminika katika jamii au jamii yenyewe kuaminika.

**Maswali**

(a) Andika ujumbe unaojitokeza katika aya nne za kwanza za makala haya kwa kifupi. (utiririko alama 1) [Alama 6]

(b) Fupisha aya nne za mwisho za makala haya. (utiririko alama 2 ) maneno 50 – 60 (Alama 6)

**3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

(a) i) Tafuatisha sauti irabu na konsonanti (Alama 1)

ii) Andika neno la silabi moja lenye sauti. mwambatono. (Alama. 1)

(b) Kwa nini ngeli ya "ku" huitwa ngeli ya kitenzijina (Alama. 3)

(c) Kanusha sentensi ifuatayo:

Wewe unapenda kuongea na kutenda. (Alama. 2)

(d) Ainisha mofimu katima alimapo.

(Alama. 2)

(e) Tunga sentensi kubainisha matumizi ya vivumishi vya majina. (Alama. 1)

(f) Unda kitenzi kutokana na kivumishi "karimu"

(g) Eleza matumizi ya viakifishi vifuatavyo: (Alama. 4)

(i) Dukuduku

(ii) Nukta pacha

(h) Nyambua vitenzi katika kauli ya kutendesha. (Alama. 2)

(i) Oa

(ii) Ona

(j) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia vishale: Wale walevi wenu wamewasili leo jioni. (Alama. 4)

(k) Kirai ni nini? Toa mfano:

(Alama. 3)

(k) Tunga sentensi kuonyesha upatanisho wa kisarufi ukitumia nomino 'Tambi'

(Alama. 2)

(l) Tumia 'gani' kama kivumishi na vile vile kama kiwakilishi

(m) Andika sentensi ifuatayo katika hali ya urejeshi; Amani yetu inatusaidia

(Alama. 1)

(n) Badilisha sentensi iwe kinyume.
Mtanashati amesifiwa kwa kukitakaba kiti chake. (Alama. 2)

(o) Andika katika hali ya kudunisha: Mboga hii inatosha hawa.
(Alama. 1)

(p) Amrisha katika wingi na umoja nafsi ya pili. (Alama. 2)

Fa____________________________________________________

(q) Sisitiza katika umoja na wingi 'ukuta' ukiwa karibu. (Alama. 2)

(r) Eleza matumizi mawili ya 'ku' (Alama. 2)

(s) Tambua vishazi katika sentensi ifuatayo.
Ijapokuwa Kipchoge hakushinda mbio hizo atatuzwa zawadi kemkem. (Alama. 2)

(t) Tunga sentensi moja kutofautisha vitate hivi.
(Alama. 2)
Mwashi
Mwasi

4. **ISIMU JAMII**
Fafanua mambo matano yaliyochangia kuenea kwa Kiswahili nchini kabla na baada ya uhuru.

# KAPSABET BOYS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
### Julai 2019
### Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

**SEHEMU A: USHAIRI**

1. Sinisumbuwe akili, nakusihi e mwandani,
Afya yangu dhahili, mno nataka amani
Nawe umenikabili, nenende sipitalini
Sisi tokea azali, twende zetu mizimuni,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mababu hawakujali, wajihisipo tabani
Tuna dawa za asili, hupati sipitalini,
Kwa nguvu za kirijali mkunyati uamini,
Kaafuri pia kali, dawa ya ndwele fulani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu akiwa hali, tumbo lina walakini
Dawa zake ni subili, au zongo huanoni,
Zabadili pia sahani, kwa maradhi yako ndani,
Au kwenda wasaili, wenyewe walo Pangani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mtu kwenda sipitali, ni kutojuwa yakini,
Daktari k'ona mwili, tonena kensa tumboni,
Visu visitiwe makali, tayari kwa paresheni,
Ukawa kama fagili, tumbo nyangwe na maini,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Japo maradhiu dhalili, kutenguliwa tegoni,
Yakifika sipitali, huwa hayana kifani,
Waambiwa damu katili, ndugu msaidieni,
Watu wakitaamali, kumbe ndiyo buriani,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

Mizimu wakupa, kweli wakueleleze undani,
Maradhiyo ni ajali, yataka vita thamini,
Ulete huku wawili, au majano na kijani,
Matunda pia asali, vitu vyake shamoni,
Nifwateni sipitali, na dawa ziko nyumbani?

**Maswali**

(a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (Alama 2)
(b) Mtunzi alikuwa na lengo gani alipotunga shairi hili? (Alama 2)
(c) Kwa nini mshairi hataki kwenda hospitali? (Alama 4)
(d) Eleza umbo la shairi hili (Alama 6)
(e) Kwa nini mshairi alitumia ritifaa katika ushairi? (Alama 2)
(f) Andika maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa kwenye shairi. (Alama 4)
(i) dhalili
(ii) azali
(iii) sahali
(iv) kensa

**SEHEMU B: riwaya – CHOZI LA HERI**

2. ***Fafanua namna mbinu ya sadfa ilivyotumiwa katika riwaya.*** (Alama20)

SEHEMU C: kigogo

SEHEMU B: TAMTHILIA YA KIGOGO

2. Uliona nini kwa huyo zebe wako? Eti mapenzi!

i) Eleza muktadha wa dondoo.
(alama 4)

ii) Andika mbinu mbili za lugha zinazojitokeza kwenye dondoo hili.
(alama 4)

iii) Taja hulka za mnenaji unaojitokeza katika dondoo.
(alama 2)

iv) Mwanamke ni kiumbe wa kukandamizwa. Thibitisha kauli hii ukirejelea tamthilia.

(alama 10

**AU**

3. Ni bayana kwamba viongozi wengi katika nchi zinazoendelea wamejawa na tamaa na ubinafsi. Thibitisha kauli hii ukirejelea tamthilia ya kigogo.
(alama 20)

SEHEMU C: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI ZINGINE

**SHIBE INATUMALIZA**

**4.** "Ndugu yangu kula kunatumaliza"

"Kunatumaliza au tunakumaliza"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Fafanua maana ya kitamathali katika kauli 'kula tunakumaliza'

(alam 10)

(c) Kwa mujibu wa hadithi hii, ni kwa namna gani wasemaji wanadai kula kunawamaliza?

(alama 6)

**AU**

5. (a) "Mame Bakari"

Kwa mujibu wa hadithi hii, ubahaimu anaotendewa mwanamke unakuwa na athari mbaya kwake. Onyesha kwa mifano mwafaka.
(alama 10)

(b) "Masharti ya Kisasa"

"…mapenzi ni mateso,ni utumwa, ni ukandamizaji , ni ushabiki usio na maana."

Thibitisha ukweli wa kauli hii kama unavyojitokeza kwenye hadithi.(alama 10)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

6. (a) Taja tanzu zozote **tano** za fasihi simulizi kisha utoe mifano miwili ya vipera vyake.
(Alama 10)
(b) Taja na ueleze sifa zozote **tano** ambazo hupotea fasihi simulizi inapoandikwa.
(Alama 10)
7. (a) Miviga ni nini?
(b) Fafanua sifa zozote **sita** za miviga.

(Alama 12)
(c) Miviga ina majukumu yapi katika jamii?
(Alama 6)

# STRATHMORE SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

1. Wewe ni mtangazaji wa kituo cha utangazaji cha Uzalendo. Studioni umetembelewa na mwanamke mtetezi wa haki za wanawake kuzungumzia namna mwanamke ametelekezwa katika jamii ya sasa. Andika mahojiano kuhusu suala hili.

   (Alama 20)

2. Kuna njia anuwai zinazoweza kutumiwa kulitandarukia tatizo la ajira nchini. Fafanua.

   (Alama 20)

3. Andika kisa kinachoafiki methali**; Mgagaa na upwa hali wali mkavu.**

   (Alama 20)

4. Tunga kisa kitakacho kamilika kwa kauli ifuatayo;

   …niliduwaa, nikasimama kisha nikaangalia nyuma huku machozi yakinitoka. Nilikumbuka wosia wa walimu na wazazi wangu, lakini kitumbua changu kilikuwa kimeingia mchanga

# STRATHMORE SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

1. **UFAHAMU (Alama 15)**

*Soma Makala yafuatayo kisha ujibu maswali.*

Yasemekana kuwa Shungwaya ndicho kitovu cha watu waishio Giriama katika janibu za pwani ya Kenya na wanaojulikana kwa jumla kana Wamijikenda. Yaaminika kuwa bado wakiwa Shungwaya, walimuua Mgalla mmoja mwenyeji wa Shungwaya na kitendo hicho kiliamsha hasira kali za Wagalla, hata ikawawia vigumu Wamijikenda kuishi kwa usalama pamoja na ndugu zao hao.

Hata hivyo, Wamijikenda hawakugura mara moja wala wote kwa pamoja bali walihama katika vipindi tofuati na katika makundi madogomadogo. Kila kundi lililofika Giriama lilijenga 'kaya' au mji wake. Kwa jumla, walihama kwa makundi tisa.

Vile vile, Wamijikenda walihama na fingo yao ambayo ilifukiwa na viongozi wao katikati ya kaya zao, palipokuwa na msitu mdogo. Hakuna ajuaye hasa mahali ilipofukiwa ila wazee hao waliopenda kufanyia baraza mahali hapo.

Mnamo mwaka wa 1870, mzee Menza na mkewe walibarikiwa kufungua kizazi kwa kupata mtoto wa kike waliyemwita Mekatilili. Walimlea vizuri na alipoanza kuzungumza, alionyesha dalili za kuwa na kipawa cha pekee. Kwanza, alipenda kujua kila kitu kilichoihusu jamii yake na pili alichukizwa sana na kiumbe aliyemdhulumu kiumbe mwenzake. Kwa mfano, aliwaonea vipepeo imani walipoliwa na ndege. Tena alizipenda sana mila na desturi za watu wa jamii yake – Wamijikenda.

Siku moja, baada ya Mekatilili kufikia utu uzima, mama yake alimwita chemba akamwambia, "Mwanangu sasa umeshabalehe, nami ningependa kuwaona wajukuu wangu kabla sijawafuata wazee waliotangulia. Waonaje tukikuoza? Mimi na baba yako tumepata mume ambaye ni kufu yako kabisa."

"Ninaelewa, maana hizi ni desturi zetu, lakini ningefurahi zaidi kama mngeniruhusu nijichagulie mume ninayempenda." Binti alimjibu mamaye.

"Mnazi na uwe mrefu, huyumba kufuata upepo." Mama akajibu. Tangu hapo binti akawa hana la kujibu ila kukubali.

Siku ya harusi, watu wengi walihudhuria na wakastarehe kwa tembo la mnazi ambalo lilikuwa limetengenezewa kwa wingi. Jioni hiyo, mekatilili alichukuliwa kwa mumewe Masendeni, karibu na mto Sabaki. Ikawa hangeonana na wazazi wake kila siku kama ingalivyokuwa mapenzi yake. Wakati huu kote nchini Kenya kulikuwa kumejaa wageni, wengi wao wakiwa walowezi na watawala wa kibeberu. Walikuwa wameanzisha mashamba ya mikonge, kahawa na chai. Walihitaji watu wa kupalilia mashamba yao hayo. Hata hivyo Waafrika hawakuwa na haja ya kulima wala pesa. Hata walipolima, ni kwa minajili ya

kubadilishana mazao na kula.Iliwabidi Wazungu kutumia mizungu ili kuwashurutisha Waafrika kuwalimia. Baadhi ya mikakati waliyobuni ni kuwateka nyara watu barobaro

na kutoza kodi. Ni katika harakati kama hizo ambapo mumewe Mekatilili alitekwa, asirudi tena kwake. Wakati uo huo, wazazi wa Mekatilili waliaga dunia.
Mambo haya yalimpa mekatilili msukumo. Baada ya muda wa kuomboleza kuisha, alijiunga na wazee wapigania ukombozi, mmoja wao akiwa Wanje, kakaye mumewe. Aliwaunganisha wanawake na kuwahimiza wasiige mila na desturi za kizungu. Aliwahutubia wanaume na kuwakumbusha kuwa ilikuwa lazima wailinde nchi yao. Siku moja alishikwa kwa kuwalisha watu kiapo. Alipelekwa bara, Kisii, mbali kabisa na kwao, Magharibi mwa Kenya na akatiwa kizuizini pamoja na Wanje. Hata hivyo, walifaulu kutoroka na kwa muda wa siku ayami walipitia kwenye mabonde na milima, misitu na nyika hadi wakarudi Giriama.
Mabeberu walikasirika sana. Hata hivyo, walikuwa wamechelewa. Katika safari yao kurudi Giriama, walifaulu kuhubiria wengi dhidi ya mgeni. Vita vya ukombozi vilikuwa vimeshika.

**Maswali**

1. Ni kwa nini Wagiriama wanajulikana kama Wamijikenda? (al.1)
2. Ni maafa gani yaliyompata Mekatilili katika maisha yake? (al.4)
3. Ni hali gani inayotawala katika makala haya. (al.2)
4. Taja masuala ya kijinsia yanayojitokeza katika makala haya. (al.2)
5. Wazungu walitumia mbinu gani ili kuwashurutisha watu kuwafanyia kazi mashambani mwao. (al.2)
6. Andika maneno mengine yenye maana sawa na;
   i) kugura……………………………………………….…………………(al.1)
   ii) kubalehe……………………………………………………………….(al.1)
7. Eleza maana ya;
   i) Mnazi na uwe mrefu huyumba kufuata upepo ………………………………………………………………………………(al.1)
   ii) Kitovu cha watu waishio Giriama ……………………………………………………………………….…(al.1)

**2. UFUPISHO (Alama 15)**

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.*

Kiswahili tunasema ni lugha yetu kwa sababu ndiyo lugha ya Kiafrika inayoongewa katika nchi nyingi barani Afrika. Ni lugha yetu kwa sababu ni lugha asilia mojawapo za Afrika. Siyo lugha iliyoletwa na watu wa nchi za nje kama vile Kiingereza, Kifaransa na Kireno. Uzuri wa Kiswahili sasa ni kuwa kimeenea kote Afrika Mashariki na Kati.
Wenyeji asilia waliokuwa wakiongea lugha hii tangu awali ni Waswahili. Waswahili hawa hata leo wako na wanaendelea kuitumia lugha hii kama lugha yao ya mama, kama vile Wakikuyu watumiavyo Kikikuyu, Wakamba, Kikamba na Wadigo lugha ya Kidigo. Makao yao Waswahili tangu jadi yanapatikana kaunti ya Pwani. Makao yao yameanzia upande wa Kaskazini Mashariki ya Kenya , na wanapakana na nchi ya Somalia huko. Wameenea katika upwa huo wa Pwani, ikiwamo Lamu, Malindi, Mombasa, Pemba, Unguja, Visiwa vya
Ngazija na kuendelea.

Lugha ya Kiswahili ina lahaja nyingi kulingana na sehemu wanamoishi. Kwa mfano, Waswahili wa Lamu huongea lahaja ya Kiswahili inayoitwa Kiamu. Waswahili wa Mombasa huongea lahaja ya Kimvita. Pemba wanaongea Kipemba, Ngazija lahaja ya Kingazija, Unguja lahaja ya Kiunguja na kadhalika. Kutokana na lahaja hizi na nyinginezo za Kiswahili ambazo hazikutajwa hapo, wataalamu wa lugha walitokea na Kiswahili sanifu. Hiki Kiswahili sanifu ndicho kitumiwacho katika mafunzo ya shule, uandishi wa vitabu na mawasiliano ya kiserikali na kibiashara.

Nchini Kenya, kwa muda mrefu Kiswahili hakikuthaminiwa kama Lugha ya Kiingereza. Sababu mojawapo ni kuwa Kiswahili hakikufanywa somo la lazima katika mitaala ya shule, wala kutahiniwa katika shule za msingi. Hata katika shule za upili, katika kufunzwa na kutahiniwa hakikupewa umuhimu wowote. Kwa ajili hii wanafunzi wengi waliacha kujifunza Kiswahili kama somo. Hali hiyo ilifanya Kiswahili kuonekana kama lugha inayoongewa na wale watu wasio na kisomo ama elimu nyingi. Kwa ajili ya fikira hizi, watu wengi wamekuwa wakikichukia, kukidunisha na kujaribu kuongea Kiingereza kila nafasi inapojitokeza.

Miaka michache iliyopita, Kiswahili kilianza kutiliwa mkazo katika shughuli zote nchini Kenya. Kwa upande wa msimamo wa nchi lugha hii ilionekana yenye manufaa katika kuleta
umoja na kuwaunganisha wananchi wote. Jambo hili ni muhimu kwa maendeleo ya nchi iwayo yote. Umoja huleta maelewano na undugu. Hali hizi mbili zinapokuwapo, amani
husambaa nchini mote.

Tukitazama mfumo wa elimu wa 8-4-4, Kiswahili kimepewa nafasi sawa katika ratiba za shule kama lugha ya Kiingereza. Kiswahili kinatahiniwa kama somo muhimu kuanzia shule ya msingi hadi shule ya upili. Kinyume na enzi za zamani, siku hizi mwanafunzi anayesoma Kiswahili, hata asipofaulu vizuri katika lugha ya Kingereza ana nafasi sawa ya kupata kazi kama wengine.

**Maswali**

a) Fupisha aya tatu za mwanzo kwa maneno 80.
(alama 7)
Matayarisho

b) Eleza vile Kiswahili hakikuthaminiwa na namna hali hii inavyobadilika. (alama 8)
Matayarisho

3. **MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

(a) Toa **maelezo** ya jinsi ambavyo hewa huzuiliwa wakati wa kutamka sauti hizi. **(alama 2)**

i) /p/...................................................................................................................
ii) /ch/.................................................................................................................
iii) /m/..................................................................................................................
iv) /r/...................................................................................................................

(b) Tenga silabi katika neno: alimhukumu. **(alama 1)**

(c) Tunga sentensi moja yenye kitenzi kishirikishi kikamilifu na vitenzi sambamba. **(alama 3**

(d) Tumia neno <u>**mji**</u> kama **kielezi cha mfanano**. **(alama 1)**

(e) Onyesha **namna tatu** za kutumia kiambishi "ji" katika **sentensi moja**, kisha ueleze **matumizi** husika. **(alama 3)**

(f) Ziweke nomino hizi katika **ngeli** zake. **(alama 2)**

i) waya ..........................................................................................................

ii) kilembwe ..........................................................................................................

(g) Tambua virai vilivyopigiwa mistari ni vya **aina** gani kisha uonyeshe **miundo** yake. **(alama 4)**

(i) <u>Kikapu kilichofumwa juzi</u> kitauzwa marikiti.

(ii) Wenzetu <u>walikuwa wakijinaki kabla ya dimba</u>.

(h) Eleza **maana mbili** za sentensi**:** Zainabu alisema atakusaidia. **(alama 2)**

(i) Onyesha **majukumu** ya mofimu katika neno**:** awaliaye **(alama 3)**

(j) **Andika kinyume:** Aliiangika picha ukutani baada ya sherehe. **(alama 2)**

(k) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo <u>bila</u> kutumia kiambishi <u>ku</u>. **(alama 2)**

i) tuma

ii) pinda

(l) Eleza tofauti iliyopo kati ya <u>ukanushaji</u> na <u>kinyume</u>. **(alama 2)**

(m) Andika kwa usemi wa taarifa: "Viungo hivi havitatosha kuunga mchuzi wenu", mpishi alalamika. **(alama 2)**

(n) Tumia **jedwali** kuchanganua sentensi ifuatayo**:** Alipotuona alitupuuza, lakini sisi tulimsalimia. **(alama 4)**

(o) Tumia vitate vya <u>jua</u> , <u>toa</u> na <u>baka</u> katika sentensi **tatu tofauti. (alama 3)**

(p) Kamilisha kwa viigizi mwafaka. **(alama 2)**

(i) Ameanguka .......................... matopeni.

(ii) Mlango ulibishwa ..............................

(q) Tofautisha sentensi. **(alama 2)**

(i) Ungalisoma kwa bidii, ungalipita mtihani.

(ii) Ungelisoma kwa bidii, ungelipita mtihani.

**4. ISIMU JAMII (Alama 10)**

**Maswali**

a) "........ unaweza kukata rufaa iwapo unaonelea kuwa umehiniwa ........."

i) Bainisha sajili ya mazungumzo haya.

(al.1)

ii) Fafanua sifa za matumizi ya lugha katika muktadha huu. (al.4)

b) Jadili changamoto zinazokumba kuimarika kwa Kiswahili katika jamii ya sasa.(al.5)

# STRATHMORE SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

**SWALI LA LAZIMA**
**CHOZI LA HERI – A MATEI**

"Maisha yangu yalijaa shubiri tangu utotoni."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)
b) Kwa kutolea mfano, bainisha tamathali ya usemi inayojitokeza katika kauli hii. (al.2)
c) Jadili athari za vita katika jumuia ya Chozi la Heri (al. 14)

**TAMTHILIA – KIGOGO - P – KEYA**
**Jibu swali 2 au 3**

2. Siwezi mimi, siwezi, sitaki kuwa gurudumu la akiba ..... hujayaacha hayo?
   a) Eleza muktadha wa dondoo (al.4)
   b) Eleza sifa nne za msemaji wa kauli hii (al.4
   c) Tambua matumizi 12 ya jazanda katika tamthilia al. 12)

**AU**

3. Kuyaopoa mataifa machanga kutoka kwa kinamasi cha madhulumu kuna gharama yake. Ukirejelea tamthilia ya Kigogo, ipatie nguvu kauli hii. (al. 20)

**HADITHI FUPI – TUMBO LISILOSHIBA – ALFA C / DUMU K.**
**Jibu swali 4 au 5**

Nizikeni papa hapa – Ken Walibora

4. "Ndugu yangu tahadhari na hawa........."
   a) Eleza muktadha wa dondoo (al.4)
   b) Eleza sifa za msemewa (al.4)
   c) Taja na ufafanue maudhui sita katika hadithi hii

(al.12 )

**AU**

5. a) Tulipokutana Tena – Alfa Chokocho
Jadili jinsi maudhui ya umaskini yalivyoshughulikiwa katika hadithi ya 'Tulipokutana Tena'. (al. 10)

**Mame Bakari**

b) Kina dada wanaobakwa wanakabiliwa na changamoto nyingi. Tetea. (al. 10)

**USHAIRI**

**Jibu swali 6 au 7**

**6. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Alikwamba wako mama, kajifanya hupuliki,
Kakuasa kila jema, ukawa ng'oo! Hutaki,
Sasa yamekusakama, popote hapashikiki,
Uliyataka mwenyewe!

Babayo lipokuonya, ukamwona ana chuki,
Mambo ukaboronganya, kujifanya hushindiki,
Sasa yamekunganya, kwa yeyote hupendeki,
Uliyataka mwenyewe!

Mazuri uliodhania, yamekuletea dhiki,
Mishikeli miania, kwako ona haitoki
Mwanzo ungekumbukia, ngekuwa huaziriki,
Uliyataka mwenyewe!

Dunia nayo hadaa, kwa fukara na maliki,
Ulimwenguni shujaa, hilo kama hukumbuki,
Ya nini kuyashangaa? Elewa hayafutiki,
Uliyataka mwenyewe!

Mwenyewe umelichimba, la kukuzika handaki,
Ulijidhania samba, hutishiki na fataki,
Machangu yamekukumba, hata neno hutamki,
Uliyataka mwenyewe!

Kwa mno ulijivuna, kwa mambo ukadiriki,
Na tena ukajiona, kwamba we mstahiki,
Ndugu umepatikana, mikanganyo huepuki,
Uliyataka mweyewe!

**Maswali**

a) Eleza dhamira ya shairi hili (al.2)
b) Tambua njia **mbili** anazotumia mtunzi wa shairi hili kuusisitiza ujumbe wake. (al.2)

c) Taja na utoe mifano ya aina zozote **mbili** za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi. (al.4)

d) Andika ubeti wa **tatu** katika lugha nathari/tutumbi (al.4)

e) Kwa kutoa mfano **mmoja mmoja** onyesha aina mbili za idhini ya kishairi katika shairi hili (al.4)

f) Bainisha toni ya shairi hili (al.2)

g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi (al.2)

i) mstahiki
ii) hupuliki

**SHAIRI**

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Nikiwa na njaa na matambara mwilini
Nimehudumika kama hayawani
Kupigwa na kutukanwa
Kimya kama kupita kwa shetani
Nafasi ya kupumzika hakuna
Ya kulala hakuna

Ya kuwaza hakuna
Basi kwani hili kufanyika
Ni kosa gani lilotendeka
Liloniletea adhabu hii isomalizika?

Ewe mwewe urukaye juu angani
Wajua lililomo mwangu moyoni
Niambie pale mipunga inapopepea
Ikatema miale ya jua
Mamangu bado angali amesimama akinisubiri?
Je nadhari hujitokeza usoni
Ikielekea huku kizuizini?
Mpenzi mama, nitarudi nyumbani
Nitarudi hata kama ni kifoni
Hata kama maiti yangu imekatikakatika
Vipande elfu, elfu kumi
Nitarudi nyumbani

Nikipenya kwenye ukuta huu
Nikipitia mwingine kama shetani
Nitarudi mpenzi mama...
Hata kama kifoni.

**Maswali**

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (al.1)

b) Tambua nafsineni katika shairi hili (al.2)

c) Eleza toni katika shairi hili (al.2)
d) Taja mambo manne ambayo mshairi analalamikia (al.4)
e) Fafanua dhamira katika shairi hili (al 2)
f) Thibitisha kuwa hili ni shairi huru (al 2)

g) Taja na ufafanue sifa mbili za mshairi (al 2)
h) Fafanua mbinu 3 za kimtindo zilizotumika katika ubeti wa tatu (al 3)
i) Eleza maana ya maneno yafuatoyo kama yalivyotumiwa katika shairi hili (al 2)

   i) hayawani
   ii) nadhari

**FASIHI SIMULIZI**

a) Maudhui na fani ya maigizo hutegemea mwigizaji. Thibitisha kwa hoja tano. (al. 5)
b) Taja aina **mbili** za miviga (al. 2)
c) Eleza hasara **tatu** za miviga (al. 3)

d) Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Ikiwa wewe kweli ni mkazamwanangu
Name ndiye nilompa uhai mwana unoringia
Anokufanya upite ukinitemea mate
Chakula kuninyima, wajukuu kunikataza ushirika,
Miungu nawaone chozi langu, wasikie kilio changu,

Mizimu nawaone uchungu wangu
Radhi zao wasiwahi kukupa,
Laana wakumiminie,
Uje kulizwa mara mia na wanao,
Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao,
Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha
Wakazawanao wasikuuguze katika utu uzima wako!

**<u>Maswali</u>**

i. Tambua aina ya mazungumzo katika tungo na utoe sababu

(al.2 )

ii. Msemaji ni nani katika tungo hili (al. 1)

iii. Tambua sifa mbili za anayeelekezewa mazungumzo haya (al. 2)

iv. Taja na ueleze sifa tano za kipera hiki cha mazungumzo (al. 5)

# MANGU HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

**1. SWALI LA LAZIMA**

Ukiwa Gavana Mtajika wa Kaunti yako umealikwa kuwazungumzia wanafunzi wa kidato cha nne katika shule ya Mafanikio. Andika Tawasifu utakayowasilisha.

**2.** Eleza jinsi udanganyifu katika mitihani utaathiri maisha ya kizazisi kijacho.

**3.** Andika kisa kitakachothibitisha maana ya methali: Mtenda mema kwa watu atendea nafsiye.

**4.** Kamilisha tukio kwa maneno yafuatayo:

"….waliwasili saa tatu baadaye. Uharibifu wa mali na maisha ulikuwa umeshatendeka wala kufika kwao hakukusaidia kwa lolote."

# MANGU HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

**1. UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.**

Waziri wa uchukuzi Bwana Msafiri ametoa mwito kwa kila mwananchi kuzingatia sheria za barabarani ili kumaliza visa vya ajali vilivyokithiri.Alisema kuwa ongezeko la ajali za barabarani linachangiwa pakubwa na watu binafsi.

Akiongea katika hafla ya kuzindua mbinu za kuhakikisha usalama barabarani, Bwana Msafiri alisema yasikitisha kuona kuwa ajali za barabarani zimeongezeka katika siku za hivi majuzi.Alielezea kuwa wizara yake imekerwa na utekelezaji wa majukumu na mapuza miongoni mwa wanaohusika na sekta ya uchukuzi.

Alisema wengi wa wenye magari wamepuza masharti mengi ambayo yaliwekwa na wizara,yaliyokusudiwa kupunguza ajali. Alisema magari mengi yamekuwa kachara na kwamba mengi yameng'olewa vidhibiti mwendo. Basi magari yanaendeshwa kwa kasi ya umeme.Hili limeongeza ajali kwa kiasi kikubwa. Mengi hayana mishipi ya usalama na wasafiri hukabiliwa na hatari wanaposafiri. Aliongeza kuwa sura ya magari hayo ni dhihirisho kuwa wenye magari wamepotoka kabisa,magari mengi yamerembeshwa hata kwa picha chafu, jambo linalodhihirisha utovo wa mbeko na kutofuata sheria mengine yanacheza muziki kwa sauti ya juu hivi kwamba hata dereva na utingo hawawezi kusikia grudumu liking'oka. Baadhi yao yanaonyesha picha chafu chafu za video na kuufanya usafiri kuwa vyumba vya sinema chafu! Alisemakutovaa sare kwa madereva na makondakta na kuwapakia abiria kupita kiasi ni kilele cha upuuzi wa sheria zilizowekwa.

'Wasafiri pia wanapuuza masharti yaliyowekwa kwa lengo la kuwafaa,'alisema waziri. Alisikitika kuwa wasafiri wengi hawafungi mishipi ya usalama hata inapopatikana, aidha wanakubali kuingia magari yaliyojaa tayari, hali inayoongezea uwezekano wa gari kupata ajali kwa kulemewa na uzito. Aliwakumbusha kuwa gali likipata ajali wakiwa wamepakiwa hivi, hawezi kugharamiwa na bima ya gari kwa vile bima yenyewe hukatiwa idadi mahususi ya wasafiri. Aliwalaumu watembeaji barabarani kwa kutozingatia sheria za kawaida. Alisema kwa mfano katika gurufu kuna mahali ambako kuna vivuko ila hawavitumii na wengine huishia kugongwa na magari.

Mwisho aliwalaumu maafisa wa trafiki wanaotekeleza majukumu yao. Akitisha kuwachukulia hatua kali, alisema kuwa yaskitisha kusikia kuwa wanachukua kadhongo na kuyaachilia magari yaliyo na kasoro badala ya kuyashtaki kulingana na sheria. Aliwaongezea lawama wasafiri kwa kunyamaza wanapoyaona haya

yakitendeka machoni. Alisababisha kicheko aliposema kuwa baadhi ya wasafiri huwahimiza makondakta watoe chai haraka ili waendelee na usafiri ya bila kujali hatari wanazojiingiza kwazo.

Akionya kuwa angechukua hatua ya kuregesha utulivu, alihitimisha kwa kusema kuwa wizara yake **limetoa ilani** kwa watumiaji wote wa barabarani. **Alitoa makataa** ya siku kumi na nne ambapo yoyote asiyefuata kaida zote za barabarani atachukuliwa hatua kisheria.

**Maswali**

a)Fafanua sababu za mwito wa waziri wa uchukuzi Bwana Msafiri? (alama 2)

b)Eleza jinsi wenye magaari wamechangia katika kukithiri kwa visa vya ajali barabarani? (alama 4)

c)Fafanua mchango wa wasafiri katika kudorora kwa hali ya usalama barabarani. (alama 3)

d)Eleza majukumu ya maafisa wa trafiki katika kudumisha usafiri kulingana na ufahamu. (alama 3)

e)Toa visawe vya maneno yafuatayo. (alama 3)

(i) kondakta:……………………………………………………………………

(ii) toa ilani:……………………………………………………………………..

(iii)toa makataa:……………………………………………………………………

**2.UFUPISHO: (ALAMA 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**.

Serikali kupitia Wizara ya Elimu imetoa mwongozo wa karo ambao unastahili kuzingatiwa katika shule za upili kufuatia hatua ya shule mbalimbali kuongeza karo kwa viwango mbalimbali. Hatua hiyo inadhamiriwa kumkinga mzazi dhidi ya kunyanyaswa kifedha walimu hasa ikizangiwa kuwa gharama ya maisha imepanda mara dufu.

Hata hivyo, ingekuwa bora ikiwa serikali ingefanya maamzi kwa ushirikiano na walimu wakuu maana kwa hakika suala la karo linahusu matumizi ya fedha ambayo pia huja na gharama zake. Gharama hii inaokana na ununuzi wa vitabu vya kiada na vya mazoezi, karatasi za uchapishaji mitihani, kwa kuwa wanafunzi sharti wasome na waandike.

Vilevile, gharama hii inatokana na ununuzi wa kemikali za kutumiwa katika maabara. Aidha, kuna gharama ya kuendesha michezo na tamasha za muziki na drama.

Wanafunzi wa shule za malazi hula na kulala na kwa sababu hiyo maamuzi ya kifedha lazima yafanywe.

Jambo ambalo linastahili kuangaliwa kwa makini ni viwango vya kupanda kwa gharama ya maisha. Lazima tujiulize gharama hiyo imepanda kwa kiasi gani na wapi? Kwa kweli haiwezekani kununua kilo moja ya mahindi kwa bei hiyo hiyo Kitale, Mombasa na Turkana. Vile vile ni muhimu kujiuliza ikiwa shule husika ni ya mashambani au ya mjini? Kwa hivyo, sharti la kifedha ni muhimu katika kuamua karo ya shule na maeneo mbalimbali nchini.

Pili, hebu tuangalie ikiwa shule inavyohusika ni ya kiwango cha kaunti ndogo, kaunti au cha kitaifa. Hili ni muhimu kwa kuwa hali ya masomo katika shule hizo

hutofautiana.Tofauti kuu hutokana na miundomisingi na programu za masomo zinazoendeshwa.

Kwa mfano, programu za kitahmini, kompyuta na zinazohusu ziara huhitaji fedha nyingi. Shule ambayo ina masomo kama vile muziki, sanaa na sayansikimu sharti zitoze karo ya juu kwa kuwa masomo hayo huandamana na gharama ya kununua vyombo na vyakula?
Sasa mbona fedha za ziada? Wanaotetea kupunguzwa kwa karo wanapunguza mchango wa motisha katika ufanifu wa masomo. Ndio, baadhi ya shule hutoza karo ya juu ili kuwamotisha walimu kwa vyakula na kwa zawadi ili kuwastahi wanapopata matokeo mema. Hali hiyo huwafanya kujikakamua kazini na kutoa huduma ya hali ya juu.

Fedha za ziada vile vile, hutumiwa kuwajiri walimu wa ziada ikizingatiwa kuwa serikali haijawaajiri walimu wa kutosha. Pia katika baadhi ya shule, wanafunzi huandaliwa vyakula spesheli tofauti na mseto wa maharagwe na mahindi almarufu ‗maram' uliozoeleka katika shule nyingi ikumbukwe kuwe lishe bora ni mojawapo ya haki za kimsingi kwa watoto ambayo sharti iheshimiwe.

Kwa marefu na mafupi yake, serikali haipaswi kuweka viwango sawa vya karo kwa kila shule kwa maana hilo huenda likazua mgogoro wa kiutawala katika shule nyingi. Shinikizo za kupunguzwa kwa karo inayotozwa hasa katika shule za upili zinafaa kutetewa kimantiki wala si kihisia.

Mambo huenda yangekuwa tofauti ikiwa serikali ingewajibika kwa upande wake kwa kuwaajiri walimu wa kutosha kuwaongeza walimu mshahara na kuwatambua kwa zawadi wanapofanya kazi nzuri na kuwapandisha vyeo.Hata hivyo, mgala muue na haki umpe; hatua kali zinapaswa kuchukuliwa dhidi ya walimu wanaowatoza wazazi karo ya juu kupindukia ili kuendeleza maslahi yao ya kibinafsi.

Naamini kuwa hatua ya Waziri wa Elimu kukutana na washikadau katika sekta ya elimu kuhusu karo na uteuzi wa wanafunzi wa kujiunga na shule za upili ni ya busara na inafaa kutoa mwelekeo mzuri kuhusu masuala tata yaliyopo kwa sasa.

(a) Fafanua mambo muhimu yanayostahili kuzingatiwa katika kutathmini viwango vya karo katika shule nchini Kenya.
(Maneno 65 - 70) (alama 8, 1 ya

mtiririko)

(b) Fupisha aya tatu za mwisho.(maneno 40 - 45) (alama 7, 1 ya mtiririko)

**3.MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Ukizingatia sehemu ya kutamkia, mwinuko wa ulimi na hali ya mdomo, tofautisha sauti zifuatazo. (alama 3)

/ e /, / i / na / u /

(b)Ukitolea mfano eleza aina **mbili** za miundo ya silabi katika Kiswahili. (alama 2)

(c)Eleza maana ya mghuno katika lugha ya Kiswahili. (alama 1)

(d)Kwa kutolea mfano mwafaka, fafanua tofauti iliyopo kati ya kishazi na kirai. (alama 2)

(e)Ukitolea mfano mwafaka, fafanua majukumu yoyote **manne** ya viambishi awali. (alama 2)

(f)Nomino zifuatazo zinapatikana katika ngeli zipi? (alama 1½)

i) chumvi:………………………………………………………………………

ii) nywele:……………………………………………………………………...

iii) mafuta:……………………………………………………………………….

(g) Eleza matumizi ya kiambishi **ku**

Kulia kwake kulisababisha msongamano wa watu alikokuwa. (alama 1½)

(h) Tunga sentensi yenye muundo wa:

N + V + T + H + N + E + U + T (alama 4)

(i) Yakinisha katika umoja: (alama 2)

Msingalivumilia nyakati ile msingalipata zawadi kubwa.

(j) Andika katika udogo.

Jijipu lilipasuka lenyewe.

(k) Ukitolea mfano fafanua njia zozote tatu zinazotumiwa katika uunjdaji wa maneno. (alama 3)

(l) Ukitungia sentensi, onyesha matumizi ya vivumishi vya nomino. (alama 2)

(m)Tunga sentensi kubainisha matumizi ya vivumishi vya nomino katika ngeli ya U - I; katika umoja na wingi . (alama 2)

(n) Ukitolea mfano mwafaka, eleza tofauti iliopo katika kauli zifuatazo.

Kutendeana na kutendana. (alama

2)
(o) Onyesha yambwa katika sentensi ifuatayo.
(alama 2)
Mwamburi alitumia ufunguo kumfungulia Rashid mlango
(p) Andika katika usemi wa taarifa:
'Nataka ufikirie sana juu ya maisha yako ya ndoa. Sitaki uishi maisha yasiyo na mweleko,' Babu alinishauri.
(alama 3)

(q) Kwa kutoa mfano, eleza matumizi mawili kila mojawapo wa alama zifuatazo:
(alama 2)
i) ritifaa

ii) koma/ kituo

(r) Eleza maana ya msemo ufuatao :
kula kitana. (alama 2)

**4.ISIMU JAMII (ALAMA 10)**
a) Eleza maana ya lugha rasmi
(alama 2)
b) Fafanua sifa zozote za lugha rasmi.
(alama 8)

# MANGU HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

**SEHEMU YA A:HADITHI FUPI**
**TUMBO LISILOSHIBA**

**1.LAZIMA**
"Rasta twambie bwana!"
(a)Weka dondo katika muktadha
(alama 4)
(b) Taja mbinu zilizotumiwa na mwandishi katika dondoo hili
(alama 2)
(c) Ni kwa vipi mzungumziwa anamchukulia mwalimu mkuu kama hambe?
(alama 4)
(d) Je, mtihani wa maisha ni amwani faafu ya hadithi hii.
(alama10)

**SEHEMU YA B:TAMTHILIA**
**KIGOGO(PAULINE KEA)**
**Jibu swali la 2 au 3**

2. "Keki ya uhuru imeliwa kwingine,mwaletewa masazo"
(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili .
(alama 4)
(b) Taja na uthibitishe tamathali ya usemi katika dondoo hili .
(alama 2)

(c) Eleza namna keki ilivyoliwa katika tamthilia hii.
(alama14)
3.Fafanua mbinu zifuatazo kwa kutolea mifano mwafaka
(i) Kwelikinzani (alama 10)
(ii) Taashira (alama 10)

**SEHEMU YA C:RIWAYA**
**CHOZI LA HERI(ASSUMPTA)**
**Jibu swali la 4 au 5**

4. "Mwanangu ,ni vyema kujifunza kuishi na wenzako bila kujali tofauti za ukoo na nasaba"
(a)Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
(b)Fafanua sifa nne za msemewa wa kauli hii (alama 4)
(c)Onyesha jinsi tofauti za ukoo na nasaba zinavyoadhiri wahusika riwayani kwa kutoa
mifano **sita** mwafaka (alama 12)
5. Fafanua mbinu zifuatazo kama yalivyotumika katika Riwaya ya Chozi La Heri
(a) Kweli kinzani (alama 10)
(b) Sadfa (alama 1)

**SEHEMU YA D: USHAIRI.**
**Jibu swali la 6 au 7**

6. **Risala za Amani**

Tungo peleka risala ,sala kwa Mwenyezi Mungu
Na watu kila kabila ,bila kujali mnengu
Waambie ukabila , kabila lao na langu
Si neno pamwe na mila , ila sote walimwengu.

Sote ni taifa hili , hili watie fahamu
Mtu ni mwenye amali , mali bora ni nidhamu
Ndio inostahili ,ili amani idumu
Yatupasa kuhimili , mili tusimwage damu

Wa bara na wa mvita , vita tusende tumika
Tutarudia kujuta , uta utapofyatuka
Kutujengea matata, ,tata zisipotatuka
Huja huku kuzorota , ota la kuthaminika.

Mijini na mashinani , nani hufuzu kwa vita ?
Taifa lenye amani , mani hupata kuota
Pakawa kutamakani , kani pasipo kuteta
Pakiwa matumaini , ini huota mafuta .
(Mwalaa Mranga Nyanje)

(a) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
(b) Nafsineni anatoa wasia muhimu kwa kila mwanajamii . Fafanua. (alama 4)
(c) Onyesha aina zifuatazo za mistari zilizotumiwa kwenye shairi.
(i) Kifu
(ii)Mshata (alama 2)
(d) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (alama 4)
(e) Eleza bahari ya utungo huu kwa kurejelea mipangilio ya maneno katika mishororo. (alama 2)

(f) Taja kwa kutolea mifano aina za urudiaji / takriri zilizotumiwa kwenye shairi. (alama 2)

(g) Eleza namna mtunzi wa shairi hili alivyotumia uhuru wake . (alama 2)

7. ***Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata.***

Naujuwa mwanzo wake, vile ulivyochipuza,
Kilofanya mkereke, na kisichowaumiza,
Ya kuwa sepata mke, katu hakuwapendeza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !
Mwasema matako hana, yako sawa kama meza,
Tena pua yako pana, kama ya kubandika,
Lakini mimi naona, yenu sitoyasikiza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Kipita nae pahali, sakubimbi hubwagiza,
Nzitonzito kauli, asengenywazo aziza,
Nywele za kipilipili, hasongi asongomeza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Munenayo ni mazito, hadi yeye humliza,
Bali kwangu ni matoto, muhali kunichukiza,
Japo miguuye fito, haitoshi mtembeza ?
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Nataka watowa khofu, kwa munayo mtangaza,
Si yule mpenda pofu, kawambia ni kengeza,
Ni mwenyewe nimeshufu, muhali kunigeuza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Tafadhalini mwachie, musilumbe kumaliza,
Unyonge musitumie, kila siku kumaliza,
Haya ni yeye na mie, yawaje mukachagiza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

Hakujiumba mwenyewe, musighafilike wenza,
Aloumba mimi nawe, ndiye aliyemtweza,

Tusijitie kiwewe, tukakufuru muweza,
Nenani mutamaliza, yeye nampenda vivyo !

**Maswali**

a) Eleza bahari za shairi hili kwa kutoa ithibati kamili (alama 3)

b) Kwa kutoa mifano mwafaka, eleza methali zozote mbili kwenye shairi (alama 4)

c) Bainisha mambo yoyote **manne** nafsineni anayazungumzia (alama 4

d) Fafanua idhini ya mshairi (alama 4)

e) Andika ubeti wa **tatu** kwa lugha tutumbi (alama 3)

f) Eleza maana za vifungu hivi kama vilivyotumika kwenye shairi

(i) sakubimbi hubwagiza (alama 1)

(ii) Musighafilike wenza (alama 1)

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

**8.** a) Eleza dhana zifuatazo.

i) Michezo ya chekechea
ii) Vivugo
iii) Kimai
iv) Maapizo
v) Simo (alama 10)

b) Fafanua majukumu **matano** ya ngomezi. (alama 10)

# PRECIOUS BLOOD SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 - Insha

**1. SWALI LA LAZIMA**

Ukiwa Gavana Mtajika wa Kaunti yako umealikwa kuwazungumzia wanafunzi wa kidato cha nne katika shule ya Mafanikio. Andika Tawasifu utakayowasilisha.

**2.** Eleza jinsi udanganyifu katika mitihani utaathiri maisha ya kizazi kijacho.

**3.** Andika kisa kitakachothibitisha maana ya methali: Mtenda mema kwa watu atendea nafsiye.

**4.** Kamilisha tukio kwa maneno yafuatayo:

"….waliwasili saa tatu baadaye. Uharibifu wa mali na maisha ulikuwa umeshatendeka wala kufika kwao hakukusaidia kwa lolote."

# PRECIOUS BLOOD SCHOOL- RIRUTA
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

1. **UFAHAMU** (Alama 15)

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Ustawi wa dola lolote lile hutegemea mseto wa nguvu, maarifa chipukizi, uchapuchapu wa barubaru, pamoja na maarifa, upevu, uvumilivu na tajriba ya wazee. Tunaweza kuumithilisha ufanisi wa nchi na jumba la ghorofa lililojengwa juu ya tegemezo: msingi huu ukiwa imara, ghorofa nyingi zaweza kuinuliwa. Nayo imara ya tegemezo hutegemea vyuma imara visivyotetereka na vifaa vinginevyo. Zaidi ya haya yote, mafundi wahusika kama vile wasanifu mjengo, wahandisi, mafundi bomba na wengineo sharti wawe na ujuzi tosha ili kufanikisha kazi inayohusika. Katika taswira hii, twaweza kuelewa ni kwa nini baadhi ya nchi zimestawi huku nyingine zikiitwa ulimwengu wa tatu. Shida za nchi hizo ni kutozistawisha taaluma ambazo ndizo msingi wa maendeleo, hivyo huwa na walakini katika utekelezaji. Matokeo yake ni kulimatia.

Nchi nyingi humu barani mwetu zimekosa kustawi kutokana na kasoro nyingi tulizo nazo katika uimarishaji wa taaluma zetu. Sababu kuu ni kuwa, wengi wetu hukimbilia kutekeleza kazi mbalimbali hata bila ujuzi wowote kwa kazi hizo. Tabia kama hii inatokana na ukweli kuwa sisi hatujali kama tuna vipawa vya kufanya kazi fulani. Wengine huvunjwa moyo na waliowazingira kuwa vipawa vyao havifai. Hivyo, si ajabu kuona kijana aliye na kipawa fulani akikosa kukivuvia kwa sababu labda hata hatambui kuwa anacho.

Wengi wa wakembe wetu hukosa kuvitambua vipawa vyao, hivyo kukosa kuendeleza utaalamu unaohusiana navyo kwa kukosekana kwa **mtalaa** wa kuvichochea katika mfumo wa elimu. Mfumo wa elimu nchini Kenya kwa sasa unasisitiza wanafunzi kupita mtihani ili kuingia vyuoni. Hata hivyo, ni muhimu kuvikuza vipawa walivyo navyo vijana ili wavitumie katika siku za halafu. Vitambuliwe mapema shuleni bali si vyuoni. Kunao wanagenzi wengine ambao, licha ya kuvitambua vipawa vyao hawavifukutii kamwe, huvipuuza na kujisukuma katika taaluma ambazo hazikuwafaa kamwe. Kunao wanagenzi wengine ambao hutamani na kuingilia taaluma fulani, si kwa kuzipenda, bali kwa kuwa wandani wao wazishiriki. Hawajui kuwa kibaya chako si kizuri cha mwenzio. **Huliona tanga la nguo wakalisahau la miyaa.** Kuna wengine ambao huziandama taaluma fulani kwa kushurutishwa na wazazi au wadhamini wao. Nao vijana hukosa ukakamavu wa kujiamulia na kukubali shingo upande maamuzi hayo. Hata hivyo, kuna wale ambao hujitosa katika taaluma hizo bila kushurutishwa ili wapate hadhi. Matokeo ni kuwa kijana huzifanya kazi hizo kwa chati wala si kwa dhati. Wengine hujipenyeza kwa taaluma fulani eti kwa kuwa wamekosa nyingine. Si ajabu basi kutokana na ukosefu wa ajira kumwona mtaalamu wa mifugo akiwa mwalimu, mwalimu akiwa dereva na tabibu akiwa mkulima hali zaraa haimudu.

Ili kupata suluhu katika jambo hili, sharti kila mmoja wetu ashiriki katika kuitambua, kuikuza, kuikomaza na kutumia taaluma ya kila kijana. Twaweza kuuiga mfano wa Wazungu wafanyavyo kwao. Wao hujitahidi kuvitambua vipawa vya watoto wangali wachanga hali ambayo huwasaidia kuzikuza taaluma zao baadaye. Naye kijana akishajua atakachofanya, afaa kufanya utafiti ili kufikia kina cha taaluma yake.

**Maswali**

(a) Eleza sababu za watu kujishughulisha na taaluma zisizo zao. (alama 2)

(b) Eleza kikwazo cha ustawi wa nchi zinazoendelea. (alama 1)

(c) Taja mambo **manne** yanayostawisha taifa. (alama 4)

(d) Taja mambo **matano** yanayokwamiza uendelezaji wa vipawa miongoni mwa vijana. (alama 5)

(e) Kuna tofauti gani kati ya Waafrika na Wazungu katika ukuzaji wa taaluma? (alama 2)

(f) Eleza maana ya 'Huliona tanga la nguo wakalisahau la miyaa'.

(alama 1)

(g) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo vilivyotumika katika ufahamu. (alama 2)
(i) kulimatia
(ii) mtalaa

**2. MUHTASARI (Alama 15)**

Tunapinga na kulaani vikali visa vya ugaidi vinavyoendelea kutetemesha usalama wa wananchi. Hivi ni vitendo vya kinyama vinavovyotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu na utu kabisa. Inaghadhabisha kuona Wakenya wasio na makosa wakiteswa na kuuawa kinyama bila huruma na watu wasio na utu. Hatuogopi wala hatuna fedheha kuamba kuwa magaidi hawa wamelaaniwa na siku zao zimehesabiwa hapa duniani. Damu ya mwananchi asiye na makosa katu watailipia. Napinga vikali pale magaidi hawa wanapohusisha vitendo hivi kuwa vita vya kidini; vita hivi si vya kidini kwani hakuna dini yoyote iliyo na imani ya kumuua kinyama binadamu asiye na makosa.

Kando na tishio la ugaidi, Wakenya pia wanakabiliwa na hatari za ujambazi, mauaji, unajisi, ubakaji na maovu mengine. Katika juhudi za kudumisha usalama, polisi wana jukumu la kutumia kila mbinu kuhakikisha kuwa haki za kikatiba za Wakenya kuhusu kulindwa kwa maisha na mali yao zimedumishwa. Lakini cha kusikitisha ni kuwa, mbinu ambazo polisi wamekuwa wakitumia hasa ile ya kufanya misako inayoishia kuwanasa mamia ya raia wasio na habari kuhusu kinachoendelea, inawaongezea Wakenya mateso. Hali hii inawaacha kwenye hatari ya kunaswa na majambazi ama polisi.

Matumizi ya mbinu hii ya misako yameishia kunasa raia wengi wasio na makosa.Wanaponaswa, hurundikwa kwenye seli usiku mzima ama siku kadha na hata kama wanaaachiliwa huwa tayari wameteseka. Huu ni ukiukaji wa haki za raia. Kadhalika, mbinu

hii inaonekana kama hila ya polisi kutaka kuonyesha wanafanya kazi lakini sio mwafaka kwani wanapokuwa wakiwanasa raia mijini na mitaani, magaidi na majambazi wanaendelea na shughuli zao.

Badala ya kusaka wakora kwa kubahatisha kwenye umati, polisi wanapaswa kubuni njia ambazo zitawapa mwelekeo mwafaka zaidi kuhusu wahalifu ili waweze kuwafuatilia. Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo. Hii itawezesha polisi kupata habari muhimu kuhusu vitisho vya uhalifu. Maafisa wa usalama pia wanaweza kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

**Maswali**

(a) Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu suala la ugaidi (alama 7,1 utiririko) (maneno 60-70)

(b) Kwa kutumia maneno yasiyozidi 50 fupisha aya **mbili** za mwisho. (alama 6, 1 utiririko)

**3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

(a) (i) Eleza jinsi kitamkwa /u/ kinavyozuiliwa (alama 2)

(ii) Andika tofauti moja kati ya sauti hizi.
(alama 1)
/t/ na /d/

(b) Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo.
(alama 2)

Mwanajamii yule alijibu maswali yote kwa makini.

(c) (i) Eleza maana ya vitenzi vishirikishi.
(alama 1)

(ii) Tunga sentensi moja moja kuonyesha aina mbili za vitenzi vishirikishi.
(alama 2)

(d) Yakinisha sentensi ifuatayo.
(alama 1)
Mtoto hakufundishwa wala kupewa vitabu.

(e) (i) Eleza maana ya silabi. (alama 1)

(ii) Huku ukitoa mifano, eleza miundo miwili ya silabi za Kiswahili.
(alama 2)

(f) Ainisha viambishi katika sentensi hii kimuundo na kidhamira.
(alama 3)
Wataonana
(i) Kimuundo:

(ii) Kidhamira

(g) Tumia nomino yoyote katika ngeli ya KU-KU pamoja na kiashiria kisisitizi cha karibu kutunga sentensi.
(alama 1)

(h) Tunga sentensi **moja** katika wakati uliopita hali isiyodhihirika
(alama 1)

(i) Tunga sentensi **mbili** ili kubainisha maana za neno: Jinsi
(alama 2)

(j) Huku ukitoa mifano, eleza matumizi mawili ya alama ya kinyota katika uakifishaji.
(alama 2)

(k) Eleza miundo **mitatu** ya vishazi tegemezi na kuitolea mifano mwafaka katika sentensi. (alama 3)

(l) (i) Eleza maana ya shamirisho kipozi.
(alama1)

(ii) Benta alimlimia mamake shamba kwa trekta. Anza kwa yambiwa (alama1)
.

(m) (i) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao.
S – KN (N/Wθ) + KT (Ts+T+RH+E) (alama 2)

(ii) Changanua kwa matawi sentensi ifuatayo: (alama 2)
Kile chake kipya kinanipendeza mno.

(n) Eleza matumizi yoyote mawili ya kiambishi KU na kuyatolea mfano mmoja mmoja wa sentensi. (alama 2)

(o) Tunga sentensi sahihi ukitumia kivumishi cha ki ya mfanano na kielezi cha namna kitumizi. (alama 2)

(p) Tunga sentensi ukitumia kitenzi cha silabi moja kinachomaanisha kuogopa katika kauli ya kutendeka. (alama 2)

(q) Eleza maana ya:
(i) Papo kwa papo kamba hukata jiwe. (alama 1)

(ii) Ua langu la waridi limechanuka. (alama 1)

(r) (i) Tunasema baraza la wazee …………………cha kuni na ……………..…… ya nguo (alama 1)
(ii) Ajuza ni kwa mwanamke mzee na …………………ni kwa msichana mchanga ilhali shaibu ni kwa mwanamume mzee na ………………………ni kwa mvulana aliyebaleghe.

(alama 1)

**4. ISIMUJAMII** **(Alama10)**

***Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Niaje wasee! *Midterm* ilibamba lakini ilkua fupi sana, tumerudi *books*, huu ni mwaka wa mwisho tujikaze jo. Msifikirie hizo hepi zetu ni *reality, kuchill* ni jambo la maana jo! ama niaje *bro…hustle ni real*, bidii ndio itatuokoa

(a) Tambua sajili inayohusishwa na kifungu hiki (alama2)

(b) Eleza sifa zozote **nne** za kimtindo zinazojitokeza katika kifungu hiki. (alama 4)

(c) Eleza sababu **nne** zinazosababisha matumizi ya lugha ya aina hii. (alama 4)

# Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

**SEHEMU A: LAZIMA: SHAIRI**
**WASIA**

Huno wakati mufti, vijana nawausia
Msije juta laiti, mkamba sikuwambia
Si hayati si mamati, vijana hino dunia
Uonapo vyang`aria, tahadhari vitakula

Japo aula kushufu, na machoni vyavutia
Dunia watu dhaifu, yaugua nasikia
Vijana nawasarifu, falau mkisikia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

Jepusheni na zinaa, mlale penye sheria
Msije andama baa, makaa kujipalia

Jepusheni na zinaa, madhara kukadiria
Uonapo yyang'aria, tahadhari vitakula.

Ngawa waone wazuri, nadhifu kukuvalia
Wajimwaie uturi, na mapoda kumichia
Si mlango nyumba nzuri, ngia ndani shuhudia
Uonapo vyang'aria , tahadhari vitakula.

Wawapi leo madume, anasa walopapia?
Wamepita ja umeme, leo yao sitoria
Shime enyi wana shime, bora kumcha Jalia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula

Nambie faida gani, nambie ipi fidia
Upatayo hatimani, waja wakikufukua
Ila kufa kama nyani, kasoro yako mkia
Uonapo vyang`aria, tahadhari vitakula.

Vyatiririka tariri, vina vyanikubalia
Alo bora mshairi, pa tamu humalizia
Nahitimisha shairi, dua ninawapigia
Uonapo vyang'aria , tahadhari vitakula.

Ewe Mola mtukuka, si shaka wanisikia
Wakingie wanarika, na anasa za dunia
Amina wangu Rabuka, dua yangu naishia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

**MASWALI:**

a) Ni ujumbe gani wanaopewa vijana kupitia shairi?. ( alama 4)
b) Bainisha tamathali mbili za usemi katika shairi hili. ( alama 2)
c) Eleza bahari ya shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. ( alama 2)
   i) Idadi ya vipande katika mshororo

ii) Mpangilio wa vina katika beti.

d) Eleza mbinu zozote mbili za kishairi zilizotumika katika shairi hili. ( alama 2)

e) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari ( alama 4)

f) Eleza toni ya shairi hili. ( alama 1)

g) Tambua: ( alama 2)

i)Nafsi neni

ii)Nafsi nenewa

h) Eleza umuhimu wa mbinu ya kimtindo iliyotumika katika ubeti wa tano. ( alama 2)

i) Eleza maana ya msamiati: ‘ aula’ ( alama 1)

**SEHEMU B : RIWAYA**

**CHOZI LA HERI.**

1. Jadili maudhui ya 'asasi ya ndoa' kama yalivyuangaziwa riwayani (alama 20)

**AU**

2. Fafanua maudhui ya nafasi ya vijana katika jamii **(alama 20)**

**SEHEMU C: TAMTHILIA**

**KIGOGO: PAULINE KEA**

2 ``Tunajivunia kuwa na kampuni kubwa zaidi ya uzalishaji sumu ya nyoka barani.’’

a) Eleza muktadha wa kauli hili. (alama 4)

b) Andika mbinu moja ya lugha iliyotumika katika kauli hii. (alama 2)

c) Kwa kutumia mifano mwafaka, onyesha kwa hoja **kumi na nne(14**) jinsi sumu ya nyoka ilivyoathiri eneo la Sagamoyo katika tamthilia ya kigogo. ( alama 14)

3. Fafanua jinsi mwandishi wa tamthilia ya kigogo alivyofaulu kutumia mbinu zifuatazo za uandishi.

a) Jazanda alama 10)

b) Majazi ( alama 10)

**SEHEMU YA D: HADITHI FUPI**

**TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE (ALIFA CHOKOCHO NA DUMU KAYANDA)**

**TUMBO LISILOSHIBA ( S. A MOHAMMED)**

4``Hakuna aliyeweza kukitegua kitendawili chenyewe lakini…’’

a)Eleza muktadha wa dondoo hili. ( alama 4)

b) Tambua tamathali ya usemi iliyotumiwa katika dondoo hili. ( alama 2)

c) Fafanua chanzo na hatima ya kitendawili kinachorejelewa katika dondoo hili. ( alama 10)

d) Eleza wasifu wa warejelewa katika dondoo hili. ( alama 4)

**SEHEMU YA D: FASI HI SIMULIZI**

**JIBU SWALI LA 5 AU 6**

5 (a) (i) Ulumbi ni nini? ( alama 2)

ii) Ulumbi hutekeleza majukumu gani katika jamii?. ( alama 5)

iii) Fafanua mambo **manne** yanayomfanya mtu awe mlumbi bora. ( alama 8)

b) Eleza namna ambavyo hadhira huhusishwa katika uwasilishaji wa fasihi simulizi. ( alama 5)

6 (a) i) Eleza sifa **sita** za maghani.
( alama 6)

ii) Fafanua aina zozote **nne** za maghani. ( alama 4)

b) i) Fafanua majukumu **manne** ya hurafa katika jamii. (alama 4)

ii) Eleza vipengele **sita** vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi. (alama 6)

# KENYA HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

**1. Lazima.**

Umepata tangazo la nafasi ya kazi ya uhariri katika shirika la uchapishaji wa vitabu vya fasihi andishi kwenye gazeti la Taifa Leo. Andika barua ya kuomba nafasi hii na uambatanishe na wasifu kazi wako kwa maelezo zaidi.

**(Alama 20)**

**2.** Utelekezaji wa mtoto wa kiume nchini ni janga kuu. Jadili. **(Alama 20)**

**3.** Andika insha inayoafikiana na methali Baniani mbaya kiatu chake dawa.

**(Alama 20)**

**4.** Andika insha itakayomalizikia kwa;

…walipofungua mlango huo hatimaye,wengi hawakuweza kuzuia hisia zao.Waliangua vilio kwa maafa waliyoyashuhudia.
**(Alama 20)**

# KENYA HIGH SCHOOL

## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM

## Julai 2019

## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

**1 UFAHAMU (alama 15)**

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Suala la mahusiano ya wanadamu katika jamii, uainishaji wake na udhihirikaji wake limewashughulisha wataalamu wa elimu jamii kwa dahari ya miaka. Suala hili huwatafakarisha wataalamu hao kutokana na umuhimu wake katika maisha ya binadamu. Msingi mkuu wa uainishanji wa mahusiano hayo ni kukichuza kipindi cha mahusiano
yenyewe. Yapo mahusiano bainaya waja ambayo yanachukua muda mfupi, kwa mfano saa au dakika chache na mengine ambayo huenda yakachukua miaka ayami.

Mahusiano ya muda mrefu kabisa ni yale yanayojulikana kama mahusiano ya kudumu. Inamkinika kudai kuwa miundo ya kijamii, kisiasa na kiuchumi huweza kuyadhibiti mahusiano hayo kwa kiasi kikubwa. Watu wengi huitakidi kuwa uhusiano uliopo baina ya mtu na jamaa yake utachukua muda mrefu, na kwa hiyo ni uhusiano wa kudumu. Hali hii hutokana na uhalisi kuwa tunahusiana na jamaa zetu kwa kipindi kirefu labda tangu ukembe hadi utu uzima wetu. Uhusiano huuhautarajiwi kuvunjwa na umbali wa masafa baina yetu;tunaendelea kuwasiliana kwa barua au, katika enzi hii ya utandawazi,kwa kutumia nyenzo za teknohama kama mtandao na simu za mkononi na kudumisha uhusiano wetuwa kijamaa. Hata hivyo, inawezekana baadhi ya mahusiano ya kijamaa yasiwe ya kudumu. Mathalan, uhusiano uliopo baina ya mke na mume, na ambao unatarajiwa kuwa wa kudumu au wa kipindi kirefu,unaweza kuvunjwa kwa kutokea kwa talaka. Talaka hiyo inavunja ule uwezekano wa uhusiano wa kudumu unaofumbatwa na sitiari ya pingu za maisha.

Katika ngazi ya pili,mahusiano ya kipindi cha wastani,kuna mahusiano yanayohusisha marafiki zetu maishani, shuleni au kwenye taasisi zozote zile, majirani zetu, wenzetu katika mahali mwa kazi,washiriki kwenye sehemu za ibada au za burudani na wenzetu kwenye vyama tofauti na makundi ya kujitolea. Inawezekanakudahili kuwa baadhi ya mahusiano haya,hususan baina ya marafiki na majirani huweza kuwa ya miongo na daima. Hali hii huweza kutegemea muundo na mfumo wa jamii. Kwa mfano, kwa wanajamii waoishi kwenye janibu fulani mahsusi, na kwa miaka tawili bila ya kuhajiri,uhusiano wao na majirani huweza kuwa wa kudumu. Hali hii **inasigana** na hali iliyoko kwenye maisha ya mijini. Maisha ya mijini yana sifa ya kubadilikabadilika. Isitoshe,kutokana na mfumo wa maisha ya kibepari **yameghoshi** ubinafsi mwingi. Mawimbi ya mabadiliko na ubinafsi huweza kuumomonyoaukuta wauhusiano wa kudumu.

Mwelekeo wa maisha ya siku hizi ya uhamaji kutoka maeneo au viambo walikoishi watu unasababisha kupombojea kwa mahusiano ya kudumu baina yao na majirani zao. Uhusiano katiya wenza katika mazingira ya kazi unahusiana kwa kiasi fulani na ule wamajirani.

Vimbunga vya ufutwaji kazi, ubadilishaji wa kazi, hali zisizotegemewa na mifumo ya kimataifa pamoja na hata mifumo ya kisiasahuweza kuathiri mshikamano wa wanaohusika kazini.

Kiwango cha mwisho cha mahusiano ni uhusiano wa mpito au wa muda mfupi. Mahusiano ya aina hii hujirikatika muktadha ambapo pana huduma fulani. Huduma hizi zinaweza kuwa za dukani, kwenye sehemu za ibada,kwenye kituo cha mafuta,kwa kinyozi, kwa msusi na kadhalika. Kuna sababu kadha zinazotufanya

kuyazungumzia mahusiano ya aina hii kama ya mpito. Kwanza, uwezekanowa mabadiliko ya anayeitoa huduma hiyo ni mkubwa. Si ajabu kuwa unaporudi kwa kinyozi au msusi unatambua aliyekushughulikia hayupo. Hata hivyo, kuna **vighairi** hususa pale ambapo mtoa huduma anayehusika ni yule yule mmoja.

Mahusiano ya mpito yanatawaliwa na'uhusiano wa chembe chembe.' Uhusiano wa chembe chembe, bidhaa ya mfumo wa kibepari, unamaanisha kuwa kinachoshughulisha mtu ni chembe ndogo tu ya mwenzake. Chembe hiyo inaweza kuwa huduma, kwa mfano, gazeti analokuuzia mtu, viatu anavyokushonea,nguo anazokufulia,ususi anokufanyia na kadhalika. Mahussiano ya aina hii yametovukwa na hisia za utu na ni zao la mifumo ya kisasa ya kiuchumi na kijamii. Mtu anayehusiana na mwenzakekwa misingi ya chembe ndogo tu, huenda asijali kama mwenzake amekosa chakula,amefutwa kazi,amefiliwa,ameibiwa na kadhalika.

Suala kuu tunalopaswa kujiuliza ni: je, tunahusianavipi na jamaa zetu, marafiki zetuna majirani zetu? Je, uhusianowetu na raia wenzetu ni wa aina gani? Je, uhusiano wetu na nchi yetu ni wa mpito au ni wa kudumu?

(a) Taja kigezo cha kuzungumzia mahusiano. (alama 1)

(b) Eleza imani ya watu kuhusu mahusiano ya watu. (alama 1)

(c) Fafanua athari ya teknolojia kwenye mahusiano ya watu. (alama 2)

(d) Eleza sababu **nne** kuu za kuharibika kwa mahusiano katika maisha ya leo.(alama 2)

(e) Taja sifa kuu za mahusiano ya muda mfupi. (alama2)

(f) Je, kifungu hiki kina ujumbe gani mkuu? (alama2)

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 3)

(h) (a) inasigana
(b) yameghoshi
(c) vighairi

**2 UFUPISHO (alama 15)**

Jamii ya leo inatawaliwa na kuendeshwa na kanuni ya maarifa. Inawezekana kusema kuwauchumi wa jamii za leo na zijazo utategemea maarifa zaidi kuliko utakavyotegemea uwezo wowote mwingine. Utambuzi wa uwezo mkubwa wa maarifa katika maisha ya binadamu ndio msingi wa watu kusema 'maarifa ni nguvu.'

Maarifa huelezwa kwa tamathali hii kutokana na uwezo wa: kuyadhibiti,kuyaendesha, kuyatawalana kuyaongoza maisha ya binadamu popote pale walipo. Mtu ameyakosa maarifa fulani huwa ameikosa nguvu hiyo muhimu na maisha yake huathirika pakubwa. Kwa msingi huu, maarifa yanawezakuangaliwa kama utajiri mkubwa ambao binadamu anaweza kuutumia kwa faida yake au kwa faida ya wanajamii wenzake. Ukweli huu ndio unaoelezwa na methali ya Kiswahili: 'Elimu ni

mali.' Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu popote alipo basi ni maarifa. Je, maarifa kwa upande wake yana sifa gani? Maarifa yenyewe hayana upinzani. Maarifa uliyo nayo huweza kuwa na watu wengine pasiwe na upinzani baina yenu kwa kuwa kila mmoja ana maarifa sawa. Kila mmoja ana uhuru wa kuyatumia maarifa hayo kama chanzo cha kuyazalisha mengine. Utumiaji wa maarifa yenyewe hauyamalizi maarifa hayo. Maarifa hayawezi kugusika ingawa mtu anaweza kuyanyumbua maarifa yenyewe kwa kuyatumia kwa namna tofauti.

Maarifa huingiliana na maarifa mengine. Maarifa aliyo nayo mtu huweza kuhusishwa na maarifa aliyo nayo mtu mwingine ili kuvyaza au kuzuka na maarifa tofauti. Maarifa yanaweza kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa namna ambavyo mtu huweza kufanya bidhaa nyingine ile. Kwa mfano, ni muhali mtu kulalamika kuwa hawezi kutembea kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa sababu ana mzigo wa maarifa kichwani.

Sifa nyingine muhimu ya maarifa ni kuwa yanaweza kuwasilishwa kwa njia au mitindo mingine ya kidhahania. Ikiwa unataka kukihamisha chombo fulani kutoka sehemu moja hadi nyingine, lazima uwazie ukubwa wake, uzito wake na labda hata umbali wa panapohusika. Maarifa huweza kubadilishwa au kugeuzwa na kuwa ishara
ambazo huyafanya kuwasilishswa kwa njia nyepesi kuliko kwa mfano ikiwa mtu atayawasilisha katika muundo wa, kwa mfano,kitabu.

Maarifa yana sifa ya uhusianaji. Kipengele fulani cha maarifa huwa na maana kinapowekwa sambabmba au kugotanishwa na kipengele kingine cha maarifa. Huo huwa muktadha mzuri wa kueleweka au kuwa na maana kwa mfano, neno 'mwerevu' huweza kuwa na maana kwa kuwekwa katika muktadha wa 'mjinga', ' mjanja', 'hodari' na kadhalika.

Maarifa huweza kunifadhiwa katika nafasi ndogo sana. Suala hili linaeleweka kwa njia nyepesi tunapoangalia maarifa katika muktadha wa teknolojia. Data zinazowahusu mamilioni ya watu,ambazo zingehitaji maelfu ya maktaba na lukuki ya vitabu, huweza kuhifadhiwa kwenye kifaa kidogo kinachoweza kutiwa mfukoni.

Maarifa hayawezi kuthibitiwa au kuzuiliwa mahali fulani yasisambae. Maarifa huenea haraka sana. Maarifa ni kitu kinachoepuka pingu za watu wanaopenda kuwadhibiti binadamu wenzao. Hata pale ambapomfumo wa kijamii au wa kisiasa unafanya juu chini kuwadhibiti raia au watu wenyewe,ni muhali kuyadhibiti maarifa yenyewe. Inawezekana kuzidhibiti njia fulani za uenezaji wa maarifa lakini maarifa hayo yatapata upenyu wa kusambaa. Ni kweli kuwa maarifa ni nguvu inayozishinda nguvu zote.

(a ) Fupisha aya ya pili na tatu (maneno 55-60)(alama 5, 1 ya utiririko)

(b) Eleza sifa kuu za maarifa kama zinavyojitokeza kuanzia aya ya nne hadi aya ya nane.
(maneno 100-110) (alama 10, 2 za utiririko)

**3 MATUMIZI YA LUGHA** (alama 40)

(a) Taja vipasuo sighuna (alama 2)

(b) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao:
kirai nomino, kirai tenzi, kirai husishi (alama 2)

(c ) Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi (alama 2)Vibarua wamefanya kazi haraka ipasavyo .
(d) SahihishaMwalimu mwenye alikuja jusi anafudisha Kiswahili vizuli. (alama 2 )
(e) Yakinisha sentensi ifuatayo
(alama 2) Hakuwapiga wala kuwalaghai.
(f) Eleza viambishi katika neno lifuatalo (alama 3)
Walichokilalia
(g) Bainisha vivumishi vilivyo katika sentensi ifuatayo:
(alama 2)
Wanafunzi wote wenye nidhamu watapewa tuzo kubwa na mwalimu wao.
(h) Changanua sentensi ifuatayo ukitumia mistari au mishale
(alama 4)
Yohana na Otieno hucheza kandanda.
(i) Andika sifa tatu zinazobainisha sentensi changamano.
(alama 3)
(j) Geuza sentensi ifuatayo iwe katika usemi halisi.
(alama 2)
Askari jela alimwuliza Kendi kama alidhani hapo ni kwao. Alimwamuru aende kwake mara moja.
(k) Toa mfano wa neno lenye muundo ufuatao wa silabi. (alama 1)
IK+KI+KI+KI
(l) Onyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo.
(alama 2)
(i) kibainishi
(ii) parandesi
(m) Tumia neno –baya kama: (alama 2)
(i) kiwakilishi
(ii) kielezi
(n) Tunga sentensi sahili ukitumia kitenzi ‘la’ katika kauli ya tendewa. (alama 2)
(o) Badilisha maneno yaliyopigiwa mstari yawe vitenzi.
(alama 2)
Yunis amepata faida kutokana na ukulima.
(p) Kwa kuzingatia maagizo andika upya sentensi ifuatayo:
(alama2)
Tinga amewafanya ng’ombe wake wanywe maji.
(Anza kwa : Mifugo wangu …………..usitumie ‘amewafanya’)
(q) Onyesha miundo miwili ya nomino za ngeli ya U-U. (alama 2 )
(r) Bainisha maana mbili zinazojitokeza kutokana na sentensi hii.
(alama 2)
Umu alimwandikisha mkewe.
(s) Tunga sentensi katika wakati uliopo hali isiyodhihirika.
(alama 1)

## 4. ISIMUJAMII (Alama 10)

(a) Lahaja huainishwa katika makundi **mawili**. Yataje (alama 2)
(b) Eleza sifa zozote **nne** za lugha ya taifa.
(alama 4)
(c )Tolea ushahidi namna **nne** kwamba Kiswahili ni lugha ya kimataifa.
(alama 4)

# KENYA HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

***SEHEMU YA A: RIWAYA***
***Assumpata K. Matei: Chozi la Heri***

***LAZIMA***

1. "Haiwezekani! Hili haliwekazi! Itakuwa kama kile kisa cha yule kiongozi wa kiimla wa kike"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

(b) Eleza kwa kifupi yaliyowapata Wahafidhina baada ya usemi huu. (alama.4)

(c) Riwaya ya ***Chozi la Heri*** inaonyesha maovu yanayotamalaki katika jamii.Thibitisha. (alama 12)

**SEHEMU B: TAMTHILIA**
***Kigogo.Pauline Kea.***

***Jibu swali la 2 au la 3***

2. Tatizo la uongozi katika bara la Afrika ni kikwazo kikubwa cha maendeleo. Kwa kurejelea matukio kwenye tamthilia ya kigogo, jadili ukweli wa kauli hii (alama 20)

**AU**

3. "Mtalipa kila tone la damu mlilomwaga Sagamoyo ;wewe na watu wako."
a) Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)
(c) Eleza sifa za mzungumzaji (alama 4)
(b) Thibitisha kwa kutoa mifano kuwa maisha ya anayezungumziwa yametawaliwa na dhuluma. (alama 12)

***SEHEMU YA C: HADITHI FUPI***

4. Kwa kurejelea hadithi ya mapenzi ya kifaurongo, onyesha jinsi jamii imegawanyika kitabaka kuegemea.
i. Kielimu
ii. Kikazi

iii. Kiuchumi (alama 20)

***SEHEMU D: SHAIRI***

**WASIA**

5. Huno wakati mufti, vijana nawausia
Msije juta laiti, mkamba sikuwambia
Si hayati si mamati, vijana hino dunia
Uonapo vyang`aria, tahadhari vitakula

Japo aula kushufu, na machoni vyavutia
Dunia watu dhaifu, yaugua nasikia
Vijana nawasarifu, falau mkisikia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

Jepusheni na zinaa, mlale penye sheria
Msije andama baa, makaa kujipalia
Jepusheni na zinaa, madhara kukadiria
Uonapo yyang'aria, tahadhari vitakula.

Ngawa waone wazuri, nadhifu kukuvalia
Wajimwaie uturi, na mapoda kumichia
Si mlango nyumba nzuri, ngia ndani shuhudia
Uonapo vyang'aria , tahadhari vitakula.

Wawapi leo madume, anasa walopapia?
Wamepita ja umeme, leo yao sitoria
Shime enyi wana shime, bora kumcha Jalia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula

Nambie faida gani, nambie ipi fidia
Upatayo hatimani, waja wakikufukua
Ila kufa kama nyani, kasoro yako mkia
Uonapo vyang`aria, tahadhari vitakula.

Vyatiririka tariri, vina vyanikubalia
Alo bora mshairi, pa tamu humalizia
Nahitimisha shairi, dua ninawapigia

Uonapo vyang'aria , tahadhari vitakula.

Ewe Mola mtukuka, si shaka wanisikia
Wakingie wanarika, na anasa za dunia
Amina wangu Rabuka, dua yangu naishia
Uonapo vyang'aria, tahadhari vitakula.

**MASWALI:**

j) Ni ujumbe gani wanaopewa vijana kupitia shairi?. (alama 4)

k) Bainisha tamathali **mbili** za usemi katika shairi hili. (alama 2)

l) Eleza bahari ya shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo. (alama 2)

i)idadi ya vipande katika mshororo

ii) mpangilio wa vina katika beti.

m) Eleza mbinu zozote **mbili** za kishairi zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)

n) Andika ubeti wa pili kwa lugha nathari (alama 4)

o) Eleza toni ya shairi hili. (alama 1)

p) Tambua: (alama 2)

i) Nafsi neni

ii) Nafsi nenewa

q) Eleza umuhimu wa mbinu ya kimtindo iliyotumika katika ubeti wa tano. (alama 2)

r) Eleza maana ya msamiati: ‘aula’ (alama 1)

***SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI***

6. a) Eleza maana ya miviga. (alama.2)

b) Eleza sifa tano za miviga.

(alama.5)

c) Miviga ina udhaifu gani. (alama.3)

d) Fafanua umuhimu wa ngomezi katika jamii. (alama.6)

e) Eleza vizingiti **viwili** vinavyokumba ngomezi. (alama.4)

# MARANDA HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

**Swali la Kwanza (lazima)**

1. Umeteuliwa kuwa katibu wa kikao kikao kitakachowaelimisha wananchi kuhusu njia mbalimbali za kupambana na umaskini nchini. Andika hotuba utakayoitoa.

2. Vijana wamekumbwa na changamoto si haba.Thibitisha.

3. Andika insha itakayodhihirisha maana ya methali:
   Samaki mkunje angali mbichi.

4. Andika insha inayoanza kwa:Nilipopata fahamu/nilikuwa

   hospitalini……..

# MARANDA HIGH SCHOOL

## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM

## Julai 2019

## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

A. **Ufahamu** (alama 15)

***<u>Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali</u>***

Ulikuwa usiku wa manane.Maria hatawahi kuyasahau yaliyotokea usiku huo na madhara yaliyoikumba aila yake;ambayo hadi wa leo huwasumbua na kuwafuata lika waendako na hata kuishi. Matokeo ya kitendo kilichotekelezwa na nduguye mnuna yamesalia kama dondandugu moyoni mwake.Yeye hujaribu kuyafutilia mbali lakini yanakataa katakata

Kuondoka fuvuni mwake hasa anapomtazama nduguye mdogo.Tom,akitaabika bila miguu

Maria alikuwa akidurusu somo la fizikia Abdallah,kakake mkubwa akimpa Tom Wosia"Tom, itakuwa bora ikiwa mtanena kwa amani na baba kuhusu tofauti zenu.

Hamna haja ya kumrushia chehche za matusi.Kumbuka kuwa heshima kwa mzazi ni taadhima kwa mterehemezi. Matokeo yake ni Baraka na **sudi** tele"Tom alikinai kuyatilia maanani mawaidha ya kaka yake.Akajitia hamnazo na kudai kuwa baba yake amemdunisha kwa mwia mrefu na angemfunza adabu.Watu wote katika familia walijaribu kumsihi lakini ikawa kazi bure.

"Upyaro haufai ndugu yangu .Hata kama una kimo kikubwa kuliko baba kumbuka kuwa ndiye mzazi aliyuekulea wewe', Alidokeza Maria

Baba yake Maria,Mugambi,alikuwa amechoshwa na vitendo vya mwanawe vya kutumia dawa za kulevya.Aghalabu Tom alikuwa akizua rabsha kila jioni baada ya kutoka shule. Mugambi alikuwa amemwadhibu mwanawe na hata kumshtaki katika kituo cha polisi lakini hakubalika.Watu walisema kuwa alikuwa na fedha nyingi kutokana la ulanguzi wa mihadarati. Jambo hili lilimwezesha kuhepa mitego ya askari kwa **kuzunguka mbuyu**. Tom akawa asiyesikia la mwadhini wala mteka maji msikitini.

"Mzee ninataka unipe urithi wangu, la sivyo, leo utaiona dunia hii paa!"Tom akamtisha baba yake. Mugambi akaja juu na kumwambia mwanawe kuwa umri wake

haukutosha kupewa urithi. Ingembidi akamilishe masomo kwanza,ajijengee msingi bora wa maisha yake ya kesho na hata kupata mali yake mwenyewe." Mimi si mtoto. Ninataka uelewe kuwa leo ilikuwa siku yangu ya mwisho kuhudhuria shule. Hiyo elimu ya wakoloni imenichosha! Katu sisomi tena,"

Akasema Tom. Punde si punde Mugambi alipandwa na za mkizi na kumwandama mwanawe kwa makonde. Ikawa vurugu si vurugu **kuwamamanua** bila mafanikio. Licha ya kuumizwa na kujeruhiwa sehemu kadha za mwili wake,Tom alishikilia kikiki na kuendelea kupambana na baba yake. Mama yake alipoona maji yamezidi unga, aliamua kuingilia kati na liwe liwalo. Kwa bahati mbaya,Tom alimrushia teke la ubavuni na kumwangusha chini pu!

"Aghrr! haya yote unayotufanyia sisi wazazi wako yatakufuata daima''Magambi alilaani huku akigaragara sakafuni kwa maumivu tele"Ninataka uniue leo, siwezi kukulea kwa dhiki na taabu tele halafu unikosee mimi na mamako heshima namna hii utaona kilichomtoa kanga manyoya", Mugambi alimwambia mwanawe akiwa na uchungu mwingi moyoni majirani mimi nikiwemo walikuja kujionea sinema ya bure."Teresia ,unaona namna Tom alivyowakosea wazazi wangu heshima?'' Maria aliniuliza.''Kwa muda mrefu, familia yetu imekosa amani kwa sababu ya Tom kuzua fujo mara kwa mara. Amewajeruhi wazazi wangu mara nyingi huku akivivunjavunja kenyekenye vyombo vya mama.Tandabelua anaozua Tom hunifanya mimi na ndugu zangu kutohudhuria shule wakati mwingine. Huwa tunahofia kuangamizwa kwa wazazi wetu, hivyo kubaki nyumbani kama walinzi wao. Tom amegeuka hayawani. Hajali habali,''alinieleza Maria huku machozi yakimtiririka tiriri; njia mbilimbili.

Nyumba yetu ilikuwa mita chache kutoka nyumbani kwa akina Maria. Nilikuwa wa kwanza kushuhudia Tom akiwatendea wazazi wake unyama pamoja na ndugu yake Abdallah. Alikuwa amewajeruhi vibaya. Abdallah alipojaribu kuwasaidia wavyele wake alirushiwa upanga uliompata barabara kwenye kisigino.Ninakumbuka namna Abdallah alivyochechemea kwa uchungu mwingi huku akiwa ameyauma meno.Ninakumbuka namna Abdallah alivyochechemea kwa uchungu mwingi huku akiwa ameyauma meno. ninakumbuka vyema

Kamsa alivyotawala nyumbani kwa mzee Mugambi.Watu wote walioshuhudia unyama wa Tom walilengwalengwa na machozi huku wakiulaani.Wanakijiji cha Umoja, waliamua

kumpiga kitutu na kumfukuza. Alipotambua wamemzidi nguvu,alikimbia kiswara kuelekea upande wa chini. Kwa bahati mbaya, alianguka shimoni na kuvunjika miguu yote miwili. Aketipo na kudhukuru vitendo alivyokuwa akiifanyia familia yake, Tom hupatwa na mjuto makubwa. Leo ameamini kuwa majuto ni mjukuu.

***Maswali***

(a) Eleza msimamo wa Mugambi kuhusu kumpa mwanawe urithi (alama 2)

(b) Taja sababu kuu iliyomfanya Tom kutekeleza vitendo vya kinyama ( alama 1)

(c) Eleza athari tano za watoto kutowatii wazazi wao kwa mujibu wa (alama 5)

Taarifa hii

(d) Kwa nini Tom aliepuka mkono mrefu wa serikali? (alama 1)

(e) Fafanua wasifu wa Tom kulingana na taarifa hii ( alama 3)

(f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa (alama 3)

i. Sudi
ii. kuzunguka mbuyu
iii. kuwamamanua

**SEHEMU B: UFUPISHO** **(alama 15)**

Dhuluma kwa wanawake sio matokeo ya siasa baada ya uhuru,bali ni matokeo ya hali iliyokuwepo tangu enzi za mababu zetu;kabla ya ukoloni. Kubaguliwa na kudhulumiwa kwa wanawake kisiasa kunaoana na kunyonywa kwake kijamii kunakoshuhudiwa miaka nenda miaka rudi.

Elimu ya jadi alimwandaa mwanamke kuwa chombo kitiifu cha mwanamume. Mwanamke aliandaliwa katika unyago na katika mfumo mzima na malezi kuwa chombo cha kumtumikia mwanamume ,kumstarehesha, kumfariji,kumlisha na kumzalia watoto. Mwanamke tangu jadi hakuruhusiwa kushiriki katika shughuli za kisiasa na utawala wala hakuna mtu aliyeamini kwamba mwanamke angeweza kushikilia wadhifa wowote wa uongozi.

Demokrasia ya jadi naihusudu sana; ambapo wazee walikaa chini ya mbuyu na kuamua mambo ya jumuiya. Mahakama ya kijiji ilikuwa aghalabu ni ya wazee na wanaume peke yao. Hakukuwa na mwanamke na mwanamke aliyeshirikishwa, hata kama alikuwa ajuza. Sifa waliyokuwa nayo wanawake ni ile ya usihiri na uganga.

Mwanamke yeyote aliyezeeka alidhaniwa kuwa bingwa na uchawi ,ulozi na ushirikina. Kwa hivyo,wanawake ndio waliokuwa washirika wakubwa, maana fursa ya kupata elimu pana zaidi hawakuwa nayo. Si ajabu kuwa mwanamke alipojitokeza na kusema jambo la busara, alipuuzwa na pengine kutukanwa hadharani

Kwa bahati nzuri, kumezuka mwamko uliotuingiza katika enzi mpya.Vita vya wanawake kujihami na kujiendeleza katika ulimwengu unaotawaliwa na wanaume vimetapakaa kote katika kila sehemu ya dunia.Wanawake wengi wamekiuka misingi na mizizi ya utamaduni na kung'oa asasi za kijamii na itikadi ambazo daima zimeendelea kupitishwa na umoja na mataifa mwaka hadi mwaka huku masuala ya wanawake ya kijamii,utu na utamaduni yakishangiliwa kupitishwa watetezi wameeleza wasiwasi wao ikiwa kupitishwa kwa maazimio kutasaidia kuleta maendeleo ya haraka kwa wanawake kimataifa au katika nch moja.Fauka ya hayo, baadhi ya wachunguzi wanaonelea kuwa maazimio mengi hayadokezi hatua za kufikiwa haki za wanawake.

Maazimio mengine yanazungumzia juu ya kuondolewa kwa ubaguzi dhidi ya wanawake kushiriki kwao katika uendelezaji wa amani ya kimataifa na ushirikiano wa kimataifa,majukumu yao katika jamii,mfuko wa umoja wa mataifa wa wanawake (unifem) na kuimarisha hadhi ya wanawake katika sekretariati ya umoja wa mataifa miongoni mwa shughuli nyingine katika mkabala huu.

Wanawake wameonyesha vipaji vyao katika nyanja mbalimbali za maisha; siasa,uchumi, utawala na kadhalika.Wanawake wamejikakamua na kudhihirisha kuwa wao pia wana jukumu muhimu la kutekeleza ili kuyaongoza maisha yao na ya watu wengine.

Wadumishaji wa dhuluma za kijinsia hawana budi kusalimu amri na kukubali ukweli huu wapende wasipende. Mtazamo juu ya haki sawa unatokana na kukubaliwa na kuondolewa kwa aina zote za ubaya dhidi ya wanawake. Kwa bahati mbaya,itikadi na mila za kiasili bado hazitupi nafasi ya kuwashangilia wanawake. Kwa bahati mbaya,itikadi na mila za kiasili bado hazitupi nafasi ya kuwashangilia wanawake wanaojitolea mhanga kutetea hadhi yao pamoja

na ya wanyonge wengine. Wao huonekana kama waasi wapinga mila na matovu wa utii.

**Maswali**

(a) Bila kubadilisha maana asilia ,fupisha aya tatu za kwanza.(Maneno 50-50) (alama 5,1 utiririko)

(b) Kwa kurejelea aya tatu za mwisho ,pambanua hoja muhimu zinazogusiwa na mwandishi

(maneno 70-80) (alama 8,1 utiririko)

**MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

(a) **Andika sauti zenye sifa zifuatazo:** (alama 2)

i. Kikwamizo sighuna cha kaakaa gumu……

ii. Kipasuo kwamizo cha kaakaa gumu……

iii. Irabu ya nyuma ,wastani………………

iv. Nazali ya kaakaa laini............

(b) **Weka shadda katika neno lifuatalo ili itoe maana mbili tofauti** (alama 2)

walakini-

(c) Tunga sentensi **moja** ukitumia nomino katika ngeli ya U-YA pamoja na kivumishi kiashiria kisisitizi cha karibu (alama 2)

(d) Onyesha mofimu katika neno: aliyemcha (alama 3)

(e) **Kanusha sentensi ifuatayo** (alama 1)

Ukimpiga utashtakiwa na kuchukuliwa hatua kali

(f) **Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo.** (alama 1)

Mwanafunzi huyo alipita kwa vile alisoma kwa bidii

Anza kwa nomino ya kitenzi jina

(g) **Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mishale** (alama 3)

Mama na nyanya walinunuliwa jozi za viatu na baba

**(h) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi**

Nikimuuliza ua hili ataweza kuifanya harusi yake iwe ya kupendeza (alama 2)

(i) **Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa:** (alama 3)

"Mito yetu imechafuka mno;itabiditushirikiane wakubwa kwa wadogo ,wamaume kwa wanawakeili tuisafishe''.Waziri wa Mazingira alituhimiza

(j) **Eleza matumizi ya 'ku' katika sentensi ifuatayo** (alama 2)

Hukumwelewa alivyoeleza namna ya kuwalisha mifugo

(k) **Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa** (alama 2)

Mtoto aliwaua nyoka kwa kuwapiga vichwa

(l) **Bainisha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo** (alama 3)

Baba yake alivamiwa na wezi waliomvunjia mlango kwa chuma

(m) Kwa kutunga sentensi eleza matumizi mawili ya mkato (alama 2)

(n) Eleza maana mbili za sentensi hii: (alama 2)

Mamake Juma na Maria walitutembelea

(o) Tunga sentensi sahihi ukitumia kitenzi 'la' katika kauli ya kutendwa (alama 2)

(p) Andika kinyume cha sentensi (alama 1)

Watoto wameombwa waanike nguo

(q) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari (alama 2)

Ubaguzi wa kijinsia umekashifiwa na

Viongozi wenye msimamo thabiti

(r) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo (alama 2)

Angalilima kwa bidii angalivuna mavuno tele

(s) Tunga sentensi zenye vivumishi vya pekee vya kuonyesha dhana zifuatazo (alama 2)

(i) umiliki

(ii) kutobagua

(t) Bumba ni kwa nyuki______________________ni kwa samaki ______ (alama1)

ni kwa siafu

**ISIMUJAMII** **(ALAMA 10)**

(a) Eleza sifa **tano** za lugha rasmi (alama 5)

(b) Eleza mambo **matano** yaliyochangia katika maenezi ya Kiswahili katika (alama 5)

Afrika Mashariki kabla ya uhuru

# MARANDA HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

**Swali la lazima**

1. **SEHEMU YA A: Ushairi** (ALAMA 20)

***Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali***

Wanafunzi sikieni ,niwape wangu wasia
Mkiwa mtihanini, muweze kuzingatia
Nataka mtambueni, Msije mkajutia
Kwa bidii darasani,mtihani mfaulu

Kufanikiwa kitaka ,watii nao walimu
Sielekeze **dhihaka**, kwao wao ni muhimu
Kwauliza mwahitajika.maswali yalo magumu
Kwa bidii durusuni,mtihani mfaulu
M rauke na mapema,msome kwa tumaini

Msije nyie kukwama. kwenye wenu mtihani
Muweze rudia vyema, mlofunzwa awalini
Kwa bidii durusuni,mtihani mfaulu

Umoja ni nguvuni, Mwafaa mfahamuni
Jiunge na makundini, masoma mujadilini
Na lile lilo gizani, takuja kulionani
Kwa bidii durusuni,mtihani mfaulu

Ilopita mitihani,kwa chudi irudieni
Mpate na taswirani, ya ule ulo mwishoni
Ya ziada kazini, ifanye sizembeeni
Kwa bidii durusuni,mtihani mfaulu

Mwelewe sana vyema,yaliyo mtaalani
Msije mkandama, Cha mtihani chumabni
Mgongeni ndipo vyema,sije mkapoteani
Kwa bidii durusuni,mtihani mfaulu

Mkiwa madarasani, kelele muepukeni
Sije mkapotezani, muda wenu masomoni
Neneni na vitabuni,vitakuja walipani
Kwa bidii durusuni.mtihani mfaulu

Michezo sipuuzeni,kwayo nyie burudika
Nishati ntapatani,kifurahia michezo
Mazoezi eleweni,ni muhimu kwa ubongo
Kwa bidii durusuni,mtihani mfaulu

Nimefika kaditama,kuweleza ya moyoni
Yafwateni hayo mema,mfaulu mtihani
Ni upuzi msiseme,muda wangu potezeni
Kwa bidii durusuni,mtihani mfaulu

**Maswali**

(a) Eleza mawaidha yanayotolewa kwa wanafunzi kuhusu namna ya kujitayarisha vyema kwa mtihani (alama 5)
(b) Eleza umbo la shairi hili ( alama 4)
(c) Eleza mbinu **tatu** zilizotumiwa katika shairi hili ili kukidhi mahitaji ya kiarudhi (alama 3)
(d) Taja na utoe mfano wa tamathali **moja** ya usemi iliyotumiwa katika shairi hili (alama 1)
(e) Eleza toni ya shairi hili (alama 1)

(f) Andika ubeti wa **pili** kwa lugha ya mjazo ( alama 4)
(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika shairi
i) dhihaka……………………………………
ii) kaditama……………………………

**SEHEMU YA B: RIWAYA**
**(Jibu swali la 2 au 3)**
***CHOZI LA HERI*** (Assumpta K matei)

2. ”…..Unatumia mantiki gani kusema kuwa sisi si watoto wa miaka hamsini?’
(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 1)
(b) Taja mbinu ya lugha inayojitokeza katika dondoo hili (alama 1)
(c) Kwa kutumia hoja nane,thibitisha wazungumziwa walikuwa watoto wa miaka hamsini (alama 8)
(d) Eleza wasifu wa msemaji wa maneno haya (alama 4)

(e) Eleza umuhimu wa msemewa wa maneno haya (alama 3)

3. Kwa kutumia hoja kumikumi eleza jinsi maudhui ya utu na uozo na kijamii Yalivyoshughulikiwa katika Chozi la Heri (alama 20)

## SEHEMU YA C:TAMTHILIA
## KIGOGO (Pauline Kea)
***(Jibu swali la 4 au 5)***

4. '' Nimekuja kuwakomboa"

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili ( alama

(b) Kwa kutumia hoja kumi na mbili,thibitisha kuwa msemewa na wenzake walistahili Kukombolewa ( alama 12)

(c) Kwa kutumia hoja **nne** eleza umuhimu wa msemewa ( alama 4)

5. Tamthilia ya kigogo ni kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika.Thibitisha (alama 20)

## SEHEMU YA D: HADITHI FUPI
## TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE
*( Jibu swali la 6 au 7)*

6. "Licha ya…..ninayopewa na wazazi wangu naona bado kuna pengo kubwa maishani mwangu

(a) Weka dondoo katika muktadha wake (alama 4)

(b) Fafanua pengo linalorejelewa na msemaji ( alama 2)

(c) Thibitisha kuwa hatua za kujaza 'pengo' ulilolifafanua hapo juu ulikumbwa na vizingiti vya kitabaka ( alama 8)

(d) Onyesha hulka **sita** za msemaji wa dondoo hili

7. Onyesha jinsi wahusika wafuatao wanavyochangia katika kufanikisha maudhui kwenye hadithi ***Masharti ya kisasa:***

(a) Kidawa

(b) Dadi

## SEHEMU YA E:
## FASIHI SIMULIZI

8. "Mwanangu dunia haitaki papara. Ikiwa unataka kufanikiwa katika mustakabali wako kuwa mtoto mtiifu na mwongofu. Kumbuka kuwa asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu….''

(a) Tambua kipera hiki cha fasihi simulizi (alama 1)

(b) Eleza sifa **tano** za kipera hiki cha fasihi simulizi (alama 5)

(c) Fafanua dhima **nne** za kipera hiki katika jamii (alama 4)

(d) Fanani anawezaje kuihusisha hadhira katika usimulizi wake? (alama 4)

(e) Eleza majukumu **sita** ya nyimbo katika uwasilishaji wa ngano (alama 6)

# SUNSHINE SCHOOL

## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM

## Julai 2019

## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

1. **LAZIMA**
   Andika insha ya wasifu wa kiongozi umpendaye

2. Mitandao ya kijamii ina faida nyingi kuliko hasara. Jadili

3. Andika kisa kitakachodhinirisha maana ya
   Methali: Ukiona vyaelea jua vimeundwa

4. Andika insha itakayoishia kwa maneno yafuatayo…….nilipomtazama namna alivyojikunyata, ndipo nilipotanabahi kuwa mtoto wa kiume ametelekezwa.

# SUNSHINE SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

**UFAHAMU** (Alama 15)

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali***

Basi huu ni mwanzo tu.*Mwanzo wa ngoma ni lele*. Huu ni mwanzo wa safari ndefu.Itatuchukua miaka na mikaka.Lakini msiwe na papara,Sharti mwanzo tutanabahi twaelekea wapi ndipo tuamue tutasafirije.Tahadhari na hatari ya hasira visasi na papara pamoja na maradhi yanayozidi yote,yaani maradhi ya matumaini yanayozidi uhalisi.Matumaini yaliyopindukia ndiyo huwalewesha watu wakadhani watapata afueni wakizifuata pepo za siasa za chama kimoja au siasa za vyama vingi.mfumo wa soko huria au mfumo wa ukiritimba,mfumo wa utandawazi au mfumo wa kibepari, utawala wa kidikteta au utawala wa kidemokrasia na udini, ujamaa na ukomunisti na kadhalika.Hatari kabisa hii ya

kujenga nyumba kwa karata.Nasema tena, tahadhari na ulevi wa ushindi.Mimi nashauri hivi;hatua ya kwanza ni elimu si elimu ya shahada na stashahada zipatikanazo vyuoni. Elimu ya kujielewa sisi nani twatoka wapi, twaelekea wapi na utu tutaurejeshaje pahali pake mahsusi toka kule mwituni kwa wanyama

Ulikotokomelea''.Amani awe mtemi!'' umati ukadai Hapana.Hata kidogo.Badala yake acha amani iwe na mtemi mpya msinivishe joho ambalo si makamo yangu kulivaa'',aliwaambia.''Kaeni mfikirie vema juu ya mustakabali wenu.Nilichodhamiria mimi ni kushirikiana na ndugu yangu madhubuti kumnyonyoa kipungu mmoja,ila sikutaka niingie pahala pake niruke juu nikijihadaa kwamba nitafika mbinguni.

Ila msikubali dhuluma.Dhuluma msikubali, Ikija dhuluma tena, msimlaumu mtu mwingine, Jilaumuni wenyewe. Nakumbusha tu ya kwamba kuwepo mamlakini kwa mtemi Nasaba bora muda wote huo si kosa lake tu.Alisema Amani.Ni kosa letu sote.Tulimruhusu sisi wenyewe kwa kimya chetu,kwa kukubali dhuluma zake na udhalili wetu.hatuwezi kumlaumu peke yake.Kwa kila mtawala katili kuna umma uliomruhusu ama kampa uwezo wa kutekeleza ukatili wake.

Punde si punde mkutano ukesha watu wakafumukana wakiwa wamestaajabu

Amani alisadiki kwamba toba ya mwalimu majisifu ilitosha.Amani alijambia mwenyewe kwamba mkono uliondika kidagaa kimemwozea ungeanidia riwaya tena na tena tamthilia na nudhuma na hadithi fupi mpaka maktaba zijae zitapike.Mwenyewe Mwalimu Majisifu alilewa chopi zaidi kuliko mwanzo,hadi siku yake ya mauko ila katika kulewa na kuleuka,akawa hawaoni tena watoto wake walemavu kama masimbi na mashata au laana kwa kosa lolote la mkewe au lake mwenyewe ama la watoto wenyewe.

''Hakuna jambo muhimu sasa kama wanangu wapendwa'',alipita akiimbaimba

akishauchapa na kuwaza vivyo hivyo alipoleuka

"Hatuwezi kuwa binadamu endapo hatuoni walemavu kama wenzetu.tuktakuwa tumelemaa ulemavu mbaya zaidi kuliko ulemavu". Kauli hii ilikuwa tokeo la funzo alilojifunza mwalimu majisifu kutokana na amali na kalima za imani kuwaelekea watoto wake walemavu.

***(Imenulikuliwa kutoka kwa riwaya ya kidagaa kimemwozea- Ken Walibora)***

(a) Kulingana na taarifa ni nini kinachochea dhuluma katika jamii ( alama 2)

(b) Eleza mabadiliko yaliyotokea katika maisha ya mwalimu majisifu ( alama 2)

(c) Taja changamoto ambayo walemavu hupitia katika jamii ( alama 2)

(d) Ni nini maana ya mwanzo wa ngoma ni lele' Ukirejelea kufungu hiki ( alama 2)

(e) Fafanua mwelekeo uliostahili kuchukuliwa ili kutimiza ndoto zao kama ilivyo katika taarifa ( alama 4)

(f) Eleza maana ya ( alama 3)
(i) waombolezaji wa kuhesabu

(ii) ukiritimba

(iii) kumnyonyoa kipungu

**UFUPISHO (ALAMA 15)**

***Soma taalifa kisha ujibu maswali yanayofuata***

Tangu mwaka huu uanze,kumekuwa na ongezeko la visa vya watu kupatikana wakiwa na pesa zinazoshukiwa kuwa bandia. Mwezi jana,polisi katika eneo la Ruiru kaunti ya Kiambu walinasa kwenye nyumba moja pesa bandia za thamani ya 32 bilioni. Pesa hizo zilikuwa mchanganyiko wa dola, Pauni na za Kenya na zilikuwa.pesa hizo zilikuwa zimeingizwa katika masanduku 20 ya mabati.Tayari washukiwa walifikishwa mahakanani kuhusiana na tukio hilo.

Siku chache baadaye polisi wamepata pesa nyingine bandia zikiwa zimehifadhiwa kwenye kasha salama ndani ya benki ya Barclays.

Polisi wanasema mteja wa benki hiyo tawi la Queens way jijini Nairobi, aliingiza pesa hizo pia zikiwa za kigeni,zenye thanani ya Sh. 2 bilioni. Awali polisi wa kitengo cha Flying Squad na wenzao wa kupeleleza uhalifu (DCI) walikuwa wamekisia kiwango cha pesa kuwa Sh. 17 bilioni vyovyote iwavyo, pesa hizi ni nyingi mno kuwa zinaweza kuwa mikononi mwa watu.kusambaa kwa pesa bandia,kunaashiria kuwa humu nchini,kuna watu ambao wana viwanda vya kutengeza fedha hizo na kuna uwezekano mkubwa kwamba baadhi ya wananchi wanazitumia bila ya kuwa na habari.

Kusambaa kwa pesa nyingi kunatukumbusha mwaka 1992 wakati aliyekuwa kiongozi wa vijana wa chama cha kanu, alipokuwa akisambaza pesa kana kwamba
alikuwa na kiwanda chake. Ni wakati huo ambapo noti ya Sh. 500 ilitolewa kwa mara ya kwanza.

Lakini matokeo yake ni kuwa uchumi wa nchi ulisambaratika wakati huo. Baada ya uchaguzi mkuu wa 1992 ambao Rais Daniel Arap Moi alishinda tena, nchi ilijikuta ikipitia kipindi kigumu cha kiuchumi.

Kusambaa kwa pesa bandia wakati huu ambapo Kenya inakubwa na madeni makubwa, ni hatari kwa uchumi wetu. Pesa zinaposambaa kwa wingi katika nchi, zinapoteza thamani yake na kufanya kila bidhaa na huduma kuwa ghali tukiendelea kuruhusu wahuni wachache wachapishe pesa za ziada na kizitumia kwenye soko letu tutakuwa tumeidhinisha kuporomoka kwa uchumi ambao tayari uko katika hali isiyoridhisha

Polisi wanaochunguza wana wajibu wa kutambua chanzo cha pesa hizo na kukikomesha kabisa.Nchi yetu inahitaji kuimarisha uchumi wake ili wananchi wanufaike kwa jasho lao na wala si kuruhusu watu wachache watuangamize kwa kutafuta utajiri kwa njia za mkato.

(imenukuliwa kutoka kwa Taifa leo tarehe 20/3/2019).

(a) Fupisha ujumbe wa aya **tatu** za mwanzo kwa maneno 70- 80 (alama 8,1 mtiririko)

Matayarisho

c) Kwa kutumia maneno 60-70,bainisha mambo muhimu yanayotokea katika aya **tatu** za mwisho matayarisho

**3. MATUMIZI YA LUGHA**
**(Alama 40)**

(a) Tunga sentensi iliyo na muundo ufuatao (alama3)

$I + N+V+T_S +T+E$

(b)(i) Eleza maana ya silabi (alama 1)

(iii) Andika neno lenye muundo ufuatao wa silabi-konsonanti + irabu + konsonanti + irabu (alama 1)

(c) Eleza sifa mbili mbili za sauti zifuatazo ( alama 2)

(i) /o/

(ii) /f/

(d) Andika visawe vya maneno yaliyopigiwa mstari ( alama 1)

(e) Tunga sentensi tatu kuonyesha matumizi ya neno 'kimya' kama: ( alama 3)
(i) Kielezi
(ii) Nomino
(iii) Kitenzi

(f) Huku ukitolea mifano onyesha matumizi matatu ya alama hisi katika lugha **(!)**
( alama 3)

(g) Eleza matumizi mawili ya kiambishi 'ji' ( alama 2)
(ii) Tunga sentensi moja kuonyesha moja ya matumizi hayo ( alama 1)

(h) Changanua sentensi ifuatayo kwa jedwali ( alama 4)
Mwanasiasa anahutubia wananchi huku wakimshangilia

(i) Andika wingi wa sentensi ifuatayo ( alama 2)
Yeye ndiye mkulima bora atakayetuzwa na katibu mkuu wa kilimo

(j) Tumia kiwakilishi kisisitizi cha mbali sana na nomino katika ngeli ya U-ZI kutunga sentensi ( alama 2)

(l) Bainisha mofimu katika neno "lililopikwa' ( alama 3)

(l) Andika katika msemo wa taarifa (alama 2)
"Sara!Sara!" Mama aliita kwa hasira

(m) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo: Japo wageni walikuwa wengi waliweza kuwatumbuiza ( alama 2)

(n) Andika udogo wa sentensi ( alama 2)
Paka alirukia mfupa uliorushiwa kwa dirisha

(o) Yakinisha sentensi ifuatayo (alama 2)
Usipofanya kazi hiyo kwa bisii hutafanikiwa

(p) Eleza matumizi ya 'ka' sentensi ifuatayo ( alama 1)
(i)Tuliamka, tukaoga, tukasali,kisha tukaanza safari

q) Bainisha kiarifu katika sentensi ( alama 2)
Mwalimu wao aliwafunza vizuri

4. **ISIMUJAMII** (Alama 10)

(a) Eleza namna kaida zifuazo zinavyoathiri matumizi ya lugha katika jamii (alama 4 )
(i) uhusiano
(ii) malezi

(b) Eleza majukumu **mawili** ya lugha ya Kiswahili kama lugha ya taifa katika nchi ya Kenya

( alama2)

(c)Taja sifa **nne** zinazotambulisha sajili ya hospitali

# SUNSHINE SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

**SEHEMU A : FASIHI SIMULIZI**

1. lazima

(a) Miviga ni nini? ( alama2)

(b) Eleza sifa **tano** za Miviga ( alama 5)

(c) Fafanua hasara **tatu** za miviga (alama 3)

(d) Eleza changamoto **tano** ambazo mtafiti hukabiliana nazo anpokusanya data ya miviga

(alama 10)

**SEHEMU B:**

***TAMTHLIA – Kigogo (Pauline Kea)***

2. Onyesha namna mwandishi alivyofanikiwa kukuza maudhui yafuatayo
 (i) Elimu (alama 10)
 (ii) Ujana (alama 10)

2. Mvunja nchi ni mwananchi 'Eleza ukweli wa kauli hii kwa kurejelea matukio katika
tamthlia ya kigogo (alama 20)

**SEHEMU YA C: USHAIRI**

B. Moyo wanambia imba,dikteta simwimbie
Moyo wanambia lumba,muhitaji mlumbie
Moyo wanambia chimba,maovu uyachimbue
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia kuwa,ila kasuku usiwe
Moyo wanambia iwa,kunguni ila usiwe
Moyo wanambia pewa,cha mnyonge usipewe
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia nenda,penye dhuluma senende
Moyo aanambia penda,mnyonyaji simpende

Moyo wanambia ponda,ateswaye simponde
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia tenda,lenye jamala litende
Moyo wanambia unda,lenye faida liunde
Moyo wanambia tunda,lisilo sumu litunde
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia ota,kuwa mwizi usiote
Moyo wanambia kata,marija yote ikate
Moyo wanambia teta,penye dhuluma patete
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia nyosha,penye na kombo panyoshe
Moyo wanambia usha,mateso yote yaushe
Moyo wanambia isha,yenye majonzi yaishe
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

Moyo wanambia waza,yalopita yawazie
Moyo wanambia kaza,mwovu njia mkazie
Moyo wanambia vuaza,lenye heri tuvyazie
Moyo wanambia woga,ndio mwazo wa maafa

***(Shairi la mbegu la E. Kezilahabi, 1988)***

(a) Fafanua dhamira ya mtunzi wa shairi hili ( alama 2)

(b) Ainisha bahari za ushauri huu kwa kutegemea
(i) Mpangilio wa maneno
(ii) Vipande vya mishororo
(iii) Idadi ya mishororo kwa kila ubeti ( alama3)

(c) Tambua aina **moja** ya urudiaji na utolee mfano ( alama 2)

(d) changua muundo wa shairi hili ( alama 4)

(e) Andika ubeti wa **tano** kwa lugha ya nathari
( alama 4)

(f) Onyesha aina **moja** ya uhuru wa kishairi aliotumia mwandishi katika shairi lake

(alama 2)

(g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumika katika ushairi
(alama 2)
(i) Dikteka
(ii) Kasuku

(iii) Mnyonyaji

**USHAIRI**

Ni mimi nizamishaye chini
Mizizi kwenye majabali
Kufyonza chumvi!

Ni mimi ninyunyizae maji
Ili mimea ifumbue
Nafasi zao hewani
Ili miti ishike mimba kuzaa
Matunda,nafaka,mizizi na viazi
Ela mimi sili hata punje moja
Nabaki mtupu!

Ni mimi tumbo kubwa,
Niliyeshiba madini
Ni mimi ninayechimba
Kupakua raslimali

Dhahabu,chuma,makaa…
ela yote yanaona
Yatiririka kwao!
Nabaki mtupu!

Vyakula vyote nazalisha mimi
Na mi' nabaki na njaa!

Nguo zote nawapa mimi
Na mi'nabaki u tupu!

Madini yote nawapa mimi
Na mi'nabaki kununua vyao!

Kazi zote nafanya mimi
Wao wabaki kunila nguvu!

Wao wanajita bora
Na mi' nabaki fukara!

***( Shairi la S.A Mohamed Jicho la ndani, Longhorn Publishers 2002)***

(a) Lipatie shairi hili anwani mwafaka ( alama 2)

(b) Fafanua aina moja ya taswira katika shairi hili ( alama 2)

(c) Eleza ujumbe mkuu wa mtunzi wa shairi hili
(alama 2)

(d) Huu ni ushairi wa aina gani.Toa sababu ya jibu lako
(alama 2)

(e) Eleza toni ya ushairi (alama 2)

(f) Mtunzi ametumia mbinu zipi kukuza ujumbe wake
( alama 4)

(g) Huku ukitolea mifano onyesha matumizi ya mistari mishata katika shairi hili
( alama 2)

(h) Onyesha umuhimu wa kinaya katika shairi hili (alama 2)

(i) Tambua nafsineni katika shairi hili
(alama 2)

**SEHEMU D:**

***Hadithi fupi (Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine)***

6 Onyesha namna nafasi ya mwanamke inavyosawiriwa kwa kuzingatia hadithi zifuatazo

(a) Ndoto ya Mashaka
(b) Masharti ya Kisasa
(c) Mapenzi ya Kifaurongo
(d) Shogake Dada ana Ndevu

7 . ….Ati umebakwa!Nani akubake wewe? Wapi utakapobakwa mji pasiwe na mtu wa kukuombea?

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
(b) Eleza sifa mbili na umuhimu wa msemaji wa maneno haya (alama 4)
(c) Jadili maudhui makuu katika dondoo hili (alama 12 (6 x 2)

**SEHEMU YA E:**

***Chozi la Heri*** (alama 20)

8. Jadili ufaafu wa anwani ***Chozi la Heri.***

# BAHATI GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

**INSHA**

**SWALI LA LAZIMA**

1. Wewe ni mtafiti wa maswala ya usalama nchini. Mwandikie barua Waziri wa Usalama wa Ndani barua ukimweleza sababu za wanafunzi wa shule za upili kujiunga na makundi ya wanamgambo, almaarufu Al Shabaab.

**CHAGUA MOJA:**

2. Utandawazi una athari mbaya katika maisha ya vijana. Jadili.

3. Andika insha inayodhihirisha maana ya 'Umdhaniye ndiye siye'

4. Kamilisha insha yako kwa maneno:

...Sitaisahau siku hiyo kwani sijawahi kufedheheka kama nilivyoaibika siku hiyo.

# BAHATI GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

**1. UFAHAMU** **ALAMA 15**

**Shule yangu ya upili**

Majio yangu katika shule hii ya upili hayakutokea kwa bahati nasibu bali kwa mipango kabambe niliyoianza tangu nikiwa shule ya vichekechea. Nikiwa siteteteki hata kwa wazazi wangu waliponisihi nijiunge na shule nyingine za karibu nikawa sisikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini. Nikawa na ragba ya mkanja nikingoja siku ya kujiunga na shule yenyewe. Kweli majuto ni mjukuu na huja kinyume.

Nilizaliwa katika aila yenye nafasi iliyotopea na kubobea katika ukwasi uliodhihirika kutokana na mitaa tulikoselelea kwa muda kabla ya baba kuaamua kununua nyumba yake mwenyewe huko upande wa Karen hivyo tukagura kutoka Runda. Wakati wa likizo tukawa tunaruka hadi pwani ambako mama yangu alikuwa amemiliki jumba lililokuwa katika ufuo wa bahari lililojengwa katika kipande kisichopungua ekari tatu alilotunukiwa wakati wa nikahi yao na wakwe wa baba yangu.

Wavyele wangu wakawa wanaendesha magari meusi ya kifahari ingawa sikuwahi kumwona mama akichangamka kuendesha magari yake ya maana, kila macheo ya siku za kazi gari lililoendeshwa na dereva ambaye alimstahi mama hadi akawa anamfungulia mlango wa gari na kuufunga baada ya mama kujitoma katika tumbo la gari lilimjia na kumrejesha kwa wakati. Nikajiunga na shule ya msingi ya kibinafsi ambako nilishughulikiwa kama kikembe. Wengi wa wale tuliosoma nao walikuwa wa tabaka langu na walikuwa wametoka katika kila sehemu nchini Kenya.

Hayawi hayawi huwa na siku ya kuripoti ikafika. Alfajiri, dereva mmoja akatumwa kwenda hadi Kisumu ili atulaki na kutusafirisha kutoka uwanja wa ndege hadi shule ya upili ambayo ilikuwa yangu ya rohoni. Nasi tukaelekea hadi uwanja wa ndege ili turuke hadi Kisumu. Safari yetu kutoka kitongoji cha kifahari hadi Airport ilikuwa njema, safari yetu tulipoabiri ndege ilikuwa bila bughudha, safari yetu kutoka Kisumu mjini haikuwa na kasoro na tulienda kulingana na mpango. Safari yetu ilikuwa mufti hadi tulipofika katika lango la shule ya kitaifa! Tulipotia ozi tu!!....jamani......jamani nikafa moyo. Labda mama aliweza kubaini mabadiliko ya hisia zangu, nilitamauka, nikawa mchege na kusema kweli niliyoyaona sikuamini. Mvua iliyokuwa imepasua hapo awali ilikuwa imeacha vitua vya maji kwenye vijia vya kutembea vilivyochakaa na kubomoka bila yeyote kujali kuvikarabati. Majengo yalikuwa makongwe yaliyojengwa miaka mia moja iliyopita na yalistahili kuitwa makafadhi badala ya pahali pa kumkaribishia mwanafunzi aliyepita kwa alama mia nne na thelathini na tano. Asiye na wake ana Mungu, nikapiga moyo konde lazima nisajiliwe katika shule ya ndoto langu. Ningewezaje kughairi wazo langu baada ya siku hizo zote za maandalizi tena mbele ya wanuna walioniona kama kielelezo chao tangu walipozaliwa. Nikasajiliwa!

Sikujua, hakika sikujua, sikujua shule ya upili ya kitaifa yaweza kuwa hivi. Kweli mwanafunzi aweza kukosa viatu na hata kushindwa kununua rangi ya kupaka viatu

hivyo iwapo amenunuliwa na wahisani? Nilimlaumu nina maana hakunieleza kuwa mtu anaweza

kula chakula ambacho mbwa wetu hawezi hata kukiangalia. Nilipoingia katika ukumbi wa chakula nilihisi kitefutefu nusura nichafukwe na moyo, makapi ya mboga na uchafu usioelezeka ulinikumba, kisha nikapewa kisahani cha plastiki na kupakuliwa kipande cha ugali ambacho bado kilikuwa na unga na kuachiwa hiari ya kukila au kukitupa. Wenzangu wakawa wanakirambatia chakula kwa kasi huku mmoja wao alipoona jinsi nilivyokiangalia changu akanihisi nimpe chote na kukimaliza fyu. Wote walikuwa na furaha kemkem na kuajabia utukufu wa shule iliyotukuka ya kitaifa ila mimi.

Baada ya mlo 'rojo rojo', tukaelekea darasani nilikopigwa na mghuma mkubwa. Tulikuwa wanafunzi hamsini na watano katika darasa moja tu! Mwalimu mmoja akaja na kutukaribisha shuleni kisha akatuarifu kuwa atakuwa mwalimu wa darasa letu. Nilipomsikia akinena nusura niishiwe na stahamala, kimombo chake kilinishangaza, hasa matamshi yake yalipungukiwa
na kudhirisha athari za lugha ya asili. Nilihisi kana kwamba ningemrekebisha lakini sikudhubutu.

Tukafululiza hadi bweni na nikajilaza kitandani chembamba huku mwingine nisiyemjua lakini asiyejua kuwa kuna nguo maalum za kulala akalala uchi katika ghorofa ya juu ya kitanda chetu. Mgeni njoo mwenyeji apone maana baada ya muda wadudu ambao sikuwahi kuwaona aushini mwangu wakanza kunishambulia. Nikaamka baada ya kumnasa mmoja wa wadudu hawa na kuuliza mmoja wa wenzangu ni wepi wadudu hawa na kwa kutojali hata kidogo, akanieleza kuwa hawana neno bali ni kunguni tu, sikujua na kwa kweli mama hakuniambia kuwa kuna wadudu wanaotafuna mtu na hunuka fye! Sikulala kwa hofu huku wenzangu wakiforota kwa njia ya kunighasi. Sikuwahi kudhani kuwa watu wengi wanaweza kulala chumba kimoja huku changu kikiwa na hamamu na vifaa vyote muhimu kikibaki bila mtu!
Tulisomeshwa na walimu wasiojali kana kwamba tunaelewa au la. Hawakushughulika iwapo tulifanya kazi za ziada au la, ndio, hakujali chochote. Kilichonishangaza ni kuwa wanafunzi waliojiunga nasi kutoka shule za umma wenye alama duni waliwapenda na kuelewa haraka walichosomeshwa na hawakujali matamshi yao, labda hawakuyatambua.

Hatimaye tukafanya mtihani wa mwisho wa muhula wa kwanza. Nilishangaa ghaya iliponibainikia kuwa aliyetuongoza alikuwa ghulamu mmoja mshamba niliyempuuza tu mvulana kutoka kijijini ambacho singetambua katika ramani ya nchi ambaye hata vitu vya kimsingi vilimpiga chenga. Nikafanya uchunguzi nikatambua mwenzangu alikuwa na alama mia mbili hamsini na tatu akitoka katika darasa la nane, nilifanikiwa kuwa nambari mia mbili hamsini na tatu kwa jumla ya wanafunzi mia tatu! Tulipofunga kwa likizo ya Pasaka nikaamua kuchukua hatua nyingine sitawahi kuhama kutoka shule hii ya upili wala kuwa zaidi ya nambari kumi!

**Maswali**

a) Thibitisha kauli kuwa msimulizi ana msimamo thabiti
(alama 2)

b) Tofautisha jinsi mwandishi alivyofunzwa katika shule ya kibinafsi na shule ya upili.
(alama 3)

c) Taja mambo matatu yanayotuonyesha kuwa msimulizi alilelewa katika aila ya kikabaila kulingana na aya ya pili. (alama 3)

d) Andika masuala matatu yaliyomshangaza katika shule ya upili (alama 3)

e) Andika tamathali mbili zilizotumika katika kifungu. (alama 2)

f) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika kifungu. (alama 3)

i) alimstahi
ii) kughairi
iii) kunighasi

**2. UFUPISHO** **ALAMA 15**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Mwana wa Adamu ni kiumbe cha ajabu! Ni kiumbe kilichopewa uwezo wa kuhodhi na kumiliki kila kitu, kiumbe kilichopewa akili na maarifa fuvu tele ili kutaratibu shughuli na mambo: kiumbe kilichopewa uwezo wa kuwasiliana na kutumia sauti nasibu ili kuwa na urari na muwala; kiumbe kilichopewa uwezo wa kufaidi viumbe wengine kwa njia mbalimbali na jumla jamala; hiki ndicho kiumbe kilichopewa idhini maalum ya kuzaana na kujaza dunia. Huyu ndiye mwana wa mama Hawa ambaye sasa amegeuka ndovu kumla mwanawe.

Kwa sababu ya bongo alizonazo, binadamu ana uwezo wa kutumia teknolojia kwa manufaa yake na ithibati zipo tele. Binadamu ametumia nyambizi kuzuru chini ya bahari, amefika mwezini, amevumbua magala: amevumbua uyoka: amevumbua tarakilishi na sasa shughuli zake ni za kutandaridhi. Mwenyewe yuasema kuwa dunia yake imekuwa kitongoji katika muumano huu.

Chambilecho wavyele, akili nyingi huondoa maarifa. Binadamu amekuwa dubwana linalojenga kushoto na kubomoa kulia na tuna sababu ya kulisoza dubwana hili kidole. Rabana ndiye msanii asiye mfanowe kwani aliisawiri murua. Rabuka akaona yote yalikuwa mema na mazuri: akamwambia binadamu," Haya twende kazi!"

Viwanda vya binadamu vinatiririsha maji-taka ovyo hadi mitoni, maziwani na baharini na matokeo yamekuwa ni vifo vya viumbe vya majini kama samaki ambavyo ni urithi aliopewa na muumba. Hakuna kiumbe kinachoweza kustahimili maisha bila maji safi. Maji yote sasa yametiwa sumu na binadamu kwa sababu ya 'maendeleo' yake. Joshi kutoa katika viwanda vivyo hivyo nalo limehasiri ukanda wa ozone ambao sasa umeruhusu jua kutuhasiri kwa joto kali mno. Siku hizi inasemekana kuwa kuna mvua ya aside inayonyesha katika baadhi ya sehemu za dunia na kuleta madhara makubwa. Labda hata mabahari yamekasirika kwa sababu hivi majuzi katika kile kilichoitwa 'tsunami', bahari lilihamia nchi kavu na kusomba maelfu ya binadamu na kuwameza wazima wazima. Vimbunga navyo vimetokea kwa wingi.

Wataalamu wanasema kuwa viwango vya miyeyuko vitazidi kwa sababu ya joto na kiwango cha maji kitazidi pia. Binadamu atatorekea wapi?
Idadi ya binadamu imezidi hadi kiasi asichoweza kukishughulikia kwa sababu anaijaza kiholela kwa sababu anadai kuwa aliruhusiwa kuijaza. Hii ni imani potovu. Anasahau kuwa alipewa ubongo wa kuwaza na kuwazua kabla ya kufanya chochote. Dhiki, maradhi na ufukara zimehamia kwa binadamu na kumtia kiwewe'

Binadamu amefyeka misitu kwa kutaka makao, mashamba, mbao, makaa, ujenzi wa nyumba na barabara na mahitaji mengine mengi. Wanyama wamefurushwa na wengi kuangamia kwa sababu ya ukosefu chakula na wengine kushindwa kuhimili mabadiliko katika mazingira. Chemichemi za maji zimekauka nalo jangwa limeanza kutuzuru kwa kasi inayotisha. Kazi ya binadamu imekuwa ya kusukia kamba motoni. Itambidi aanze kujenga kwa matofali ya barafu.

a) Bila kupoteza maana iliyokusudiwa na mwandishi wa taarifa, fupisha aya ya kwanza.
(Maneno 40-50) (alama 5)

b) Kwa kuzingatia aya 4 za mwisho, eleza mambo muhimu yanayoshughulikiwa na mwandishi (maneno 95-105) (alama 8)

**<u>3. MATUMIZI YA LUGHA.</u>** **ALAMA 40**

a) Taja sifa mbili bainifu za irabu /u/
(alama 2)

b) Tunga sentensi kwa kutumia kiwakilishi huru cha nafsi ya tatu umoja.
(alama 2)

c) Andika umoja wa sentensi zifuatazo. (alama 2)
i) Wakitaka tuwasamehe waje watuombe radhi kwa waliyotufanyia.
ii) Yaliyosemekana kuwa ni yao yameharibiwa na binamuo

d) Yakinisha (alama 2)
Hasikii la mwadhini wala la mteka maji msikitini.

e) Bainisha shamirisho **kipozi** na **kitondo** katika sentensi ifautayo.
(alama 2)
Mama alimpikia mwanawe chakula alichokitamani sana.

f) Tunga sentnesi moja yenye chagizo ya mahali na ya wakati.
(alama 2)

g) Onyesha mfumo wa sauti katika tungo: Mtumbwini. (alama 2)

h) Tambulisha vipashio **vitatu** vya sarufi ya Kiswahili. (alama 3)

i) Huku ukitoa mfano, eleza mantiki inayopatikana katika kauli ya kutendua.
(alama 2)

j) Taja matumizi manne ya kiambishi "ki". (alama 2)

k) Eleza maana mbili ya sentensi ifuatayo. (alama 2)
Jambazi lilimwibia Okoth gari jipya.

l) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo.
(alama 2)
Nitaenda maktabani ingawa ninaumwa na kichwa.

m) Andika katika kauli ya kutendesha
(alama 1)
Ile pombe aliyokunywa Chacha ilimfanya alewe.

n) Changanua kwa kutumia mtindo wa kielelezo matawi.
(alama 4)
Mtoto ambaye amefika ni ndugu yangu.

o) Andika kinyume cha sentensi ifautayo. (alama 2)
Huzuni alisifu nduguye aliyekusanya takataka zote.

p) Tumia neno 'vibaya' kama:
i) kivumishi
ii) Kielezi

q) Tunga sentensi yenye kihuhishi cha 'A' - unganifu katika ngeli ya U - ZI.
(alama 1)

r) Mbwa wetu amekatwa mkia. Geuza katika hali ya ukubwa.
(alama 2)

s) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya maneno haya.
(alama 1)
Mkembe, mkebe

t) Tumia ngali kutunga sentensi ili kuleta maana ya:
(alama 2)
i) Tendo katika hali ya kuendelea

ii) Tendo kutoweza kufanyika kwa sababu ya wakati kupita

**4. <u>ISIMUJAMII</u> (ALAMA 10)**

**a)** Kwa nini kulikuwa na haja ya kusanifisha lugha ya Kiswahili. Toa sababu tano.
(alama 5)

**b)** **"**….sote tunajua kwamba ni kudura. Makiwa!"

**i.** Tambua sajili iliyotumika katika dondoo hili. (alama 1)

**ii.** Eleza sifa nne za sajili hiyo. (alama 4)

# BAHATI GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

1. **LAZIMA: RIWAYA: CHOZI LA HERI NaAssumptaMatei ALAMA 20**

"…Nimeonja shubiri ya kuwa mtegemezi kihali na mali.lakini katika yote hayo, nimejifunza mengi…"

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)
b) Bainisha tamthilia ya usemii nayo jitokezaka katika kauli hii. (alama 2)
c) Thibitisha ukweli wa kauli iliyopigiwa mstari kwa kumrejelea mzungumzaji. (ala 14)

2. **USHAIRI**
**ALAMA 20**
**Soma mashairi haya kasha ujibu maswali yanayo fuata**

**SHAIRI A** **SHAIRI B**

Wewe,
Utazame mlolongo wa Dunia kitendawili, hakuna ateguaye;
Wajaunaoshikanjialikiwapo; Dunia kamatapeli, hadaanyingiujuye; Unaofuatapembe za barabarazisokuwapo,
Dunia mwenyeakili, inampikunayeye;
Kwendakuisakaauni, Dunia inamizungu, tenayapikamajungu. Kuitafutakaziinayowalachenga.
Dunia nayakehali, hupumbazahatimaye;
Itazamemigongoyawachapakazi, Dunia inaakili, binadamusichezeye;
Watokwaonajashokapakapana, Dunia uwenamali, huiwezidhorubaye;
Wanaotafunwauhainajualiso Dunia inamizungu,tenayapikamajungu. huruma:

Wakiinuavyumanamagunia,
Wakiinuamakontena, Dunia wenyemuali, ambaowaichezeye;
Wakichubukamashambani, Dunia kipigo kali, huwakumbahatimaye;
Wakiumiaviwandani, Dunia wakajakuli, "menipataninimiye?"
Wakitesekamakazini, Dunia inamizungu, tenayapikamajungu.

Halafu
Uangalieuleujirawakijungumeko,
Mshaharausokifuhaja,
Nguozisizositirimiilidhaifu,
Kilo chao kisichokuwanamachozi,

Na

UjiangalieMwiliwakounaomeretaujanawaufanisi,
Garilako la kifaharilililozibwavioo,
Jumbalako la kujishashakamauwanjamdogo,
Malaki yapesa unayo miliki,
Ujii tapo mwajiri kwa raha, hunusiusahawa hali yao?

**Maswali**

(a) Je, mashairi haya mawili niyaa ina gani? Toa sababu. (alama 2)

(b) Taja dhamira kuu katika kila shairi. (alama 2)

(c) Kwa kutoa hoja zozote **tatu** linganua mashairi haya kiumbo. (alama 3)

(d) Taja na uelezee **nafsinenewa** katika mashairi haya mawili. (alama 2)

(e) Kwa kutolea mfano **mmojammoja** eleza matumizi ya mbinu hizi za kimtindo katika shairi la A. (alama 2)

(i) Kweli-kinzani
(ii) Mishata

(f) Tambua **idhini** ya kishairi iliyotumika katika neno "Waichezeye" na uelezee dhima yake katika utoshelezi wa kiarudhi. (alama 1)

(g) Dondoa mfano **mmojammoja** wa mbinu ya tashhisi kutoka kwenye mashairi yote mawili. (alama 2)

(h) Andika ubeti wa **tatu** katika **shairi la A** kwa lugha anathari. (alama 4)

(i) Eleza maana ya msamiati huu kama ulivyotumika katika vifungu hivi. (alama 2)

(i) Inampiku.
(ii) Makontena.

## 3. FASIHI SIMULIZI — ALAMA 20

i) Umepewa jukumu la kutafiti kuhusu michezo ya watoto katika jamii yako.

a) Taja eneo ambalo utafanyia utafiti wako. (alama 2)
b) Fafanua mbinu ambazo utatumia kukusanyia data huku ukionyesha sababu za uteuziwako.

(alama 18)

**Au**

ii) a) Ni nini maana ya ulumbi (Alama 2)
b) Eleza sifa **nne** za mtendaji katika ulumbi (Alama 8)
c) Ngomezi zina majukumu yapi **manne** katika jamii yako? (Alama 8)
d) Toa mifano **miwili** yangomezi katika jamiiyako (Alama 2)

**TAMTHILIA: KIGOGO Na Pauline Kea**
**ALAMA 20**

i) "…kulindauhai, kulindahaki, kulindauhuru…"

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
b) Taja nau fafanue maudhu imawili yanayojitokeza katika dondoo hili (alama 4)
c) Msemaji wamaneno hayaa lifanikiwa kulinda uhai, kulinda haki nakulinda uhuru.
Dhibitisha kwa kurejelea tamthilia nzima (alama 12)

Au

ii) Fafanua aina zozote kumi za migogoro ijitokezayo katika tamthilia ya kigogo (alama 20)

**4. HADITHI FUPI: TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE Na Alifa Chokocho Na Dumu Kayanda**
**ALAMA 20**

**i) Shibe Inatumaliza- Salma Omar Hamad**

"…lakini kulakuna tumaliza vipi?"

a) Eleza muktadha wadondoo hili. (alama 4)
b) Eleza jinsi kulakunavyo tumaliza kwa mujibu wa hadithi. (alama 6)

**Mame Bakari-Mohammed Khelef Ghassany**

c) Eleza maudhui yafuatayo kama yalivyojitokeza katika hadithi ya Mame Bakari
 i) Uwajibikaji (alama 6)
 ii) Ukatili (alama 4)

**Au**

ii) Hukuu kirejelea hadithi ya**Tumbo Lisiloshiba** na **Shibe Inatumaliza,**fafanua maudhui ya **ukiukaji wa haki.** (al.20)

# KABARAK HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

**Swali la kwanza ( lazima)**

1. Wewe ni Gavana wa gatuzi mojawapo katika nchi ya Kongomano. Wakaazi wa mji wa Songambele wamekiuka sheria zilizowekwa na baraza la gatuzi hilo. Waandikie ilani

2. Jitihada za kumwinua mtoto wa kike zimepeleka kudhalilishwa kwa mtoto wa kiume. Jadili.

3. Andika kisa kitachodhihirisha maana ya methali.
   Ulimi huuma kuliko meno

4. Tunga kisa kitakapomalizika kwa kauli ifuatayo.
   ……………………. Nilijitazama na kujidharau. Kwani nini nilijiingiza katika hali hii? Nilijuta.

# KABARAK HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

**A. UFAHAMU** **(ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali**

Ajali haina kinga. Watu wengi wanapotajiwa neno ajali, fikira zao hukimbilia moja kwa moja hadi barabarani. Mara chachemawazo yao huenda viwandani, mashambani au
kwenye viwanja vya michezo. Ni nadra sana watu kufikiraia kuwa nyumbani ndiko ajali nyingi zinztokea.

Idadi kubwa ya ajali nyumbani hutokea kimchezo tu. Watu wengi wameteleza msalani na wanapata majeraha mabaya. Wengine wameteleza walipokanyaga vitu vyenye unyevu sakafuni, kama vile mafuta, mabaki ya chakula au hata maganda ya ndizi. Ulemavu walio nao watoto na hata watu wazima hutokana na ajali kama hizi wasizofikiria wtu wengi.

Ajali vilevile hutokea watu wanapozama katika shughuli au kupata jazba kuu ya kutenda. Katika hali hii, huweza kujiumiza au kuwaumiza wengine bila kujua.
Hapa tunazungumzia watu ambao hujaribu kubebe mizigo yenye uzani wasiokadiria. Madhara huwa kuteguka viungo na kuchanika misuli. Aghalabu hulemewa na kubanwa. Mwandishi wa makala haya siku moja alipanda kibao kuangika picha ukutani. Ingawa alikuwa mfupi, ari ilimsukuma kuchuchumia. Matokeo ni kibao kilijisukuma nyuma. Mhusika alianguka akajigonga kidevu. Kitendo hiki kilisababisha yeye kujiuma ulimi vibaya. Kuvunjika jino na hata kuzirai. Bahati ni kuwa alikuwepo mtu aliyempa huduma ya kwanza na kumkimbiza hospitalini.

Hat hivyo ajali nyingi hutokana na vifaa vya nyumbani. Zana hizi ni pamoja na visu, meko ya gesi, mashine zinazotumia umeme na kadhalika na huwa hatari sana, hasa kwa watoto. Kitu kidogo hata kama wembe huweza kusababisha

madhara makubwa. Kwa hakika hakuna yeyote kati yetu, hata waliokulia katika makasri ya fahari asiye na kovu. Makovu haya ambayo tunayaficha katika mavazi yetu ni ishara ya majeraha kutokana na ajali nyumbani. Je una kovu lolote? Unakumbuka ulivyolipata?

Ingawa ajali hizi haziepukiki, yawezekana kuzipunguza. Ni muhimu kukuza tabia na mazoea ya kuwa waangalifu nyumbani. Kwa mfano, ni hatari kuepua chungu chenye

maji yanayotokota mekoni kwa mikono mitupu. Aidha ni kutowajibika kuchanganya kitu chochote chenye unyevu na mafuta moto mekoni. Watu wengi wamebambuka
ngozi na nyumba kuteketea kwa namna hii. Kwa hivyo ni vizuri kupata ujuzi wa jinsi ya kutumia vifaa na kuhakikisha tunavirudisha ipasavyo.

Jambo la tatu na muhimu zaidi ni kuwepo kwa vifaa pamoja na uwezo wa kutoa huduma ya kwanza. Inawezekana kuokoa maisha au kuounguza majeraha kwa kuchukua hatua za dharura.

**Maswali**

1. Eleza maana ya methali 'Ajali haina kinga' (alama 2)
2. Kwa nini mwandishi anasema ajali nyumbani hutokea kimchezo? (alama 3)
3. Ni mambo gani mengine yanayosababisha ajali nyumbani? (alama 3)
4. Onyesha vile invyowezekana kupunguza ajali nyumbani. (alama 3)
5. Eleza maana ya: (alama 4)
   (i) jazba
   (ii) makasri
   (iii) makovu
   (iv) kuepua

**B. UFUPISHO** **(Alama 15)**

**Soma kifungu kifuatacho kasha ujibu maswali**

Ardhi ni mali ya taifa. Hivyo inampasa kila raia kuinafidhi. Hii ina maana kwamba hatuna budi kuwarithisa wana na wajukuu, vitukuu na vilembwe, vining'ina na wapwa zetu ardhi yenye rutuba. Ardhi ndiyo chanzo cha riziki zote. Fauka ya hayo, ardhi ni dafina kubwa.

Tangu asili ardhi hii imefunikwa na joho la miti na majani. Rutuba ilienea kila mahali. Lakini wakati ulifika ambapo wanadamu hawakuvumilia kukaa bila kuitumia johari hii. Walishika maparange na mashoka. Wakafyeka majani na miti yote. Wakalima wakapanda na kuvuna.
Kisha walihama hapo. Waliendelea kufanya hivyo mwaka hadi mwaka. Hali ya kufyeka sehemu mbalimbali za nchi, kuchoma mioto ovyo, kuwa na mifugo mingi na kutojua kuhifadhi ardhi vizuri kulileta mavuno hafifu kila mwaka.

Mvua iliponyesha matone ya mvua yaligonga ardhi. Maji yakajiri kwa nguvu na kutawanya chembe za udongo. Wakati wa kiangazi udongo ulipokauka, upepo mkali ulichukua tabaka la juu. Hivyo ikawa mazao hayawezi kustawi. Hatimaye nchi ikawa kama mkuranga. Mambo haya yakasababisha mmomonyoko wa juu juu halafu mwanzo wa michirizi na mwisho makorongo na maporomoko ya ardhi.

Walakini basi ya kale hayapo. Sasa wakuu wa serikali yetu ya Insafu wamekuhimizeni, ikiwa mu wakulima, mpande zaidi. Wamewashauri namna ya kuongeza mavuno katika mashamba yenu kwa maarifa bora ya zaraa, kama vile kuunafidhi udongo, kutumia mbolea, njia za kunyunyizia dawa makondeni ili kuua wadudu wanaoharibu mimea, na kutumia maarifa malihi katika kupanda mbegu. Kwa wale ambao si wakulima, serikali yetu ya Insafu imeweka shule za mafundisho maalum na kumhimiza kila mmoja wao aongeze maarifa yake na afanye kazi kwa tabasuri na bidii ili aongeze mapato yake na mapato ya serikali pia. Katika sehemu nyingine maelezo ya wakuu wa serikali yamefuatwa barabara, na kumetokea maongezeko malihi ya mazao.

Walakini pia katika sehemu hizo maongezeko yake hayakutosha sana. Katika sehemu nyingine kwa bahati mbaya watu wamepotezwa na watu wakaidi ambao kwa kutaka ushaufu, wamewaambia watu kuwa njia rahisi na nyepesi ya kujipatia serikali ya kujitawala yenyewe, na wamewashawishi na kuwatisha baadhi ya watu waasi amri za
serikali zihusuzo zaraa. Wahaini hao wametibua mambo. Ni watu wa kuaili na ni afkani.

**Maswali**

a. Fupisha ujumbe wa aya tatu za kwanza kwa maneno 80. (alama 9, 1 ya mtiririko)

b. Eleza masuala ambayo mwandishi anaibua katika aya mbili za mwisho kwa maneno 60. (alama 6, 1 ya mtiririko)

**C. MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Taja sauti **mbili** ambazo huitwa likwidi (alama 1)

(b) Andika neno lililo na muundo wa silabi ufuatao (alama 1)

IKKI …………………………………………………………

(c) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo (al. 2)

yafutikayo……………………………………………………………………………

(d) Tambua aina mbili za sentensi ukizingatia uamilifu na utoe mfano mmoja

kwa kila moja
(ala. 2)

(e) Ainisha vielezi vya namna katika sentensi hii (ala. 2)
Mzee huyu mkongwe alicheka kijinga huku akila haraka haraka

(f) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo
(ala. 2
Kijana aliyezungumza na nyanyake ameingia katika darasa lililochafuliwa na wanafunzi

(g) Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mstari
(ala. 3)
Mwanafunzi mwerevu sana aliyekuwa mgonjwa jana amepelekwa nyumbani

(h) Bainisha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo
(ala. 3)
Somo aliukata mti kwa kisu jana asubuhi

(i) Andika kwa usemi wa taarifa (ala. 3)
Karani: Njoo nikutume kwa babu yangu.
Karanja: Sitaki kupita njia ya kwa babu

(j) Eleza matumizi ya 'ni' katika sentensi hii
(ala. 2)
Ingieni darasani mara moja ili niwape zoezi ambalo ni rahisi

(k) Eleza maana ya sentensi zifuatazo
(ala. 2)
(i) Ningalisoma kwa bidii ningalipita mtihani
(ii) Ningesoma kwa bidii ningepita mtihani

(l) Andika katika udogo wingi
(ala. 2)
Mti wa msonobari unatengeneza meza nzuri sana

(m) Tambua miundo yoyote mitatu ya ngeli ya LI-YA
(ala. 3)

(n) Eleza maana **tatu** za sentensi ifuatayo (ala. 3)
Alisema angeenda kwao

(o) Andika upya sentensi ifuatayo katika hali ya 'a'
(ala. 1)
Mwanafunzi anasoma darasani

(p) Tumia neno 'hadi' kuonyesha mahali na wakati katika sentensi
(ala. 2)

(q) Yakinisha katika hali ya mazoea. (ala. 2)
Asiyeugua hahitaji daktari

(r) Tunga sentensi ukitumia neno 'komaa' kama (ala. 2)
(i) kivumishi

(ii) nomino

(s) Taja matumizi yoyote mawili ya <u>kistari kirefu</u> (ala. 2)

**D. ISIMU JAMII**

(a) Kwa nini kulikuwa na haja ya kusanifisha Kiswahili? Toa sababu tano (ala. 5)

(b) Fafanua sifa za lugha ya kazi (ala. 5)

# KABARAK HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

***<u>SEHEMU A:</u>***

***<u>"Tumbo Lisiloshiba na hadithi nyingine"</u>***

**<u>Swali la lazima</u>**

1. "Akanyangapo chini ardhi inatetemeka…………………..

Amejitia hamnazo. Kabwela kama mimi nina faida gani?

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala. 4)

(b) Fafanua mbinu **tatu** za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili (ala. 6)

(c) Eleza madhila **kumi** yaliyompata Kabwela (ala. 10)

***SEHEMU B:***

***Chozi la heri***

***Chagua swali la 2 au 3***

2. "…………. wanahofia kusema wasije wakavikata viganja vinavyowalisha…………..

   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala. 4)

   (b) Taja maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili na ueleze (ala. 2)

   (c) Kwa kutoa hoja kumi, eleza namna maudhui uliyotaja hapo juu (2b) yanavyojitokeza katika riwaya (ala. 10)

   (d) Eleza sifa nne za msemaji (ala. 4)

3. (a) Migogoro ni maudhui muhimu katika riwaya hii. Fafanua (ala. 10)

   (b) Uozo umetamalaki katika jamii ya *Chozi la Heri*. Tetea kauli hii kwa kutolea hija kumi zilizoelezwa (ala. 10)

**SEHEMU C: TAMTHILIA**

**Kigogo**

**Jibu swali la 4 au 5**

4. "Na mwamba ngoma huvuta wapi?"

   (a) Eleza muktadha wa dondoo hili (ala. 4)

   (b) Tambua tamathali mbili za sauti zilizotumika katika muktadha huo (ala. 2)

   (c) Fafanua sifa za msemewa wa maneno (ala. 6)

   (d) Thibitisha ukweli kuwa kila mwamba ngoma huvuta kwake ukirejelea Tamthilia nzima ya Kigogo (ala. 8)

5. "Utawala wa Majoka katika jimbo la Sagamoyo umejaa sumu ya nyoka"

Jadili usemi huo kwa kurejelea tamthilia ya Kigogo
(ala. 20)

## SEHEMU D: USHAIRI

**Jibu swali la 6 au la 7**

**6. Shairi**

La adhabu hili wingu, lataka kutunyeea
Himahima kwalo vungu, pasi nako kuchelea,
Kujikinga hili wingu, sije katunyeshea.

Wengineo hawajali, wasinayo wasiwasi,
Tahadhari hawabali, wajiunge nasi
Aidha watafakali, mengine yalo hasi.

Vua hili halibagui, jinsia wala umri,
Na kama hawajui, tuwajuze vizuri,
Kwani siso adui, kuwao msumari.

Tangazo haliwapiku, wahimizwa kujikinge,
Wingu hili la usiku, ukicheza likuringe,
Latutia usumaku, daima likunyonge.

Vumilia kwalo vungu, nje kuna dhoruba,
Yavuma kwa machungu, bila lolote huba,
Tunza chako kijungu, fungia kwalo juba.

Japo nafika tamati, nawaacha tafakari,
Madhara linalo wananti, wingu hili sukari,
Daima mwape kujiseti, mjitunze kujijari

**Maswali**

1. Eleza ujumbe wa mwandishi katika ubeti wa nne (ala. 2)
2. Onyesha ufundi wa kimuundo wa mwandishi katika utunzi wa shairi hili (ala. 4)
3. Eleza namna jazanda imetumika katika utungo huu. (ala. 2)
4. Kwa kuzingatia idadi ya mishororo katika beti tambua aina ya ushairi huu

   (ala. 1)
5. Tamthini ustadi wa mshairi katika matumizi yaidhini ya kishairi (ala. 3)
6. Litie shairi hili katika bahari tatu tofauti (ala. 3)
7. Andika ubeti wa **nne** kwa lugha ya tutumbi (ala. 4)
8. Eleza sifa moja ya nafsi neni katika shairi hili (ala. 1)

**7. Ushairi**

**Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yanayofuata**

1. Maendeleo ya umma

   Sio vitu maghalani

   Kama tele vimesaki

   Lakini havishikiki

   Ama havikamatiki

   Ni kama jinga la moto

   Bei juu

2. Maendeleo ya umma

   Sio vitu gulioni

   Kuviona madukani

Kuvishika mikononi
Na huku wavitamani
Kama tama ya fisi
Kuvipata ng'o

3. Maendeleo ya umma
Sio vitu shubakani
Dhiki ni kwa mafakiri
Nafuu kwa matajiri
Ni wao tu washitiri

Huo ni ustiimari
Io! Warudia

4. Maendeleo ya umma
Ni vitu kumilikiwa
Na wanyonge kupatiwa
Kwa bei kuzingatiwa
Bila ya kudhulumiwa
Na hata kuhadaiwa
Hiyo ni haki

5. Maendeleo ya umma
Dola kudhibiti vitu
Vijapo nchini mwetu
Na kuwauzia watu
Toka nguo na sapatu
Pasibakishiwe na kitu
Huo usawa

6. Maendeleo ya umma

   Watu kuwa na kauli

   Katika zao shughuli

   Vikaoni kujadili

   Na mwisho kuyakubali

   Maamuzi halali

   Udikteta la

7. Maendeleo ya umma

   Watu kuwa waungwana

   Vijakazi na watwana

   Nchini kuwa hakuna

   Wote kuheshimiana

   Wazee hata vijana

Maswali

(a) Toa anwani mwafaka ya shairi hili (ala. 1)

(b) Shairi hili ni la aina gani? Toa sababu zako (ala. 2)

(c) Eleza dhamira ya mwandishi kuandika shairi hili (ala. 3)

(d) Toa mifano miwili ya urudiaji katika shairi hili, Je urudiaji huu una kazi/majukumu gani? (ala. 4)

(e) Onyesha matumizi mawili ya tamathali za usemi katika shairi hili (ala. 4)

(f) Eleza toni ya mshairi. Toa sababu (ala. 2)

(g) Nafsineni ni nani? (ala. 1)

(h) Toa mfano mmoja wa twasira katika hili. Je, twasira hiyo inajengwa na nani? (ala. 3)

***SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI***

8. (a) Fafanua sifa za matambiko katika jamii (ala. 4)

(b) Eleza tofauti kati ya maigizo ya kawaida na maonyesho ya sanaa (ala. 10)

(c) Taja shughuli zozote mbili zinazoonyesha matumizi ya Ulumbi katika jamii ya kisasa (ala. 2)

(d) Tofautisha dhana zifuatazo

(i) Miviga na maapizo (ala. 2)

(ai) Ngoma na ngomezi (ala. 2)

# ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL

## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM

## Julai 2019

## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

**Swali la kwanza ( lazima)**

1. Wewe ni mwenyekiti wa kamati ya kupigana na ufisadi nchini Kenya na umealikwa, kuhutubia kongamano la kitaifa kuhusu athari za ufisadi huku

ukipendekeza hatua za kukabiliana na janga hili. Andika hotuba utakayoitoa.

(Alama 20)

2. Nyimbo za kitamanduni zilikuwa na nafasi kubwa katika ufanisi wa jamii kwa jumla.
   Eleza. ( Alama 20)

3. Andika kisa kitakachodhihirisha ukweli wa methali isemayo;.
   Bahati ni chudi
   (Alama 20)

4. Andika insha itakayomalizia kwa maneno yafuatayo;
   ……………………. Hapo ndipo iliponibainikia kuwa nilikuwa nikiogelea baharini pekee kinyume na wenzangu wote.
   (Alama 20)

# ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

**E. UFAHAMU (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali**

Hakuna dakika inayopita bila kisa cha kuchelewa. Mikutano karibu yote huchelewa kuanza kwa sababu wahusika hawafiki wakati ufaao. Ibada nazo hucheleweshwa kwa uzembe wa waumini. Na mazishi je? Taratibu hucheleweshwa vilevile. Ingawa hapa yaweza kufikiriwa kuwa pengine wampendao marehemu hawataki kuharakisha safari yake ya kwenda
kuzimuni. Lakini hata arusi ambazo huwa na misururu ya mikutano ya maandalizi,

siku
itimiapo shughuli huchelewa. Si ajabu sherehe kuendelea mpaka usiku ambapo ratiba ilionyesha zingekomea masaa ya alasiri.

Uchunguzi unabainisha kuwa watu huchelewa kwa sababu mbalimbali. Sababu mojawapo ni kutowajibika; yaani, watu wengi hawaoni umuhimu wa kuzingatia saa. Wengine hufanya hivi kwa kisingizio kuwa ni kawaida ya mwafrika kutozingatia muda. Huu ni upuuzi mtupu. Wazee wetu walizingatia muda ipasavyo tangu jadi ingawa hawakuwa na saa wala kalenda. Hii ndiyo sababu walipanda mimea walipohitajika, wakavuna na hatimaye wakapika na kuandaa ipasavyo. Wahenga hawa walituachia methali nyingi kama funzo, kwa mfano; 'Chelewachelewa utakuta mwana si wako', na hata wakasindikiza kuwa, 'Ngoja ngoja huumiza matumbo'.

Watu wengine huchelewa kwa sababu ya kutojiandaa kwa yale yatakayojiri. Watu wasiopanga shughuli zao na badala yake kuzifanya kwa kushtukia aghalabu hushindwa kuhudhuria hata mahojiano ya kuajiriwa kazi kwa wakati ufaao. Hawa huwa neema kwa washindani wao. Kujitayarisha si jambo gumu. Anachopasa kujua mhusika ni saa ya miadi na hali ya usafiri.

Hivi viwili vitamwezesha kujua muda wa safari na hivyo kukadiria wakati wa kuondoka. Ni wangapi wameiona milolongo ya watu nje ya milango ya benki wakiwasihi mabawabu na pengine kuwahonga wawaruhusu kuingia? Hawa huwa si wageni. Ni wateja wanaojua ratiba ya kazi lakini hushindwa kupanga mwenendo wao barabara.

Mikutano, sherehe na shughuli nyingi huchelewa kuanza kwa masaa mengi kwa sababu eti mgeni mashuhuri amechelewa kufika. Muda wa kungoja huwa mrefu zaidi kutegemea ukubwa wa cheo cha mhusika. Watu hawa huchelewa makusudi kwa sababu pengine ya kiburi. Majivuno haya huwafanya wafurahi wanaposubiriwa na watu wadogo. Wakubwa hawa wanapofika badala ya kuomba msamaha, hujigamba kuhusu majukumu yao mengi na makubwa.

Aidha kuna watu ambao hupenda kutekeleza mambo mengi kwa wakati mmoja. Tujuavyo ni kuwa mambo mawili yalimshinda fisi. Pia watu wanaposhika mengi, mahudhurio yao katika baadhi ya mambo hutatizwa na hivyo huchelewa. Isitoshe, kuna watu wa aina hii hata wanapopewa ratiba mapema, hujikokota na hivyo kupitwa na wakati.

Ingawa sababu tulizozitaja hutokana na watu wenyewe, kuna zile zinazosababishwa na dharura nyingine. Hizi ni pamoja na misongamano ya magari, kuchelewa kwa vyombo vya usafiri na hata kuharibika kwa vyombo. Hii ndiyo sababu inashauriwa kuwa mtu anapoamua kutekeleza jambo, atenge muda takribani wa dakika 30 kwa ajili ya dharura fulani. Kwa hivyo hata anapopata tuseme pancha njiani bado atafika kwa wakati ufaao.

Kuchelewa hakuudhi tu watu wanaocheleweshwa bali huwa na matokeo mengine mengi. Mara nyingi watu waliochelewa huharakisha mambo ili kufidia muda walioupoteza. Kama wanaendesha gari, kwa mfano, basi huzidisha kasi matokeo huweza kuwa ajali ambayo mara nyingine huleta ulemavu au vifo.

Ratiba ya mambo ichelewapo watu waliofika mapema hupoteza muda kusubiri. Muda huu wangeutumia kwa harakati muhimu. Mfumo wa uchumi wa kisasi unahitaji mamilioni ya watu kukurubiana, kutagusana na kuendesha shughuli zao kwa ujima. Aidha, watu
hawana budi kubadilishana bidhaa na huduma. Mambo haya yanapocheleweshwa basi gharama huwa kubwa.

Tatizo hili hubainika sana katika ofisi za umma.

Ni kwaida watu kufika kazini dakika nyingi baada ya wakati wa kufungua milango ya kazini. Ajabu ni kuwa wafanyakazi wawa huwa wa kwanza kufunga kazi kabla ya kipindi rasmi. Inakisiwa Kenya hupoteza shilingi bilioni 80 kila mwaka kupitia uzembe wa kutozingatia wakati.

Jambo la kwanza ni kuweka sera ya kitaifa inayolenga kuwaelimisha wananchi umuhimu wakuzingatia saa. Halikadhalika kanuni iwekwe ya kuwafungia nje watu wanaochelewa kuhudhuriashughuli za mikutano au hafla. Wananchi nao wazinduliwe kuwa ni haki yao kufumkana muda washughuli unapowadia kabla mgeni wa heshima kufika. Nchi ya Ekwado (Ecuador) imefanikiwakutekeleza haya. Kenya pia haina budi kuandama mwelekeo huo. Hii
ndiyo njia mojawapo ya kufufua uchumi na kuhakikisha taifa linapiga hatua kimaendeleo.

**Maswali:**

1. Kipe kifungu hiki anwani mwafaka (ala. 1)
2. Taja watu **watatu** walio na mazoea ya kuchelewa katika shughuli walizoalikwa (ala. 3)
3. Taja sababu zinazofanya watu kushindwa kutimiza miadi (ala. 4)
4. Taja na ueleze njia **nne** zinazoweza kuondoa tatizo la kuchelewa (ala. 4)
5. Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa (ala. 3)
   a) ujima
   b) miadi
   c) pancha

**F. UFUPISHO (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yote**

Takriban kila siku vyombo vya habari hueleza kuhusu mateso ya watoto; cha kusikitisha zaidi ni kwamba mbali na visa vinavyoripotiwa, kuna vingine chungu nzima ambavyo havijaripotiwa. Mateso kwa watoto hawa ni ya aina mbalimbali. Mwezi wa Julai, 2005 wavamizi walipowaua watu zaidi ya sabini Kaskazini mwa Kenya, walianza

kwa kuwauwa watoto katika shule ya msingi ya Mabweni. Waliwauwa watoto ishirini na wawili huku mamia wakijehuriwa.

Kuna wazazi ambao huwapiga watoto wao mithili ya kumpiga nyoka. Utaona watoto wakiwa na majeraha yanayofanya malaika kusimama mwilini. Visa vingi vimeripotiwa ambapo wazazi au walevi huwakata au kuwadhuru watoto sehemu fulani za mwili kama vile masikio, miguu au mikono. Vilevile, kumetokea visa vya kuwachoma watoto na wengine kuwachwa bila chakula.

Kenya ni mojawapo ya nchi zilizotia sahihi mkataba wa kulinda haki za watoto. Serikali yetu ina idara katika ofisi ya makamu wa rais inayoshughulikia maslahi ya watoto. Mwezi wa Julai 2005, Serikali ilianzisha kampeni kabambe za kukomesha mateso dhidi ya watoto. Ajabu ni kwamba watu wengi na hata watoto wenyewe hawajui haki zao. Sheria ya watoto ilipitishwa ili kutetea haki za

watoto katika nchi ya Kenya.

Baadhi ya haki za watoto ni kama vile kulindwa kutokana na ubaguzi wowote, kutunzwa na wazazi na kupewa elimu. Watoto wana haki ya elimu ya kiakademia na
dini. Vilevile wana haki ya kulindwa kiafya. Watoto hawatakikani kunyanyaswa kiuchumi au kwa njia nyinginezo kama vile kusajiliwa kupigana katika vita. Kila mtoto akiwemo mlemavu, ana haki ya kuheshimiwa katika jamii.

Hata hivyo, sharti pia watoto wawajibike ipasavyo kwa wazazi, walezi na jamii kwa jumla. Mtoto anapaswa kuheshimu wakuu wake na kuwasaidia panapo haja. Watoto
wana jukumu la kudumisha na kuimarisha umoja wa jamii na raia kuendeleza maadili mema katika jamii.

Maswali:

(a) Fupisha aya ya kwanza na ya pili kwa maneno 60-80 (ala. 6, mtiririko 1 )

(b) Bainisha mambo muhimu aliyoyajadili mwandishi katika aya tatu za mwisho. (Maneno 100 – 120 ) (ala. 20, mtiririko 1)

## G. <u>SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA</u> (ALAMA 40)

(a) Taja vipasuo <u>viwili</u> vya ufizi (alama 2)

(b) Onyesha maumbo <u>mawili</u> ya silabi funge kwa kutolea mifano katika maneno (alama 2)

(c) Bainisha mofimu za neno 'kilichonywewa' (alama 3)

(d) Unda nomino moja moja kutokana na nomino zifuatazo (alama 2)
- (i) Madhara
- (ii) Kitenzi

(e) Tambua virai vihusishi katika sentensi ifuatayo (alama 2)
Wengine wao waliegesha kando ya barabara iliyokarabatiwa na kampuni ya Kichina

(f) Andika sentensi zifuatazo upya kwa kutumia 'po' (alama 2)
- (i) Raia wakipatana maendeleo yataimarika
- (ii) Mkiwatesa watoto wenu mtashtakiwa

(g) Andika kwa ukubwa hali timilifu (alama 3)
Mtego ulimnasa ndovu huyo

(h) Andika sentensi ifuatayo upya ukibadilisha neno lililopigiwa mstari kuwa kivumishi (ala. 2)

Msichana amepigwa <u>vibaya</u>

(i) Ainisha yambwa na chagizo katika sentensi ifuatayo (alama 4)
Wanafunzi walimwatikia mwalimu mkuu miche ya matunda nje ya nyumba yake kwa ustadi wakitumia vijiti.

(j) Andika visawe viwili vya neno 'vurumai' (alama 2)

(k) Taja na utolee mifano matumizi mawili ya mshazari (alama 2)

(l) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao kisha uichanganue kwa matawi (alama 4)
S – KN (N + V) + KT (T + E)

(m) Andika kwa usemi halisi (alama 2)
Kyalo alikiri kuwa kama wangefika mapema wangekamilisha shughuli zote

(n) Tofautisha maana ya sentensi zifuatazo (alama 2)
(i) Alipokelewa mgeni
(ii) Alipokezwa mgeni

(o) Andika kinyume (alama 3)
Vijana walivunja kambi baada ya macheo

(p) Kanusha (alama 3)
Asha aliwapelekea wageni chakula na akawanavya mikono

## H. ISIMU JAMII (ALAMA 10)

(a) Eleza sifa zozote tano za lugha ya itifaki (alama 5)

(b) Hakiki sifa zozote tano za sajili ya kituo cha polisi (alama 5)

# K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
# Julai 2019
# Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

## SEHEMU A: Riwaya

1. **LAZIMA**

**Assumpta K. Matei: Chozi la heri**

"Hili lilimtia …………. uchungu, akajiona kama aliyedhalilishwa na mwanamke."

(a) Yaweke maneno haya katika muktadha wake (alama 4)

(b) Taja suala linalodokezwa katika dondoo hili (alama 1)

(c) Kwa kutumia hoja kumi na tano, eleza namna suala ulilolitaja hapo juu 1 (b) linalijitokeza (ala. 15)

## *SEHEMU B: Tamthilia*
## *Kigogo (Pauline Kea)*

**Jibu swali la pili au la tatu**

2. "Kubali pendekezo letu la kufungwa kwa soko……… huoni hii ni fursa nzuri ya kulipiza kisasi?"

(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili (alama 4)

(b) Kufungwa kwa soko ni ukatili. Mbali na ukatili huu, toa mifano mingine ya ukatili kwenye tamthilia. (alama 9)

(c) Msemaji wa maneno haya ni mshauri mbaya. Thibitisha kutoka kwenye dondoo na kwingineko tamthiliani. (alama 7)

3. (a) Fafanua mbinu kumi anazotumia Majoka katika kuuendeleza uongozi wake (alama 10)

(b) Eleza namna mbinu ya ishara ilivyotumiwa katika tamthilia ya Kigogo (alama 10)

## *SEHEMU C: Hadithi Fupi*

### *Tumbo Lisiloshiba na Hadithi Nyingine ( Alifa Chokocho na Dumu Kayanda)*

### *Jibu swali la 4 au la 5*

4. "…………… Ningeondoka ….. mapema niende niibe au niue ili niwe mtu wa maana."
   (a) Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)

   (b) Onyesha vile Kinaya kinavyojitokeza katika dondoo hili (alama 2)

   (c) "Kinaya kimetumika kwingine katika hadithi husika. Thibitisha kwa kutumia hoja tisa (alama 9)

   (d) Eleza umuhimu wa msemaji katika hadithi hii (alama 5)

5. (a) Eleza namna maudhui ya ndoa yalivyosawiriwa katika hadithi ya Masharti ya Kisasa (alama 13)

   (b) Kwa kurejelea hadithi ya Shibe inatumaliza, eleza namna maudhui ya ufisadi yanavyojitokeza (alama 7)

## *SEHEMU D: Fasihi Simulizi*

**6. Soma utungo ufuatao kisha ujibu maswali**

Heri ujue mapema
Nasaba yetu haina woga
Woga haumei kwetu, humea kwa kina mamako.
Tulichinja jogoo na fahali ili uwe mwanaume.

Ah! Kisu cha ngariba ni kikali ajabu.
Iwapo utatikisa kichwacho.
Uhamie kwa wasiotahiri,
Ama tukwite njeku.

Mpwangu kumbuka hili,
Wanaume wa mlango wetu
Si waoga wa kisu
Wao hukatwa mchana hadi usiku
Wala hawalalamiki.

Siku nilipokatwa
Nilisimama tisti
Nikacheka ngariba kwa tashtiti
Halikunitoka chozi.

Iwapo utapepesa kope

Wasichana wa kwetu na wa mbali
Wote watakucheka
Ubaki ukinuna.

Sembe umepokea
Na supu ya makongoro ukabugia
Sema unachotaka
Usije kunitia aibu

**Maswali;**

(a) Taja na uthibitishe shughuli zozote za kiuchumi za jamii ya wimbo huu (alama 4)

(b) Ni nani mwimbaji wa wimbo huu na anawaimbia nani? (alama 2)

(c) Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha (alama 2)

(d) Mwimbaji wa wimbo huu ana taasubi ya kiume. Thibitisha kauli hii. (alama 2)

(e) Eleza wajibu wa nyimbo katika jamii (alama 6)

(f) Ijapokuwa nyimbo ni nzuri, zina ubaya wake. Thibitisha kauli hii (alama 4)

**SEHEMU E: Ushairi (alama 20)**
**Jibu swali la 7 au la 8**

**7. Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Kama dau baharini, duniya inavyoyumba,
Limeshamiri tufani, kila mmoja lakumba,
Viumbe tu hali gani!

Duniya yatishika, utahisi kama kwamba,
Vilima vyaporomoka, na kuvurugika myamba,
Viumbe tu hali gani!

Tufani hilo la kusi, languruma na *kutamba*,
Linapuliza kwa kasi, hapana kisichoyumba,
Viumbe tu hali gani!

Mujiwe ni kubwa sana, mfanowe kama nyumba,
Yazuka na kugongana, wala hatuna la *kwamba*,
Viumbe tu hali gani!

Mibuyu hata mivule, kama usufi na pamba,
Inarusha vilevile, *seuze hiyi migomba*

Viumbe tu hali gani!

Ni kipi kilotuliya, tuwazeni na kudumba,
Mandovu kiangaliya, yagongana na masimba,
Fisi wako hali gani!

Hata papa baharini, tufani limewakumba,
Walioko mikondoni, kila mmoja *asamba*,
Dagaa wa hali gani!

Mashehe wa mdaduwa, kwa ubani na uvumba,
Tufani hilo kwa kuwa, kusoze kwake kutamba,
Itokee afueni!
**(Shairi la 'Tufani' la Haji Gora Haji, katika *Tamthilia ya Maisha*, uk 62)**

**Maswali;**

(a) Taja na ueleze mikondo ya shairi hili (alama 4)

(b) Eleza dhamira ya shairi hili (alama 2)

(c) Taja tamathali za usemi zilizotumiwa katika shairi hili. (alama 2)

(d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)

(e) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa tano. (alama 3)

(f) Onyesha matumizi ya idhini ya kishairi . (alama 3)

(g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kwa mjibu wa shairi hili (alama 2)
   (i) Mdaduwa :
   (ai) Kutamba :

8. **Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali**

Daima alfajiri na mapema
Hunipitia na jembe na kotama
Katika njia iendayo Kondeni
Kama walivyofanya babuze zamani;
Nimuonapo huwa anatabasamu
Kama mtu aliye na hamu
Kushika mpini na kutokwa jasho
Ili kujikimu kupata malisho.

Anapotembea anasikiliza
Videge vya anga vinavyotumbuiza

Utadhani huwa vimemngojea
Kwa usiku kucha kuja kumwimbia
Pia pepo baridi kumpepea
Rihi ya maua zikimtetea
Nao umande kumbusu miguuni;

Na miti yote hujipinda migogo
Kumpapasa, kumtoa matongo;
Na yeye kundelea kwa furaha
Kuliko yeyote ninayemjua
Akichekelea ha ha ha ha ha ha …….

Na mimi kubaki kujiuliza
Kuna siri gani inayomliwaza?
Au ni kujua au kutojua?
Furaha ya mtu ni furaha gani?
Katika dunia inayomhini?
Ukali wa jua wamnyima zao
Soko la dunia lamkaba koo;

Dini za kudhani zamsonga roho
Ayalimia matumbo ya waroho.
Kuna jambo gani linalomridhisha?
Kama si kujua ni kutojua
Lait angalijua, laity angalijua!

**Maswali:**

a) Eleza hali ya mzungumziwa katika shairi hili. (alama 2)
b) Huku ukitoa mifano, onyesha aina mbili za uhuru wa kishairi uliotumiwa katika shairi hili (ala. 4)
c) Fafanua aina tatu za taswira ukirejelea ubeti wa pili (alama 3)
d) Maswali ya balagha katika shairi hili yanasisitiza maudhui yapi? (alama 2)
e) Kwa kutoa mifano, bainisha vipengele vitatu vya Kimtindo katika shairi hili (alama 3)
f) Eleza toni ya shairi hili (alama 2)
g) Bainisha nafsineni katika shairi hili (alama 1)
h) Eleza muundo wa shairi hili (alama 3)

# SACHO HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

**1. Lazima**

Wewe ni mhariri wa gazeti la Mzalendo. Andika tahariri kuhusu athari za mitandao ya kijamii kwa wanafunzi wa shule nchini Kenya.

**2.** Unywaji wa pombe haramu una madhara mengi.
Fafanua.

**3.** Tunga kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ifuatayo:

Nazi mbovu harabu ya nzima.

**4.** Tunga kisa kinachoanza kwa kauli ifuatayo:

Nilipigwa na butwaa nilipomwona, sikujua nifurahi au nihuzunike….

SACHO HIGH SCHOOL
K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM

# Julai 2019
# Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

**1. SEHEMU A: UFAHAMU** (Alama. 15)
***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.***

"Asubuhi moja alinipata ndani ya afisi ya mwalimu mkuu wa Shule ya Msingi ya Kilimo. Mwalimu Mkuu, Bi. Tamasha, alisikiliza kadhia yangu kwa makini. Hakuonyesha kushtuka kwa yaliyonipata katika umri wangu mdogo hivi.
'Unaweza kuanza masomo katika darasa la pili. Nitamwomba mzazi mmoja akupe hifadhi,' alisema Bi. Tamasha. Huo ndio uliokuwa mwanzo wa maisha yangu katika makao ya wafanyakazi wa mashamba ya chai. Bwana Tenge na mkewe, Kimai, walinichukua kunilea pamoja na watoto wao watano. Wenzangu, nyinyi hamjui adha zinazowapata wafanyakazi wa kima kidogo. Mtajuaje na hamjawahi kukilalia kitanda hiki mkafahamiana na kunguni wake? Ninayowaambia ni asilimia ndogo mno ya niliyoyaona. Chumba cha wafadhili wangu kilikuwa hicho hicho kimoja; ndicho cha malazi, ndicho cha mapokezi, ndicho jikoni. Sebule na chumba cha malazi viligawanywa na shuka moja nyepesi. Usiku sisi watoto tulilala juu ya vigodoro ambavyo ni kama viliwekwa mvunguni mwa kitanda cha wazazi.

"Usiniulize niliyaona na kuyasikia mangapi katika chumba hiki ambacho kiligeuka *danguro* wakati Bi. Kimai alipokuwa ameenda mashambani. Wakati huu Bwana Tenge angeamua kumleta mwanamke mmoja baada ya mwingine, hapo hapo, mbele ya macho ya wanawe, hadi usiku wa kuamkia siku ya kurudi kwa Bi. Kimai. Mara mojamoja Bi. Kimai angerudi bila kutarajiwa na kumshika ugoni mke mwenzake! Mwaka mmoja, miwili, mitatu …. hata nikaona kwamba, mbali na dhiki za *kisaikolojia* nilizozipata kwa kushuhudia vituko vya kila aina, nilikuwa mzigo mkubwa kwa wahisani wangu. Si kwamba waja hawa walinibagua, la! Kusema hivyo kutakuwa kuwapaka mashizi bure. Hata hivyo nilihisi kwamba nimepata mbavu za kufanya angaa kibarua kidogo, na kuwatua wawili hawa mzigo wa kuninunulia sare na madaftari.

"Nilianza kuchuna majanichai kwa malipo kidogo nikiwa katika darasa la tano. Wakati mwingine ningerauka alfajiri na mapema kufanya kazi kabla ya kwenda shuleni saa kumi na mbili asubuhi. Jioni nilipitia huko huko. Nyakati nyingi nililala humo humo katikati ya michai, wakati mwingine kwa marafiki wanfu, kwa Bwana Tenge, na juu ya uchaga mkubwa wa saruji uliotumiwa kama karo na wauza chakula sokoni. Hakuna mmoja kati ya walimu wangu aliyejua mabadiliko haya hadi pale nilipoufanya mtihani wangu wa darasa la nane na kufuzu vyema.

"Wakati huo Bwana Tenge alikuwa ameisha kupewa uhamisho, akaenda kufanya kazi katika shamba lingine. Ndivyo wafanywavyo wafanyakazi hawa; kuhamishwa kila uchao bila mtu kuwazia kwamba wana watoto wanaoenda shule, na kwamba kuhamahama huku kunawavurugia masomo wana hawa."

**Maswali**

(i) Eleza namna wazazi wanavyoweza kuchangia katika kuzorotesha maadili ya watoto katika jamii. (alama 2)

(ii) Onyesha namna haki za watoto zilivyokiukwa katika kifungu. (alama 3)

(iii) Wafanyakazi wa kima kidogo hupitia dhiki zipi kulingana na kifungu? (alama 3)

(iv) Eleza sifa **tatu** za mkewe Tenge – Kimai. (alama 3)

(v) Eleza namna ndoa inavyosawiriwa katika kifungu. (alama 2)

(vi) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika kifungu. (alama 2)

(a) Danguro
(b) Kisaikolojia

2. **SEHEMU B: UFUPISHO** (Alama 15)

***Soma kifungu kisha ujibu maswali.***

Ripoti za kila mara kuhusu uharibifu wa pesa za umma katika serikali za kaunti ni za kusikitisha. Kuna mabilioni ya pesa za mlipa ushuru ambazo hufujwa katika serikali kuu, na hivyo basi wananchi wanakosewa sana wanapoona mtindo huu ukiendelea pia katika serikali za kaunti. Wakati katiba ilipopitishwa mwaka wa 2010, Wakenya wengi walikuwa na matumaini mno kwamba ugatuzi ungewatatulia matatizo ambayo walikuwa wakipitia katika tawala zilizotangulia, hasa katika maeneo yaliyotengwa kimaendeleo.

Miaka tisa baadaye, kuna mafanikio ambayo yamepatikana ila hatua kubwa zaidi inaweza kupigwa katika kuboresha maisha ya aina raia kama mianya inayotumiwa kufuja pesa za umma itazibwa. Wizi huu unaojumuisha pia jinsi magavana wanavyobuni nafasi za kazi zisizo na maana ambazo wakati mwingi hupeanwa kwa jamaa na marafiki wao, ni sharti ukomeshwe mara moja.

Kuna wananchi wengi ambao tayari wameanza kufa moyo kuhusu umuhimu wa ugatuzi ilhali ukweli ni kwamba hatungependa kurejelea utawala ulio chini ya serikali kuu pekee. Changamoto za ugatuzi zinazosababishwa na ulafi wa viongozi wachache zinatoa nafasi kwa wakosoaji wa mfumo huu wa uongozi kushawishi wananchi na hata wahisani wasishughulike kuchangia katika maendeleo ya kaunti zao.

Juhudi zozote zile za maendeleo haziwezi kufanikishwa bila ushirikiano kutoka kwa wananchi na wahisani na hivyo basi ni jukumu la viongozi kuonyesha nia ya kutumia mamlaka walizopewa kwa manufaa ya raia. Tume ya maadili ya kupamban ana ufisadi (EACC) kufikia sasa imeonekana kufanya kazi nzuri kwa kuwasaka na kuwashtaki magavana walio mamlakani na wengine walioondoka, kwa kushukiwa kufuja mali za umma. Tungependa asasi zote zinazohusika na masuala ya kupambana na uhalifu, pamoja na wadau wengine katika jamii wenye nia njema kwa wananchi wasifumbie macho maovu yanayotendwa katika kaunti zetu.

Nchi hii inatawalwa kwa misingi ya kisheria na hivyo basi hakuna sababu kumhurumia kiongozi yeyote anayekiuka sheria anapokuwa mamlakani kwa msingi wa mamlaka aliyoshikilia. Ni kupitia adhabu kali za kisheria pekeee ambapo tutafanikiwa kukomesha uongozi mbaya kwani kama wananchi watakuwa wakisubiri kuwaadhibu wahusika kwa kuwaondoa mamlakani pekee, watakuwa wametoa nafasi ya ufujaji kwa viongozi wapya kila miaka mitano.

*(Kutoka gazeti la Taifa Leo)*

(a) Fupisha ujumbe wa aya **tatu** za kwanza kwa maneno 80.
*(alama 8, 1 ya mtiririko)*

(b) Fupisha aya **mbili** za mwisho kwa maneno 70. *(alama 7, 1 ya mtiririko)*

**3. SEHEMU C: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA** (Alama 40)

(a) Andika sifa **mbili mbili** za sauti zifuatazo. (ala. 2)
i) /e/
ii) /ch/

(b) Unda maneno yenye muundo ufuatao wa sauti.
(ala. 2)
i) KIKIKI
ii) IKKI

(c) Onyesha shadda inapowekwa katika maneno yafuatayo: (ala. 1)
i) mwanafunzi
ii) Alhamisi

(d) Tunga sentensi **moja moja** kuonyesha matumizi ya viakifishi vifuatavyo: (ala. 2)
i) Vifungo
ii) Kibainishi

(e) Maneno yafuatayo yako katika ngeli gani? (ala. 2)
i) Changu
ii) Manowari

(f) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa.
(ala. 2)
*Ndege hao wana manyoya mengi*

(g) Ainisha viambishi katika neno lifuatalo:
(ala. 3)
*Mliyempikia*

(h) Tumia kielezi cha kiasi badala ya kile kilichopigiwa mstari.
(ala. 1)
*Msichana yule alizungumza kitausi.*

(i) Bainisha vishazi katika sentensi ifuatayo.
(ala. 2)
*Ingawa alitia bidii masomoni, alifeli mtihani.*

(j) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali/vijisanduku.
(ala. 3)

*Mvua kubwa inayonyesha itasababisha mafuriko.*

(k) Andika upya sentensi ifuatayo ukianzia na yambwa tendewa.
(ala. 2)

*Kirwa alimjengea mama huyo nyumba kwa matofali.*

(l) Kanusha sentensi ifuatayo kwa wakati ujao hali ya kuendelea.
(ala. 2)

*Walimu wanafunza.*

(m) Geuza sentensi ifuatayo katika usemi halisi.
(ala. 2)

*Muliwa alimwambia Farida kuwa angewatembelea wazazi wao siku hiyo jioni.*

(n) Tunga sentensi **moja** kubainisha maana **mbili** za neno 'hema'
(ala. 2)

(o) Amrisha katika nafsi ya <u>tatu wingi</u>.
(ala. 1)

*Lala*

(p) Andika sentensi ifuatayo upya ukitumia vinyume vya maneno yaliyopigiwa mstari. (ala. 2)

*Mama <u>alijitwika</u> kikapu mgongoni baada ya <u>kuinjika</u> chungu mekoni.*

(q) Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mstari. (ala. 2)

*Mhadhara <u>huo tata</u> ulitolewa <u>jana jioni</u>.*

(r) Tunga sentensi **moja** itakayodhihirisha matumizi matatu ya 'na' (ala. 3)

(s) Tunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli ulizopewa mabanoni.
(ala. 2)

i) Paka (*tendata*)
ii) Choma (*tendua*)

(t) Andika sentensi zifuatazo kwa lugha ya tafsida.
(ala. 2)

*i) Mama huyo alizaa mtoto msichana.*
*ii) Mtoto ameenda kukojoa.*

**4. SEHEMU D: ISIMUJAMII** (Alama 10)

***Soma mazungumzo yafuatayo kisha ujibu maswali.***

Kibiko: Hujambo dada Cheupe?
Cheupe: (*Akikohoa*) Sijambo ndugu Kibiko.
Kibiko: Unaendelea namna gani?
Cheupe: *Niko poa* isipokuwa maumivu kidogo ya *chest.*
Kibiko: Usijali nitakupa *pain relievers* utakuwa sawa.
Cheupe: Asante sana, nashukuru.

<u>**Maswali**</u>

a) Eleza muktadha wa mazungumzo haya.
(ala. 2)

b) Taja na ueleze sifa za lugha inayotumika katika mazungumzo haya.
(ala. 8)

# SACHO HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

**SEHEMU A: RIWAYA**

**Assumpta K. Matei:** *Chozi la Heri*

**1.** **Lazima**
Riwaya ya Chozi la Heri inayasawiri matatizo ya wanajamii. Jadili. (al. 20)

**SEHEMU B: TAMTHILIA**

**P. Kea:** *Kigogo*

*Jibu swali la **2** au la **3***

**2.** "Huku ni Sagamoyo, naomba kukumbusha kuwa serikali na katiba ni mambo mawili tofauti kabisa."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)
b) Eleza sifa **tatu** za mzungumzaji. (al. 3)
c) Fafanua umuhimu wa mzungumziwa. (al. 3)
d) Onyesha ukweli wa kauli katika dondoo hili. (al. 10)

**3.** a) Onyesha namna maudhui ya elimu yalivyoshughulikiwa katika tamthilia ya Kigogo. (al. 10)
b) Eleza mbinu ambazo jamii ya Sagamoyo ilitumia kupambana na uongozi mbaya wa Majoka. (al. 10)

**SEHEMU C: HADITHI FUPI**
**A. Chokocho na D. Kayanda:** *Tumbo lisiloshiba na Hadithi nyingine*

*Jibu swali la **4** au la **5**.*

**Alifa Chokocho:** *"Masharti ya Kisasa"*

**4.** "Kweli mwalimu mkuu ana kazi nyingi na nyingine lazima aende usiku usiku kuzipunguza. Lakini leo ni leo …."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (al. 4)

b) Taja na utolee mfano mbinu zozote **mbili** za lugha katika dondoo hili. (al. 4)

c) Eleza matukio yoyote **sita** yaliyotokea baada ya kauli hii. (al. 12)

5. Huku ukirejelea hadithi zifuatazo eleza namna unyanyasaji umeshughulikiwa.
a) Tumbo lisiloshiba (al. 4)
b) Shibe inatumaliza (al. 4)
c) Mame Bakari (al. 4)
d) Kidege (al. 4)
e) Tulipokutana tena (al. 4)

## ***SEHEMU D: USHAIRI***

***Jibu swali la 6 au la 7.***

**6.**

Angawa mdogo, dagaa, amekomaa
Kaanga kidogo, dagaa, atakufaa
Kalia kinaya, dagaa, h'ondoa njaa

Wa kwako udogo, kijana, sio balaa
Na sio mzigo, kijana, bado wafaa
Toka kwa mtego, kijana, sinyanyapaa

Nasaha kidogo, kijana, ukubwa jaa
Jikaze kimbogo, kijana, acha kukaa
Chimbua mhogo, kijana, usibung'aa

Na wake udogo, dagaa, hajambaa
Kuliko vigogo, dagaa, hajambaa
Hapati kipigo, dagaa, hauna fazaa

Maisha si mwigo, kijana ushike taa
Sihofu magego, kijana, nawe wafaa
Kazana kidogo, kijana, kugaaga

Maswali

a) Lipe shairi hili anwani mwafaka. (al. 2)

b) Eleza arudhi zilizofuatwa katika kutunga shairi hili. (al. 4)

c) Onyesha jinsi malenga alivyotumia uhuru wake. (al. 3)

d) Tambua bahari katika shairi hili kwa kutegemea: (al. 3)

i) Vipande vya mishororo

ii) Mpangilio wa vina
iii) Idadi ya mishororo

e) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari. (al. 4)

f) Tambua mbinu za lugha zilizotumika katika shairi. (al. 2)

g) Eleza toni ya shairi hili. (al. 2)

**7.**

Eti
Mimi niondoke hapa
Niondoke hapa kwangu
Nimesaki, licha ya risasi
Vitisho na mauaji, siondoki

Mimi
Siondoki
Siondoki siondoki
Niondoke hapa kwangu!
Kwa mateke hata na mikuki
Marungu na bunduki, siondoki

Hapa
Siondoki
Mimi ni pahame!
Niondoke hapa kwangu!
Fujo na ghasia zikizuka
Na kani ya waporaji, siondoki

Haki
Siondoki
Kwangu siondoki
Niondoke hapa kwangu!
Nawaje; waje wanaokuja
Mabepari wadhalimu, siondoki

Kamwe
Siondoki
Ng'oo hapa kwangu!
Katizame chini mti ule!
Walizikwa babu zangu, siondoki

Sendi
Nende wapi?
Si hapa kitovu changu
Niondoke hapa kwangu
Wangawa na vijikaratasi
Si kwamba hapa si kwangu, siondoki

Katu
Siondoki
Sihitaji karatasi
Niondoke hapa kwangu
Yangu mimi ni ardhi hii
Wala si makaratasi, siondoki

<u>Maswali</u>

a) Shairi hili ni la aina gani? Kwa nini? (al. 2)
b) Taja masaibu anayopitia mzungumzaji. (al. 4)
c) Eleza toni ya shairi hili. (al. 2)
d) Eleza muundo wa shairi hili. (al. 3)
e) Tambua matumizi ya mbinu ya usambambe. (al. 2)
f) Andika ubeti wa tano kwa lugha nathari. (al. 4)
g) Tambua idhini moja ya mtunzi. (al. 1)
h) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi. (al. 2)
   i) karatasi
   ii) nimesaki

## ***<u>SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI</u>***

8. a) Eleza maana ya ngomezi. (a. 2)

b) Fafanua sifa **nne** za ngomezi. (al. 8)

c) Eleza majukumu ya ngomezi. (al. 5)

d) Ungekuwa ukitafiti kipera cha ngomezi, ni changamoto zipi ungekabiliana nazo? (al. 5)

# FRIENDS SCHOOL KAMUSINGA

## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM

## Julai 2019

## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

**1.** Wewe ni mwanahabari katika shirika la Tangaza. Andika mahojiano kati yako na waziri wa Kilimo nchini kuhusu athari za baa la njaa na hatua zinazochukuliwa na serikali katika kukabili tatizo hili.

(alama 20)

**2.** Ufisadi umekita mizizi nchini Kenya. Jadili madhara yake huku ukipendekeza suluhu.

(alama 20)

**3.** Andika insha itakayothibitisha ukweli wa methali :

**Mchelea mwana kulia, hulia yeye.**

(alama 20)

**4.** Andika insha itakayomalizia kwa :

.... walipofungua mlango huo hatimaye wengi hawakuweza kuzuia hisia zao. Waliangua vilio kwa maafa waliyoyashuhudia.

(alama 20)

# FRIENDS SCHOOL KAMUSINGA

## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM

## Julai 2019

## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

**1. UFAHAMU**

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Ufisadi ni uhalifu unaohusu kuzitumia njia za ulaghai kujipatia pesa, mali au vitu hasa vya umma.

Nchini Kenya ufisadi hujitokeza kwa njia mbalimbali na kila mojawapo ina athari zake. Kwa mfano, kuna maafisa wa serikali wajipatiao pesa kwa kuuza stakabadhi za serikali kama vile pasi, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya kumiliki mashamba, vitambulisho na nyinginezo kwa raia, kuna hatari kubwa kwa sababu watu wasio raia wa Kenya wameweza kusajiliwa kama wakenya na kuendeleza uhalifu kamaugaidi, wizi na ulanguzi wa dawa za kulevya.

Wengine hujipatia vibali vya kufanya kazi na kuajiriwa kazi ambazo zingefanywa na wakenya.

Hii imechangia ongezeko la uhaba wa kazi nchini. Watumizi wengine wa umma huuza mali ya serikali kama vile magari, nyumba na ardhi na kufutika pesa za mauzo mifukoni mwao. Wengine wao hujinyakulia na kufanya vitu hivyo kuwa mali yao. Ufisadi wa aina hii umegharimu serikali kiasi kikubwa cha fedha. Serikali imelazimika kununulia maafisa wake magari baada ya muda mfupi, kulipia wafanyikazi wake kodi za nyumba na kukosa viwanja vya upanuzi na ujenzi wa shule hospitali, vituo vya polisi na taasisi zingine maalumu.

Baadhi ya wataalamu kama madaktari huiba dawa kutoka hospitali za umma kupeleka vituo vyao vya afya. Pia hutumia wakati wao mwingi katika kazi zao za kibinafsi na kuwaacha wagonjwa katika hospitali za umma wakihangaika. Sio madaktari tu, kuna masoroveya, wahandisi, mawakili, walimu na mahasibu ambao hukwepa **majukumu** yao serikalini na kufanya kazi za kibinafsi. Wengine wasio wataalamu huendesha biashara za aina tofauti, na huku wanaendelea kupokea mishahara.

Wanafunzi wanaotaka kujiunga na vyuo na shule bora za umma na hawakuhitimu wakati mwingine hulazimika kusalimu amri na kutoa hongo hili wapate nafasi za kusoma. Kiasi cha pesa kinachohitajika huwa kikubwa hivi kwamba ni wachache humudu hizo rushwa. Wale **wasiojimudu** kifedha hubaki **wakilia ngoa**. Kuna wazazi ambao hutumia vyeo vyao na 'undugu' kupata nafasi zilizotajwa, jambo ambalo huwanyima wanafunzi werevu kutoka jamii maskini nafasi ya kupata elimu. Matokeo huwa ni kuelimisha watu wasiostahili na ambao mwishowe hawaziwezi kazi wanazosomea wakihitimu na kuanza kuhudumia jamii.

Ufisadi **umekita** mizizi na **kushamiri** katika sekta za umma za kibinafsi kwa upande wa kuajiri wafanyakazi. Ni vigumu kupata kazi ikiwa hujui mtu mkubwa katika shirika linalohusika au uzunguke mbuyu. Matokeo ni kuajiri wafanyakazi wasiohitimu na wasiowajibika kazini.

Vyeo na madaraka katika baadhi ya mashirika hutolewa kwa njia ya mapendeleo na ufisadi. Kwa hivyo, wafanyakazi wenye bidii hufa moyo kwa sababu hawasaidiwi ipasavyo. Badala yake wale wasioleta bidii hupandishwa vyeo na kuwaacha palepale.

Hata hivyo, mbio za sakafuni huishia ukingoni. Serikali imetangaza vita dhidi ya ufisadi. Tayari tume kadhaa zimebuniwa kuchunguza visa vya ufisadi uliotekelezwa hapo mbeleni. Mojawapo ya tume hizo ni Tume ya kuchunguza **Kashfa** ya "Goldenberg" ambapo pesa za umma (mabilioni) ziliporwa na mashirika na watu binafsi kwa njia siziso halali. Watakaopatikana na hatia ya kushiriki ufisadi huo watahitajika kurudisha pesa hizo.

Serikali pia imeunda kamati ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi **waliohasiriwa** na mawakili walaghai ambao hupokea ridhaa kwa niaba ya wateja wao na kukosa kuwalipa au kuwatetea mahakamani ilhali wamekwishalipwa. Ni matumaini yetu kuwa ulaghai huu utaangamizwa kabisa kwani hakuna refu lisilokuwa na ncha.

**Maswali**

**a)** Eleza aina nne za ufisadi zilizotajwa katika kifungu ulichosoma. (alama 4)

**b)** Kulingana na kifungu ulichosoma,ufisadi umeathiri nchi yetu kwa njia gani ? (alama 2)

**c)** Serikali inafanya jitihada gani ili kukomesha ufisadi ? (alama 3)

**d)** Kwa maoni yako, unafikiri ufisadi husababishwa na nini ? (alama 2)

**e)** Toa msamiati mwingine wenye maana sawa na rushwa. (alama 1)

**f)** Eleza maana ya msamiati ufuatao kama ulivyotumiwa kifunguni: (alama 3)

i) shamiri

ii) waliohasiriwa

iii) wakilia ngoa

**2. MUHTASARI (ALAMA 15)**
**Soma taarifa ifuatayo kisha ujibu maswali uliyopewa.**

Taifa la Kenya limekuwa na tatizo la njaa kwa muda mrefu na hili ni tatizo ambalo hutokea mwaka baada ya mwaka. Kuna sababu kadhaa ambazo zimelifanya tatizo hili likithiri. Wananchi wengi hutegema ukulima kujipatia pato pamoja na chakula. Jambo hili limekuwa shida kubwa kwa vile kilimo hutegemea mvua isiyotabirika. Watabiri wa hali ya hewa huwashauri wakulima wapande mbegu zitakazohimili jua lakini mvua nayo inakuwa nyingi na kuharibu mimea.

Bidhaa za ukulima kama mbegu za kupanda, mbolea, dawa za kunyunyizia n.k, zimekuwa ghali. Kuna sehemu kubwa ya ardhi ambayo ni kame na haiwezi kutumika kwa kilimo. Mazao yanayotolewa shambani hayahifadhiwi vizuri. Mengine yanaharibikia shambani na mengine yanavamiwa na wadudu kiasi kwamba hayawezi kutumika.

Tatizo lingine ni vita vya kikabila. Kabila tofauti zinapopigana, watu huhama na kuacha mashamba ilhali wengine huchoma maghala ya chakula. Wafanyabiashara pamoja na serikali huwanunulia wakulima mazao yao kwa bei ya chini sana mpaka wanakosa shauku ya kuyashughulikia mashamba,yao. Siku hizi wakulima hawashughuliki tena kuzuia mmomonyoko wa udongo. Hivvo mvua inaponyesha rotuba yote inachukuliwa. Serikali haina sera mwafaka za kukabiliana na njaa. Hii ndiyo sababu sehemu zingine kama Turkana zimekabiliwa na njaa kwa muda mrefu.

Tatizo hili linaweza kutatuliwa ikiwa wakulima wataelimishwa juu ya mbinu bora za ukulima. Pia wakulima waishio katika sehemu ambazo hazina mvua ya kutosha wapewe mbegu ambazo zitahimili kiangazi. Ukulima wa kunyunyuzia mimea maji unafaa kuzingatiwa.Mazao yanayotolewa shambani yahifadhiwe vizuri kwa kuwekwa dawa za kuwaua wadudu.

Sehemu kubwa za ardhi ambazo hazitumiwi zitolewe kwa kilimo. Ni muhimu wakulima waelimishwe kuhusu jinsi ya kuzuia mmomonyoko wa udongo na umuhimu wake. Wakulima wanunuliwe mazao yao kwa bei nafuu ili wajibidiishe katika kazi yao. Serikali
inafaa iwe na sera mwafaka ili iweze kutatua tatizo hilo ambalo limekuwa ni janga kuu.

**a)** Fupisha aya tatu za mwanzo (maneno 70) (alama 8)

**b)** Fupisha aya mbili za mwisho. (Maneno 60 (alama 7)

**3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

**a)** Eleza tofauti kati ya sauti (alama 2)

i) | d |

ii) | t |

**b)** Andika maneno yenye miundo ifuatayo: (alama 2)

i) KKKI

ii) II

**c)** Andika katika umoja. (alama 2)
Machaka haya hayazai maua meusi

**d)** Andika kinyume cha sentensi ifuatayo: (alama 2)
Dada aliinama na akasimama ndani ya nyumba.

**e)** Tambua aina ya vishazi katika sentensi hii: (alama 2)
Ijapokuwa ni mgonjwa tutamwandalia karamu leo.

**f)** Bainisha matumizi ya 'ki' katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
<u>Ki</u>toto hiki kilinichezea <u>ki</u>jinga.

**g)** Tumia neno 'mle' kwenye sentensi kama : (alama 3)
i) kivumishi
ii) kiwakilishi
iii) kielezi

**h)** Andika katika ukubwa. (alama 2)
Kiti kilichokuwa kimebebwa na mvulana kilivunjika.
**i)** Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo: (alama 3)
Atieno alijengewa nyumba na mamake kwa matofali.

**j)** Changanua sentensi hii kwa kutumia mtindo wa jedwali. (alama 4)
Wanafunzi wageni waliofika shuleni mapema walibeba vitabu vingi ajabu.

**k)** Eleza maana ya dhana ya chagizo kisha uonyeshe kwa kupigia mstari chagizo katika sentensi ifuatayo. alama 2)
Mkuliwa hodari zaidi atatuzwa kwa bidii yake.

**l)** Kwa kutoa mifano katika sentensi, onyesha matumizi mawili ya kistari kifupi. (alama 2)

**m)** Andika katika usemi halisi. (alama 3)
Mwalimu aliwasisitizia wanafunzi kuwa kulikuwa na umuhimu kuwatii wazazi wao kwani hilo lingeongeza siku zao duniani.

**n)** Tunga sentensi sahihi ukitumia hali ya 'a' isiyodhihirika. (alama 2)

**o)** Ainisha vitenzi katika sentensi ifuatayo:
Wazazi walikuwa wangali harusini. (alama 2)

**p)** Tumia o-rejeshi badala ya amba-
Wachezaji ambao hucheza kwa bidii ndio ambao hufaulu maishani. (alama 2)

**q)** Nyambua kitenzi 'ja' katika kauli ya kutendewa. (alama 1)

**r)** Nimenunua dawa ili iwamalize wadudu wanaotusumbua hapa kwetu nyumbani. (alama 2)
Aanza: Wadudu ............

**4. ISIMUJAMII**
"Anachukua mpira, kisigino anatuliza, kengeuka, kulia, kushoto, hesabu wa kwanza tesa wa pili,baki peke yake na goalkeeper.
**a)** Taja sajili inayorejelewa na maneno haya. (alama 2)
**b)** Fafanua sifa za sajili hii. (alama 8)

# FRIENDS SCHOOL KAMUSINGA
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

**SEHEMU A : USHAIRI**

1. **Soma shairi lifuatalo kwa makini kisha ujibu maswali.**

Niokoa Muokozi, uniondolee mashaka
Kuyatukua siwezi, mjayo nimedhikika
Nimekithiri simanzi, ni katika kuudhika
Mja wako nasumbuka, nipate niyatakayo

Mja wako nasumbuka, nataka kwao afua
Nirehemu kwa haraka, nami nipate pumua
Naomba hisikitika, na mikono hiinua
Mtenda ndiwe Moliwa, nipate niyatakayo

Mtenda ndiwe Moliwa, we ndiwe Mola wa anga
Mazito kuyaondoa, pamoja na kuyatenga
Ukauepusha ukiwa, ya pingu zilonifunga
Nikundulia muwanga, nipate niyatakayo

Muwanga nikundulia, nipate toka kizani
Na huzuni n'ondolea, itoke mwangu moyoni
Mambo mema niegheshea, maovu nisitamani
Nitendea we Manani, nipate niyatakayo

Igeuze yangu nia, dhaifu unipe mema
Nili katika dunia, kwa afia na uzima
Moliwa nitimizia, yatimize yawe mema
Nifurahike mtima, nipate niyatakayo

**a)** Shairi hili ni bahari gani ? Eleza. (alama 2)
**b)** Taja madhumini ya shairi hili. (alama 3)
**c)** Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
**d)** Thibitisha namna uhuru wa kishairi unaibuka katika shairi. (alama 4)
**e)** Andika ubeti wa pili katika lugha nathari. (alama 4)
**f)** Toa maana ya :
i) Nimedhikika
ii) Muwanga nikundulia
iii) Nifurahike mtima (alama 3)

**SEHEMU B : RIWAYA**

**Assumpta K. Matei : Chozi la heri**

**Jibu swali la 2 au la 3**

**2.** "Vipi, binadamu anavyoweza kuyazoa maji yaliyomwagika?"

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

**b)** Tambua mbinu ya lugha iliyotumika. (alama 2)

**c)** Jadili sifa tatu za msemaji. (alama 3)

**d)** Hakiki jinsi binadamu alivyomwagikiwa na maji katika riwaya. (alama 11)

**Au**

**3.** Fafanua changamoto zinazoikabili jinsia ya kike katika riwaya ya Chozi la Heri. (alama 20)

**SEHEMU C : TAMTHILIA**

**Pauline Kea : Kigogo**

**Jibu swali la 4 au la 5**

**4.** "Ukitaka kuwafurusha ndege, kata mti. Hawa wangekuwa sasa wametuliza nafsi zao.

**a)** Eleza muktadha wa kauli hii. (alama 4)

**b)** Tambua mbinu mbili za uandishi zilizotumika. (alama 4)

**c)** Onyesha jinsi wahusika kadhaa walivyofurushwa kama ndege. (alama 12)

**Au**

**5.** Tamthilia ya Kigogo ni taswira kamili ya matatizo yanayokumba mataifa mengi barani Afrika. Fafanua ukirejelea tamthilia nzima. (alama 20)

**SEHEMU D**

**Alifa Chokocho na Dumu Kayanda: Tumbo Lisiloshiba na Hadithi nyingine**

**Jibu swali la 6 au la 7**

**6.** Ukirejelea hadithi zifuatazo, eleza jinsi maudhui ya mapenzi na asasi ya ndoa yanavyojitokeza.

(alama 20)

**a)** Mapenzi ya Kifaurongo

**b)** Masharti ya Kisasa

**c)** Ndoto ya Mashaka

**d)** Mtihani wa Maisha

**Au**

**Shibe inatumaliza : Salma Omar Hamad**

**7.** "Hiyo ni dharau ndugu yangu. Kwa nini kila siku tunakula sisi kwa niaba ya wengine ?"

**a)** Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

**b)** Eleza sifa za msemaji. (alama 6)

**c)** Eleza jinsi viongozi wanavyokuwa wabadhirifu. (alama 10)

**SEHEMU E : FASIHI SIMULIZI**

**8. a)** Miviga ni nini ? (alama 2)

**b)** Fafanua sifa zozote sita za miviga. (alama 12)

**c)** Miviga ina majukumu yapi katika jamii ? (alama 6)

# NAIROBI SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

1. Hivi karibuni kumekuwa na visa vya wawaniaji wa nyadhifa mbalimbali kulalamika kuhusu matokeo ya uchaguzi. Wewe ni mwanahabari katika shirika la utangazaji la Tabasamu. Andika mahojiano kati yako na mwenyekiti wa Tume Huru yauchaguzi na mipaka kuhusu vyanzo vya malalamishi haya na namna yakusuluhisha tatizo hili.

   (Al. 20)

2. Kutoka na na ongezeko la visa vya ukosefu wa usalama, eleza namna usalama unavyoweza kuimarishwa nchini

   (Al. 20)

3. Andika kisa kitakachodhihirisha ukweli wa methali 'Mkokoto wa jembe si bure yao' (Al. 20)

4. Kamilisha kwa maneno haya …wote waliokuwepo waliinama na kuvitikisa vichwa vyao, kisha wakaviinua na kukubaliana kwakauli moja kuwa vijana wanastahili kushirikishwa katika ujenzi wa taifa

   (Al. 20)

# NAIROBI SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

**1. UFAHAMU** **(ALAMA 5)**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali**

Ilikuwa siku ya Jumapili moja yalipotokezea mambo hayo. Kwa kawaida, Jumapili ni siku yangu ya kupumzika. Siku ya kuachana na vitabu na shughuli nyingine za masomo baada ya kazi ngumu za juma zima. Nilihisi **nastahiki** kupumzika, anagalau siku moja kwa wiki. Nipumzike kwa kufanya nililopenda.

Kwangu mimi kupumzika kulikuwa na maaana tofauti na maaana ya kupumzika kwa watu wengine. Kupumzika kwangu mimi ni kuwasaidia wazazi wangu kuchunga ng'ombe na mbuzi ili nipate fursa ya kuweko vichakani peke yangu. Nipate kuwa karibu na maumbile. Niwe karibu nayo huku nimetulia kimya huku natazama mandhari na maumbile ya kijiji chetu.

Mara nyingine hali hii ya utulivu wa maumbile hunifanya niimbe kwa sauti ya juu au kimyakimya. Pengine husinzia hapo na kuota ndoto za hamu yangu. Kuota baadaye yangu na mema ninayojitakia. Naam, haya yote ndiyo yaliyokuwa na maana ya kupumzika kwangu. Yote haya na zaidi ya haya ambayo nitayataja baadaye.

Leo lakini, kinyume na unavyodhani wewe, nilikuwa nimejaa mchanganyiko wa huzuni na furaha wakati mmoja. Kule mwituni nilikokuwa nikichunga ng'ombe, kumbe sikufuatwa **kuposwa** kama nilivyofikiri. Nilifutwa ili kumwonyesha yule mteja mifugo aliyotaka kununua. Baba na mama waliamua kuwauza wanyama wetu wote hatimaye. Baba alisema kuwa mjomba Kasimu, aliyefariki miezi sita iliyopita, ameacha kibanda huko jijini. Na yeye baba na mama wameamua kuenda kuishi huko jijini ili wanipe fursa ya kusoma na kuelimika zaidi, Sasa nadhani utaweza kufahamu maana ya mchanganyiko wangu wa huzuni na furaha. Furaha, kwa sababu ndoto yangu imeitikiwa hatimaye. Yale maombi yangu niliyoyaomba karibu na mbingu yamekubaliwa. Sasa niko tayari kwenda jijini kutimiza wajibu wangu.Kwenda kuikabili kazi ngumu. Kuitumia fursa hiy ya kusoma na kujielimisha zaidi kuliko huku kijijini. Niko tayari kusoma na kujituma kwa bidii zangu zote ili nifike **ukomo** wa masomo yote ni nayoweza kufikia.

Kwa upande mwingine lakini, nilikuwa mzito kuondoka kwa sababu nyingi. Kwanza, kwa jinsi nilivyokipenda kijiji chetu. Pili, sikuwa tayari kutengana na wale mifugo wetu ambao kwa muda mrefunimefanya urafiki nao. Leo ghafla wamenunuliwa na kuchukuliwa na mtu mwingine. Nilihitaji muda mrefu kuweza kuwasahau.Kama ningeweza kamwe. Tatu, niliona aibu, na aibu zikanitia huzuni kwa kuwafikiria vibaya wazazi wangu. Kwa nini niliweka
mbele hamu yangu tu?Kwa nini nilionyesha ubinafsi wangu tu? Kwa nini nilisahau mapenzi na ahadi ya watu hawa wanaonipenda kuliko kitu chochote? Kwa nini niligeuka haini mara
moja bila ya kufikiri. Kwa nini sikutaka hata kusadikisha ukweli au uongo wa ile fikira ya posa?

(*Kutoka kwa**Vipawa vya Hazina**, na Said A Mohamed, OUPEA.*)

**Maswali**

a) Ipe taarifa hii kichwa mwafaka (al. 1)
b) Taja msimulizi wa habari hii (al. 1)
c) Msimulizi anasema ya kwamba kupumzika kwake na kwa watu wengine kulikuwa tofauti, dhihirisha. (al. 2)
d) Kulingana na kifungu, utulivu anaoudai mwandishi ulikuwa na faida gani kwake(al. 2)
e) Fafanua hasara mbili za msimulizi kuhamia mjini (al. 4)
f) '…sasa niko tayari kwenda jijini kuitimiza wajibu wangu. Kwenda kuikabili kazi ngumu…' Msimulizi alimaanisha nini aliposema haya. (al. 2)
g) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu (al. 3)
i) nastahiki
ii)kuposwa
iii)ukomo

**2. <u>UFUPISHO</u> (ALAMA 15)**

**Soma makala yafuatayo kasha ujibu maswali**

Maradhi ya kipindupindu yameendelea kuripotiwa katika sehemu mbalimbali nchini. Kufikia sasa watu zaidi ya sita wameripotiwa kufariki na wengine zaidi ya mia tatu kulazwa hospitalini. Maradhi haya yamebainika kuchangiwa na maji ama chakula chenye vidudu vya kolera. Hujitokeza kwa mtu kuharisha majimaji na pia kutapika.
Hii si mara ya kwanza kwa Kenya kushuhudia maradhi haya na yameonekana kujitokeza zaidi katika miaka ya hivi punde. Kati ya Desemba 2014 hadi Januari 2016, visa zaidi ya elfu kumi na moja vya kipindupindu viliripotiwa huku kukiwa na vifo mia moja sabini na nane kote nchini.
Kufikia Aprili 2016, visa 1,629 vilikuwa vimeripotiwa na vifo 18 kutokea Mandera. Chama cha madktari humu nchini. Kimeripotiwa kusema kuwa kunapoanza kutokea mikurupuko ya maradhi kama hayo ni ishara ya mfumo wa matibabu kuwa na kasoro. Maradhi haya yameonekana pia kuwa changamoto kuu na watafiti kuhofia kuwa baadhi ya viini vyake hasa Nairobi ni sugu, havitibiki na dawa zilizopo na vimewahi kuchangia vifo vingi katika mikurupuko iliyotokea Haiti, Rwanda na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo. Wahusika wakuu katika masuala ya afya ya umma walionekana kusita mwanzoni kujitokeza wazi na kuanza kukabiliana na tatizo hilopamoja na kurushiana lawama.
Hata hivyo ni muhimu kwa wanaohusikana afya ya uma pamoja na matibabu kuchukua hatua zinazostahili mapema na sio wakati wote kusubiri mukurupuko kuanza kutaka kuonekana kuwa wako kazini.

Wanapaswa kujua kama wanaopika kando ya barabara na kwenye vibanda wamechunguzwa kiafya kupikia watu.
Tunatoa wito kwa wananchi wasisubiri serikali bali na wao wachukue hatua ya kukabiliana na ugonjwa huu. Lazima wajali kuhusu maisha yao pamoja na kuwajali wengine,
Kuna watu ambao wamekuwa wakiuza mboga kwa kutumia maji ya maji taka na kuna wanaoendesha biashara za maji, ambayo huyachota kutoka sehemu zisizo salama na kisha kuyauzia wengine wasiokuwa na habari bila kujali madhara wanayoeneza kwa wengine.

Juhudi za kila mmoja zinahitajika kukabiliana na kipindupindu na watakaogundua ishara watafute tiba mara moja badala ya kujitibu kama ilivyo desturi kwa wengi hadi wanapozidiwa.
*(Taifa Leo Jumatano Julai 26, 2017)*

**Maswali**
a) Bila kupoteza maana, fupisha aya tatu za mwanzo (maneno 60-69) (al. 7, utiririko 3)

b) Kulingana na aya tatu za mwisho, ni hatua zipi ambazo zinaweza kuchukuliwa kuzuia ugonjwa huu hatari wa kipindupindu (maneno 50) (al. 5)

**3. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (ALAMA 40)**
a i) Andika vigezo viwili vya kuianisha konsonanti (al. 2)

ii) Tofautisha /sh/ na /ch/ (al. 1)

b) Tumia kiimbo katika sentensi mbili tofauti sahihi kudhihirisha uamilifu wake(al. 2)

c) Eleza maana za maneno yafuatayo kwa kuzingatia mahali ambapo shadda imewekwa (al. 2)
'ala
a'la
d) Fafanua dhana ya sauti mwambatano kwa kutolea mfano sahihi (al. 2)

e) Bainisha majukumu ya viambishi katika fungutenzi hili:
nimsubiriaye (al. 2)

f) Weka nomino hizi katika ngeli mwafaka
i) debe ………………………………………………………………… (al. 1)
ii) mtaimbo ……………………………………………… (al. 1)
g) Yakinisha
Mgonjwa yule hasikii wala kusema lolote (al. 2)

h) Andika kwa ukubwa wingi
Panya huyo alinaswa mtegoni na nyama kubwa mdomoni (al. 2)

i) Geuza katika kauli iliyo kwenye mabano
i) Wanyama wa pori huwavutia watalii (tendwa) (al. 1)

ii) Viota hivyo vya ndege vilivamiwa na wadudu (tenda) (al. 1)

j) Andika katika usemi halisi (al. 3)
Daktari alitaka kujua kama kulikuwa na jamaa wake yeyote ambaye alikuwa ameugua ugonjwa huo

k) Tumia kiwakilishi cha pekee chenye kuleta dhana ya msisitizo katika sentensi sahihi (al. 2)

l) Changanua kwa njia ya jedwali
Waswahili husema chema chajiuza, kibaya chajitembeza (al. 4)

m) Andika sentensi upya kulingana na maagizo (al. 2)
Ongezeko la visa vya uhalifu linatishia kuangamiza amani katika miaka ya hivi karibuni.( anza Amani…)

n) Tunga sentensi moja kwa kutumia kirai kihusishi kisha upigie mstari (al. 2)

o) Bainisha vishazi
Tangu awasili kutoka Marekani amewasaidia mayatima wengi (al. 2)

p) Eleza matumizi mawili ya alama ya mkato (al. 2)

q) Onyesha shamirisho na chagizo katika sentensi ifuatayo (al. 3)
Mwanamwali alirembeshwa nyusi kwa wanja taratibu

r) Kamilisha methali ifuatayo (al. 1)
Mfamaji haachi

**4. <u>ISIMU JAMII</u> (ALAMA 10)**

a) Taja mambo **matatu** yanayopelekea kufifia na kufa kwa lugha (al. 3)

b) Isimujamii ina umuhimu gani kwa mwanafunzi wa shule ya upili (al. 4)

c) Andika sifa **tatu** za lugha utakayotumia kuwatangazia watu kuhusu kinyang'anyiro cha soka (al. 3)

# NAIROBI SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

**SEHEMU A. SWALI LA LAZIMA RIWAYA: CHOZI LA HERI**

**1**."Lakini itakuwaje historical injustice,nawe Ridhaa,hapo ulipo sicho kitovu chako?"

a) Eleza muktadha wa dondoo. (alama 4)

b) Eleza tamathali mbili za lugha zilizotumika kwenye dondoo hili. (alama 4)

c) Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya. (alama 6)

d) Ni mambo gani yaliyo wakumba wale ambao sio wa kitovu kinachorejelewa. (alama6)

**SEHEMU B HADITHI FUPI:TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

**2**. " Usiteketeze umati kama kuni zinavyoteketeza moto. Rudi,rudi kwa Mola wako."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama4)

b) Fafanua sifa za msemewa. (alama6)

c) Tambua tamathali ya usemi iliyotumika hapo juu. (alama2)

d) Ni kwa nini msemewa anatakikana kurudi kwa Mola wake? (alama8)

**AU**

**3**. Huku ukirejelea hadithi ya Tumbo Lisiloshiba na Shibe Inatumaliza, fafanua maudhui ya ukiukaji wa haki. (alama20

**SEHEMU C. TAMTHILIA: KIGOGO**

**4**. "Oooh bebi, miaka yaenda mbio sana, nayo sura yako inachujuka……"

a) Weka dondoo hili katika muktadha wake.

(alama4)

b) Mhusika anayehusishwa na wimbo huu ana msimano gani wa kimapinduzi?

(alama 8)

c) Taja sifa zozote nane za muhusika huyu.

(alama8)

**AU**

**5**. Tamthilia ya 'Kigogo' ni kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika.Thibitisha. (alama 20)

## SEHEMU D: USHAIRI.

5. Lisome shairi lifuatalo kisha uyajibu maswali yaliyoulizwa.

**WENYE VYAO WATUBANA**

1. Wenye vyao watubana, twaumia maskini,
La kufanyiza hatuna, hali zetu taabani.
Kwa sasa kilo va dona, bei mia ishirini,
Wakubwa tuteteeni, wenye vyao watubana.

2. Washindana matajiri -kwa bei siyo utani,
Na pigo kwa mafakiri tunao hali ya chini,
Wazeni kutafakari, wanyonge tu madhilani,
Wakubwa tuteteeni,wenye vyao watubana

3.Limekuwa kubwa zogo, hakuendeki madukani.
Fungu moja la muhogo, sasa shilingi miteni,
Huo mkubwa mzigo , watulemaza kichwani,
Wakubwa tuteteeni ,wenye vyao watubana.

4. Si hichi wala si kile, hakuna cha afueni,
Bei imekuwa ndwele, wenye macho lioneni
Ukiutaka mchele, pesa jaza mfukoni,
Wakubwa tuteteeni ,wenye vyao watubana.

5. Waliko hao samaki, huko ndiko uchawini.
Wachuuzi hawacheki , zimewatoka huzuni,
Vibuwa havishikiki, kimoja kwa hamsini,
Wakubwa tuteteeni , wenye vyao watubana.

6. Maisha yetu viumbe ,yamekuwa hilakini,
Vvenye vyao kila pembe ,wametukaa shingoni,
Nyama ya mbuzi na ng'ombe, sasa hali maskini,

Wakubwa tuteteeni wenve vyao watubana.

7. Maji vamezidi unga, kwa lodi wadarajani,
Kajitolea muhanga, kwa bei hawezekani,
Mvao wake wa kanga, ni shilingi elifeni
Wakubwa tuteteeni,wenye vvao watubana.

***Maswali;***

a) Fafanua toni ya shairi hili. (alama2)

b) Nini dhamira ya nafsi neni ? (alama2)

c) Andika ubeti wa sita kwa lugha tutumbi. (alama4)

d) Fafanua kwa kutoa mfano mbinu moja aliyotumia mshairi kutosheleza mahitaji ya arudhi katika shairi hili. (alama2)

e) Taja na ueleze bahari mbili za shairi hili ukizingatia. (alama4)
i) Vipande
ii) Vina

f) Taja kwa kutoa mifano katika shairi hili hadhira tatu lengwa. (alama6)

**SEHEMU E : FASIHI S1MULIZ1**

7.(a) (i) Ngano ni nini? (alama1)

(ii) Eleza tofauti iliyoko kati ya visasili na visakale. (alama2)

(iii) Fafanua umuhimu wa ulumbi katika jamii. (alama5)

(b)(i) Eleza umuhimu wa vitendawili katika jamii. (alama5)

(ii) Tega na utegue vitendawili vyovyote viwili vilivyo na lugha ya takriri na lugha ya mlio. (alama4)

(iii) Taja sifa zozote tatu za methali. (alama3)

# MOI GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

1. Wewe ni balozi mteule wa nchi yako katika nchi ya kigeni. Andika tawasifu utakayotoa katika siku ya kutoa stakabadhi zako kwa rais wa nchi uliyoteuliwa kuwa balozi.

2. Utumizi wa afyuni [mihadarati} katika taasisi za masomo nchini ni suala ambalo ni muhali kutatuliwa. Jadili.

3. Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mwenye kovu usidhani kapoa.

4. Andika kisa kitakachomalizikia kwa: ... hivyo ndivyo ukurasa mpya katika kitabu cha maisha yangu ulivyofunguka.

# MOI GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

**Sehemu A: Ufahamu**

**Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali yafuatayo**

Halmashauri ya mpwito nchini imetoa mwongozo kuhusu majukumu yanayofaa kutekelezwa na serikali za kaunti kote nchini kuanzia Julai mosi mwaka huu.

Mwongozo huo utasaidia kuondoa wasiwasi ambao baadhi ya mashirika yasiyo ya serikali yalielezea kuwa huenda baadhi ya sekta zizipate ufadhili kutokana na utata kuhusu ni serikali ipi inafaa kuzishughulikia.

Shughuli hizi zinajumuisha kilimo ambapo zitahakikisha maendeleo ya mimea, mifugo na uvuvi. Serikali za kaunti pia zitashughulikia huduma za afya kuhakikisha kuna sawa na vifaa vya kutosha katika zahanati na hospitali.

Uhifadhi wa mazingira na tamaduni za kijamii kama vile makavazi, maktaba na majumba ya burudani vilevile zitakuwa chini ya usimamizi wa kaunti.

Serikali hizo pia zitasimamia masuala ya uchukuzi kwa kushughulikia ukarabati wa barabara, taa za kudhibiti msongamano wa magari na bandari.

Kulingana na taarifa iliyochapishwa kwenye vyombo vya habari, serikali hizo pia zitashughulikia maendeleo ya biashara na vyama vya ushirika.

Serikali za kaunti zitajihusisha na kudhibiti mipaka na matumizi ya kawi, elimu ya chekechea na vyuo vya ufundi katika ngazi za vijijini, taarifa hiyo ilisema.

Halmashauri hiyo ilisema kuwa serikali hizo zitasimamia uhifadhi wa masitu, ardhi, huduma za maji kupambana na mikasa ya moto, sawa za kulevya na picha za ngono.

Taarifa hiyo iliyotiwa sahihi na mwenyekiti wa halmashauri ya Mpwito ilisema pia serikali za kaunti zinapaswa kuhakikisha kuwa umma umeshirikishwa katika usimamizi wa rasilimali za vijiji.

Kulingana na kipengee cha 15 cha katiba ya Kenya, binge la kitaifa katika muda usiopita miaka mitatu kutoka Siku ya uchaguzi linahitajika kuunda sheria za kuhakikisha kuwa serikali za kaunti zimepata uwezo wa kuendeleza shughuli zake.

Aidha kipengee cha 23 kuhusu ugatuzi kinahitaji halmashauri ya mpwito kutambua shughuli zitakazo tengewa serikali za kaunti kutoka serikali kuu punde to baada ya uchaguzi mkuu. Shughuli hizo zilitayarishwa kupitia hati ya sheria nambari 16 ya 2013.

Katiba katika kipengee cha 24 inatoa masharti ya kufuatwa kabla serikali za kaunti kuanza rasmi shughuli zake za kutoka huduma kwa wananchi.

**Maswali.**

1. Yape makala haya kichwa mwafaka. (Alama 1)

2. Je, kaunti inawajibikaje katika kuwahudumia wananchi? (Alama 2)

3. Utawala wa kaunti unaweza kupunguza vipi maafa yanayotokea kutokana na mapuuza ya mwanadamu? (Alama 3)

4. Bunge la kitaifa lina wajibu gani katika serikali ya kaunti? (Alama 2)

5. Ni changamoto zipi zinazoweza kukabili suala la ugatuzi nchini? ( alama 3)

6. Ni kwa njia gani serikali ya kaunti inaweza kufufua uchumi wa nchi na kuinua kiwango cha maisha ili kufikia ruwaza ya 2030. ( alama 2)

Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika ufahamu. (alama 2)
a.) uchukuzi
b.) ugatuzi

**SEHEMU B : UFUPISHO**

Miezi mitano iliyopita,serikali ya kitaifa na zile za kaunti ziliwasilisha makadirio yao ya bajeti,miezi miwili kabla ya mwaka wa kifedha kuisha kama zinavyohitajika na katiba.

Serikali hizo zilieleza jinsi zinavyonuia kutumia mabilioni ya pesa kufadhili shughuli zao mwaka ujao was kifedha was 2017 / 2018.
Serikali ya Raid Uhuru Kenyatta ilisema itatumia shilingi 1.6 trilioni kufadhili maendeleo na shughuli za sekta na idara zake tofauti. Makadirio haya ambayo yaliwasilishwa na kiongozi was kitita hicho kitakavyopatikana. Nasema hivi kwa sababu kuna habari ambazo zimenipa
tumbojoto na wasiwasi mkubwa. Imebainika kuwa kufikia mwishoni mwa Machi mwaka huu, Kenya ilikuwa inadaiwa shilingi 1.8 trilioni na wafadhili was humu nchini na wa kigeni.

Kama habari hizi hazijakushtua sitakulaumu kwa sababu huenda ukawa hujui ukubwa wa kiasi hiki cha fedha. Ili uweze kuelewa, nitazigawanya fedha hizi miongoni mwa wakenya milioni 40 ili tujue kila mkenya anadaiwa kiasi gani. Kila mkenya nchini, wakiwemo watoto na wazee wakongwe, anadaiwa shilingi 45,000! Hivyo basi ili deni hili liweze kulipwa, kila mkenya atalazimika kutoa kiasi hicho cha fedha.
Ni deni ambalo Rais Uhuru Kenyatta alirithi kutoka kwa mtangulizi wake,Rais Mwai Kibaki ambayo utawala wake ulivunja rekodi ya kukopa. Wahenga hawakukosea waliposema dawa ya deni no kulipa. Deni hili linapaswa kumkosesha usingizi Rais Kenyatta ambaye anapaswa kutafuta njia za kulilipa bila kuathiri uchumi, maendeleo na utekelezaji was ahadi nyingi alizowapatia wakenya wakati wa kampeni.

Hili halitafanyika kama serikali itatenga fedha nyingi kuwalipa maafisa wake mishahara na marupurupu minono pamoja na kuwapa mabilioni ya pesa kununulia magari ya kifahari.

Pengine rais hajafahamishwa kuwa mwaka ujao was kifedha serikali itajipata pabaya kwani Halmashauri ya Ukusanyaji ushuru nchini (KRA), haitaweza kukusanya kiwango kilichowekewa na serikali baada ya shughuli ya ukusanyaji ushuru kutatizwa na hofu iliyotanda wakati was uchaguzi mkuu.
KRA ilikuwa imekusanya shilingi 560 bilioni kufikia mwishoni mwa mwaka ilhali ilikuwa imeagizwa kukusanya shilingi 881 bilioni.
Serikali za kaunti, ambazo zingali changa, zimependekeza kutumia mabilioni ya fedha ambazo hazitaweza kukusanya. Badala yake zimeiomba serikali kuu ijaze pengo hilo au zipewe idhini ya kukopa.
Rais Kenyatta hana budi kuchukua hatua za dharura kuhakikisha kuwa wakenya hawataendelea kuandamwa na madeni maishani mwao.

***(Imenukuliwa kutoka Taifa Leo- Mei 9,2017)***

**MASWALI**

a) Kwa maneno yasiyozidi 70, fupisha aya za kwanza nne. (alama 10)

b) Kwa nini serikali haitaweza kulipa madeni yake.(maneno 40-50) (alama 5)

**C. MATUMIZI YA LUGHA**

a) Linganisha sauti /o/ na /w/. ( alama 2)

b) Eleza maana ya silabi funge na utoe mfano mmoja wa neno na uiibainishe. ( alama 2)

c) Eleza miundo miwili ya nomino katika ngeli ya U-ZI na utoe mfano mmoja wa kila muundo. (alama 2)

d) i) Eleza maana ya kiambishi. ( alama 1)
ii) Ainisha viambishi katika neno hili: (alama 3)
humfisha

e) Tunga sentensi iliyo na muundo ufuatao: ( alama 3)
KN(W+V+E)+KT(T+KE)

f) Andika katika usemi wa taarifa. ( alama 2)
"Sitakuja shuleni kesho." Asha alisema.

g) Tunga sentensi moja ukitumia kiwakilish kiashiria cha karibu katika ngeli ya KU-KU.
(alama 2)

h) Tunga sentensi moja moja kwa kila jozi kubainisha maana ya maneno yake. ( alama 2)
sima /zima
dada /tata

i) Eleza maana mbili za sentensi hii. ( alama 2)

Mwanafunzi alimwendea mwalimu ofisini.

j) Unda aina za nomino zilizo mabanoni kutokana na maneno uliyopewa. ( alama 2)

i. refu (kitenzi jina)

ii. erevu (dhahania)

k) Tunga sentensi **moja** katika wakati uliopita hali ya kuendelea. (alama 2)

l) Yakinisha sentensi ifuatayo katika wingi. (alama 2)

Nisipomlipa pesa zake, hataniamini tena wakati ujao.

m) Akifisha sentensi hii. ( alama 3)

labeka maria alimjibu mamake nisubiri hadi alhamisi

n) Bainisha aina za vitenzi katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Wewe ulikuwa ukifunga mabao mengi kwa sababu u mchezaji bora.

o) Andika sentensi ifuatayo upya katika hali ya mazoea. ( alama 2)

Nguo zinazochafuka ndizo zinazofuliwa.

p) Eleza matumizi ya "po" katika sentensi ifuatayo. ( alama 2)

Ali**po**ona ali**po**keti palikuwa na vumbi, alisimama.

q) Tambua na ueleze aina za virai katika sentensi hii. (alama 2)

Mama mzee alikuwa anatabasamu.

r) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli ya kutendeshwa. (alama 1)

i) la

ii) nywa

## D. ISIMU-JAMII (ALAMA 10)

(a) Eleza **maana** ya lugha (alama 1)

(b) Andika sifa **nne** za lugha. (alama 4)

(c) Eleza sifa **tano** za sajiri ya maabadini. (alama 5)

# MOI GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM
## Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

**RIWAYA: CHOZI LA HERI**

**LAZIMA**

1. **.Fafanua ufaafu wa anwani Chozi la Heri** **(alama 20)**

**SEHEMU YA B**

***Tamthilia : Kigogo ; Pauline Kea***

***(Jibu Swali la 2 au 3)***

1. "Ukitaka kuwafurusha ndege, kata mti"
   (a) Weka dondoo hili katika muktadha wake (alama 4)
   (b) Onyesha mbinu nyingine zinazotumiwa na wahusika Hawa kutimiza malengo yao. (alama 16)

2. Tamaa na ubinafsi zinaathari kubwa kwa jamii ukiirejelea tamthilia ya kigogo ; Jadili. (alama 20)

**SEHEMU C**

**Diwani Tumbo lisiloshiba na Hadithi Nyingine; Alifa Chokocho na Damu Kayanda (Wahariri)**

***(Jibu Swali la 4 au 5)***

3. "Ingawa vingi , sauti havina sauti zavyo zinamezwa tu na mipumuo……………."
   (a) Eleza muktadha huu (alama 4)
   (b) Fafanua 'mipumuu' inayorejelewa katika dondo hili. (alama 16)

4. Shibe inatumaliza; Salma Omar
   (a) Jazanda ni mbinu mojawapo ya mbinu za lugha ziizotumiwa kwa ukamilifu. Ukirejelea hadithi shibe inatumaliza fafanua mifano kumi. (alama 10)
   ***Mame Bakari*** Mohammed Khelef

   (b) Athari za ubakaji ni donda sugu katika jamii. Thibitisha kauli hii kwa mujibu wa hadithi hii. (alama 10)

**SEHEMU YA D:**
**USHAIRI**

**JIBU SWALI LA 6 AU LA 7**

**SOMA SHAIRI HILI KISHA UJIBU MASWALI YANAYOFUATA**

Ndege mwema na muruwa, katu haishi tunduni
Hataki kufadhiliwa, muda yumo utumwani
Japo mnyonyoe mbawa mwisho wake atahuni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa.

Ndege ataka yoyoma, nasiyahi msituni
Apite akisimama, shinani na mitawini
Haridhiki kwa mtama, na maji ya kikombeni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mwema wa hishima mwema mno wa kughani
Tundu huliona chama, japo liwe la thamani
Huporomosha yakwe kima, na kufanya faraghani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mpambe kwa zari, na lulu na marijani
Upambe yake suduri, kwa almasi kidani
Tunduni atahajiri, ili awe huriani

Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege mwema wa busara, hatoishi kifungoni
Anayo kubwa hasara, kukosa nyumba ya mani
Lamkera lamkera, tundu la dhahabu kwani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Ndege maumbile yake, na waja hayalingani
Yeye hutaka wenzake wafukuzane hewani
Jambo la kuishi mpweke, kamwe humridhiani
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

Baiti zangu ni haba, nakonea kituoni
Ndege huficha mahaba, kama yumo kifungoni
Hali ndege akashaba, kwani yumo adhabuni
Ndege kuishi tunduni, ni nguvu amezidiwa

**Maswali**

(a) Lipe shairi anwani mwafaka (alama 1)
(b) Fumbua maana ya ndege anayerejelewa (alama 1)
(c) Shairi hii ni la mkondo gani? (alama 3)
(d) Eleza muundo wa ubeti wa nne (alama 3)

(e) Fafanua uhuru aliotumia mshairi (alama 4)
(f) Andika ubeti wa tatu kwa lugha ya nathari (alama 4)
(g) Jadili dhamira ya mshairi (alama 2)
(h) Fafanua maana ya msamiati ufuatao kama ilivyotumiwa na mshairi
i) Atahuni
ii) Baiti

7. **Soma shairi hili kasha ujibu maswali yanayofuatia**

**MKULIMA**

Mtazameni ………nguzo ya Afrika
Mtumwa wa watumwa walioridhiya!

Amekita jembe lake akilisujudia
Kwa tambo liloumbuka na kuselehea
Uso ukifuka ukata ulojifanya tabia
Na machungu ya maonevu alovumilia

Moyo wako mzito *ulokokomaa* kama kuni
Haujui tena kutarajia wala kutamani
Unakufa ganzi, kutohisi raha wala huzuni

Basi iteni fikira mambo mukiyafikiri
*Siku hamaki yake itapochafuka kama bahari*
Siku ukweli wa hali yake utapodhihiri
Umejiandalia vipi…

Huo mkono ulomuumbua na kumkausha
Hizo pumzi zilomzimia taa ya maisha
Kumfunga kizuizi, gizani kumtowesha?

Ni jawabu gani alowekewa na wakati
Kuipoza ghadhabu ya kiu ingawa katiti
Kuiliwaza hamaki ya njaa hii ya dhati
Njaa ya maisha itakayo kushibishwa

**MASWALI**
(a) Eleza mambo muhimu yanayojitokeza katika shairi hili (alama 4)
(b) Taja na utoe mifano ya aina zozote **mbili** za usemi zilizotumika katika shairi hili.
(c) Eleza maundo wa shairi hili (alama 3)
(d) Onyesha umuhimu wa matumizi ya kihisishi katika shairi (alama 2)
(e) Fafanua maana ya:
(i) siku hamaki yake itapochafuka kama bahari (alama 2)

(ii) kuipoza ghadhabu ya kiy ingawa katiti (alama 2)

(f) Eleza maana ya msamiati ufuataokama ulivyotumiwa katika shairi

i) tambo

ii) ulokokomaa

iii) kumtowesha

(alama 3)

**SEHEMU YA E**
**FASIHI SIMULIZI**

8. (I) Jamii ya waluo wana ohangla,
Waluhya wana Isukuti,
Wakikuyu wana mwomboko
Wakamba wana wathi na kilumi
Waswahili wana chakacha

(a) tambua kipera kina chorejelewa katika maelezo haya (alama 2)

(b) fafanua dhima ya kipera hiki (alama 8)

(ii) Eleza udhaifu wa mahojiano kama mbinu ya ukusanyanji wa data katika fasihi simulizi (alama 10)

# ALLIANCE BOYS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)
## Mwongozo wa Kusahihisha

1. a) Haya ni mahojiano .
   b) Azingatie mtindo wa tamthlia.
   c) Ahusishe wahusika wawili na majina na majukumu yao yabainike wazi mwanahabari na mtaalam.

**HOJA.**

i) Ufisadi
ii) Ulevi
iii) Ukahaba
iv) Utapeli kanisani.
v) Kuteleke za watoto.
vi) Vavyaji wa mimba.
vii) Ulaghai.
viii) Ubadhilifu wa fedha.
ix) Uuzaji wa bidhaa ghushi.
x) Unafiki wa wa viongozi .
xi) Matumizi mabaya ya vyombo vya .mawasiliano bila muzangano.

2. Utovu wa usalama.
   i) Vifo /mauaji
   ii) Wizi
   iii) Ubakaji
   iv) Njaa.
   v) Uharibifu wa mali.
   vi) Elimu kuzorota / kuathirika.
   vii) Kuzorota kwa uchumi.
   viii) Uhamaji / ukimbizi.
   ix) Chuki baina ya wanajamii.
   x) Kulemaza watu.

3. Hii ni insha ya methali. Mtahiniwa atunge kisa kitakachodhihirisha maana ya methali ambayo ni mtu akivumilia changamoto anazokumbana nazo akishughulikia jambo
4. Fulani, mwishowe hufurahia ufanisi . mtahiniwa ashughulikie pande zote mbili za methali.
5. Hii ni insha ya mdokezo. Kisa kisheheni hisia za furaha (mwisho mwema) sharti amalize kwa maneno aliyopewa.

# ALLIANCE BOYS HIGH SCHOOL

## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019

## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

## Mwongozo wa Kusahihisha

1. Dawa za kulevya / mihadarati. 1x1=1
2. zinatesa na kufisha wazee kwa vijana na kuwa zinaathiri bila kuchagua jinsia, tabaka , rangi wala umri. 2x1=2
3. i) kunusa
   ii) kuvuta
   iii) kumeza
   iv) kujidunga sindano. 4x1=4
4. kukosa amani

Kutumia hela nyingi kuwalipia ada ya hospitali. 2x1=2

5. washukiwa mara nyingi hukosa kufikishwa mahakamani kwa sababu jamii hukosa ushahidi wa kutosha dhidi ya tabia hiyo. 1x1=1)
6. serikali imepiga marufuku uuzaji wa miharati. (2x1=2.
7. i) mawakala – wanao tumiwa kuuza mihadarati kwa niaba ya wengine.
   ii) Kadamnasi – wazi, hadharani, mbele ya watu.
   iii) washauri nasaha – wanaelekeleza / kutoa mawaidha kwa waathiriwa wa dawa za kulevya. (3x1=3)

MWONGOZA WA KUSAHIHISHA .

**UFUPISHO**

a) i) Lugha hutofautisha kazi ya fasihi na isiyo ya fasihi.
ii) Jinsi anavyotumia lugha na kiwango cha usanii ndiyo alama inayomtofautisha.
iii) msisitizo mkubwa katika maudhui .
iv) uhakiki kuonyesha mshairi alivyotawala lugha yake vizuri.
vi) Haiwezekani kutofautisha maudhui na usanii.
vii) mwanadamu kujua lugha yake ni kumeza" mfumo wa lugha yake.
viii)katika lugha kuna mitindo inayotumika kutegemea nyanja tofauti.
Mtuanayejualughavizuriawezekutumiainavyokubalika.

xi) mtu anayejua lugha vizuri aweze kuitumia inavyokubalika.
x) mwandishi awe mtafiti ili ajue yale matumizi asiyo kuwa na haya nayo.
Zozote 5x1=(utiririko)

UFUPISHO .

i. Mwanadamu kujua lugha ni kumeza mfumo wa lugha yake.
ii. Ujuzi alionaoni sawa na wengine wanaozungumza lugha moja.
iii. Aweze kutumia katika mahusiano yake na wanajamii wengine.
iv. Kuna mitindo mingi inayotumika siasa, sharia ,dini.
v. Mtindo wa kawaida unaotuka katika mawasiliano ya kila siku(rejesta)
vi. Anayejua lugha vizuri aweze kuitumia katika mitindo iliyokubalika.
vii. Mwandishi wa habari awe "amefuzu" kuelewa matumizi tofauti ya lugha.
viii. Mwandishi awe mtafiti ili achore jamii yake inavyostahili.

( Zozote 6x1)

a) i) vivinge ,ya kati, ya nyuma. ½ x1 = ½

ii) Mbele,juu,tandaza. ½ x1 = ½

iii) Nazali,mdomo,ghuna ½ x1 = ½

iv) kaakaalaini, ghuna, kikwaruzo/kikwamizo. ½ x1 = ½

b) Silabi funge ni silabi inayoishia kwa konsonati m.f maktaba, muhtasari.
ii) silabi wazi ni silabi inayoishia kwa irabu m.f oa, iga. Kueleza ½ kutoa mfano ½

c) I) swali
ii) kauli
iii) mshangao
iv) rai
v) amri

3x1=3

d) i) **w**imbo
ii) **m**uundo
i)**p**azuri
ii) darasa**ni**.

4x1/2= 2

d) i) Mfano – batamzinga ,askarijeshi, mwanahewa. 1x1=1

ii) kusoma, kuimba, kula. 1x1=1
f) Wakimbizi – wale 1x1=1
Tanzania – kule 1x1=1

g)i) koma
- pumziko fupi katika sentensi.
- kuorodhesha.
Kuonyesha mwanzo/ mwisho wa usemi halisi.
- Kuandika anwani.
- Baada ya kutajajina la mtu anayepewa habari.
- Kutenganisha sentensi zenye masharti .
-

- kuandika tarehe.
- Kuandika tarakimu zinazozidi elfu.

ii) . Mshazari
- kuandika tarehe.
Kuonyesha kumbukumbu.
Kuonyesha visawe.
Kuonyesha au.

iii) . Ritifaa .
- Kuonyesha herufi imeachwa.
- Kuonyesha shadda/ mkazo.
- Katika sauti za vingo'ongo.
- Kufupisha
- Kuandika miaka yenye namba zilizoachwa.

iv) Vifungo.
- Kuzingira nambari/ herufi katika orodha.
- Kuonyesha maelezo ya vitendo vya msemaji katika mazungumzo/ tamthiliya.
- Kutoa maelezo zaidi.
- Kuonyesha visawe.

4x1/2=4

h) KI- VI mf. Kiti – viti.

CH- VY mf. chura – vyura. 2x1=2

i) Asingesoma kwa bidii asingeenda chuo kikuu.

ii) Sijaenda Nairobi kununua gari.

2x1=2

j.) Haraka – polepole.
Alikumbuka – alisahau.

2x1=2

k) Kigoma/ kijigoma hicho chake kilibwa na kijizi kile. 2x0=2

i) Kamau alimkemea **na** kumwambia **a**jichunge **kwani** mienendo **yake** **inge**mwonyesha cha mtema kuni.

6x1/2=3

m) Yesu alifia dhambi zetu 2x0=2

n) gesi – hewa.
Kesi – daawa/ mashtaka.

| S | | | | |
|---|---|---|---|---|
| KN | | KT | | |
| N | V | T | N | S |
| Baba | Yake | Amemnunulia | baiskeli | Aliyomwahidi mwanka jana |

8x1/2=4

p.i) Hakuandika – kikanushi cha wakati uliopita.

ii) nafsi ya pili umoja – alikusalimia jana.

q. KN(W+RV) +KT(T+RE)
m.f Yule mzuri alisafiri kwa ndege.

2x1=2

r) kipozi – tembo
kitondo - wakazi.
Ala- nazi

3x1=3

**ISIMU JAMII.**

a) sajili mkahawani/ hotelini. 1x1=1
b) Msamiati maalum – order, ngombe, kuku wakupaka.
c) – lugha ya ucheshi na utani.
d) Kuchanganya ndimi.
e) Kuhamisha ndimi.
f) Lugha isiyo sanifu.

g) Lugha ya mkato.
h) Kuamrisha.
i) Kauli fupi fupi.
j) Lugha ya heshima inayotumiwa na mhudumu.
k) Matumizi ya tarakimu.
l) Majibizano.

**Tanbihi mwanafunzi afafanue kwa kutoa mifano mwafaka 9x1=9**

# ALLIANCE BOYS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

1. a) i) Hadithi
   ii) Hurafa
   (2X1=2.)

   b) i) Hadithi hadithi …… hadithi njoo.
   ii) Paukwa pakawa ……
   (2x1=2.)

   c )
   i. huburudisha wanajamii
   ii. huhifadhi historia ya jamii.
   iii. Hukuza lugha miongoni mwa wanajamii.
   iv. Huleta wanajamii pamoja.
   v. Huhifadhi utamaduni wa wanajamii.
   vi. Hukuza ujasiri wa kuzungumza.
   vii. Hukuza uwezo wa kukumbuka
   viii. Huelimisha wanajamii (5x1=5)

d) i) Wahusika huwa ni wanyama.
ii) Wahusika huwa na tabia za binadamu.
iii) Huhusisha kazi ya ubunifu.
iv) Hutoa mafunzo kwa njia ya kuchekesha.
v) Hutumia mbinu ya uhaishaji / tashihisi.
vi) Hutoa matumaini kwa wanyonge. (5x1=5)

E)
E (I)
i) Hutoa hadhira kutoka ulimwengu halisi na kuwaweka katika ulimwengu wa hadithi.
ii) Hushirikisha / huleta hadhira na mtambaji pamoja.
iii) hutambulisha au hutangaza mtambaji.
iv) Huvuta makini au usikivu wa hadhira.
v) Huashiria mwanzo wa hadithi .
vi) ii) Huashiria mwisho wa hadithi. (3x1=3.)

E (II)
a) Hutangaza funzo kwa wasikilizaji/ hadhira.
b) Humpisha mtambaji anayefuata.
c) Hupisha shughuli inayofuata ikiwa kipindi cha utambaji kimekwisha.
d) Baadhi ya viishio huwapa hadhira changamoto ya kuwa watambaji mashuhuri wa ngano.
e) Huitoa hadhira katika ulimwengu wa ubunifu/usimulizi.
f) Huashiria mwisho wa hadithi.
(3x1=3)

**TAMTHLIA YA KIGOGO.**

2. a) i) Msemaji ni majoka.
ii) alikuwa anamwambia babu katika ndoto .
iii) walikuwa katika chumba cha wagonjwa.
iv) hii ni baada ya kupata habari ya kifo cha mwanawe Ngao Junior.
(4x1=4)

b) i) Jazanda – safari
- uongozi
ii) msemo – dhahiri shahiri.
iii) nidaa – dhahiri shahiri babu! (2x2=4.)

- c) Mauaji - jabali aliuawa na uongozi wa Majoka.
- kufungwa kwa soko la Chapakazi.
- njaa
- Ufisadi
- Kufungwa jela kiholela.
- vikuchapwa na askari.
- uchafuzi wa mazingira.
- migomo
- Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya .
- Kutowajibika kwa viongozi.
- Ubadhirifu wa mali ya umma

- Kudhibiti vyombo vya habari
- Usaliti
- Ulipizaji wa kisasi.

Utabaka. (12 x1= 12.)

**TAMTHILIA KIGOGO.**

- Wanawake wamechorwa kama wasomi . mf Tunu, Ashua
- Watetezi wa haki .m.f Tunu
- Wenye msimamo dhabiti .m.f Tunu
- Walezi wema .M.f Bi. Hashima
- Wenyebidii .M.f Ashua
- Wafanyabiashara haramu.M.f Asiya
- Ni washerati. M.f Asiya
- Ni washauri wema .M.f Tunu
- Ni wapenda anasa.M.f Husda
- 
- Ni fisadi . m.f Asiya
- Ni adui wa mwanamke mwenzake.M.f Husda kwa Ashua
- Wamesawiriwa kama jasiri .m.f TTunu Na Ashua
- Ni wazindushii .M.f Tunu anawazidua wanasagamoyo.
- Wamesawiriwa kama wenye tamaaya mali k.m Ashua Anadai kuchoka kupendwa kimaskini na Husda aliolewa na majoka kwa sababu ya tamaa ya mali.
- Wanawake wanadhalilishwa , majoka anawadunisha Tunu na Ashua.
- Wameschorwa kama pambo la kumfurahisha mwanamume.k,m Husda
- Wenye matumaini . Tunu
- Wamesawiriwa kama watu walio na ushirikiano Bi. Hashima, kuwalea watoto wa Ashua.

- Wamesawiriwa kama wenye utu.m.f Bi. Hashima (zozote 20)

**RIWAYA**

- Wahusika katika riwaya ya Chozi la Heri wanakumbwa na matatizo mbalimbali . matatizo hayo ni ya kiuchumi na kijamii.
- Vyanzo vya matatizo yenyewe ni tofauti tofauti, kuna yale yanasababishwa na wahusika wenyewe ilhali mengine yanaletwa na watu wengine .
- Tunaweza kusema kuwa matatizo mengine ni mwiba wa kujindunga huku mengine yakiwa ya kudungwa na wengine.

i) Jumba moja la Ridhaa linabomolewa kwa kuwa alilijenga katika ardhi iliyotengewa ujenzi wa barabara katika mtaa wa zari. Hakuchunguza uhalali.

ii) Terry mkewe Ridhaa anapuuza maonyo na maneno ya mumewe kuhusu mkasa ambao ungetokea hivyo anateketea.

iii) Ami wamwangeka anaagamia katika mkasa wa moto alipoenda kuwasaidia watu waliokuwa wanateketea.

iv) Walioteketea katika moto wa lori walijiigiza matatani wenyewe kwani walikuwa wameonywa kulikuwa na hatari.

v) Uhasama, migogoro na ukosefu wa mahitaji muhimu unaoikumba familia ya Mwimo Msubili hii ni kwa sababu ya yeye kuwaoa wake wengi.
vi) Kufutwa kazi kwa Lunga Kangata Kiriri baada ya kukataa kukubali mahindi ya jano kuuziwa wananchi ni mwiba wa kujidunga.
vii) Mauti yanayowakumba vijana waliokuwa wakiadamana baada ya sherehe za kuapishwa kwa kiongozi mpya.
viii) Tendo la Subira kuondoka nyumbani na kumwacha mumewe na watoto ni mwiba wa kujindunga kwa mumewe.

ix) Pete anapokubali kuolewa na Nyangumi bila kufanya uchunguzi wa kina.
x) Tukio la Zohari kupata mimba na kutumbukia katika mateso mengi.
xi) Tendi la Mwangeka na Mwangemi kufanyia babu yao mzaha, kwa kuwa usiku mmoja aliamua kuwalipua viboko.
xii) Mwangeka anakubaliana na Tila kuigiza maombolezi ya Dedan Kimathi ambayo yanamfanya babake kumwadhibu kwa kutowajibika.
xiii) Kukamatwa kwa Sauna na mwajiri wake Bi. Kangara kwa kujihusisha na Biashara ya ulanguzi wa watoto.
xiv) Tuama anaathirika vibaya baada ya kupaswa tohara na kulazwa hospitalini ni tendo alilolitenda kinyume na mapenzi ya baba yake.
xv) Walevi wenza wa Shamsi ambao wanapoteza uwezo wa kuona au uhai wao kwa kubugia vileo.
xvi) Mumwewe Selume anamfukuza mkewe kwa kuwa si wa kabila lake baadaye anamlea mtoto peke yake.
xvii) Mandu anapouawa katika vita akiwa ughaibuni ni mwiba kwani huenda hangepoteza maisha kama hangeenda huko mapema.
xviii) Fujo zinazosababishwa na uhafidhina baada ya uchaguzi ambapo wanapoteza uhai na mali.
xix) Wakimbizi waliohamia katika mimea na baadaye kufukuzwa ulikuwa mwiba kwani si halali kulima msituni.
xx) Naomi kumwacha mumewe Lunga Kiriri na watoto na baadaye kuwatafuta baadhi ya kifo cha bwanake ulikuwa mwiba wa kujindunga.

Zozote (20 x 1) = 20)

**CHOZI LA HERI**

5. KINAYA.

i. Ni kinaya Sauna kujifanya mzuri uhali unaiba watoto.
ii. Neema kupeleka mtoto kwa makazi ya watoto na mwishowe kwenda kupanga mtoto huko.
iii. Naomi kutoroka mumewe na wanawe na kujilaumu baadaye.
iv. Nchi ambayo ina miaka 50 kuonekana kama mtoto wa miaka 50.

v. Wafrika kuwa wafanyakazi katika mashamba yao chini ya wakoloni.
vi. Watu walioishi na Ridhaa kwa amani kugeuka na kuchoma nyumba yake pamoja na familia yake.
vii. Vijana kumbaka Lime na Mwanaheri mbele ya mazazi wao.
viii. Mama mkwe kufukuza Subira kwa kuwa hawakuwa wa jamii moja.
ix. Mzee Maya kumbaka mwanawe Sauna.
x. Wazazi wa Zohali ambao ni wasomi kumtesa kwa ajili ya ujauzito .
xi. Tuama kuusifu utamaduni wa tohara za kike illhali ndiyo sababu ya kuwa hospitali.

xii. Watu wa nchi ya Wahafidhina kumkataa kiongozi wa kike na ndiye anayewafanyia kazi mwekeru.
xiii. Pete kutaka kijiua kwa kuwa na watoto watatu akiwa na umri chini ya miaka 21.
xiv. Ridhaa anasema bila ya jamii kushirikiana amani waliyoyokuwa nayo ni ya kifaurongo tu.
xv. Uchafuzi uliotokea baada ya uchaguzi unaashiliwa na Ridhaa akisema kuwa vijana waliweza kujigongesha jahazi mwamba badala ya kuliongoa jahazi – taifa.
xvi. Ridhaa anamwambia Mwangeka mwanya wake wa meno uliopendeza sana ni ndoano aliotumia kumvulia mamake.
**xvii.** Ridhaa alitamani mwanawe aweze kuoa tena kwa kusema anajua siku moja atapata hurulaini ambaye ataponya kiharusi chake. **hurulaini: mwanamke mrembo , Kiharusi : matatizo**

xviii. Ridhaa anasema hurulaini hiyo anafungua kufuli iliyofunga moyo wake. – **kufuli: majozi au upweke.**
xix. Selume alipolia kwa kuacha mwanawe Ridhaa anamwambia asilie kwani hata kama simba ni mkali vipi awezi kumrarua mwanawe.

b) **MBINU REJESHI.**

i) Ridhaa anakumbuka mlipuko na kilio cha mkewe.
ii) Ridha anakumbuka milio ya kereng'ende na bundi.
iii) Anakumbuka jinsi watoto walivyo mtenga shuleni anakumbuka majumba yake yanavyobomolea.
iv) Anakumbuka mjadala aliokuwa akifanya na mwanawe Tila.
v) Mwangeka anakumbuka mafunzo ya dini.
vi) Kaizari anasimulia ridhaa jinsi familia yake ilivyovamiwa.
vii) Mwanaheri anakumbuka kwenda kwa mamake kupitia kwa barua .
viii) Mwangeka anakumbuka maisha yake na Mwangemi utotoni.
ix) Kijana aliyekuwa amevaa sharti ambalo lilikuwa limeandikwa H**itman** anaeleza jinsi aliwandanganya vikongwe kumchagua kiboko ambaye hawakumtaka.

( zozote 5x1)

c) **SADFA .**

i) Wakati selume alipotaka kuacha kazi katika hospitali ya umma ndio Ridhaa anamaliza kujenga hospitali ya mwanzo mpya.
ii) Siku ya kuzaliwa kwa Umu ndio siku ya kuzaliwa kwa Mwangemi .

iii) Neema akienda ofisini alikiona kitoto kimetupwa.
iv) Umu na Dick wanakutana kisadfa katika uwanja wa ndege.
v) Mwaliko kupagwa na binamuye Mwangeka aliyempanga nduguye .
vi) Dick alipokuwa akiwaza kuhusu nduguye Umu, alikuwa nyuma yake.
vii) Kukutana kwa wana wa Lunga katika hoteli ya Majaliwa.
viii) Umu anapowaza sana kuhusu maisha yake wenzake wana matatizo kumliko.

( zozote 5x1)

d) **Jazanda**

i) Tila anapomwambia babake kuwa nchi ya Wahafidhina ni watoto wa miaka 50- bando ni wategemezi licha ya kupata uhuru.
ii) Tila anamwambia babake wanahitaji kiongozi yeyote awe wa kike au wa kiume ila kama ataweza kuilekeza jahazi katika visiwa vya hazina.( jahazi – nchi, visiwa – kuimarika kiuchumi.)
iii) Baada ya kuangamizwa kwa familia ya Ridhaa anaelewa maana ya vijikaratasi vilivyokuwa vimesambazwa kuwa kutakuwa na gharika baada ya kuapishwa kwa msumbi( Gharika – fujo)
iv) Lunga anatumia neno Eden kurejelea mahali pazuri pa wanyama .
v) Mamake Ridhaa anamwambia unyonge haukuumbiwa majimbi ila makoo( majimbi – mwanaume, makoo- wanawake)
vi) Kuikoleza nundu mafuta kunaonyesha kuwa mhafidhina hasaidiki kutokana na mzungu .
vii) Mshahara wanaopewa wahafidhina unitwa mkia wa mbuzi kuonyesha ulikuwa mdogo.
viii) Ridhaa baada ya familia yake kuangamia haamini kuwa mwangeka angerudi. inasemekana ameuawa na bafe.

( zozote 5x1)

**HADITHI FUPI .**

6. a) ) Mapenzi ya kifaurongo.

i) Dennis na wanafunzi wengine wanakaliwa na ugumu wa masomo katika chuo kikuu.
ii) Umaskini matatiza masomo na mapenzi ya Dennis Machora.
iii) Utabaka baina ya wanafunzi chuoni.
iv) Ukosefu wa ajira baada ya kuhitimu chuo kikuu kwa Dennis na Penina.
v) Mapuuza ya wahadhiri k.m Dkt. Mabonga.
vi) Migogoro ya mapenzi rafiki wa kwanza wa Penina wanatengana na pia tunamwona Penina wakitengana na Dennis.
vii) Kutamauka masomo chuoni yanakuwa unagumu kiasi kwamba wanafunzi wanahiari kufanya kazi ya matatu na kukusanya kodi.
viii) Njaa- Dennis alikuwa na unga wa kutengeneza uji kikombe kimoja bila sukari.
ix) Kuna mapenzi ya kiholela miongoni mwa wanafunzi wa chuo kikuu, walitembea wakishikana mabega.
x) Shirikizo la rika – Dennis alitamani kuvaa kama wenzake na vile vile kuwa na vifaa vya kieletroniki kama vya wenzake.

( zozote 10x1)

b) **SHOGAKE DADA ANA NDEVU.**

a) Mapenzi miongoni mwa wanafunzi yanaathiri masomo yao.
b) Mimba za mapema miongoni mwa wanafunzi k.m safia.
c) Kuna uavyaji wa mimba. K.m Safia .
d) Mauti kifo cha Safia.
e) Unafiki wa kidini k.m Safia na Kimwana.

f) Mapuuza ya wazazi yanapelekea watoto wao kupotoka kimaadili.
g) Kuna undanganyifu wa vijana kwa wazazi wao k.m Safia kumdanganya mamake.
h) Kuna utovu wa maadili miongoni mwa vijana k.m Mkadi alikuwa na vitendo viovu kushinda shetani.
i) Vijana wanapata changamoto katika maandalizi ya mtihani wa mwisho ndipo Safia wanaungana kudurusu pamoja na Kimwana.
j) Kutokuwepo kwa mawasiliano baina ya wazazi na watoto wao unawakosesha maelekezi mema.
( zozote 10x1)

T**UMBO LISILOSHIBA : MAME BAKARI.**

7. a) i) Msemaji ni babake Sara.
ii) Akimwambia Sara.
iii) Walikuwa hospitali katika chumba cha daktari.
iv) Alikuwa ameenda kufanyiwa vya ujauzito na Beluwa, alipowakuta wazaziwe wakisubiri katika chumba hicho.

(4x1=4)

b) Mbinu za lugha .
i) swali la balagha unanini?
ii) takriri unaogopa.

Zozote (2x1=2)

c) Mrejelewa ni Sara.
i) Mpenda masomo.
ii) mwoga.
iii) mwenye mapenzi ya dhati.
iv) mwenye busara anamua kujiua sio suluhisho.
v) mwenye utu hakutaka kuavya mimba.
vii) Msiri
viii) Mvumilivu
ix) Msamehevu.
xxi) mwenye madili
xxxi) mwenye majuto.

Zozote 6 x 1= 6)

d) Babake Sara

i. Kupitia kwake tunapata athari ya ukali kupita kiasi wa wazazi kwa wanao.
ii. Nikielelezo cha wazazi ambao wako tayari kubadili msimamo wao mkali kwa watoto wao.
iii. Anaonyesha umuhimu wa wazazi kushirikiana katika maelezi.

iv. Anaonyesha umuhimu wa kuweka siri katika masuala tata ya familia.
v. Ni kielelezo cha wazazi wanaouenzi utamaduni wa jamii yake.

(4x1=4)

e) Malezi /mapenzi

g) Malezi – babake Sara anakuwa mkali kwa Sara.
Babake Sara anabadilika na kumwonyesha mapenzi, anamsaidia.
Mapenzi – kuna mapenzi ya dhati kati ya Sara na sarina.
Salina anamsaidia sara anapokuwa mjamzito.
Salina aidha anamsaidia sara kuweka siri ya ujauzito na kufanyiwa vipimo na mipango ya kujifungua.

( 3x1=3.

8. **USHAIRI.**

i. Nifwateni sipitali/nifwateni sipatali dawa ziko nyumbani / dawa ziko nyumbani/ dawa. (1x1=1)
ii. - Tangu zamani wao huenda mzimuni.
   - Madawa ya asili yapo.
   - Hapendi upasuaji.
   - Mtu anaweza kupoteza maisha.
   - Anafuata kielelezo cha mababu zetu.

   3x1=3.
iii. Mtu akienda hospitali ni kwa kutojua vizuri. Kuwa daktari akiona mwili atasema ni saratani ya tumbo. atavitia visu makali kujitayarisha kufanya upasuaji /oparesheni atakukata viungo vya ndani .kwa nini kwenda hospitali ilhali dawa ziko nyumbani.

   (4x1=4)
iv. Mtiririko
v. Mathnawi.
vi. Mgonjwa / anayeugua.
vii. Huzuni/ masikikitiko / lawama/malalamiko.
viii. Beti sita .
ix. Kila ubeti una mishororo mitano / takhimisa.
x. Kuna ukwapi na utao katika kila mshororo.
xi. Kuna kibwagizo isipokuwa ubeti wa sita .
xii. Kuna urari (usawa wa vina – li,ni
xiii. Kila mshororo una mizani 16. Ukwapi 8, utao 8,
   4x1=4
xiv. Inkisari – tabani- taababi.,- wambiwa – unaambiwa , sipitali- hospitali.
xv. Tabdila – afiya- afya.
xvi. Mazda – nenende – nende. (2x1=2
xvii. dhalili – hafifu /isiyo na nguvu.
xviii. azali – zamani /kale /jadi/ kitambo..

2x1=2

# KAPSABET BOYS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)
## Mwongozo wa Kusahihisha

1. **INSHA**
   - Mwanafunzi azingatie muundo waratiba
   - Anwani/mada
   - Saa
   - Tukio/shughuli

   **TANBIHI**
   - Shughulizifafanuliwevizuri
   - Matukioyafuatanevilivyo

2. Mikakati iliyo wekwa na serikali kukabiliana na Magaid inchini:
   i) Kuwapa mafunzo na kuwaajiri walinda usalama.
   ii) Kuhamasisha na kuwataka raia wawe macho.
   iii) Kuanzisha mpango wa nyumba kumi-kila mtu amfahamu jirani yake.
   iv) Kuweka kamera zasiri /CCTV katika maeneo muhimu.
   v) Kuimarisha ukaguzi na ulinzi mipakani
   vi) Kukabiliana na makundi haramu kama vile al-Shabaab – huko Somalia.
   vii) Kuongeza zana za kutumiwa kulinda usalama.
   viii) Kushauri vijana kuto jiingiza katika makundi haramu.
   ix) Kuhimiza uhusiano mwema na majirani.
   x) Kutwaa silaha haramu baina ya wananchi.n.k

3. Mwanafunzi atunge kisa kinacho sabihiana na methali yenyewe kuwa ukimbembeleza mtoto na kumdekeza bila kumwelekeza vyema akiwa na tabia mbaya yakuelekea kukuasinakukutia aibu utataabika mwenyewe.

4. Mtahiniwa atunge kisa kinachoashiria kujuta kwa ajili ya kukosa kutilia maanani nasaha/wosia/mawaidha.

- Kisakioanena Maneno aliyopewa, la si vyo atuzwe BKO.
  - LazimaMtahiniwa amalize insha kwa maneno aliyopewa, la si vyo apewe Bk 03
  - Mtahini waajihusishe na kisa hicho. Asipojihusisha amejitungia swali, kwa hivyo apewe Bk 03

# KAPSABET BOYS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha
## Mwongozo wa Kusahihisha

1. **Ufahamu**

(a) - Rais Kenyatta alihimiza viongozi wahutubie watu kwa Kiswahili.

- Rais Kenyatta alihutubia umma kwa Kiswahili.
- Tume iliundwa ya kuimarisha Kiswahili.
- Chama cha KANU kilipendelea Kiswahili kiwe lugha ya taifa.
- Kiswahili kitumiwe Bungeni.
- Rais Moi alitumia Kiswahili kuhutubia. ***Zozote 4 x 1 = 4***

(b) Mashiriki ya utangazaji kama BBC, sauti ya Amerika na sauti China hutangaza kwa Kiswahili. ***(1 x 2 = 2)***

(c) - Viongozi kuenzi Kiingereza.

- Kiswahili kushukulikiwa kama lugha duni.
- Vyombo vya habari kutokuwa na vipindi vingi vya Kiswahili.
- Kiswahili kuwa na vipindi vichache shuleni ukilinganisha na Kiingereza.
- Lugha potovu ya sheng.

(d) Kielezo cha ratiba kinachopendekeza Kiswahili kuwa lugha ya taifa. ***(2 x 1 = 4)***

(e) (i) Heshimiwa/Hupendwa na wengi. ***(1)***

(ii) Mipango/Mikakati/Mbinu za/ Namna ya kutenda. ***(1)***

(iii) Njia/Mbinu ***(1)***

(iv) Nchi za ng'ambo / mbali ***(1)***

**2. UFUPISHO – MWONGOZO**

(a) - Uwezo wa kudanganya huonekana mapema.

- Katika kila aina ya watu duniani.
- Mtu huanza uongo kutokana na mazingira wanayokulia.
- Wengine hutambua uongo hufanya mtu kuadhibiwa.

- Watoto huwa hatari zaidi wanapotanabahi uongo wao. ***(Zozote 6 x 1 = 6)***

(b) - Kuna wanaodhani watoto hudanganya zaidi kuliko watu wazima.

- Watu wazima ni hatari zaidi katika kudanganya.
- Wapo watu ambao ni wajuzi katika udanganyifu.
- Udanganyifu unalaaniwa na wasomi kadhaa.
- Hakuna sababu ya watu kudanganya.
- Uongo ni mbaya zaidi kuliko kifo, kazi ngumu au mateso ya aina yoyote.
- Udanganyifu huharibu uaminifu wa mtu au jamii.

***(Zozote 6 x 1 = 6)*** **Ondoa makosa**

***Sarufi = Makosa 6 = ½ x 6 = Alama 3***

***Hijai 6 = ½ x 6 = Alama 3***

***3.*** (a) (i) Irabu hutamkwa kwa ulaini ilhali konsonanti hubanwa ***(Alama 1)***

(ii) Nywa/Pwa, nya ***(Alama 1)***

(b) - Nomino zake hutokana na kiambishi ***(Alama 1)***

- Kuomba kama nomino – Kuomba kwake kunasaidia. ***(Alama 1)***
- Kuomba kama kitenzi – Amekwenda kanisani kuomba. ***(Alama 1)***

(c) Wewe hupendi kuongea wala kutenda. ***(Alama 2)***

(d) - a – Lim – a – po

- nafsi –.
- lim –mzizi
- a – kiishio
- po –i wakati au mahali ***(Zozote 4 x ½ = 2)***

(e) Msichana kiziwi ametuzwa.
Mwanafunzi shujaa ameshinda vita. ***(Alama 1)***

(f) Kirimu/Kirimia/Kirimiwa ***(Alama 1)***

(g) - Kuonyesha maelezo yanayoandikwa yanaendelea ingawa hayajaandikwa. Kwa mfano; Mariam kwa nini…

- Kuonyesha maneno yanatanguliwa na mengine ambayo hayajaandikwa.Mfano:- ..... hata ingawa sikujui mtakusaidia.
- Kuonyesha kukatizwa usemi katika mazungumzo.
  Mfano:
- Kutotaja maneno yenye utovu wa nidhamu au matusi. ***(Zozote 2 x 1 = 2)***

(h) (i) Oza
 (ii) Onya/onyesha

(i) S → KN + KT
KN = V + N + V
V – Wale
N → Walevi
V → Wenu
KT → T + E + E
T → Watawasili
E → Leo
E → Jioni ***(Zozote 8 x ½ = 4)***

(j) Ni fungu la maneno lenye maana isiyokamilika. Juu ya safu, mtoto, wetu, Leo jioni.
***(Alama 2)***

(k) Tambi <u>hizi</u> <u>zi</u>tawashwa kesho.
***(Alama 2)***

(l) Ng'ombe <u>gani</u> aliyechinjwa?
***(Alama 1)***

(m) Amani itakayotusaidia ni yetu.
Amani ambayo itatusaidia ni ile yetu.
***(Alama 1)***

(n) Mtanashati ame<u>kashifiwa</u> kwa kuku<u>chafua</u> kiti.
***(Alama 2 x 1 = 2)***

(o) <u>Kiji</u>boga <u>hiku</u> <u>kina</u>tosha <u>vijitu</u> <u>hivi</u>.
***(Alama 1)***

(p) Kufa! (umoja)
Kufeni! (wingi)

(q) Ukuta <u>uu</u> <u>huu</u> utafaidi sana.

(r) - Ku – Ngeli ya jina kitenzi.
- Ku – Nafsi ya pili.
- Ku – Kama kikanushi cha 'li' – wakati uliopita.
- Kiambishi cha mahali.

(s) Ijapokuwa Kipchoge hakushinda mbio hizo – Kishazi tegemezi.
***(Alama 1)***
atatuzwa zawadi kemkem - Kishazi huru.

*(Alama 1)*

(t) Sentensi iwe moja -Mwashi – mjenzi
- Mwasi – Aliyeasi/kiuka sheria (kanuni fulani)

***Makosa***

(a) ***Sarufi – Ondoa nusu alama kulingana na alama zilizotuzwa katika kila kisehemu.***

(b) ***Hijai – Jumla ya makosa 6 = ½ x 6 = Alama 3***

4. - Misafara ya watu waliokuwa wakishiriki katika biashara ya pwani na sehemu za bara.
   - Maingiliano ya watu waliokuwa wakifanya biashara ya utumwa, pembe za ndovu. n.k.
   - Sababu za kisiasa ambapo wakoloni walitaka kutumia Kiswahili ili kuendeleza utawala wao.
   - Juhudi za kutoka kusambaza dini ya Kiislamu na kikristo miongoni mwa wenyeji.
   - Matumizi ya vyombo vya – babari magazeti, redio nk.

***(Zozote 5 x 2 = 10)***

***Ondoa makosa***

***(a) Sarufi – Makosa 6 = ½ x 6 = Alama 3***

***(b) Hijai – Makosa 6 = ½ x 6 = Alama 3***

# KAPSABET BOYS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

**1. USHAIRI**

(a) Matibabu ya kiasili/dawa za asili/dawa za kisasa (Al. 2)

(b) Kuonyesha kuwa dawa asili zinafaa kwa matibabu kuliko za kisasa. Watu wasirejelee. (Al. 2)

(c) - Ana matibabu ya kiasili.
   - Hospitali kuna operesheni ya visu
   - Kuna dawa za asili zisizopatikana hospitali (2 x 2 = 4)

(d) - Beti sita
   - Takhmisa/mishororo mitano
   - Mtiririko-Vina vya ukwapi na utao vinafanana katika beti zote
   - Mathnawi – Vipande viwili

- Mizani ni 8, 8
- Lina kiishio – Mshororo wa mwisho unarudiwa beti hadi beti katika beti zote.

(e) Kupata idadi ya mizani inayotakikana. (Al. 2)

(f) (i) Dhalili – Kudharauliwa, nyonge, maskini, dhaifu

(ii) Azali – Zamani

(iii) Sahali – Urahisi/wepesi

(iv) Kensa – Iri/saratani (4 x 1 = 4)

***2.*** **TAMTHILIA –** ***Chozi la Heri***

Jibu sadfa ni matukio mawili ambayo hayakupangwa kutokea Wakati mmoja. Sadfa imejitokeza katika mazingira yafuatayo.
Kukutana kwa Umu na Dick kwenye uwanja wa ndege lakini cheti chake cha usafiri kikawa kimechelewa. Safari ikawa leo na ndipo Umu na Dick wakakutana. Ni sadfa kuwa wakati Umu anampa Dick ushauri wakiwa katikai safari, ndipo Dick alikuwa ameamua kuyabadilisha maisha yake Ni sadfa kuwa Mwangeka ndiye mlezi wa Umu no Dick naye binamu yake Mwangemi ndiye mlezi wa Mwaliko lkumbukwe kuwa Umu, Dick na Mwaliko ni ndugu. Ni sadfa kuwa hoteli aliyoichagua Mwaliko kumpeleka babake ill amnunulie chakula cha mchana ndiko akina

Umu walikuwa na wazazi wake. Kukutana kwa Mwaliko na ndugu zake wawili ilikuwa ni sadfa. Hakujua kuwa wangekutana kwenye Hotel ya Majaliwa. Ni sadfa kuwa siku yake Umu ya kuzaliwa ilikuwa ndiyo siku ya kuzaliwa kwa Mwangemi. Ni sadfa kuwa siku aliyoitwa Ridhaa kwenda kumhudumia mgonjwa ndiyo siku aila yake iliangamizwa na kumponyoka. Mwanafunzi aongezee hoja

**<u>SEHEMU B</u>**

**KIGOGO**

a) i) – Maneno ya Majoka
- Anamwambia Ashua
- Ofisini mwa Majoka
- Ni baada ya Ashua kumkataa Majoka Kimapenzi alipokwenda kutaka msaada kwake

**1 x 4 = 4**

ii) Mbinu – Swali la balagha – uliona nini kwa huyo zebe wako? (al 2 )
- Nidaa – Eti mapenzi! (al 2 )
- Kutaja alama 1
- Mfano alama 1

iii) Hulka za Majoka
- Dharau/ bezo – Eti mapenzi!
- Mpyaro – zebe ( mjinga / mpumbavu) 1 x 2 = 2

**1 x 2 = 2**

iv) **<u>Ukandamizaji wa mwanamke</u>**
- <u>kupigwa:</u> Ashua akiwa gerezani anapigwa na askari
- <u>kubezwa / kukejeliwa</u>: Tunu anakejeliwa na Ngurumo na walevi wengine
- <u>Chombo cha mapenzi</u>. Majoka anamtaka Ashua kimapenzi anapokwenda

kumwomba msaada.

- Kijakazi nyumbani. Majoka anamtuma chopi kumuagiza mkewe kumpikia kuku na nyama na kumuokea chapatti
- Kutusiwa. Boza anamwambia Sudi kuwa asifikiri kuwa yeye anauza nyong'a kama Tunu wake.
- Kufungwa. Ashua anafungwa na Majoka
- Kunyimwa kura/uongozi. Ngurumo anamwambia Tunu kuwa kama hampi kura Majoka ni heri ampe paka wake. Majoka lakini si mwanamke Tunu.
- Kunyimwa ajira. Licha ya Ashua kufuzu taaluma ya ualimu, hakuajiriwa na serikali. Anaishia kuchuuza maembe sokoni la chapakazi.
- Kuozwa bila hiari. Majoka nataka kumwoza Tunu kwa mwanawe Ngao Junior bila hiari yake.
- Kunyimwa fidia. Majoka alitaka kumnyima Hashima fidia baada ya kifo cha mumewe

**b) Zozote Tamaa ya viongozi.**

i) Tamaa ya uongozi. Majoka ana tama ya kuongoza bila upinzani toka yeyote Yule. Anaamua kumwangamiza Jabali mpinzani wake.

ii) Tamaa ya kuwarithisha jamaa zao uongozi. Majoka anataka kumrithisha mwanawe Ngao Junior Uongozi pude tu atakapotoka ngambo.

iii) Starehe na anasa. Majoka anaenda kula na kuogelea katika hoteli yake ya Majoka and Majoka modern resort.

iv) Ulinzi: Majoka alitaka ulinzi kutoka askari wake.

v) Tamaa ya kujenga nyumba za kifahari. Majoka alitamani kujenga nyumba /hoteli ya kifahari katika Soko la Chapakazi.

vi) Tama ya mapenzi na wake za watu. Majoka ana tamaa ya kushiriki mapenzi na Ashua mkewe Sudi.

vii) Tama ya kuoza wanao wake waliosoma. Majoka anataka Ngao Junior amwoe Tunu, msichana aliyesomea sheria hadi kiwango cha shahada ya uzamifu.

viii) Tamaa ya kupewa sifa sufufu. Majoka ni lazima atangazwe kupitia vyombo vya habari na mjumbe.

ix) Tamaa ya kuungwa mkono. Majoka anapata uungwaji mkono kupitia watu kama Ngurumo, Asiya na Boza na ambao wanapewa hongo kwa ajili – hii.

x) Tamaa ya shule zao kufunzwa na walimu waliofuzu vyuoni. Majoka anataka Ashua afunze katika shule zake kwani tayari anefuzu na kupata shahada ya elimu.

Tamaa ya kupata sanamu. Majoka anataka Sudi amtengenezee

xi) sanamu itakayotumiwa katika sherehe za uhuru.

xii) Tamaa ya kupata kodi. Majoka anawatoza kodi wafanyibiashara wa soko la chapakazi kwa manufaa yake mwenyewe.

**Zozote 10 x 2 = 20**

**SEHEMU C TUMBO LISILOSHIBA**

**MWONGOZO**

4.a)

- Kauli ya kwanza ni ya Mbura
- Kauli ya apili ni ya Sasa.
- Walikuwa nyumbani kwa Mzee Mambo
- Mzee Mambo alikuwa ameandaa hafla ya kusherekea mtoto wake kusajiliwa kwenye shule ya nasari na wa pili meno yalikuwa yamepasua ufizi.
- Wanasema haya baada ya kula sana kwenye sherehe hiyo. **4 x 1 = 4**

b)

- Mzee Mambo kuwa waziri kivuli wa wizara zote – anapokea mshahara lakini hana kazi yoyote.
- Wafanyikazi ni watepetevu-wanafika kazini lakini hafanyi lolote pale kazini.
- Vyeo vya mzee Marobo vinampa fursa ya kupakuwa mshahara (yeye anachota tu hapewi) uk 37.
- Mzee Mambo kuandaa sherehe kubwa ambayo inaangaziwa na vyombo vya habari.
- Wizara moja inaendeshwa na mawaziri wawili – Sasa na Mbura wanadai kuwa wao ni mawaziri wa Wizara ya Mipango na Mipangilio.
- Sasa na Mbura kuendesha wizara kwa namna ya kujifaidi. Wanasema wizara inawaendesha hasa. Uk 37.

- Magari ya serikali kutumiwa vibaya kwenye sherehe ya Mzee Mambo kuleta jamaa zake, kuleta sherehe havipikwi hapo bali vinaagizwa kwa mali ya umma. Uk 39.
- Mbweo anayoitoa Mbura (uk 40) ni ishara ya shibe aliyonayo. Hizi ni dalili za majitapo/kiburi cha viongozi kuridhika na hali yao ya kuendelea kufaidi kwa wizi wa mali ya uuma.
- Maelezo ya jinsi Sasa na Mbra wanafakamia chakula upsei yanatupa taswira ya jinsi wenye uwezo wanapapia mali ya umma bila kuona haya.
- Mbweo anayoitoa Mbura (uk 40) ni ishara ya shibe aliyonayo. Hizi ni dalili za majitapo/kiburi cha viongozi kuridhika na hali yao ya kuendelea kufaidi kwa wiziz wa mali ya umma.
- Matajiri hawajali lawama kutokana na wizi wao wa mali ya umma.
- DJ kwenue sherehe ya Mzee Mambo hajali lawama kwa kulipwa mabilioni ya pesa kutoka kwenye hazina ya umma.
- DJ ana duka la dawa ambalo mtaji wake ni bohari kubwa ya dawa za serikali.
- DJ na wenzake wanapaata huduma za kimsingi kama vile maji ya umeme huku raia wakiumia. **(Hoja zozote 10 x 1=10)**

c)

- Magonjwa yanayosababishwa na kula lishe isiyobora mfano sukari, presha, saratani, obesti n.k
- Kuna mauaji- watu wanauana kwa kutumia silaha za maangamizi kama vile risasi na mabomu au hata kunyongana kutokana na unyakuzi wa mali ya umma.
- Kuna hai ya kuuna kifikira na kimawazo.
- Uhalifu wa kunyang'anyana mali.
- Kutovukwa na utu/ukosefu wa heshima.
- Kutojirudi kutokana na makosa wafanyayo/kukosa kukiri na kuomba msamaha watendapo maovu.
- Kuhalalisha wizi/unyakuzi – inasemwa kuwa aliyepewa hapokonyeki (ubinafsi)

5. a)

- Tukio la kubakwa linampotesea fahamu na anaaibika sana anapozinduka na kujipata akiwa uchi uk 47
- Mwanamke kujeruhiwa – Baada ya Sara kubakwa na janadume lile, anaharibiwa na kuvuja damu.
- Mwanamke kuvunjiwa ujanajike na utu wake.
- Maisha ya mwanamke kuingiliwa na kuharibiwa.
- Masomo yake yanakatizwa – mwalimu mkuu alimkabidhii Sara barua ya kumfukuza shuleni (uk 49)
- Mwalimu mkuu hamsikilizi wala kumhurumia – badala yake aliongoza kumkejeli na kumweleza ile haikuwa shuke ya wazazi bali wa wasichana. Anasema hawafundishi wanawake hapo.
- Mwanamke anateseka kiakili – Sara anaingiwa na mawazo mengi jinsi atakvyoukabili ule ujauzito. Anafikiria hata kuitoa ile mimba, kuhama kwao na hata kujiua.
- Mwanamke katika umri mdogo anabebeshwa mimba jinsi Sara alivyofanysihwa. Mzigo huo ungekuwa na changamoto nyingi kutokana na umri wake mdogo.
- Kuishi adhabu ya wazazi – Sara anahofia babake angemchinja kwa ujauzito wake.

- Kuogopa kutoa taarifa ya kubakwa kwa wazazi kwa sababu wazazi hawangemwamini.
- Kuishi maisha ya kimaskini – msimulizi anaeleza kuwa Sara angekunjiwakunjiwa matambatra yake na kurushiwa nje.
- Kila mara mwanamke anapobakwa, anayelaumiwa ni mwanamke na hata huonwa kama shetani. Uk 48

**(hoja 10 x 1 = 10)**

b)

Mtahiniwa azingatie masharti ambayo mwanamume anafaa ayazingatie pamoja na athari zake katika maisha y andoa.)

- Dadi ndiye mchuma riziki-yeye ni muuza samaki na apatacho kinatumiwa kuilisha jamaa yake. Pesa za mkewe ni za kununua mavazi ya fasheni mpya mpya na mapambo.
- Dadi anasaidia kazi za nyumbani lakini mkewe Kidawa hatosheki na hayo.
- Kidawa hakubali kuwa mwanamume kazi ni za nje si za ndani na kuwa Dadi kufanya kazi za ndani ni hisani tu. Uk 60.
- Dadi analazimika kushika shughuli za upishi kama vile kukuna nazi na kutia mboga tui.
- Dadi anaosha nyumba, kufagia, kufua na hata kupiga nguo pasi.
- Wanandoa kujiwekea masharti ya uzazi. Wanahiari kumzaa mtoto mmoja tu kutokana na athari za usasa.
- Dadi hataki mkewe atembeze bidhaa za kuwauzia wateja. Kila mara mkewe anapofanya hivyo, anaumia sana. Anaiona hiyo kama fursa ya mkewe kuhusiana na wanaume wengine . Uk 61.
- Dadi anaona ugumu wa masharti ya mkewe katika maisha ya ndoa lakini anashinda kumweleza.

Licha ya kuwa Dadi aliona ugumu wa kuzingatia masharti aliyowekewa na mkewe, hangeyavunja. Angefanya hivyo

- ndoa yao ingevunjika na huko kungekuwa ni kumvunja yeye pia.

- Dadi kushuku mkewe ana uhusiano wa kimapenzi na mwalimu mkuu. Hali hiyo inampa wasiwasi sana hata anashindwa kula.
- Kila mara Dadi alitarajiwa kuwa baada ya kula angeviondoa vyombo mezani na hata kuvisafisha.
- Dadi anapoamua kuzua mpango wa kupeleleza uhusiano wa mkewe na mwalimu mkuu, anafumaniwa na watu akiwa amepanda paipu na anaaguka na kuumia vibaya sana jambo linalomshutua sana mkewe pamoja na mwalimu mkuu anayelazimika kumwitia ambulensi impeleka hospitalini

**FASIHI SIMULIZI**

(a) Tanzu za fasihi simulizi na mifano:

(i) Ushairi simulizi

- Mifano – Nyimbo
  - Maghani
  - Mashairi
  - Ngonjera

(ii) Hadithi - Visasili
- Visaviini
- Visakale
- Mighani
- Hekaya

(iii) Semi - Methali
- Vitendawili
- Nahau
- Misimu
- Lakabu

(iv) Maigizo - Michezo ya watoto – Miviga
- Michezo ya jukwani Ngomezi
- Ngonjera

(v) Mazungumzo - Malumbano ya utani
- Ulumbi
- Mawaidha nk

Kutambua utanzu alama 1 = 5 x 1 = 5

Mifano/vipera 2 x ½ = 1, 10 x ½ = 5

(b) Taja na ueleze sifa zozote tano ambazo hupotea fasihi simulizi inapoandikwa.
- Hakuna kubadilisha sauti
- Miondoko ya mwili haiwezi kuandikwa
- Maleba hayatumiki
- Mikunjo ya uso haimo/ishara za uso hazimo
- Uimbaji wa hadhira na mtambaji hutoweka
- Uchezaji haumo/uigizaji
- Hadhara haiwezi kuuliza maswali

Kutaja 5 x 1 =5

Maelezo 5 x 1 = 5

**FASIHI SIMULIZI**

3. (a) Mviga ni sherehe maalumu za kitamaduni zinazoambatanishwa na nyimbo na ngoma.

(b) Sifa za miviga
- Huambatana na utamaduni

- Huongozwa na watu maalumu
- Hufanywa mahali maalumu kama – mwituni, kando ya mito
- Hufanywa kwa utaratibu maalumu
- Kuna kula kiapo/viapo na matambiko kutolewa
- Hufanywa wakati maalumu – Kutawazwa uongozi, mazishi, arusi nk
- Huambatana na ulumbi, mawaidha
- Kuna kutolewa kwa kafara
- Sadaka hutolewa (6 x 2 = 12)

(c) - Kuburudisha
- Kuelimisha
- Kuelekeza
- Kukuza mila na desturi
- Kuhifadhi historia ya jamii
- Kuipa jamii utambulisho Zozote 6 x 1 = 6

# STRATHMORE SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM- Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)
## Mwongozo wa Kusahihisha

1. Wewe ni mtangazaji wa kituo cha habari cha uzalendo. Studioni umetembelewa na mwanamke mtetezi wa haki za wanawake kuzungumzia namna mwanamke alivyotelekezwa katika jamii ya sasa. Andika mahojiano kuhusiana na suala nzima.

Mwanafunzi azingatie

Kuweko au kutekelezwa kwa mwanamke au mtoto msichana.

Mwanamke ametengwa:

- Nyumbani- ugavi wa raslimali, majukumu na hata mali humpendelea mwanamume.
- Kijijini- uongozi kama vile wazee wa vijiji, viongozi wa mabaraza tofauti ni wanaume.
- Kanisani- uongozi wa makanisa, huduma za kidini kwa misingi kuwa wahubiri na mitume wote walikuwa wanaume.
- Uongozi wa nchi: serikali za magatuzi na serikali kuu. Mwanafunzi anawezatoa mfano wa mswada uliokataliwa bungeni kuhusu kutengewa nyadihifa za wanawake.
- Mashirika ya kiserikali – baadhi ya viongozi wa mashirika haya ni wanaume.
- Bungeni – idadi kubwa ya wenyekiti wa kamati mbalimbali za bunge la kitaifa na seneti ni wanaume.
- Sekta ya elimu – walimu wakuu wengi katika shule za msingi na upili ni wanaume, hata katika shule ambazo ni za wasichana pekee. Hali ni hiyo hiyo katika vyuo anuwai na vyuo vikuu.

**TANBIHI**

Mwanafunzi azingatie sura ya mahojiano la sivyo aondolewe alama 4 (- 4S) baada ya kutuzwa.

**2. Kuna njia anuwai zinazoweza kutumiwa kulitandarukia tatizo la ajira nchini. Tetea.**

- Pana haja ya wananchi kubadilisha mtazamo wao kuhusu ajira ya serikali na badala yake wategemee kujiajiri
- Mashirika ya kifedha kutoa mikopo ya riba ya chini kwa vijana na wajasiri amali wengine ili waweze kujiendeleza na kujitegemea
- Serikali iondoe vikwazo na urasmi mwingi katika mchakato mzima wa kuanzisha biashara na ajira
- Serikali kubuni hazima maalum kupitia kwa Wizara ya Fedha ambapo vijana wanaweza kupata mikopo ya kujiendeleza.

- Makongamano na semina maalum ziandaliwe ili wananchi wapate mafunzo kuhusu namna ya kuchagua na kuendeleza biashara

- Vyuo vikuu viratibu upya kozi zake ili ziakisi soko la kazi
- Vyuo vikuu vitathmini na kuondolea mbali baadhi ya kozi ambazo hazina umuhimu wowote ikizingatiwa soko la kazi
- Vyuo zaidi vya kiufundi vijengwe ili kutoa mafunzo kwa vijana
- Vituo vya talanta vijengwe katika kila gatuzi ili kutoa nafasi au jukwaa kwa vijana kunoa talanta zao na kuziendeleza
- Ufisadi unaoshuhudiwa katika sekta ya ajira umulikwe na wahusika kuchukuliwa hatua za kinidhamu ili wanaostahili ajira wapate kuajiriwa
- Umri mahsusi wa kustaafu uwekwe na kuzingatiwa ili kuhakikisha kuwa kizazi kichanga pia kinapata ajira
- Serikali ihakikishie wasomi wote ajira pindi wanapofuzu kutoka vyuoni
- Serikali iwekeze zaidi katika vyuo vya kiufundi (ujenzi na ununuzi wa vifaa muhimu)
- Serikali kufanya ubia na mataifa mengine katika sekta ya ajira ambapo wasomi na wataalam kutoka nchini wanaweza kuruhusiwa kufanya kazi katika mataifa ya kigeni
- Wasimamizi wa idara za Kitaaluma kuwapa wanafunzi uelekezi hasa kuhusiana na uteuzi wa kozi
- Hamasisho litolewe kwa vijana kutotegemea kuajiriwa na badala yake washiriki katika kilimo biashara
- Serikali ianzishe mchakato wa kufufua viwanda vilivyoporomoka(Rivatex,Kicomi,Webuye,Paper Mills)

**Tanbihi**

Mtahiniwa ajadili angaa hoja nane

Mtahiniwa apendekeze hatua zinazofaa kuchukuliwa ili kulitatua tatizo hili la ukosefu wa ajira nchini.

3. **Andika kisa kitakachoafikiana na methali: Mgagaa na upwa hali wali mkavu.**

Kisa kionyeshe hali ambapo mhusika au wahusika wanahangaika /wanafanya juhudi za hapa na pale na mwishowe wanazoa matunda.

Ufanisi uonekane kutokana na juhudi za mhusika.

**Tanbihi**

Kisa kionyeshe pande mbili za methali: kujibidiisha hapa na pale, na kule kufanikiwa.

4. **Andika insha itakayomalizikia kwa:**

**... niliduwaa, nikasimama kisha nikaangalia nyuma huku machozi yakinitoka. Nilikumbuka wosia wa walimu na wazazi wangu lakini tayari kitumbua kilikuwa kimeingia mchanga.**

Mtahiniwa abuni kisa kitakachomalizikia kwa maneno aliyopewa.

Kisa kionyeshe majuto ya mwandishi kwa kutofuata maagizo/sheria au ushauri wa wazazi na walimu.

Kisa kidhihirishe machungu, maafa, mashaka na magumu yaliyomkumba mtahiniwa maishani kutokana na kutofautiana na ushauri wa walimu na wazazi.

Kudinda kufuata maagizo na hatimaye kuingia au kupata hasara kukuzwa vizuri katika

utungo wa mwanafunzi. Sababu ya kujuta kwake ionekane wazi katika hadithi yake.

**Tanbihi**
Kisa kizingatie nafsi ya kwanza umoja. Mwandishi ajihusishe katika usimulizi la sivyo atakuwa amejitungia swali.
Wakati uliopita uliopita uzingatiwe.
Mtahiniwa asibadili mdokezo kwa namna yoyote.

# STRATHMORE SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha
## Mwongozo wa Kusahihisha

1.Ni kwa nini Wagiriama wanajulikana kama Wamijikenda? (al.1)

***Walihamia Giriama kutoka Shungwaya katika makundi tisa na kila kundi likajenga kaya au mji wake – miji yote ikawa tisa. (1×1)***

2.Ni maafa gani yaliyompata Mekatilili katika maisha yake? (al.4)

***i) Mumewe alitekwa nyara kupelekwa utumwani.***
***ii) Wazazi wake walifariki.***
***iii) Aliozwa – wazazi wake wakumruhusu ajichagulie mume.***
***iv) Alishikwa na kufungwa gerezani kwa sababu ya siasa. (4×1)***

3.Ni hali gani inayotawala katika makala haya. (al.2)

***Hali ya wasiwasi wakati wa ukoloni. (2×1)***

4.Taja masuala ya kijinsia yanayojitokeza katika Makala haya. (al.2)

***i) Ndoa za lazima***
***ii) Usawa wa kijinsia (Mwanamke Mekatilili kupigania uhuru)***

5.Wazungu walitumia mbinu gani ili kuwashurutisha watu kuwafanyia kazi mashambani mwao. (al.2)

***i) Waliwateka nyara watu na vijana barobaro.***
***ii) Walitoza kodi.***

6.Andika maneno mengine yeney maana sawa na;

Kugura –***Kuhama*** (al.1)
Kubalehe –***kuvunja ungo/ kuwa mpevu*** (al.1)

7.Eleza maana ya;

iii) Mnazi na uwe mrefu huyumba kufuata upepo (al.1)
***Lazima Mekatilili angefuata mila na desturi (1×1)***

iv) Kitovu cha watu waishio Giriama (al.1)
***Asili/ Chanzo cha Wamijikenda/ Wangiriama. (1×1)***

c) Fupisha aya tatu za mwanzo kwa maneno 80. (alama 7)

- Kiswahili ni lugha ya Kiafrika inayoongewa katika nchi nyingi Barani Afrika.
- Lugha asilia mojawapo za Afrika
- Kiswahili kimeenea kote Afrika Mashariki na Kati.
- Wenyeji asilia waliokuwa wakiongea Kiswahili tangu awali ni Waswahili.
- Waswahili wanaendelea kutumia Kiswahili kama lugha yao ya mama.
- Makao ya Wasahili ni kaunti ya Pwani.
- Kiswahili kina lahaja nyingi kulingana na wanamoishi.

- Kutokana na lahaja hizi na nyinginezo za Kiswahili wataalamu wa lugha walibuni Kiswahili sanifu
- Kiswahili sanifu hutumiwa katika mafunzo shuleni, uandishi wa vitabu na mawasiliano ya kiserikali na kibiashara.

***(Hoja 6, Mtiririko 1)***

d) Eleza vile Kiswahili hakikuthaminiwa na namna hali hii inavyobadilika. (alama 8)

- Kiswahili hakikuthaminiwa kama lugha ya Kiingereza.
- Kiswahili hakikufanywa somo la lazima katika rasimu za shule
- Hakikutahiniwa katika shule za msingi wala za upili.
- Hakikupewa umuhimu wowote.
- Kiswahili kilianza kutiliwa mkazo katika shughuli zote nchini Kenya.
- Ilionwa kama lugha yenye manufaa katika kuleta umoja na kuwaunganisha wananchi wote.
- Kiswahili kimepewa nafasi sawa katika ratiba za shule kama Kiingereza .
- Kinatahiniwa kama somo muhimu kuanzia shule ya msingi hadi shule ya upili.
- Mwanafunzi anayesoma Kiswahili, asipofaulu vizuri katika lugha ya Kiingereza ana nafasi ya kupata kazi kama wengine.

(Alama 7, Mtiririko 1)

(2) <u>MATUMIZI YA LUGHA</u>

(a)Toa maelezo ya jinsi ambavyo hewa huzuiliwa wakati wa kutamka sauti hizi. (al 2)

(i) /p/ ***Hewa huzuiliwa / hubanwa kabisa kisha kuachiliwa ghafla / kwa nguvu***

(ii) /ch/ ***Hewa huzuiwa, kisha nafasi ndogo huachwa ili ipite ikiwa na mkwaruzo***.

(iii) /m/ ***Hewa hupita kinywani na puani***.

(iv) /r/ ***Ulimi hugotagota ufizini***. **(2× $^1/_4$)**

(b) Tenga silabi katika neno: Alimhukumu. (alama 1)

***a-li-m-hu-ku-mu***

***(1/0)***

(c)Tunga sentensi moja yenye kitenzi shirikishi kikamilifu na vitenzi sambamba. (al

3)
***<u>Ameshinda</u> shuleni ambako <u>amecheza akisoma</u>.***
***t vitenzi sambamba***

***<u>Tulikuwa</u> ibadani na <u>tumeimba tukamsifu</u> Mungu***
***t vitenzi sambamba***

***(3/0)***

(d) Tumia neno <u>mji</u> kama kielezi cha mfanano. (alama 1)
***Sherehe iliendeshwa <u>kimji</u>.***
***(1/0)***

(e) Onyesha namna tatu za kutumia kiambishi "ji" katika sentensi moja, kisha ueleze matumizi husika. (alama 3)

***<u>Ji</u>cho la <u>ji</u>paka lime<u>ji</u>fumba.***

***Jicho - Baadhi ya nomino katika ngeli LI-YA***
***Jipaka - nomino za ukubwa***

***Limejifumba – kujitendea/ kiima ni mtenda/ kirejeshi cha mtenda***

***Matumizi mengine: Mwimbaji – kuunda nomino kutoka kwa vitenzi.***
***(3×1)***

(f) Ziweke nomino hizi katika ngeli zake. (alama 2)
(i) waya ***U-ZI***
(ii) Kilembiwe ***A-WA*** ***(2×1)***

(g) Tambua virai vilivyopigiwa mistari ni vya aina gani na uonyeshe miundo yake. (alama 4)
(iii) <u>Kikapu kilichofumwa juzi</u> kitauzwa marikiti.
***Kirai nomino – Nomino + kishazi tegemezi/kivumishi kirejeshi***

(iv) Wenzetu <u>walikuwa wakijinaki kabla ya dimba</u>.
***Kirai kitenzi – kitenzi kisaidizi, kitenzi kikuu, kihusishi na nomino*** **(2×2)**

(h) Eleza maana mbili za sentensi: Zainabu alisema atakusaidia. (alama 2)
***Zainabu alisema <u>yeye mwenyewe</u> atakufaa.***
***Zainabu alisema <u>mtu mwingine</u> atakufaa.*** **(2×1)**

(i) Onyesha majuku ya mofimu katika neno: awaliaye (alama 3)
***a – nafsi***
***wa – watendwa***

*l – mzizi*
*i – kauli*
*a – kiishio*
*ye – kirejeshi*

**(6×1/2)**

(j) Andika kinyume: Aliiangika picha ukutani baada ya sherehe. (alama 2)
***Aliiangua** picha ukutani **kabla ya** sherehe.*
***(2×1)***

(k) Unda nomino kutokana na vitenzi vifuatavyo bila kutumia kiambishi ku. (alama 2)

Tuma - ***mtume / utume / mtumwa***
Pinda - ***upinde*** ***(2×1)***

(l) Eleza tofauti iliyopo kati ya ukanushaji na kinyume. (alama 2)
***Kukanusha ni kukataa jambo ilhali kinyume ni upande wa pili wa jambo.***
***(2/0)***

(m) "Viungo hivi havitatosha kuunga mchuzi wenu", mpishi alalamika. (alama 2)
***Mpishi alilalamika kuwa viungo hivyo havingetosha kuunga mchuzi wao.***
***(4×1/2)***

(n) Tumia visanduku kuchangana sentensi ifuatayo. (alama 4)

Alipotuona alitupuuza lakini sisi tulimsalimia.

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **S** | | | | | |
| **KN** | | | | **KT** | |
| **KN** | | **KT** | | **KN** | **KT** |
| **N/W** | **Ś(Kishazi)** | **T** | **U** | **W** | **T** |
| **Ø** | **Alipotuona** | **alitupuuza** | **lakini** | **sisi** | **tulimsalimia** |

(o) Tumia vitate vya jua, toa na baka katika sentensi mbili tofauti.
(alama 3
***Nilimchua kwa maji moto mguuni alipoumia.***
***Hili embe sitalila kwa kuwa lina doa.***

***Atalipaka jengo lote rangi nyeupe.***

***(3×1***

(p) Kamilisha kwa viigizi mwafaka. (alama 2)

(i) Ameanguka ***tapwi*** matopeni.

(ii) Mlango ulibishwa ***ngongongo***. ***(2×1)***

(q) Tofautisha sentensi.
(alama 2)

(i) Ungalisoma kwa bidii, ungalipita mtihani.
***Hakuna uwezekano** wa kupita wala nafasi ya kusoma kwa bidii.*

(iii) Ungelisoma kwa bidii, ungelipita mtihani.
***Kuna uwezekanano** wa kupita mtihani akisoma kwa bidii.*

***(2×1)***

**5. ISIMU JAMII (Alama 10)**
**Maswali**

d) "........ unaweza kukata rufaa iwapo unaonelea kuwa umehiniwa ........."

iii) Bainisha sajili ya mazungumzo haya.
(al.1)
***Sajili ya mahakamani / kortini / sheria*** ***(1×1)***

iv) Fafanua sifa za matumizi ya lugha katika muktadha huu.
(al.4)

i) Kunukuu na kurejelea vifungu vya sheria za nchi ili kudhibitisha hoja.
ii) Kudadisi / kuuliza maswali na kujibu maswali ili kuthibitisha ukweli wa mambo.
iii) Lugha ya unyenyekevu, heshima na dabu hasa upande wa mshtakiwa kwa hakimu ili kudumisha uhusiano mwema mahakamani k.m Bwana Jaji, hakimu n.k
iv) Matumizi ya msamiati wa kukopwa kutoka kwa lugha nyingine ili kuhifadhi maana asilia ya neno k.m msamiati wa kilatini k.v harbeas corpus/amisus curiae
v) Msamiati wa kawaida huwa na maana maalum unapotumiwa katika muktadha wa kisheria k.m 'My learned friend' kumaanisha, mwanasheria mwenzangu.
vi) Matumizi ya sentensi ndefu ili kutoa hoja zilizokamilika kama ushahidi.
vii) Sarufi huzingatiwa kwa uangalifu sana na ukiukaji wake hauruhusiwi kwa kuwa ukiukaji unaweza ukabadilisha mkondo wa uamuzi utakaofanywa na kumfanya mtu apoteze kesi.
viii) Matumizi ya msamiati wa kipekee/maalum unaoenda sambamba na shughuli inayofanyika kortini k.m wakili, jaji, korti, kata rufani n.k

Maelezo au mifano itolewe. (4×1)

e) Jadili changamoto zinazokumba kuimarika kwa Kiswahili katika jamii ya sasa.(al.5)

a. Matumizi kiholela ya lugha bila kuzingatia kanuni za kisarufi miongoni mwa wananchi.
b. Athari za lugha nyingine za kiafrika.
c. Athari za sheng' mingoni mwa vijana.
d. Uhaba wa machapisho kwa lugha ya Kiswahili.

e. Somo la Kiswahili kutengewa vipindi vichache shuleni ikilinganishwa na somo la Kiingereza.
f. Masomo mengi shuleni hufunzwa kwa lugha ya Kiingereza kuanzia shule za malezi isipokuwa somo la Kiswahili.
g. Matumizi mabaya ya Kiswahili kwenye vyombo vya habari ambavyo vinahitajika kukuza kiswahili.
h. Kasumba ya kikoloni miongoni mwa wananchi kuwa Kiswahili ni lugha ya hadhi ya chini inayotumika na wasiosoma.
i. Kutokuwa na sera madhubuti inayoelekeza kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili.

***(5×1)***

# STRATHMORE SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM – Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

**MWONGOZO**

**1. CHOZI LA HERI**

"Maisha yangu yalijaa shubiri tangu ututoni."

a) Eleza muktadha wa dondoo hili (al. 4)

- ***Haya ni maneno ya Chandachema. Anawaambia Kairu, Umu, Zohali na mwanaheri wako katika shule ya Tangamano***
- ***Chandachema anawasimulia wenzao dhiki alizopitia maishani mwake baada ya kuzaliwa***

b) Kwa kutolea mfano, bainisha tamathali ya usemi inayojitokeza katika kauli hii. (al. 2)

- ***Nahau – kujaa shubiri / Jazanda ya shubiri***

c) Jadili athari za vita katika jumuia ya Chozi la Heri (al.14)

- Vifo: Vita baina ya pande za mwekevu na ule wa mpinzani wake wa kisiasa vilisababisha mauaji
- Uharibifu wa mali: Aila ya ridhaa kuangamizwa katoka moto; nyumba na mali kuteketezwa
- Ukosefu wa makazi bora – kaizari na wenzake wamekosa makazi bora kule msitu wa mamba walikotorokea. Vibanda vinasongamana
- Huzuni – ridhaa alihuzunika sana baada ya aila yake na mali kuteketezwa kwa

moto

- Hasara kwa wafanyibiashara – wahalifu waliingia katika maduka ya kibiashara za kihindi, kiarabu na kiafrika na kupora mali ya wenyewe
- Kutiwa nguvuni : waporaji waliopora maduka/mali wakati wa vita walitiwa nguvuni na kukabiliana na mkono wa kisheria hapo baadaye
- Watu kutoroka makwao: Wahafidhima walihama makwao wakati wa vita bila kujue walikokuwa wajuelekea / ukimbizi
- Utegemezi: kukosekana kwa chakula katika kambi ya msitu wa Mamba kulifanya watu kutegemea msaada ya chakula toka kwa wahisani k.v shirika la msalaba mwekundu
- Majeruhi: kuna mwanaume aliyevamiwa na kuumizwa kwenye mgogoro wa kupigania ardhi katika eneo la tamuchungwa. Alilazwa katika kituo cha Mwanzo Mpya.
- Kukatiziwa masomo ka vile Lime na Mwanaheri
- Kusababisha uyatima - vita katika kambi ya Msitu wa Mamba vinasababisha walinda usalama kuua wazazi na kuwaacha watoto peke yao
- Kuporwa – wafanyabiashara wanaporwa bidhaa zao fujo za baada ya uchaguzi zinapozuka.
- Kukatwa - subira anavamiwa na kukatwa na wahuni
- Kubakwa – baada ya fujo kuzuka, Lime na Mwanaheri wanabakwa na wahuni
- Kukwama kwa usafiri – vijana wanalemaza shughuli za usafiri kwa kwenda barabarani na kuanza kuchoma magari
- Magonjwa – Ridhaa aliugua shinikizo la damu kutokana na mshtuko wa kupotea jamaa zake.
- Kusubaratishwa kwa jamaa / familia
- Athari za kisaikolojia

Hoja zozote 14 x 1 = 14

**2. TAMTHILIA - KIGOGO**

**<u>Maswali</u>**

"Siwezi mimi, siwezi mimi. Sitaki kuwa gurudumu la akiba … hujayaacha hayo?"

a) Eleza muktadha wa dondoo (Alama 4)

Msemaji ni Majoka
Msemewa ni Ashua
Wako ofisini mwa Majoka
Majoka alikuwa akimshawishi Ashua kimapenzi
(Hoja 4)

b) Eleza sifa nne za msemaji wa kauli hii. (Alama 4)

Sifa zake Majoka

(i) Mpenda anasa – anamtaka Ashua ambaye ni mke wa Sudi kimapenzi.

(ii) Mwenye majigambo – anasema , wewe wafikiri waliniita ngao kwa nini? Kifua kipana. (uk. 24)

(iii) Ni mpyaro- anamtusi Sudi: "uliona nini kwa huyo zebe wako? Eti mapenzi! Aliyekudanganya yanapikiwa watoto ubwabwa ni nani? (uk. 24)

(iv) Fisadi- kupitia kwake Asiya na Ngurumo wanapata kandarasi ya kuoka keki za kutumiwa katika sherehe za uhuru. Pia, amemmegea Mzee Kenga sehemu ya ardhi sokoni Chapakazi kutokana na kuungwa mkono naye katika Nyanja za kisiasa.
(v) Ni mzinzi – anamtaka Ashua kimapenzi.
(vi) Katili- anafunga soko na kukosesha akina Ashua kipato. Anaamuru waandamanaji washambuliwa na askari.

(vii) Mwenye dharau- analidharau soko la chapakazi kiasi cha kusema hayuko tayari kutoa fedha za kulisafisha, kwani ni la wachochole.
(viii) Mwenye tamaa – anafunga soko la chapakazi kwa tama ya kutaka kujenga hoteli ya kifahari katika soko hili.
(ix) Ni dikteta – anataka kuwashurutisha wafadhili wa akina Tunu waondoke sagamoyo ndipo wasiendele kuwafadhili msichana huyu na watu wake wanaoendelea kupigania haki kwa wote.
(x) Mwenye mapuuza – badala ya kulishughulikia maandamano yanayoendelea na ambayo yanaupaka matope uongozi wake, anayapuuza. Ni kutokana na kupuuza kiini cha maandamano haya ambapo mwishowe anaondolewa uongozini.
(xi) Mwenye vitisho – Tunu anapomfahamisha kuwa yeye na watu wake ni wauaji, anamtisha kwa kumwambia achunge maneno yake asije akamtia ndani.
(xii) Ni muuaji – Alisababisha kuuawa kwa Jabali.

(Hoja 4)

c) Tambua matumizi kumi na mbili ya jazanda katika tamthilia. (Alama 12)

JAZANDA – ni mbinu ya kutumia kitu Fulani ili kutoa maana fiche ya jambo fulani.
Mifano
(i) Bahari mchafukoge- ni jazanda ya mambo kumwendea mrama sudi. Kenga anamaanisha sudi atakumbwa na matatizo au changamoto kali za kimaisha iwapo hataacha kuingilia maswala ya uongozi mbaya wa mzee majoka.
(ii) Keki ya taifa – ni raslimali za nchi ambazo zinanuiwa kuwanufaisha watu wote katika jamii ya sagamoyo. Rslimali hizi zinawafaidi watu wachache kama vile majoka na vibaraka wake.
(iii) Makombo ya keki ya uhuru – (uk. 17) ni jazanda ya raslimali chache wanazopata watu kutoka kwa viongozi.
(iv) Asali – ni jazanda ya mapenzi mjo wa ashua unamfanya majoka kumwona mwanamke huyu kama mtu anayetaka maswala ya mapenzi kutoka ka majoka.
(v) Kutafuta nyuki – ni jazanda ya kutafuta mapenzi/mwanamume ili amkidhie mahitaji yake ya kimwili.

(vi) Ala moja haikai panga mbili – ala inaashiria Ashua nazo panga mbili ni sudi na majoka. Majoka anamfahamisha ashua kuwa wanaume wawili hawawezi kuwa na mwanamke mmoja. Kwa hivo ashua achague kuishi na mmoja wao.
(vii) Milango i wazi – (uk 23) majoka anatumia kwa ashua kama mbinu ya kumwonyesha kwamba, ingawa ameolea yuko tayari kumchukua na kukaa naye.
(viii) Kutoa tonge kinywani (uk. 27) – husda anatumia jazanda hii kumaanisha

mumewe ambaye anashuku kuwa tayari amenyakuliwa na ashua. Ni kutokana na hili ambap yuko tayari kumshambulia mwanamke huyu.

(ix) Kuku na kanga (uk. 28) – Husda anatumia kama njia ya kuonyesha kuwa , kama ashua ameshindwa kumtunza mumewe kama ataweza kumtunza majoka ambaye ni wa kiwango cha juu akilinganishwa na mumewe ashua, bwana Sudi.

(x) Vidhibitimwendo (uk. 33) – hii ni ishara ya kuwazua tunu na wengine wanaoongoza maandamano kukomesha tabia hii yao, na hatimaye kumaliza kabisa.

(xi) Kuwaweka mahalimpao (uk. 34) – hapa kenga anamaanisha yuko tayari kuwaua wote wanaoongoza maandamano na wanaopinga utawala wa majoka mmoja baada ya mwingine hadi waishe.

(xii) Kuota mizizi na kukita na kumea pembe (uk. 35) – kenga anatumia kumwonyesha majoka kwamba Tunu na wapinzani wengine wa mzee majika walianza mambo polepole kasha baadaye wakapata nguvu zaidi hadi sasa wanateleza vitrndo vinavyoenda kinyume na matakwa ya majoka bila woga wowote kama vile kuandaa maandamano.

(xiii) Kutotumia bomu kuulia mbu (uk. 35) – majoka anamfahamisha kenga kwamba hakuna haja ya kutumia nguvu nyingi kupambana na wapinzani wake kama vile akina tunu. Kwake anawaona wakiwa watu wadogo sana ambao wanahitaji nguvu kidogo kuwaangamiza.

(xiv) Kucheza na simba anayenyonyesha (uk. 37) simba ni ishara ya majoka ambaye ni hatari kama simba , huku kutia mikono katika mdomo wa simba ni ile hali ya tunu kuingilia uongozi wa Majoka kwa namna ya kutaka kuuporomosha. Hapa majoka anamwonya tun kwmba ni hatari sana kuingilia utawala wake kwa njia hii.

SWALI LA TAMTHILIA

Kuyaopoa mataifa machanga kutoka kwa kinamasi cha madhulumu kuna gharama yake. Ukirejelea tamthilia ya kigogo, ipatie nguvu kauli hii.

(i) **Kuuawa**

Wapinzani wa uongozi Sagamoyo wanauawa katika jitihada za kuisaidia Sagamoyo. Jabali aliuawa kwa kuwa mpizani wa majoka.

(ii) **Kushambuliwa na vijana.**

Vijana walitumwa kumvamia Tunu, nia ikiwa kumuua. Aliishia kuumizwa vibaya kiasi cha kufanya atumie kiti cha magurudumu.

(iii) **Kudhihakiwa**

Tunu anadhihakiwa na waliouunga mkono uongozi wa Majoka. Alipokwenda Mangweni, anadhihakiwa kwa kuambiwa kwanza aolewe.

(iv) **Vifungo**

Ashua anafungwa kwa kukataa matakwa ya majoka. Kufungwa kwake kulikuwa na nia ya kumshinikiza Sudi amchonge Majoka kinyago.

(v) **Kugotanishwa**

Tunu na Sudi wanachochewa kukosana ili waachane na harakati za ukombozi. Tunu anachochewa dhidi ya Sudi kwa kuambiwa kuwa yeye na Ashua ndio walikuwa wakiwinda roho yake.

(vi) **Kukatiziwa vyanzo vya riziki.**
Sudi na Ashua wanaachwa bila namna ya kupata riziki baada ya soko la chapakazi kufungwa na majoka.

(vii) **Vitisho**
Sudi anatishwa na Kenga kuwa ulimi wake ungemtoma kwenye bahari mchafukoge.

(viii) **Umaskini**
Ashua anavaliwa na uhitiaji kiwango cha kumwendea Majoka kutafuta usaidizi. Watoto wao na Sudi (Pili na Pendo) wanalala njaa.

(ix) **Watu kufurushwa makwao**
Jamii ya kina Siti inaandikiwa vibarua vya kusema wahame Sagamoyo. Hii inatokana na wao kutouunga mkono uongozi wa Majoka.

(xi) **Matusi**
Sudi anarejelewa na Majoka kama Zebe. Majoka ananuia kumdunisha machoni pa mkewe Ashua.

(xii) **Ndoa zao kuingiliwa**
Majoka anapania kuisambaratisha ndoa ya Sudi na Ashua. Anamshawishi Ashua aachane na Sudi na akubali kuolewa naye.

(xiii) **Vyombo vya habari kufungwa**
Baadhi ya vyombo vya habari kama vile runinga ya Mzalendo inafungwa kwa kupeperusha habari kuhusu watetezi wa haki.

(xiv) **Kupigwa marufuku kwa maandamano**
Kenga anamshauri Majoka kutangaza kuwa maandamano yote ni haramu.

(xv) **Kukabiliwa kwa nguvu wanapoandamana.**
Polisi wanatumia nguvu kupita kiasi kuwakabili waandamanaji. Matumizi haya ya nguvu yalipelekea kuumizwa kwa watu na kuuawa kwa vijana kiwandani.

(xvi) **Usaliti kutoka kwa wenzao.**
Juhudi za kuleta ukombozi zinapingwa na baadhi ya Wanasagamoyo kama vile Ngurumo, Asiye na Boza.

(xvii) **Kutimuliwa kwa wafadhili wa watetezi wa haki**
Majoka anatoa pendekezo la wafadhili wa harakati za ukombozi kuvunja kambi.

(xviii) **Kukabiliwa na taasubi ya kiume**
Tunu anapuuzwa na baadhi ya watu kwa kuwa ni mwanamke. Ngurumo

anasema, "Heri nimpe paka (kura)...lakini si mwanamke."

(xix) **Kupumbazwa kwa baadhi ya wananchi**
Baadhi ya wananchi wanapinga harakati ya ukombozi kwa kuwa walipumbazwa na Majoka na watu wake kwa kuachiwa kitu pale mangweni.
Kutenganishwa wakati mikutano muhimu
Wakati Tunu na Sudi wanaenda kwa Majoka kusema naye, majoka anawatenga ili aweze kukabiliana na kila mmoja.

Kuishi kwa hofu na wasiwasi
Bi. Hashima anaeleza jinsi ambavyo wanaishi kwa wasiwasi kutokana na dhiki wanazokutishwa na uonghozi wa Majoka.

Kukosa muda wa kuwa na familia
Sudi alikuwa na shughuli nyingi za kiukombozi, zilizomfanya kukosa muda wa kuwa familia yake.

***4. a)*** *Maneno ya rafiki ya Otii*
Msemewa ni Otii
Walikua katika klabu moja Mombasa
Ni baada ya Otili kuanza urafiki na Rehema Wanjiru

b) Sifa za Otii
- Bidii
- Mvumilivu
- Mchunguzi
- Tamaa
- Mapuuza
- Mpenda starehe
- Msimamo dhabiti
- Hasira
- Kumbulazi

c) Maudhui katika hadithi
- Ukimwi
- Ajali Barabarani
- Usafiri
- Utekelezajichezaji soka
- Ukalili / Dhuluma
- Usaliti
- Uanahabari
- Teknolojia
- uzalendo

5. Maudhui ya umaskini
- Watoto kukosa elimu – wazazi wa Bogoa walishindwa kuelimisha
- Wazazi kushindwa kuwalea watoto wao
- Kudharauliwa kwa watoto maskini
-Watoto wa maskini kufanyishwa kazi za sulubu

- Maskini kukosa mavazi
- Kukosa nauli
- Watoto wa maskini kudhulumiwa
-Masini kubaguliwa ( Pogogo ni ya watu wa chini
- Watoto kuwalaumu wazazi wao – Bogoa hapendi wazazi
- Maskini wanalaumiwa bila hatia – waliokosa kuenda shule walidhaniwa watoto
- Ukosefu wa upangaji uzazi unazidisha umaskini.

5. Mame Bakari

b) Kina dada wanaobakwa wanakabiliwa na changa moto nyingi. Tetea. (al. 10)

- Tukio la kubakwa linampotozea fahamu na anaaibika anapozinduka na kujipata akiwa uchi
- Mwananmke kujeruhiwa – Sara anavuja damu nyingi
- Mwananmke kuvunjiwa ujanajike na utu wake
- Maisha ya mwanamke kuingiliwa na kuharibiwa
- Kukatizwa masomo
- Kukejeliwa – mwalimu mkuu
- Mwanamke anateseka kiakili – Sara ana mawazo mengi
- Mwanamke kubebeshwa mimba katika umri mdogo
- Kuishi adhabu ya wazazi – Sara anahofia babake
- Kuogopa kutoa habari ya kubakwa kwa wazazi kwa sababu hawangemwamini
- kuishi maisha ya kimaskini
- Kulaumiwa hata kama ni yeye aliyebakwa

Majibu

a) Eleza dhamira ya shairi hili (al.2)

- Kueleza madhara ya kutofuata mawaidha / ushauri wa baba na mama
- Kuonyesha hasara/shida zinazowapata watu walio na kiburi, majivuno, tamaa

***2 x 1 = 2***

b) Tambua njia mbili anazotumia mtunzi wa shairi hili kuusisitiza ujumbe wake. (al.2)

- Matumizi ya kibwagizo
- kurejelea methali k.m "majuto ni mjukuu huja kinyume 2 x 1 = 2

c) Taja na utoe mifano ya aina zozote mbili za tamathali za usemi zilizotumika katika shairi. (al.4)

- Swali la balagha – ya nini kushangaa?
- anyemelea
- Jazanda – umelichimba la kukuzika handaki
- Istiari – ulijidharia samba 2 x 2 = 4

d) Andika ubeti wa tatu katika lugha nathari/tutumbi (al.4)

- Yale uliyoyaona kuwa bora ndiyo sasa yamekuletea shida. Mamia ya matatizo hayaishi kwako. Iwapo ungetambua hapo awali basi hungekuwa ukitatizika. Wewe mwenyewe ndiwe chanzo cha haya. 4 x 1 = 4

e) Kwa kutoa mfano mmoja mmoja onyesha aina mbili za idhini ya kishairi katika shairi hili (al.4)
- Inkisari – alikuamba badala ya alikwambia
- Kuboronga sarufi – alikwambia huko mama badala ya alikwambia mama yake
- Lahaja – huaziriki / hupuliki 2 x 2 = 4

f) Bainisha toni ya shairi hili (al.2)
   i) Toni ya majuto – anashangaa mambo yanavyomwendea
   ii) Toni ya kusikitika – anasikitika mishikeli haitoki kwake ( matatizo yameganda)

2 x 1 = 2)

g) Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika shairi (al.2)
   i) mstahiki - ***mheshimiwa***
   ii) hupuliki - ***husikii / husikizi***

***2 x 1 = 2***

**Majibi**

a) Lipe shairi hili kichwa mwafaka (al.1)
- Mama nitarudi
- Nitarudi
- Kizuizini 1 x 1 = 1

b) Tambua nafsineni katika shairi hili (al.2)
- Nafsineni ni mfungwa aliye kizuizini. Anauliza iwapo mamake angali anasimama na kusubiri akitazama kule kizuizini aliko nafsineni2 x 1 = 2

c) Eleza toni katika shairi hili (al.2)
- Toni ya masikitiko / uchungu wa moyoni/huzuni. Anasikitikia hali yake ya kuvaa matambara, njaa, kufanyiswha kazi tele n.k
- Toni ya matumaini. Mshairi ana matumaini kwamba siku moja atatoka kizuizini

2 x 1 = 2

d) Taja mambo manne ambayo mshairi analalamikia (al.4)
- Kuachwa njaa
- Kufungwa
- Kufukuzwa
- Kutopewa nafsi ya kupumzika, kulala na kuwaza
- Kuvaa matambara
- Kufanyizwa kazi kama mnyama 4 x 1 = 4

e) Fafanu dhamira katika shairi hili (al 2)
- Mshairi anadhamiria kulalamikia/kukashifu namna anatumiwa vibaya kizuizini
- Mshairi anakashifu madhila na mateso ambayo wafungwa hutendewa
- Kumpa mamake matumaini kwamba atatoka kizuizini siku moja

2 x 1 = 2

f) Thibitisha kuwa hili ni shairi huru (al 2)
- Mistari mishata k.m ya kulala hakuma
- Idadi ya mishororo inahatilikabadilika kutoka ubeti mmoja hadi nyingine
- Vina
- mizani

2 x 1 = 2

g) Taja na ufafanue sifa mbili za mshairi (al 2)
- Ni mwenye kulalamika – analalamikia hali yake ya kuwa na njaa, kupigwa
- Mwenye matumaini – anatumai kuwa siku moja atatoka kizuizini
- Mwenye mapenzi – anampenda mamake na kumwita mama mpenzi

2 x 1 = 2

h) Fafanua mbinu 3 za kimtindo zilizotumika katika ubeti wa tatu (al 3)
- Takriri – neno 'nitarudi' lilmerudiwarudiwa
- Mdokezo – nitarudi mama mpenzi
- Tashibihi – "kupitia mwingine kama shetani"
- Taswira
- balagha

i) Eleza maana ya maneno yafuatoyo kama yalivyotumiwa katika shiari hili (al 2)

i) Hayawani - ***mnyama***

ii) Nadhari - ***fikira***

**FASIHI SIMULIZI**

a)Maudhui na Fani ya maigizo hutegemea mwigizaji. Thibitisha kwa hoja tano. (al5)
- ✓ sharti mwigizaji aigize kwa ujasiri ili aweze kupitisha ujumbe wake kwa ufasaha
- ✓ awe na uwezo wa kubadilisha uigizaji wake papo hapo kutegemea hadhira yake na kutoa mifano inayofahamika kutoka kwa mazingira ya hadhira yake.
- ✓ Awe na ubunifu wa hali ya juu
- ✓ Ni mwenye ujuzi wa kutumia ishara za uso, za mwili na miondoko ambayo inaoana na hali anayoigiza.
- ✓ Ni mwenye ujuzi na ufasaha wa lugha.
- ✓ Anaielewa hadhira yake ili abadilishe mtindo wa uigizaji kulingana na kiwango na matakwa yao
- ✓ Anapaswa kuvaa maleba yanayooana na nafasi anayoigiza
- ✓ Aweze kubadilisha toni na kiimbo kulingana na hali tofauti tofauti za matukio anayoigiza
- ✓ Hushirikisha hadhira kwa kuuliza maswali ya balagha ili kuondoa uchovu wa kutazama na kusikiliza tu uigizaji na kumsaidia kuboresha uwasilishaji

b) **Taja aina mbili za miviga (al 2)**
- ✓ Jando
- ✓ Harusi
- ✓ Matanga
- ✓ Sherehe za ulaji kiapo
- ✓ Matambiko
- ✓ Sherehe za kutawazwa kwa viongozi
- ✓ Sherehe za kuzaliwa kwa mtoto
- ✓ Shughuli za posa
- ✓ Ibada
- ✓ Shughuli za kufukuza pepo

c) **Eleza hasara tatu za miviga (al 3)**

- ✓ baadhi ya miviga kama vile kutiwa unyagoni kwa wasichana na kurithi mke wa mtu aliyeaga zimepitwa na wakati na huhatarisha maisha na afya ya wanajamii
- ✓ baadhi ya miviga hukinza malengo ya kitaifa km kutia unyagoni kwa lazima na ukeketaji wa watoto wa kike ni ukiukaji wa haki za binadamu
- ✓ hujaza watu hofu. Km miviga inayohitaji kafara ya binadamu katika baadhi ya jamii huogofya
- ✓ baadhi ya miviga huhusisha ushirikina
- ✓ baadhi ya sherehe za miviga hugharimu kiasi kikubwa cha pesa na kuacha familia katika hali duni kiuchumi.

1. Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali

Ikiwa kweli wewe ni mkazamwanangu,
Nami ndiye nilompa uhai mwana unoringia,
Anokufanya upite ukinitemea mate,
Chakula kuninyima, wajukuu kunikataza ushirika,
Miungu nawaone chozi langu, wasikie kilio changu,
Mizimu nawaone uchungu wangu,
Radhi zao wasiwahi kukupa,
Laana wakumiminie,
Uje kulizwa mara mia na wanao,
Usiwahi kufurahia hata siku moja pato lao,
Watalokupa likuletee simanzi badala ya furaha,
Wakazawanao wasikuuguze katika utu uzima wako!

**Maswali**

a)Tambua aina ya mazungumzo katika tungo na utoe sababu (al2)

- ✓ **Maapizo –mhusika anamuomba Mungu kumwadhibu mkaza mwana wake kwa hila zake**

b) Msemaji ni nani katika tungo hili (al1)

- ✓ **mzazi wa mume wa anayezungumziwa**

c Tambua sifa mbili za anayeelekezewa mazungumzo (al2)

- ✓ **mchoyo – anamnyima chakula mzazi**
- ✓ **mwenye dharau- anamtemea mzazi**

d) Taja na ueleze sifa tano za kipera hiki cha mazungumzo (al5)

- ✓ maapizo hutolewa kwa watu ambao walienda kinyume na matarajio ya jamii zao. Km wabakaji, wezi, wauwaji, na waliowatusi wazazi
- ✓ yalitolewa kabla ya ulaji viapo
- ✓ yanaweza kutolewa moja kwa moja na yule aliyeathirika.
- ✓ Huaminiwa kuwa yataleta maangamizi kwa jamii, kwa hivyo wanajamii hushauriwa kuyaepuka kwa kutenda mema
- ✓ Hutumia lugha fasaha (ulumbi)
- ✓ Hutumia lugha kali inayonuiwa kujaza woga ili kuonya dhidi ya maovu.

# MANG'U HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

## Mwongozo wa Kusahihisha

**1. Muundo**

Zingatia lugha ya mtiririko.

i) Kujitambulisha – Jina
- Kuzaliwa/Eneo/Kaunti nk.
- Malezi yake
- Elimu - Msingi - Sekondari - Vyuo mbalimbali alivyosoma

ii) **ii) Tajiriba** - Kazi aliyofanya/alizofanya kabla ya kuwa Gavana. - Siasa – kiwango/viwango gani? - Anatajika kwa jambo/mambo gani. Mifano: - Elimu ya juu – shahada kadha. - Miradi ya maendeleo. - Ziara alizofanya. - Uwajibikaji wake/maadili kazini. - Falsafa yake ya maisha. - Malengo yake. - Changamoto alizozipitia. - Ruwaza/maazimio yake. Lugha – Mtahiniwa atumie nafsi ya kwanza. Usemi ya taarifa. Lugha rasmi itumiwe.

**2. Hoja**

- Maadili yatazorota.
- Njia za mkato maishani.
- Uzembe kazini.
- Ukosefu wa uwajibikaji.
- Mapuuza.
- Kutothamini mitihani.
- Elimu kudorora.
- Kuathirika kwa taaluma mbalimbali.
- Utendakazi utaathirika.
- Nidhamu kutoweka.

**3. Mtenda mema kwa watu atendea nafsiye.**

**Maana:** Kuwafanyia wema watu ni sawa na kujiwekea akiba. Huenda nao wakakutendea wema utakapouhitaji. **Funzo:** Usidhani unafanya kazi ya bure unapomfaa mtu Fulani. **Matumizi:** Inaweza kuhimizwa anayefikiria kuwa wema uatendao ni wa bure na kuwa hatafaidika hata akiendelea. Mtahiniwa aandike kisa kitakachodhihirika pande zote mbili.

**4. Maumbo ya kuzingatiwa.**

i) Kisa kinachofaa kuwa katika wakati uliopita. ii) Mtahiniwa azingatie kumaliza kisa chake kwa maneno yote yaliyodokezwa. iii) Mahali pa tukio patajwe. iv) Baadhi ya matukio;
- Moto
- Wizi
- Ugaidi
- Baharini/majini
- Ajali barabarani

# MANG'U HIGH SCHOOL

## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019

## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

## Mwongozo wa Kusahihisha

**1.UFAHAMU**

(a) Kumaliza visa vya ajali vilivyokithiri (wananchi kuzingatia sheria za barabarani.) (1 x 2 = 2)

(b)
- Kupunguza masharti yaliyowekwa na wizara.
- Magari mengi yamekuwa kachara.
- Magari mengi yameng'olewa vidhibiti mwendo.
- Magari kuendeshwa kwa kasi ya umeme.
- Magari hayana mishipi ya usalama.
- Magari kucheza mizigi kwa sauti ya juu.
- Kuwapakia abiria kupita kisai. (zozote 4x1 = alama 4)

(c)
- Wasafiri kupuuza masharti yaliyowekwa.
- Hawafungi mishipi ya usalama.
- Wasafiri wanakubali kuingia katika magari yaliyojaa tayari.
- Watembeaji barabarani kutozingatia sheria za kawaida.
- Kutotumia vivuko wakati wa kuvuka barabara.
- Wasafiri kunyamazia makosa kwenya magari. (zozote 3x1 = alama 3)

(d)
- Kuchukuwa kadhongo.
- Kuyaachilia magari yaliyo na kasoro.
- Kutoshtaki magari yaliyo na kasoro kulingana na sheria.

(e)
- Kondakta - utingo, tandiboi
- Toa ilani - toa onyo / tangazo
- Toa makataa - toa mapatano

**2.UFUPISHO**

(a)Mambo muhimu yanayostahili kuzingatiwa katika kutathmini viwango vya karo katika shule nchini Kenya. (Maneno 65 - 70)
-Kushirikiana na walimu wakuu.
-Gharama ya vitabu, karatasi za uchapishaji wa mitihani.
-Ununuzi wa kemikali katika maabara.
-Gharama za kuendesha michezo na tamasha za muziki.
-Gharama ya shule za malazi.
-Kupanda kwa gharama ya maisha.
-Maeneo yapatikanapo shule.
-Kiwango cha shule.

-Programu za kitathmini shuleni / mfumo wa masomo katika shule husika - gharama ya kununua vyombo vinavyohitajika katika masomo haya.
-Motisha ya walimu na wafanyakazi wengine.
-Kuwaajiri walimu wa ziada.

-Gharama ya lishe bora. (hoja zozote 8, alama 8, 1 ya mtiririko)

(b)Fupisha aya tatu za mwisho. (maneno 40 - 45)
-Serikali haipaswi kuweka viwango sawa vya karo kwa kile shule.
-Hili huenda likazua mgogoro wa kiutawala.
-Shinikizo la kupunguzwa karo katika shule ya upili zinafaa kutetewa kimantiki na wala si kihisia.
-Serikali ingewajibika kwa kuwaajiri walimu wa kutosha.
-Walimu wangeongezewa mshahara, kuwazidi na kuwapandisha vyeo.

-Hatua zichukuliwe dhidi ya walimu wanaowatoza wazazi karo ya juu.
-Hatua ya waziri wa Elimu kukutana na washikadau katika sekta ya elimu ni ya busara.
-Hii inafaa kutoa mwelekeo mzuri kuhusu maswala tata yaliyopo kwa sasa.
(hoja zozote 5x1 = alama 5)

**3.MATUMIZI YA LUGHA**

(a)

| | Sehemu ya kutamkia | Mwinuko wa ulimi | Hali ya midomo |
|---|---|---|---|
| / e / | mbele | wastani | tandazwa |
| / i/ | mbele | juu | tandazwa |
| /u / | nyuma | juu | viringwa |

(atuzwe alama 3 anapoata sehemu zote. Akikosa hata moja atuzwe sufuri)

(b) -Irabu pekee - o / a
-Konsonanti moja na irabu - wa, ya, la, ki, ni, na
-Konsonanti moja - m - tu
-Silab mwambatano - cha, mchwa, n.k.
-Siabi funge - mak-taba, ek-sirei, daf-ta-ri. 1x2 = 2)

(c)
- Mghuno
- mtikisiko wa nyuzi sauti / glota.
- Mrindimo wa nyuzi sauti / glota
- Mtetemeko wa nyuzi sauti / glota.
- Msepetuku wa nyuzi sauti / glota. (1x2 = 2mks)

(d) Kishazi - ni sehemu ya sentensi iliyo na kiarifa na hubeba maana kamilifu au isiyo kamilifu.
Kirai - maneno aghalabu mawili au zaidi yanayowekwa pamoja na hutekeleza juumu sawa (hufanya kazi pamoja) kwenye sentensi./fungu la maneno lisilo na maana kamili/fungu ;la maneno lisilo na muundo wa kiima kiarifu

(e)
- Nafsi
- Wakati / njeo / hali
- Matarajio
- Urejeshi
- Ukanushaji
- Ngeli
- Kitendwa / mtendwa

(f) Chumvi - I - I
Nywele - U - ZI
Mafuta - YA – YA

(g)
- Kiambishi cha ngeli
- Ngeli
- Mahali (3 x ½ = 1½ )

(h) Tajiri mlevi alipigwa (hakiki jibu la mwanafunzi) na wahuni vibaya lakini hakufariki. ( 8 x ½ = 4_

(i) Ungalivumilia wakati ule ungalipata zawadi kubwa.(2 x 1 = 2)

(j) Kijipu kilipasuka chenyewe.
(1x1 = 1)

(k)
- Kuunganisha maneno mawili.
- Uundaji kutoka lugha nyingine / ukopaji / kutohoa.
- Kuzua maneno mapya.
- Unyambuaji / uambishaji.
- Kufananisha sauti zitokazo kwa kifaa fulani.
- Vifupi vya maneno / finyazo.
-Uundaji kutokana na nomino, kivumishi, na maneno mengine.(3 x 1 = 3)

(l) Askari jela, mwana muziki n.k.
(m)Mti umekatwa. U - I
Miti imekatwa (hakiki majibu ya mwanafunzi na sentensi iwe katika umoja na wingi).(2x1 = 2)
(n) Kutendeana - kila mmoja kufanya kwa niaba ya mwenzake.
Kutendana - kuathiriana wenyewe (mwanafunzi atoe mfano).(2x1 = 2)
(o) Yambwa tendwa (kipozi) - mlango.
Yambwa tendewa (kitondo) - Rashid
Ala / kitumizi - ufunguo
(p) Babu yangu alinishauri ya kuwa / kwamba angetaka nifikirie sana juu ya maisha yangu ya ndoa kwa vile hangetaka niishi maisha yasiyokuwa na mwelekeo. (3 x ½ = 3)
(q) Ritifaa
- Kubainisha sauti ya nazali k.v. ng'ombe
- Kuonyesha tarakimu k.v. ‗97
- Kuonyesha herufi imeachwa k.v. mt'choka. (2 x ½ = 1)

Koma / Kituo
- Kuorodhesha vitu
- Kupumua kwenye sentensi ndefu
- Anwani
- Baada ya vina kwenye ushairi. (2 x ½ =1)

r) Maana ya msemo kula kitana ni kukumbwa na taabu au mashaka.

**4. ISIMU JAMII**

(a) Lugha rasmi ni lugha inayotumika katika shughuli za kiserikali k.v. bungeni, utawala na katika utungaji wa sheria.

(b) Sifa za lugha rasmi.

- Lazima itambuliwe na serikali husika.
- iwe na msamiati tosha wa kisayansi na ufundi.
- Sio lazima iwe na wazungumzaji wengi katika nchi husika.
- Inaweza kutumiwa katika kiwango cha kitaifa na kimataifa.
- Inaweza kuwa na hadhi kamili au hadhi isiyo kamili.
- Hutumia sentensi ndefu nefu ambazo huw azimekamilika.
- Hushehenitasfida kwa sababu ya heshima ya kiutawala.
- Baadhi hutumia lugha mseto hata kuhamisha msimbo.
- Lugha huwa fasaha na yenye kuzingatia kanuni za matumizi ya lugha hiyo.
- Haina utani, rasmi pekee ndio hutawala.
- Matumizi ya msamiati maalum kulingana na mazingira na taaluma husika mf. sheria, utabibu, kilimo. (alama 8x1 = 1)

# MANG'U HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

**SEHEMU YA A:HADITHI FUPI**
**TUMBO LISILOSHIBA**
**1.LAZIMA**
**a) Weka dondo katika muktadha (ala 4)**

Maneno ya wanafunzi wa shule ya Busukalala.
Akimwambia Rasta/ Samueli Matandiko.
Walipokuwa shuleni.

Samueli alikuwa ametoka katika afisi ya mwalimu mkuu kuchukua matoke yake ya mtihani.Marafiki waliomjua wanamtaka awaelezee alama zake.

**b) Taja mbinu zilizotumiwa na mwandishi katika dondoo hili (ala 2)**
i)Utohozi -rasta ii) nidaa-Rasta twambie bwana!
**c) Ni kwa vipi mzungumziwa anamchukulia mwalimu mkuu kama hambe? (alama 4)**
Mwalimu mkuu wa shule ya Busukalala hakuwahi kumwamini Samueli hata siku moja kama anaweza kufaulu mtihani

Mwalimu mkuu hakuamini Samueli aliposema kuwa amelipa ada mpaka alipohakikisha kwa kuangalia nyaraka na kumbukumbu zake.
Anamwonyesha Samueli dharau kwa kumrushia karatasi kama mbwa; anarejelea kile alichokuwa akifanya na kumpuuza.
Mwalimu mkuu hakumpa ushauri wowote Samueli ambo unmgemsaidia kupokea matokeo yake ambayo hayakuwa mazuri hata kidogo.
Mwalimu mkuu alimjibu Samueli kwa karaha, alipomwita kuwa ni fidhuli. Anamjibiza kwa kuuliza iwapo wanafunzi wengine wanalipa mawe au majani.
**d) Je, mtihani wa maisha ni anwani faafu ya hadithi hii. (alama10 )**

i. Mtihani wa Maisha ni anwani ambayo imesawiri maudhui ya hadithi hii kwa kiwango kikubwa.
ii. Samueli anafanya mtihani wake wa shule ya upili na kuenda kuyachukua matokeo. Kabla ya kufikia zamu zake Samueli anajichunguza na kujipima uwapo ameufanya vizuri. Mawazo kuhusu mtihani huo yanamtawala.
iii. Alianza kuwachunguza wanafunzi waliokuja kuchukua matokeo ya mtihani wanaopotoka mlangoni ili kujaribu kuona iwapo wamefaulu au la.
iv. Samueli anajaribu kujiaminisha kuwa yeye atakuwa amefaulu mtihani wakati akiwa kwenye foleni ya kuchukua matokeo.
v. Samueli anajiaminisha kuwa yeye ni mjanja na angemshangaza mwalimu mkuu.
vi. Anagundua kuwa amefali mtihani huo. Safu za alama ya D na ilimkodolea macho. Herufi hizo zilimfedhesha na akalemewa.

vii. Nyumbani baba yake aliyengoja matokeo kwa hamu hakuyapata.
viii. Samueli anadanganya kwamba ana salio la karo.
ix. Baba anarauka na kutembea kilomita sita kwenda kuchukua matokeo ya mtihani.
x. Anapogundua ni uwongo anapandwa na hamaki.
xi. Samueli anaamua kujitosa bwawani ili aondokane na athari za kufeli mtihani huu wa kitaaluma. Hata hivyo amaokolewa na mpita njia.
Mama yake anamwambia kuwa ingawa amefeli mtihani wa shule, asikate tamaa, bado ana mtihani wa maisha ambao anaweza kufaulu. Anwani hii inafaa sana

## SEHEMU YA B:TAMTHILIA
## KIGOGO (PAULINE KEA)

**Jibu swali la 2 au 3**
2. "Keki ya uhuru imeliwa kwingine,mwaletewa masazo"
(a) Fafanua muktadha wa dondoo hili . (alama 4)
(b) Taja na uthibitishe tamathali ya usemi katika dondoo hili .
(alama 2)
(c) Eleza namna keki ilivyoliwa katika tamthilia hii.

(alama14)

(a)-msemaji ni Sudi
-Anawaambia Kombe na Boza
-katika soko la Chapakazi

-baada ya kutembelewa na Kenga kisha akawaachia kipande cha keki
**ZOZOTE 4×1=4**
(b) -Istiari/Jazanda-----keki inaashiria rasilimali za nchi **1×2=2**
(c) -rasilimali za nchi zinafujwa na wachache.Majoka ana Majoka and Majoka company,Majoka acdemy n.k
- soko la chapakazi kunyakuliwa na Majoka
-maskini wanakosa pahali pa kupata riziki baada ya chapakazi kufungwa
- njaa imesambaa kote.watoto wa Sudi wanakosa chakula cha kutia tumboni ilhali Majoka anastarehe kwa vyakula mbalimbali
- wafanyikazi hawana bima ya hospitali kwa mfano babake Tunu
- ajira kwa kazi zipo kwa wachache ambao wanachangamkia uhuni
- kandarasi hupeanwa kwa kujuana.mamapima anauza uroda kwa Ngurumo na kupewa kibali cha kuoka keki
- mamapima anapewa kibali cha kuuza pombe haramu kinyume cha katiba
- kuhalalishwa kwa pombe haramu

**zozote7x2=14**

3. Fafanua mbinu zifuatazo kwa kutolea mifano mwafaka
(i) Kwelikinzani (alama 10)
(ii) Taashira

**Kweli kinzani**
-Habari zinazotolewa na mjumbe katika rununu ni za kinaya, kuwa Wanasagamoyo wasirudishe maendeleo nyuma bali wafurahie ufanisi ambao umepatikana katika kipindi cha miaka tisini baada ya uhuru.
-Ujumbe huu ni kinaya kwa vile Sagamoyo hakuna maendeleo wala ufanisi.Watu wana njaa na wanakosa mambo ya kimsingi kama vile maji, elimu na matakwa mengine mengi.
-Boza anadai kuwa kulipa kodi ni kujenga nchi na kujitegemea. Kauli hii ni kinaya kwa vile kodi wanayolipa wanasagamoyo haitumiki kujenga nchi kwa vyovyote vile.
-Sudi anasema kuwa katika kipindi cha mwezi mzima wa uhuru wale mali walizochuna kwa miaka sitini. Ni kinaya kwa kuwa hakuna walichovuna, viongozi hujilimbikizia mali.
-Boza anamwambia Sudi kuwa wanatia doa kwa kila jambo nzuri.Ni kinaya kwa vile hakuna mambo mazuri ambayo Majoka amefanya Sagamoyo
-Wanasagamoyo kusheherekea miaka sitini ya uhuru ni kinaya kwani hakuna cha muhimu kusheherekewa, hakuna maendeleo Sagamoyo.
-Boza anadai kuwa kinyago chake chapendeza na kufanana na shujaa Marara Bin Ngao, ni kinaya kwani kinyago hicho hakifanani na shujaa huyo.
-Mzee Majoka kudai kuwa anamheshimu sudi ni kinaya.Majoka hana heshima kwa

raia wake, nia yake ni kutaka Sudi amchongee kinyago
-Kenga kumwambia Sudi kuwa ipo siku atamtafuta mzee Majoka ni kinaya kwani Sudi hana haja naye.

-Majoka kudai kuwa takataka za soko zitaaribu sifa nzuri za jimbo la Sagamoyo ni kinaya kwa vile hakuna sifa nzuri Sagamoyo.Viongozi wanaendeleza maovu na hata kupanga mauaji.
-Kauli ya Husda kuwa Ashua ni kimada wa Majoka ni kinaya kwa vile Ashua hana nia yoyote na Majoka.Amefika kwake kuomba msaada.
-Ni kinaya kwa polisi Sagamoyo kutawanya waandamanaji.Polisi wanapaswa kulinda na kutetea haki za wananchi.
-Majoka kusema kuwa Sagamoyo wanajiweza ni kinaya.Watu wana matakwa mengi, ni maskini, wana njaa na hata kupata ufadhili kitoka nje kwa miradi isiyo muhimu.
**zozote 10×1=10**

**Taashira**
-Kinyago cha shujaa anachochonga Sudi kwamba shujaa huyo ni mkubwa kuliko jina lake na urembo wa shujaa huyo ni bora zaidi.Shujaa anayerejelewa hapa ni Tunu,yale ambayo anatendea Sagamoyo ni makuu kuliko jina lake, kutetea haki za wanyonge.
-Husda anamwambia Ashua kuwa hawezi kumtoa tonge kinywani hivi hivi.tonge ni Majoka bwanake Husda kuwa Ashua hawezi kumnyanganya bwana.
-Husda kumwita Majoka pwagu, pwagu ni mwizi na Majoka amewaibia wanasagamoyo;ananyakua ardhi, anaiba kodi na kuwalaghai wanasagamoyo
-Husda anamwambia Ashua kuwa ameshindwa kufuga kuku na kanga hatamweza.Kuku ni mumewe Sudi, na Kenga ni Majoka, kwamba Ashua ameshindwa kumtunza Sudi na Majoka hampati

-Tunu kuwekewa vidhibitimwendo ni kukomeshwa au kuwekewa vikwazo ili afe moyo kutetea haki za wanasagamoyo.
-Majoka anasema kuwa hatatumia bomu kuulia mbu.Anamrejelea Tunu kuwa mbu kunaanisha hatatumia nguvu nyingi kumwangamiza
-Majoka anasema ili kuongoza Sagamoyo ni lazima uwe na ngozi ngumu, kumaanisha ni lazima uwe mkali na mwenye nguvu.
-Jukwaa kupakwa rangi kwa ajili ya sherehe ya uhuru ni kufunika uozo ulio Sagamoyo.
-Majoka anaposema salamu zinamgoja Sudi kwake,salamu ni Ashua mkewe aliye ndani ya jela.
-Majoka anamshauri Sudi anawe mikono iwapo anataka kula na watu wazima.Kunawa mikono ni kukubali kuchonga kinyago ndiposa Ashua mkewe aachiliwe.
-Chopi anamwambia Sudi iwapo shamba limemshinda kulima aseme.Shamba anarejelea Ashua kuwa iwapo Ashua amemshinda kutunza, aseme atunziwena Majoka.
-Siafu huwa wengi na si rahisi kuwamaliza.Siafu ni wanasagamoyo ambao ni wengi kuliko Majoka na si rahisi kuwashnda.Hatimaye raia wanamshinda Majoka. (uk52)
**zozote 10×1=10**

## SEHEMU YA C:RIWAYA
## CHOZI LA HERI(ASSUMPTA)
**Jibu swali la 4 au 5**

4.a)Haya ni maneno ya mamamake Ridhaa akimwambia Ridhaa wakiwa nyumbani kwa Ridhaa iliyo kwenye msitu wa Heri baada ya Ridhaa kudai kwamba hataki shule kwani amebaguliwa na wanafunzi wenzake kwa kukataa kucheza na yeye mchezo wa kavuta na kumwita mfuata mvua

b)Msemaji ni mamake Ridhaa
-mwenye busara –anamwelekeza Ridhaa namna ya kuishi na wanafunzi wengine
-mpenda amani-anatakaa wanafunzi waishi kwa umoja ili wasome
-mshauri mwema-anamshauri Ridhaa kumwambia ni vyema kujifunza namna ya kuishi na marafiki zake bila kujali tofauti za ukoo na unasaba.
-ni mwenye taasubi ya kiume-anamwambia Ridhaa kwamba unyonge haukuumbiwa majimbi ulitunukiwa makoo.Anawadunisha/kuwadharau wanawake kwa kusema wao ndio wanafaa kulia ovyo ovyo

c) –mzee Kedi alimchomea Ridhaa nyumba yake pamoja na aila yake hadi ikaangamia
- Ridhaa alibaguliwa na wanafunzi wenzake huko shuleni kwani wlikataa kucheza nay eye na kumwona yeye kama amekuja kuwashinda mitihani.Tena walimwona kama mfuata mvua.
-Ridhaa aliyapoteza majumba yake moja likiwa kwenye mtaa wa Zari kwa kuambiwa limejengwa barabarani ambapo pamepangiwa ujenzi wa barabara mbadala(by-pass).Tena alilipoteza jumba jingine lililochomeka la upagazi na kuambiwa limechomeka kutokana na hitilafu za nguvu za umeme

-Ridhaa alirushiwa vijikaratasi baada ya kutawazwa kwa kiongozi mwingine akitahadhirishwa kwamba kuna gharika .Hayo yote yalitokana na tofauti za ukoo.
-Jirani wa Ridhaa alikata guu mara moja
-mke wa jrani wa ridhaa analalamikia kuuziwa kwa mashamba kwa wageni kumbe pale Ridhaa alivyo anaoekana kama mgeni.
-Selume alibaguliwa na wakweze zake wakidai kwamba mume wake alimuunga mkono mwekevu na tena wkadai yeye alimtorosha mtoto wa kikwao na kumwoa
-Ndoa ya Lucia ilipingwa sana na ami zake kwa kuwa kumekuwa na tofauti kuu kati ya ukoo wa waombwe na ule wa Anyamvua kwani waombwe ni watu walafi sana.
-Subira alibaguliwa sana na mavyaa wake kwa kuwa subira ni mwenye ukoo wa Bamwezi.Subira alionekana kama yeye ndiye chanzo cha wao kuchomewa
-Kiriri alisekuliwa kwenye mtaa wa matunda na mali yake kufilisika kwa kuwa alionekana kama mgeni
-Billy alimwendea mpenzi wake(sally) ughaibuni kwani hakupendezwa na wanawake kutoka bara la giza
-Rafiki wa kaizari anamshauri kaizari ahame kwani tofauti za ukoo zimezua uhasama na anamhakikishia atamlindia nyumba yake

-Subira alishambuliwa na vijana watano wakidai Kaizari alimuunga mkono mwekevu
-lime na mwanaheri walishambulia na vijana watano na wakawabaka na haayo yote

yalitokana na tofauti za ukoo

5. (a)Kweli kinzani
-Tila kusema kuhusu mtoto wa miaka hamsini na hakuna mtoto mwenye umri wa miaka hamsini
-Mwangeka aliienda kulinda usalama mataifa mengine na kwao hakuna usalama
-Wanakijiji walimwona Ridhaa kama mgeni na yeye ndiye alipabadilisha mahali hapo pa msitu wa heri.
-Viongozi wananchi wanawapeleka watoto wao kusomea ng'ambo
-Wana wa kiriri walikataa kurudi kwao
-Annette alimnyima ushirika wa watoto wake
-Naomi kutoroka na kuwaacha watoto ambao wanahuhitaji mkubwa wa mzazi wa kike
-Mavyaa wa Subira anamwona subira kama muki
-Wanakijiji walisababisha mauko ya Lemi na hakuwa na makosa
-Tuama kumuasi babake kwa kujificha kwenda kupashwa tohara
**ZOZOTE 10**

(b)Sadfa
-Mwangeka na mwangemi wanakutana mahali pamoja bila kupanga
-Dick na Umu walikutana kwenye uwanja wa ndege kisadfa
-Dick,Umu na Mwaliko walikutana kwenye hoteli ya Majaliwa
-Neema alikiokota kitoto pipani
-Familia ya Ridhaa iliangamia wakati alipokuwa ameenda kufanya kazi yake ya udaktari
-Siku ya kuzaliwa kwa Umu ilisadifiana na siku ya kuzaliwa kwa mwangemi

-Tina na mwangeka walipokuwa wakiigiza mazishi ya Dede babake alikuwa amejibanza kiambazani akiwatizama.
-Mwangeka alimwoa mjane kama yeye
-Apondi aliolewa na Mwangeka ambaye alikuwa akifanya kazi ya kulinda usalama kama bwana Mandu
-Umu na Mwaliko walipangwa na wazazi ambao walikuwa ami-mwangeka na mwangemi
**ZOZOTE 10**

**SEHEMU YA D :USHAIRI.**

6.
(a)-mishororo mine kila ubeti.
-vipande viwili kila mshororo .
-vina vya ndani na nje vinabadilika kila ubeti .
-mizani 16 kila mshororo wa ubeti .
-kituo kinabadili ka kila ubeti.
**-beti 4** **zozote** 4×1=4

(b)-ukabila na mila visitutenganishe .
-nidhamu huleta amani .
-tusintumike kuzua na kushiriki vita .

-palipo na amani pana maendeleo **zozote 4×1=4.**

(c)-Mstari kifu ni ule umejitosheleza kimaana na kiujumbe .Mishororo yote ya kila beti ni kifu isipokuwa wa tatu ukwapi ubeti wa 2 .
-MSHATA ni mshororo ambao haujajitosheleza kimaana na kiujumbe – mshororo wa 3 ubeti wa pili ukwapi . **zozote2×1=2**

(d)-wananchi woto tusikubali kupigana .
-baada ya vita huja majuto .
-tutakosana bila maelewano .
-hali itazorota hata tukose kuthaminiana .
**Zozote 4×1=4**
(e)-KIKWAMBA – kuna urudiaji wa maneno katika kila mshororo **.** **1×2=2**

(f)-Takriri neno –hili – hili
-Takriri silabi –vina **zozote 2×1=2**

(g)-INKISARI – inostahili ,tusende nk
-KUBORONGA SARUFI/MIUNDO NGEU – vita tusende tumika
**Zozote2×1=2**

7
a) Bahari za shairi
– Tarbia – Lina mishororo 4 katika kila ubeti
– Mathnawi – Lina pande 2 katika kila mshororo
– Ukara – Vina vya nje vinatiririka ilhali vya ndani havitiririki. (zozote 3 x 1 = 3)

b) Methali
(i) Akipenda, kipofu huita kengeza (ubeti wa tano)
– Mwenyewe amemkubali alivyo na hawawezi kumgeuza ingawa wanamsengenya.

ii) Aliyekupa wewe kiti ndiye aliyenipa mimi kumbi (ubeti wa saba)
– Hakuna aliyejiumba hivyo waache kusema udhaifu wake.

iii) Pilipili usiyoila yakuashani? (ubeti wa 6 mStari wa 3) (zozote 2 x 2 = 4)

c) Maudhui
– Msimulizi anampenda vile alivyo – mwenyewe amemkubali
– Wanakerwa kwani hawana mke
– Wanayoyasema hayawahusu wao bali ni kati yake na yeye
– Anayezungumziwa hakujiumba mwenyewe bali ni mungu (muumba)
– Anawaambia wasitumie udhaifu wake kumsengenya
– Ingawa wanayoyasema yanamliza Aziza, yeye hajali.
– Wadaku wanatahadharishwa wasikufuru (zozote 4 x 1 = 4)

d) Uhuru/idhini ya mshairi
– Tabdila k.m. nae – naye
– Mutafanya – mtafanya
– Inkisari k.m kilofanya – kilichofanya
– Nampenda – ninampenda
– Kuboronga sarufi k.m – Hadi yeye humliza – hadi humliza yeye
– Lahaja k.m naujuwa – naujua
– Khofu – hofu (zozote 2 x 2 = 4)

e) Lugha nathari/tutumbi
– Nikipita naye popote wadaku/wafitini wanamsengenya Aziza kwa maneno mazito k.m kuwa hatengenezi nywele. Semeni tu mtasita (au mtaacha) mjue mimi ninampenda alivyo)

(3 x 1 = 3)

Au Msimulizi anasema kuwa akienda na Aziza popote wadaku wanatoa maneno mazito ya kumsengenya k.m hatengenezi nywele. Anawaeleza waendelee tu bali yeye anampenda alivyo. (3 x 1 = 3)
f) (i) Sakubimbi hubwagiza – wadaku (wasengenyaji hutupa maneno ovyo).
(ii) Musighafilike wenza – msiumie/msighadhabike (2 x 1 = 2)

## SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI

**8.**

a) i) **Michezo ya chekechea** Michezo ya watoto ambapo wanaigiza shughuli au mambo wanayoyaona katika mazingira yao kama upishi, ukulima, arusi nk. **(alama 2)**

ii) **Vivugo** Ni tungo za kujisifu au kujigamba. Anayejigamba huwa mwanasanaa (mshairi) anaelewa kwa undani analozungumzia. **(alama 2)**

iii) **Kimai**
- Nyimbo zinazohusishwa na shughuli za majini (mabaharia).
- Huhusishwa na maisha ya wavuvi, shughuli za uvuaji/uvuvi. **(alama 2)**

iv) **Maapizo**
- Ni maombi maalumu ya kumtaka Mungu/miungu/mizimu kumwadhibu mhusika hasidi, mkinzani au mwovu.
- Maapizo ni dua ya laana au maombi mabaya kutoka kwa mtu ambaye anahisi ametendewa wovu.

**(alama 2)**

v) **Somo**
- Ni maneno ambayo sio rasmi yanayotumiwa katika lugha ya maongezi na kikundi Fulani cha jamii. Pia ni semi za kimafumbo huhusishwa na kikundi kidogo cha wanajamii.

**(alama 2)**

**b)** **Majukumu ya ngomezi.** i) Kitambulisho cha jamii – ufundi wa jamii huonyeshwa kwa kutumia vyombo vya muziki. Ujumbe wa kuzaliwa kwa mtoto huweza kupitishwa kwa mapito tofauti ya ngoma.

ii) Nyenzo ya kukuza uzalendo – wanajamii hufunzwa kuionea fahari mbinu hii yao ya kuwasiliana.

iii) Hukuza ubunifu – wanajamii wanabuni mitindo mpya ya kuwasilisha ujumbe kwa ngoma, hivyo kuimarisha ubunifu.

iv) Njia rahisi ya kuwalisha ujumbe bila kutegemea sauti ya mtu

v) Huhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii kutoka kizazi hadi kingine.

vi) Ni nyenzo yakupisha ujumbe wa dharura kuhusu matukio ya dharura kama vile vita – yaani hutumiwa kutoa matangazo rasmi

# PRECIOUS BLOOD SCHOOL - RIRUTA
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)
## Mwongozo wa Kusahihisha

**1. Muundo**

Zingatia lugha ya mtiririko.

i) Kujitambulisha – Jina
- Kuzaliwa/Eneo/Kaunti nk.
- Malezi yake
- Elimu - Msingi - Sekondari - Vyuo mbalimbali alivyosoma

ii) **ii) Tajiriba** - Kazi aliyofanya/alizofanya kabla ya kuwa Gavana. - Siasa – kiwango/viwango gani? - Anatajika kwa jambo/mambo gani. Mifano: - Elimu ya juu – shahada kadha. - Miradi ya maendeleo. - Ziara alizofanya. - Uwajibikaji wake/maadili kazini. - Falsafa yake ya maisha. - Malengo yake. - Changamoto alizozipitia. - Ruwaza/maazimio yake. Lugha – Mtahiniwa atumie nafsi ya kwanza. Usemi ya taarifa. Lugha rasmi itumiwe.

**2. Hoja**
- Maadili yatazorota.
- Njia za mkato maishani.
- Uzembe kazini.
- Ukosefu wa uwajibikaji.
- Mapuuza.
- Kutothamini mitihani.
- Elimu kudorora.
- Kuathirika kwa taaluma mbalimbali.
- Utendakazi utaathirika.

• Nidhamu kutoweka.

**3. Mtenda mema kwa watu atendea nafsiye.**

**Maana:** Kuwafanyia wema watu ni sawa na kujiwekea akiba. Huenda nao wakakutendea wema utakapouhitaji. **Funzo:** Usidhani unafanya kazi ya bure unapomfaa mtu fulani. **Matumizi:** Inaweza kuhimizwa anayefikiria kuwa wema uatendao ni wa bure na kuwa hatafaidika hata akiendelea. Mtahiniwa aandike kisa kitakachodhihirika pande zote mbili.

**4. Maumbo ya kuzingatiwa.**

i) Kisa kinachofaa kuwa katika wakati uliopita. ii) Mtahiniwa azingatie kumaliza kisa chake kwa maneno yote yaliyodokezwa. iii) Mahali pa tukio patajwe. iv) Baadhi ya matukio;

- Moto
- Wizi
- Ugaidi
- Baharini/majini
- Ajali barabarani

# PRECIOUS BLOOD SCHOOL - RIRUTA
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM – Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha
## Mwongozo wa Kusahihisha

1. **UFAHAMU** **(Alama 15)**

   (a) Eleza sababu za watu kujishughulisha na taaluma zisizo zao. (alama 2)

   **Kutojali kuwa wana vipawa vya kufanya kazi fulani.**
   **Kuvunja moyo na waliowazingira kuwa vipawa vyao havifai. (2×1=2)**

   (b) Eleza kikwazo cha ustawi wan chi zinazoendelea. (alama 1)

   **Kutozistawisha taaluma ambazo ndizo msingi wa maendeleo.**

   (c) Taja mambo matatu yanayostawisha taifa. (alama 3)

   **Maarifa chipukizi**
   **Uchapuchapu wa barubaru**
   **Maarifa**
   **Uvumilivu**
   **Tajriba ya wazee** **(Tatu za 3×1=3)**

   (d) Taja mambo **manne** yanayokwamiza uendelezaji wa vipawa miongoni mwa vijana. (alama 4)

   1) **Kukosekana kwa mtalaa wa kuvichochea**
   2) **Kuvipuuza na kujisukuma katika taaluma ambazo hazikuwafaa kamwe.**
   3) **Kuingilia taaluma fulani kwa sababu wandani wao wanashiriki.**

**4) Kushurutishwa na wazazi wao.**
**5) Kuingilia taaluma fulani kwa lengo la kupata hadhi.**
**6) Kukosa taaluma nyingine. (Nne za kwanza 4×1=4)**

(e) Kuna tofauti kati ya Waafrika na Wazungu katika ukuzaji wa taaluma? (alama 2)

**Wazungu hujitahidi kuvitambua vya watoto wangali wachanga hali hii ni kinyume Afrika. (2/0)**

(f) Eleza maana ya 'Huliona tanga la nguo wakasahau la miyaa'. (alama 1)

**Hukimbilia taaluma za kifahari ili kupata hadhi na kusahau taaluma za kimsingi zinazoafikiana na vipawa vyao.**

(g) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo vilivyotumika katika ufahamu. (alama 2)

**(i) kulimatia- kubaki nyuma/kuchelewa/kutaahiri.**
**(ii) mtalaa –mpango wa utaratibu wa masomo (2×1=2)**

**2. UFUPISHO (Alama 15)**

(a) Ni nini maoni ya mwandishi kuhusu suala la ugaidi? (alama 7, 1 utiririko)

1) Tunapinga na kulaani visa vya ugaidi
2) Ugaidi ni kitendo cha kinyama kinachotekelezwa na watu waliokosa ubinadamu.
3) Ugaidi hauna uhusiano na dini yoyote.
4) Polisi wanazembea katika kuzuia matendo ya kigaidi.
5) Polisi wabuni njia mbadala ya kukabiliana na ugaidi badala ya kunasa raia waio na hatia.
6) Wakenya wasio na makosa huteswa na kuuawa kinyama.
7) Magaidi watalipia matendo yao.
8) Wakenya wana haki ya kulindwa.

(Hoja zozote 7×1=7, alama 1 ya utiririko)

(b) Kwa kutumia yasiyozidi 50, fupisha aya mbili za mwisho. (alama 6,1 ya utiririko)

1) Raia wasio na hatia hunaswa.
2) Hurundikwa kwenye seli na kuachiliwa huru kama wameteseka.
3) Huu ni ukiukaji wa haki za binadamu.
4) Hii ni hila ya polisi kujionyesha kuwa wanafanya kazi.
5) Magaidi huendeleza shughuli zao.
6) Polisi wanapaswa kubuni njia zitakazowapa mwelekeo mwafaka kuhusu wahalifu.
7) Ushirikiano baina yao na majasusi uwepo.
8) Maafisa wa usalama kupata habari muhimu kutoka kwa raia.

(Hoja zozote 6×1=6, alama 1 ya utiririko)

(a) Ondoa ½ alama kwa kila kosa la sarufi hadi makosa sita kila litokeapo kwa mara ya kwanza.
(b) Ondoa ½ alama kwa kila kosa la hijai hadi makosa sita kila

litokeapo kwa mara ya kwanza.

**3. MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

a)(i) Eleza jinsi kitamkwa /u/ kinavyozuliwa
(alama 2)

1. **Ulimi huinuliwa juu huku ukijipinda nyuma**
2. **Hutamkwa midomo ikiwa imeviringwa. (2×1=2)**

(ii) Andika tofauti moja kati ya sauti hizi.
(alama 1)
/t/ na /d/
**/t/ ni sauti hafifu/sighuna na /d/ ni sauti ghuna (alama 1/0)**

b)Bainisha kiima na chagizo katika sentensi ifuatayo.
(alama 2)
Mwanajamii yule alijibu maswali yote kwa makini
**Kiima: mwanafunzi (yule), CH – kwa makini. (2×1=2)**

c)(i) Eleza maana ya vitenzi vishirikishi. (alama 1)

1. Vitenzi vinavyoonyesha tabia/ hali fulani iliyopo au isiyokuwepo kwa mtu/kitu.
2. Hushirikisha vitu mbalimbali kihali, kitabia na kimazingira. (1×1=1)

(ii) Tunga sentensi moja moja kuonyesha aina mbili za vitenzi vishirikishi.
(alama 2)

d)Yakinisha sentensi ifuatayo. (alama 1)
Mtoto hakufundishwa wala kupewa vitabu. **(2/0)**
**Mtoto alifundishwa na akapewa vitabu.**

e)(i) Eleza maana ya silabi. (alama 2)

1. Kipashio kinachotamkwa kwa pamoja kama fungu moja.
2. Muungano wa sauti unaotamkwa kwa mpigo mmoja.
3. Sehemu ya neno moja inayotamkika/ tamko moja katika neno.
4. Pigo katika neno. (2/0)

(ii) Huku ukitoa mifano, eleza miundo miwili ya silabi za Kiswahili. (alama 2)
I - oa
K - mtu
KI - bata
KIK - daftari
KKI - ndege
KKKI - mbweha
IK – alfajiri **(2×1=2)**

f) Ainisha viambishi katika sentensi hii kimuundo na kidhamira. (alama 3)
Wataonana
(i) Kimuundo: **viambishi awali – wa-ta**
**Viambishi tamati an-a (2× ½ =1)**
(ii) Kidhamira

**wa- nafsi/ngeli**
ta- wakati/njeo
an – kauli ya kutendana
a –kauli ya kutenda **(4× ½ =2)**

g) Tumia nomino yoyote katika ngeli ya KU-KU pamoja na kiashiria kisisitizi cha karibu kutunga sentensi. alama 1)
k.m: Kuandika kuku huku kunapendeza sana. (upatanisho uwepo) . **(1/0)**

h) Tunga sentensi moja katika wakati uliopita hali isiyodhihirika (alama 1)
**k.m: Maisha yalikuwa yamwendea vyema. (1×1=2)**

i) Tunga sentensi mbili ili kubainisha maana za neno: Jinsi (alama 2)
1. Njia ya kutekeleza jambo. K.m: Nionyeshe jinsi ya kupika chai.
2. Mwendo . k.m: Alishangiliwa kutokana na jinsi alivyocheza mpira.
3. Aina. K.m: Watu wa namna/jinsi hii wanahitajika kufungwa. (2×1=2)

Huku ukitoa mifano, eleza matumizi ya alama ifuatayo ya uakifishaji. *
1. Kuonyesha maendelezo mabaya. K.m:* Rara hapa.
2. Kuonyesha ufafanuzi zaidi umetolewa chini. Km: uhandisi ni muhimu*
3. Kusisitiza/ uzingativu wa jambo. (2×1=2)

j) Eleza miundo mitatu ya vishazi tegemezi na kuitolea mifano mwafaka katika sentensi. (alama 3)
1. **Vinavyohusisha 'O' rejeshi**
   Kilichopotea ni kile.
2. **Vinavyohusishwa kirejeshi amba-**
   Mwanafunzi ambaye alisajiliwa amewasili.
3. **Vinavyohusisha ki ya masharti**
   Ukinitembelea nitakutuza.
4. **Vinavyotokana na hali ya nge, ngali/ ngeli**
   Ungesoma kwa bidii ungepita mtihani.
5. **Vinavyotokana na sentensi zinazoanza kwa viunganishi.**
   Ingawa tulimpenda sana, Mola alimpenda zaidi.
6. **Vinavyohusisha hali ya Po**
   Nivuapo au Ninapovua samaki wengi hutuzwa.

**(4×1=4) Ataje muundo na kueleza**

(k) (i) Eleza maana ya shamirisho kipozi. (alama 1) **Ni nomino inayotendwa.**
**Nomino inayopokea athari ya moja kwa moja kutoka kwa kitendo**


(ii) Benta alimlimia mamake shamba kwa trekta. Anza kwa yambiwa (alama1)
**Mamake alilimiwa shamba na Benta kwa trekta**

(m) (i) Tunga sentensi yenye muundo ufuatao.
S – KN (N/Wθ) + KT(Ts+T+RH+E) (alama 2)

**Atakuwa akitembea kando ya barabara jioni**
(**Kadiria majibu mengine**) **(2/0)**

(ii) Changanua kwa matawi sentensi ifuatayo: (alama 2)

Kile chake kipya kinanipendeza mno.




(n) Eleza matumizi yoyote mawili ya kiambishi KU na kuyatolea mfano mmoja mmoja wa sentensi. (alama 2)

1. Hutumiwa kama kiambishi cha awali cha vitenzi-jina.
   Kucheza kwa gwiji yule kulinivutia.
2. Hutumiwa kuonyesha shamirisho/ yambwa/ mtendewa.
   Mtendwa wa nafsi ya pili
   Alikupiga jana Au Walikupigia.
3. Kiambishi cha mahali kusikodhihirika/ kwa jumla.
   Hu<u>ku</u> ndiko <u>ku</u>le anakoishi.
4. Kiambishi cha kuonyesha ukanushaji wa wakati uliopita,
   Hakufika jana alivyotarajiwa.
5. Huambishwa kwenye vitenzi vya silabi moja katika kauli ya kutenda.
   Alikuja jana.
6. Huambishwa mwanzoni mwa vitenzi vikuu katika sentensi yenye vitenzi sambamba.
   Yesu alikuja kutuokoa **(zozote tatu 3×1=3)**

(o) Tunga sentensi sahihi ukitumia kivumishi cha ki ya mfanano na kielezi cha namna kitumizi. (alama 2)

**Nguo <u>za kifalme</u> hazivaliwi na watu wanaotembea <u>kwa miguu</u>.**
**(kadiria majibu mengine) alama 2/0**

(p) Tunga sentensi ukitumia kitenzi cha silabi moja kinachomaanisha kuogopa katika kauli ya kutendeka. (alama 2)

**Mungu <u>huchika</u> katika maeneo mengi barani Afrika.** **Alama 1/0**

(q) Eleza maana ya:

(i) Papo kwa papo kamba hukata jiwe.
**(alama 1)**

**Ukifanya bidii, hata jambo liwe na changamoto zipi, hatimaye hutimilika. (1/0)**

(ii) Ua langu la waridi limechanuka. (alama 1)

**Mpenzi wangu amefurahi. (1/0)**

(r) (i) Tunasema baraza la wazee …………………… cha kuni na ……………………. ya nguo (alama 1)

**Kitita cha kuni**

**Bahasha ya nguo (2× ½ =1)**

(ii) Ajuza ni kwa mwanamke mzee na ………………ni kwa msichana mchanga ilhali shaibu ni kwa mwanamume mzee na …………………………ni kwa mvulana aliyebaleghe.

(alama 1)

Kigoli/kigori kwa msichana (alama ½)

Ghulamu/barobaro/rijali/shababi kwa mvulana aliyebaleghe. (alama ½)

**4. ISIMUJAMII** (Alama10)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Niaje wasee! Midterm ilibamba lakini ilkua fupi sana, tumerudi books, huu ni mwaka wa mwisho tujikaze jo. Msifikirie hizo hepi zetu ni reality, kuchill ni jambo la maana jo! ama niaje bro…hustle ni real, bidii ndio itatuokoa

(a) Tambua sajili inayohusishwa na kifungu hiki (alama2)

**Sajili ya mtaani / Lugha ya vijana**

(b) Eleza sifa zozote nne za kimtindo zinazojitokeza katika kifungu hiki. (alama4)

(**i**) Matumizi ya takriri k.m jo

(ii) Sentensi fupifupi k.m niaje wasee

(iii) Lugha hisishi k.m niaje wasee!

(iv) Kuchanganya msimbo k.m hizo hepi zetu ni reality

(c) Eleza sababu nne zinazosababisha matumizi ya lugha ya aina hii. (alama4)

(i) Ukosefu wa msamiati tosha

(ii) kuipa lugha ladha

(iii) Kukubalika katika kikundi fulani

(iv) Kudumisha usiri / kuficha ujumbe fulani (v) Kufahamu lugha zaidi ya moja

# PRECIOUS BLOOD SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

1. **LAZIMA: SHAIRI**

a) i) Kujitahadhari na vyote vinavyong`ara sababu zitawadhuru
ii) Kujiepusha na zinaa
iii) Wasiandame baa.
iv) Wasifikirie wanaovalia kinadhifu na kujipondoa ndio wazuri na kuwaandama .
v) Wasiandame/ wasipapie anasa
vi) Kumcha Jalia
vii) Kuvumilia na kujikaza

Zozote 4 x 1 = 4

b) I) Tabaini – si hayati si mamati ub 1
ii) Msemo - makaa kujipalia ub 2
kaza kamba.
iii) Methali - si mlamgo nyumba nzuri… ub 4
iv) Tashbihi- wamepita ja umeme ub 5
kufa kama nyani ub 6

Zozote 2 x 1 = 2

c) Mathnawi – migao miwili kila mshororo.
ii) Ukara – vina vya ndani vinatofautiana lakini vya nje vinafanana kila ubeti. ( 2 x 1= 2)

d i) Tabdila - huno - huo ubeti 1
ii) Inkisari – mkamba - mkaamba ubeti 1
juta – kujuta ubeti 1
alo – aliye ubeti 8
ngia – ingia ndani
iii) utohozi - sitoria ub 5
iv) Lahaja - hino – hiyo ubeti 1
v) kuborogha sarufi – makaa kujipalia

Madhara kukadiriazozote 2 x 1= 2

e) Ingawa vitu vitaonekana bora na kuvutia machoni.
ii) Dunia ina udhaifu na maovu mengi.
iii) Vijana ninawasarifu / nawasihi iwapo mtanisikia.
iv) Tahadhari na vyote vinavyong`ara kwani vinaweza kukudhuru. 4 x 1= 4

f) Toni ya ushairi- mshairi anawashauri vijana dhidi ya kutotahadhari na ya dunia. 1x 1= alama 1

g) Nafsi neni – mshauri/ mzazi/ mhenga alama 1
Nafsi pokezi – vijana alama 1

h) i)Balagha – wawapi leo madume, anasa walopapia?
Umuhimu – kuibua hisia za nafsi nenewa kuhusu kupapia anasa na raha.
ii) Bora/ zuri ( alama 2)

**CHOZI LA HERI**

Ndoa ni maafikiano rasmi baina ya mwanamume na mwanamke ili waweze kuishi pamoja kama mke na mume.

Ridhaa alikuwa na mke kwa jina Terry. Walibarikiwa kuwa na watoto wafuatao: Mwangeka, Tila na marehemu Dede. Ndoa hii haikudumu kwani janga la moto iiliisambaratisha aila hii na ndipo Terry, Til a, Lily na Becky wakaiaga dunia. Ridhaa akabaki mjane. Mwangeka alikutana Lily Nyamvula katika chuo kikuu na kumwoa. Walibarikiwa na mtoto mmoja kwa jina Becky. Ndoa hii haikudumu kwani Lily na Becky waliangamia kwenye janga la moto. Baada ya ndoa ya mwanzo kusambaratika, Mwangeka alimwoa

Apondi. Walibarikiwa na mwana wa kiume kwa jina Ridhaa. Mwangemi alimwoa mwanamke kwa jina Neema. Hawakufaulu kupata mwana wao kindakindaki japo walipanga mwana wao kwa jina Mwaliko.

Kangata alikuwa na mke wake kwa jina Ndarine. Walibarikiwa na wana wafuatao. Lunga Kiriri, Lucia Kiriri na Akelo Kiriri.

Lucia Kiriri -Kangata – alikuwa ameolewa

Kangata walishangaa mwana wao akaozwa kwa watu ambao huvaa nguo nje na pia huzaa majoka.

Kaizari alikuwa na mke kwa jina Subira. Waliborika no mabinti wawili, Lime na Mwanaheri.

Lunga alikuwa na mke kwa jina Naomi. Walikuwa wa watatu, Umu, Dick no Mwaliko. Ndoa hii haikudumu

mahari kutoka kwa buda mmoja kwa jina Fungo aliyemuoa kama bibi wa nne. Ndoa hii haikudumu kwani Pete alihiarikumwacha baba huyu.

**Mwanafunzi aongezee hoja. Zozote**
**AU**

2. Katika riwaya hii vijana Ni wasomi- vijana kama Tila, Umu na Mwaliko walikuwa wenye bidii masomoni.

   Walanguzi wa dawa za kulevya — Dick alikuwa akilangua za kulevya kwa muda wa miaka kumi.

   vijana wengine wa kike walikubali wakikeketwa Wengine waliiaga dunia na wengine kulazwa zahanatini Wapenda fujo- vijana ndio waliotumiwa na wanasiasa kutekeleza uovu wa mauaji na kuyaharibu mali ya wenzao./ vijana waliowabaka mabinti wake Kaizari na kumuumiza mke wake

   Wasio no huruma- vijana wengine walikuwa wakiwaua wenzao bila huruma.

   Wasio na msimamo dhabiti- vijana wengine wakipotoshwa na wanasiasa bila kuwaza na kuwazua madhara waliyosababisha.(**mwanafunzi aongeze )**

**KIGOGO**

3. a) Ni sauti ya mtangazaji/ mjumbe katika redio ya rununu ya Sudi. Wanaosikiza redio ni Sudi, Boza na Kombe wakiwa kwenye karakana yao sokoni chapakazi. Tangazo ni kuhusu sherehe za uhuru ambazo zitachukua muda wa mwezi mzima ( alama 4)

b) i) Jazanda - sumu ya nyoka
ii) Utohozi - kampuni ( alama 2)
c) **Athari ya sumu ya nyoka**
i) Vifo mfano Ngao junior
ii) Watu wanageuka vipofu
iii) Ukengeushi mf. Ngurumo
iv) Kuanguka chini ovyo ovyo na kugaragara
v) Wanafunzi katika shule ya Majoka wamegeuka vichwa maji.
vi) Hawatambui athari za ulevi.
vii) Hawaoni athari ya soko kufungwa
viii) Kupotosha vijana ( gume gume)
ix) Kupotoka kwa maadili
x) Kuvunjika kwa ndoa
xi) Waathiriwa wanatumiwa na viongozi kutekeleza maovu( chatu) mf. Ngurumo
xii) Utepetevu ( uzembe) wanashida ulevini
xiii) Kuwaunga mkono viongozi wasiowajibika baada ya kupewa vipeni. ( vibaraka)
viv) Kutumia lugha chafu/ matusi mf Ngurumo kumtusi Tunu.

xv) Kukosa wachumba/ ukapera mf Ngurumo

xvi) Kuvuja pesa
xvii) Kutofuata maagizo – Chopi hakufuata maagizo ya kumuua Tanu.
Zozote 14 x 1 = 14 ( alama 14)

4. a) Jazanda / Sitiari

Maana; maelezo ya kimafumbo yanayoashiria jambo fulani au hali fulani inayofahamika kubeba hali nyingine tofauti.

i)Uvundo uliohanikiza katika eneo la soko la chapakazi unaoashiria uozo wa kijamii kama vile utepetevu wa viongozi.

ii)Uchongaji wa kinyago kizuri cha mwanamke ambaye ni Tunu akiwa na kinasa sauti ni kuanagazia nafsi ya mwanamke katika jamii: ana uwezo wa kuwa kiongozi.

iii)Uchongaji wa kinyago cha mhenga fulani wa Boza unaashiria uhafidhina na ubarakala unaoendelezwa katika jamii na baadhi ya watu.

iv)Kombe anaposema kwamba keki ya uhuru imeliwa kwingine kisha wao waletewa masazo kuonyesha utabaka na ukoloni mamboleo unaoendelezwa na viongozi na vibaraka wao wanaojifaidi pekee.

v)Majoka anapomwambia Ashua kuwa hangeacha kula mkate kwa kuchelea kiungulia. Hali hii inaashiria uendelezaji wa anasa na uozo wa viongozi wanaotaka kutumia madaraka ya kutimiza ufuska wao hata kwa wake wa watu bila hofu yoyote.

vi)Kenga anaposema kuwa ukitaka kuwafurusha ndege kata mti kwa maana ya kuangamiza viongozi wa makundi pinzani inadhihirisha maudhui ya ukatili na siasa za mauaji.

vii)Sudi anapomwambia Ashua kuwa siasa yao imesukumiza kwenye chombo wasichotaka kuabiri anamaanisha imebidi washiriki katika harakati za ukombozi. Aidha, maudhui ya asasi ya ndoa yanaangaziwa kupitia mzozo wao. ( Sudi na Ashua)

vii)Chopi anawaambia Sudi kuwa shamba likimshida kulima aseme anaamanisha pengine Sudi ameshidwa kumkidhia Ashua mahitaji yake kama mke hivyo kuendeleza maudhui ya ndoa na mapenzi.

viii)Babu anasema kuwa chombo chenye rubani imara huhimili vishindo na hasira ya mawimbi kumaanisha uongozi mzuri hutegemea kiongozi aliyeimara na mwajibikaji.

ix)Babu anaporejelea mshumaa kuwaka na kuwasha mishumaa mingine anamaanisha kiongozi anastahili kuwafaa raia. Aidha, anadokezea umuhimu wa umoja na ushirikiano katika jamii.

x)Ashua anamwambia Majoka kuwa ushahidi hauwezi kupatikana ikiwa kipanga ndiye hakimu katika kesi ya kuku kumaanisha ukiukaji wa haki katika jamii.

xi)Babu anamwambia Majoka kuwa labda chombo chake kinakwenda kinyumenyume badala ya kwenda mbele kumaanisha utawala wa Majoka haujaonyesha mabadiliko yoyote yaliyoleta manufaa bali umeendeleza ukoloni mamboleo.

MAJAZI

b) i) Majoka -nyoka kubwa kupita kiasi. Ana tabia ya nyoka kubeba fimbo ya nyoka na maumbo ya nyoka. Kutengeneza sumu ya nyoka. Kufuga nyoka( swila)

ii) Tunu –kitu cha dhamana( zawadi)
ni mwanamke wa kipekee anayekabiliana na viongozi dhalimu.

iii) Sudi -bahati njema. Ni bahati njema kwa Sagamoyo. Anajitolea kupigana na uongozi mbaya.

iv) Kenga-kumfanya mtu aamini jambo lisilo la kweli ( uongo)

v) Husda-kuonea mtu gere/ kijicho/wivu. Anamwonea Ashua wivu kwa sababu amesoma, mrembo na apendwa na Majoka.

vi) Kombe-mmea unaotambaa ambao utomvu wake ni sumu inayopakwa katika kigumba cha mshale.
Ana tabia ya kutoonyesha msimamo dhabiti.

vii) Ngurumo- sauti ya mvumo inayosikika angani wakati wa mvua. Anahusika kuwaua na kuwapiga wapinzani wa Majoka

viii) Chopi-kulewa chopi/ chakari. Hakufuata maagizo anayopewa na Majoka kwa sababu ya kulewa.
ix) Mama Pima-kazi yake ni kupima na kuuza pombe
x) Asiya-sehemu ya kitu au mbaki. Mfano Majoka anamuona kama mbaki linalostahili kuondolewa baada ya kifo cha Ngurumo.
xi) Boza-mjinga/ mpumbavu. Mfano anaunga mkono serikali kijinga, mkewe azini na Ngurumo.
xii) Hashina-mwenye heshima, anawafundisha wengine kuwa na heshima.
xiii) Saga moyo-kufanya kitu kiwe unga unga( saga) . Watu wanaoishi katika jimbo hili wanapitia maumivu makali ya moyo.
xiv) chapakazi- mahali pa kufanyia kazi kwa bidii.
Zozote 10 x 1 = 10

4

a) i) Hii ni kauli ya mwandishi
ii) anarejelea tukio la ulafi wa Jitu
iii) mahali ni katika mkahawa mshenzi wa Mzee Mago
iv) watu wamepigwa na butwaa kwa tendo la ulafi wa Jitu.
4x1=4

b) i) nahau- kukiangua kitendawili ( alama 2)
ii) jazanda - neno `kitendawili' kurejelea jambo fulani lililofichika
( yoyote: kutaja alama 1, kutoa mfano mmoja alama 1)

**c) Chanzo**

i)Kuwepo kwa uvumi na nong`ono kuhusu uwezekano wa kunyakuliwa ardhi ya Wanamadongoporomoka.
ii)Mzee Mago kuwahamasisha raia kuhusu haja ya kutetea kazi zao.
iii)Mikutano ya kuandaa mikakati ya kutetea haki za Wanamadongoporomoko inayofanyika katika mkahawa.
iv)Jitu kuwasili mkahawa mshenzi na kuzua taharuki
v)Jitu kuamrisha kuhudumiwa na kula chakula chote kilichoandaliwa.
vi)Watu kupigwa na butwaa kwa ulafi wa jitu na kuwazia tendo hili

**Hatima**

- Jitu kuahidi kurudi keshoye kula maradufu ya siku hiyo.

i)Hatimaye jitu kufika na mabuldoza
ii)Askari wa baraza kuandamana na jitu
iii)Jeshi la polisi kuwalinda askari wa baraza
iv)Watu kupigwa virungu bila hatia
v)Vibanda kubomolewa
vi)Watu kujenga upya` vibanda mshezi' zaidi ya hapo awali
(**Hoja zozote 5 za chanzo na 5 za hatima jumla ni alama 10)**

d) Wasifu wa warejelewa katika dondoo hili.
i)Wazalendo halisi; wanaendeleza harakati za kupigania haki zao za kumiliki na kukomboa ardhi yao.
ii)Wenye bidii: hawasiti /hawakomi kuandaa mikakati ya kupigania haki zao . mfano: mikutano yao.
iii)Wenye umoja na ushirikiano : wanashirikiana kwa kukutana na kupanga utetezi wa haki zao.
iv) Wakakamavu/ jasiri: wanakaidi hatua ya Jitu na kuikomboa ardhi yao

iliyonyakuliwa.

v)Wenye hekima/ busara: wanabaini hila za wenye nguvu kutaka kunyakua ardhi yao na kujiandaa kukabiliana nao.

- ( zozote 4X1=4)

5a) i) Ulumbi ni uhodari wa kutumia lugha kwa ufundi wa kipekee. Ni utumiaji wa lugha kwa mvuto na ufasaha. ( alama 2)

ii) i)Hukuza uwezo wa kujieleza hadharani
ii)Hukuza ujuzi na ufasaha wa lugha
iii)Msingi wa kuteua viongozi
iv)Huhifadhi utamaduni wa jamii
v)Huburudisha
vi)Hukuza uzalendo
vii)Huweza kutumiwa kuwasilisha ujumbe muhimu
viii)Ni kitabulisho cha utabaka
Zozote 5 x 1= 5

iiii) i)Aweze kutumia lugha kwa njia yenye mvuto ili kuchangamsha hadhira
ii)Aweze kutumia chuku kwa ufanifu mkubwa.
iii)Awe mcheshi ili kunasa makini ya hadhira
iv)Awe na uwezo wa ufaraguzi ili kuweza kubadilisha lugha kulingana na hadhira
v)Aweze kutumia ishara na maso -lugha kikamilifu.
vi)Kuelewa utamaduni wa hadhira yake ili asikaidi miiko katika uwasilishaji wake
vii)Awe jasiri ili aweze kuzungumza kwa ukakakmavu

viii)Apaaze sauti ili asikike
ix)Kuhusisha hadhira yake
x)Awe na uwezo wa kutumia miondoko jukwaani
xi)Uigizaji/ udramatishaji
xii)Mavazi/ maleba yavutie na kuadili
( za Kwanza 8 x 1 = 8)

b) i) kuuliza maswali
ii) kujibu maswali
iii) kuwahusisha katika nyimbo
iv)kucheka pamoja
v)Kupiga makofi
vi)Kushangilia
vii)mdokezo
viii)Kuuliza maswali ya balagha ili kuibua hisia
ix)Mtuo wa kidrama.

6a) **Sifa za maghani**

i)ni tungo la kishairi , yaani yana muundo wa ushairi
ii)husimulia matukio kwa kirefu hasa yanapotambwa.
iii)Hufungwa papo kwa hapo na husemwa mbele ya hadhira

iv)Ufundi mkubwa hutumika kutunga
v)Hutolewa na mhusika mmoja au kundi la watu
vi)Kuna kujisifu / kujigamba kwa anayeghani
vii)Huambatana na ala za muziki
viii)Kuna majigambo mengi
( zozote 6 x 1)

ii) **Aina za maghani**

- Tendi – huitwa pia ushairi wa kishujaa kwani hujumuisha sifa zinazoonyesha mafanikio ya mashujaa na mbolezi zinazoonyesha anguko la utawala/ shujaa
- Rara- hadithi fupi na nyepesi za kishairi zinazopitishwa kwa mdomo.
- Tondozi - tungo zinazoghaniwa na huwasifu watu, wanyama na vitu
- Sifo – mashairi ya sifa ambayo hughaniwa kumsifu mtu fulani kutokana na matendo ya kishujaa.
- Pembezi- ni tondozi inayotolewa kusifu watu fulani pekee kama vile viongozi.

( zozote 4 x 1)

c) i) **Majukumu ya Hurafa**

i)Huelimisha jamii
ii) Hukuza uwezo wa kukumbuka
iii) Huonya na kushauri kupitia kwa wahusika wake
iv) Huhifadhi na kuendeleza historia ya jamii

v)Huhifadhi utamaduni wa jamii
v i)Ni kitambulisho cha jamii
vii)Hukuza ujasiri wa kuzungumza hadharani
viii)Ni nyenzo ya burudani
ix)Hukuza ubunifu
x)Hukuza utangamano , watu wanapokuja pamoja kutambiana hadithi.
( zozote 4 x 1) = 4

**ii) vipengele vya kuzingatia katika uchanganuzi wa hadithi**
i)Dhamira – lengo/nia inayokusudiana na hadithi

ii)Maudhui- mambo yanayoelezwa katika hadithi k.m hekaya
iii)Ploti – mtiririko wa utushi ama tukio katika hadithi.
iv)Mandhari- mazingira ya wakati , hali au kimaeneo. Ya kuogofya, yenye misitu na majitu au mazimwi.
v)Wahusika- viumbe wa hadithi wa aina gani.
vi)Usimulizi- hadithi inasimuliwa katika nafsi ya kwanza au ya tatu.

vii)Muundo- miundo maalum ya kuanza na kufunga hadithi

viii)Lugha- lugha ya moja kwa moja( sahili) na inayoweza kutumia tamathali za lugha.

( zozote 6 x 1)= 6

# KENYA HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)
## Mwongozo wa Kusahihisha

1. *Umepata tangazo la nafasi ya kazi ya uhariri katika shirika la uchapishaji wa vitabu vya fasihi andishi kwenye gazeti la Taifa Leo. Andika barua ya kuomba nafasi hii na uambatanishe na wasifu kazi wako kwa maelezo zaidi. (Alama 20)*

**(a) Muundo wa barua rasmi - yenye anwani 2**

i) Ina anwani ya kwanza: - Mwandishi - mtahiniwa abuni anwani yake – Iwe wima (Alama1)

ii) Tarehe - Chini ya anuani ya kwanza (Alama½)

iii) Anwani ya pili Mwandikiwa- mkurugenzi wa shirika la uchapishaji(Alama1)

iv) Maamkizi - Kwa Bwana/ Bibi, (Alama½)

v) Mtajo / mada - <u>KUH/MINT/ YAH: KUOMBA KAZI YA UHARIRI</u> (Alama2)

vi) Mwili wa barua –

a) Utangulizi _ Asili ya habari kuhusu nafasi ya kazi – tangazo
b) Maelezo ya kibinafsi kwa kifupi.
c) Ufaafu wake kwa hiyo nafasi
(Alama4)
**d) Maelekezo kwa wasifu kazi kwa maelezo zaidi.**

vii) Hitimisho - Sahihi ya mwandishi , jina na cheo kama anacho (Alama1)

**(b)Wasifu kazi/ Tawasifu kazi**

(i) Habari za kibinafsi – Jina
- Jinsia
- Umri / Tarehe ya kuzaliwa
- Ndoa – ameolewa au la /Hadhi

- Anwani - Barua pepe, meme/webu nambari ya simu.
- Dini
- lugha uzijuazo (Alama2)

(ii) Elimu – Orodha ya shule – Aanze kwa kiwango cha juu zaidi na kumalizia shule ya msingi.
Ataje hadhi na jina la taasisi, kipindi cha wakati, cheti alichohitimu. (Alama 2)

(iii) Tajriba – Ujuzi wa kikazi/ maarifa. Ataje tajriba aliyonayo katika utendaji kazi anayoiomba.
Ujuzi alionao uonyeshe shirika au kampuni alipofanya kazi. (Alama2)

(iv) Ufanisi - Ataje na aeleze ufanisi wake. (Alama1)

(v) Uraibu - Ataje mambo ambayo anapenda kufanya wakati wa ziada au anapokuwa hayumo kazini. K.m. kusoma, kusaidia jamii n.k. (Alama1)

(vi) Wadhamini/ Warejelewa wawili au zaidi.
Habari zifuatazo kuhusu wadhamini zitolewe.
- Wawe wawili au watatu.
- Jina /majina
- Vyeo/ Taaluma/ kazi
- Anwani
- Nambari ya simu
- Kipepesi.

(alama2)

*2. Utelekezaji wa mtoto wa kiume nchini ni janga kuu. Jadili.*

<u>Jinsi ametelekezwa</u>
Kukosa waelekezi
Kuwachwa kujikidhi pekee.
Kutopigiwa debe kama msichana.
Kutwikwa majukumu angali mchanga.
Kutoajariwa na mashirika ya ufadhili.
Vyama vya kupigania mvulana kutowajibika.
Kunyimwa nafasi ya masomo.
Kukosa mashirika ya utafiti kuhusu wavuluna.

<u>Janga</u>
Anaacha masomo
Anaingilia dawa za kulevya na anasa.
Anaungana na vikundi vya ugaidi.
Wanakosa hadhi ya mwanamume.
Kuchangia kuporomoka kwa misingi ya kifamilia.
Kukosa viongozi wa kesho.

<u>TANBIH</u>I

1. *Lazima aonyeshe pande mbili, asipo atuzwe nusu ya alama.*
2. *Kuwe na kichwa au mada.*
3. *Atimize maneno kati 350 – 400*
4. *Kadiria hoja nyinginezo.*

*3. Andika insha inayoafikiana na methali Baniani mbaya kiatu chake dawa.*

**Maana.**

*kiatu* cha baniani ni kitu au kundi la watu ambalo limechukiwa au kudharauliwa.

*Dawa*: Kitu husika huenda kikawa ndicho jibu au jawabu au suluhisho kwa tatizo fulani maishani mwa mtu au katika jamii

Mtahiniwa aandike kisa kuthibitisha matumizi haya ya methali

Mtahiniwa anaweza kutumia methali nyingine zenye maana sawa kama;

- Matango na matikiti ndio maponya njaa
- Wembamba wa reli gari moshi hupita
- Nyumba nzuri si mlango fungua uingie

Utuzaji

(i) Pande zote za methali zishughulikiwe.Anayeshughulikia upande moja asipite alama C 08/20

Anayetaja tu upande wa pili bila maelezo kikamilifu achukuliwe kuwa amelenga lakini ana udhaifu wa maudhui

(ii) Anayekosa kulenga katika kisa chake amepotoka kimaudhui alama D 03/20

*4. Andika insha itakayomalizikia kwa;*

*…walipofungua mlango huo hatimaye,wengi hawakuweza kuzuia hisia zao.Waliangua vilio kwa maafa waliyoyashuhudia.*

Mtahiniwa ahitimishe insha yake kwa maneno aliyopewa

Kisa chake kifungamane na mawazo ya kauli aliyopewa

Kisa kilenga tukio lililozua taharuki miongoni mwa wahusika

Tukio lenyewe lazima lidhihirishe maafa /maangamizi

Lazima litokee kwenye sehemu iliyozingirwa kama vile ndani ya nyumba,katika gari n.k

Mtahiniwa atumie *nafsi ya tatu hali ya wingi*(warejelewa)

Atumie *wakati uliopita.*

# KENYA HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha
## Mwongozo wa Kusahihisha

**1 UFAHAMU**

(a) Kukichuza/kupima/kukadiria/kuchunguza kipindi cha mahusiano.(alama1)
(b) Ni wa kudumu/ni wa muda mrefu/hautavunjika/ni wa milele. (alama 1)
(c) (i) Huwezesha watu walio mbali kuwasiliana.
(ii) Ni nyenzo ya kudumisha uhusiano.
(Mojawapoalama 2)
(d) (i) Talaka
(ii) Maisha ya mjini ambayo yanabadilikabadillika.
(iii) Mfumo wa maisha ya kibepari/ubinafsi mwingi.
(iv) Uhamaji
(v) Ufutwaji kazi
(vi) Ubadilishaji kazi
(vii) Hali zisizotegemewa
(viii) Mifumo ya kimataifa
(ix) Mifumo ya kisiasa
(Zozote 4 x1 = 4)
(e) Hujiri katika muktadha wa huduma fulani/Ni uhusiano wa chembe chembe/Ni uhusiano ulio tovukwa na hisia za utu.
(Mojawapoalama 2)
(f) Aina tofauti za mahusiano/mahusiano katika jamii/Tuhakiki /tuchunguze , mahusiano ya jamii.
( Mojawapoalama 2)
(g) (i) inasigana – inatofautina/inapingana/inakinzana/inahitilafiana (alama 1)
(ii) yameghoshi – yamejaa/yamesheheni/yamebeba/yametawaliwana/yameseta/ yamerundika/yazidisha/yameongeza (alama 1)
(iii) vighairi – kinyume/tofauti (alama 1)

***Kukosoa – h – 6 x ½ =al.3***
***s- ½ kwa kila kosa. Asikosolewe zaidi ya ½ ya alama alizotuzwa.***

**2 UFUPISHO**

(a) (i) Maarifa huyadhibiti, huyatawala, huyaendesha na kuyaongoza maisha ya binadamu.
(ii) Anayekosa maarifa huathirika pakubwa.
(iii)Maarifa ni utajiri mkubwa ambao binadamu huutumia kwa faida yake na wanajamii wenzake/Elimu ni mali/Msingi wa utajiri na maendeleo ya binadamu ni maarifa.
(iv) Elimu ni chimbuko la maarifa muhimu maishani.

(v) Maarifa hayana upinzani.
(vii) Utumiaji wa maarifa hauyamalizi.
(vi)Kila mtu ana uhuru wa kutumia maarifa kuzalisha maarifa mengine./Anaweza kunyumbua maarifa na kuyatunza kwa namna tofauti.
(viii) Maarifa hayagusiki.

8 x ½ =4

(b) (i)Maarifa huingiliana na maarifa mengine.
(ii) Hayawezi kuchukuliwa kutoka sehemu moja hadi nyingine.
(iii) Yaweza kuwasilishwa kwa njia ya ishara au mitindo ya kidhahania.
(iv) Huweza kubadilishwa/kugeuzwa na kuwa ishara.
(v) Yana sifa ya uhusianaji.
(vi) Huweza kuhifadhiwa katika nafasi ndogo.
(vii)Hayawezi kudhibitiwa/kuzuiliwa mahali fulani yasisambae/Huenda haraka sana.
(viii) Huepuka pingu za watu kudhibiti wenzao.
(ix) Ni nguvu inayoshinda nguvu zote.

***(Zozote 8 x 1=8)***

***a = 4***
***b = 8***
***u = 3***
***Jumla = alama 15***

***Kukosoa – h – 6 x ½ =3***
***s – 6 x ½ =3***

**3 MATUMIZI YA LUGHA**

(a) /p/, /t/, /j/, /k/ 4 x ½
(b) (i) kazi – shamirisho
(ii) haraka ipasavyo – chagizo
(2 x ½ )
(c) K. m. Mtoto yule aliadhibiwa vikali na mama yake.
(d) Mwalimu <u>aliyekuja juzi anafundisha</u> Kiswahili <u>vizuri</u>.
(4 x ½ =2)
(e) Aliwapiga na kuwalaghai. (alama 2)
(f) Wa – nafsi/ngeli
li – wakati

cho – kirejeshi
ki – kitendwa
i – kauli/kinyambulishi
a –kiishio
(6 x ½ =3)
(g) wote – kivumishi cha pekee
wenye – kivumishi cha pekee

kubwa – kivumishi cha sifa
wao – kivumishi kimilikishi
(4 x ½ =2

(h) S – KN + KT
KN – N + U + N
N – Yohana
U – na
N – Otieno
KT – T + N
T – hucheza
N – kandanda
(8 x ½ =4

(i) (i) Huwa na kirejeshi.
(ii) Huwa na vitenzi viwili au zaidi.
(iii) Huwa na vishazi viwili; huru na tegemezi.
(3 x 1=3)

(j) Askari jela alimwuliza Kendi, ''Unadhani hapa ni kwenu? Kuja kwangu mara moja. (2 au 0)

(k) K.m. Alhamisi, alfajiri n.k.

(l) (i) K.m. ng'ombe, '14, n'taenda n.k. (al. 1)
(ii) Mwalimu (wa Historia) ametuzwa n.k. (al.1)

(m) (i) K.m. Kibaya kimetupwa. (al. 1)
(ii) K.m. Alicheza vibaya. (al. 1)

(n) liwa
K.m. Chakula chote kililiwa na paka. (al. 2)

(o) Yunis alifaidika kwa kulima.
Yunis alifaidika kutokana na kulima.
(Yoyote 2 x 1=2)

(p) Mifugo wangu wamenyweshwa maji na Tinga. (al. 2)

(q) (i) werevu, wema, wokofu, wivu n.k. (al.1)
(ii) uovu, ulevi, uwongo,uchungu n.k (al. 1)

(r) (i) Umu alimfanya aajiriwe.
(ii) Umu alimfanya aandike.
(iii) Umu alisababisha kitendo cha jina lake kuandikwa.
(iii) Aliyeandikwa ni mke wa Umu.
(v) Aliyeandikwa ni mke wa mtu mwingine.
(Zozote 2 x 1=al. 2)

(s) K.m. Kerich acheza vizuri. (al. 1)

***Kukosoa - h -6 x ½ =3***
***s- Kilakosa ½ - Asikosolewe zaidi ya nusu ya alama alizotuzwa.***

**4 ISIMUJAMII**

(a) (i) Kijamii

(ii) Kijiografia/kimaeneo

(2 x 1=2)

(b) - Huwa na wazungumzaji wengi.
- Huwa ni lugha ya kwanza ya kikundi cha watu inayokiwezesha kikundi husika kupokezana utamaduni.
- Huwa na muundo wakiisimu unaofanana na ule wa baadhi ya lugha za watu wa nchi husika.
- Lazima iwe mojawapo wa lugha asilia.

(4 x 1=4)

(c)– Kiswahili kinazungumzwa na watu wa Afrika Mashariki na Kati.
- Kiswahili hufundishwa katika shule za Kenya, Uganda na Tanzania.
- Kiswahili hufundishwa katika vyuo vya Afrika Mashariki, Marekani na Ujerumani.
- Hutumika katika mikutano ya kimataifa kama vile Umoja wa Afrika.
- Kiswahili hutangazwa katika idhaa za Kimataifa kama vile B.B.C, Redio China na Idhaa ya Kijerumani.
- Kwa sasa hutumika katika mtandao.

(Zozote 4 x 1=4)

***Kukosoa – h -4 x ½ =2***
***s- 4 x ½ =2***

# KENYA HIGH SCHOOL

## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019

## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi

## Mwongozo wa Kusahihisha

LAZIMA

1. (a) -Maneno ya Tetei, Mwanaharakati
-Anawaambia wananchi/wapiga kula.
- Baada ya mwekevu kutawazwa/ Kiogozi mwanamuke
- Watu walishukuwa silaha kupigania uhuru wao.

(b) - Watu walishukuwa silaha kupigania uhuru wao.
- Mlio ya buduki ilisikika.
- Vilio vilijaa hewani.
- Vyombo vya dola vilitumwa kudumisha amani.
- Msafara ya watu ilionekana ikimaha kwao.
- Mazao yalichomwa mashambani
- Majumba yalichomwa
- Watu waliuliwa.

Zozote nne (1 x4)

(c) - Nyumba ya Ridhaa inateketezwa
- Luga anafutwa kazi bila sababu.
- Lime na Mwanaheri kunajisiwa
- Fumba kuringa mwanafunzi wake mimba
- Familia ya Ridhaa kuteketezwa na majirani.
- Pete kuozwa Mzee Fungo
- Subira kubaguliwa Kwa sababu za kiukoo.
- Naomi kuwatelekeza wanawe.
- Uharibifu wa mazingira – serikali inakata miti.
- Chandachema chema anadhumiwa kimapenzi na mwalimu wake Fumba.
- Shamba lao Shamsi linanyakuliwa.
- Pete anakeketwa.
- Ndoa za mapema/pete
- Uuzaji wa pombe haramu
- Ulaguzi wa madawa ya kulevya - Dick
- Ulaguzi wa watoto - Sauna

TANBIHI Kadiliria jawabu la mwanafunzi zozote kumi na mbili. (12x1)

2. **KIGOGO**

Ufisadi

- Wafanyabiashara wanalazimishwa kutoa hongo kombe anasema lazima tutie tonge
Kinywani na tuwape wenye nchi kitu kidogo
- Mapendeleo ya kinasaba
- Majoka anamteua Kenga binamuye kuwa mshauri wake mkuu (maneno ya sudi uk 9)
- Majoka anapanga kumtambulisha Ngao Junior kama mrithi wake (uk 36)
- Usaliti/ukiukaji wa majukumu
- Watawala wanasaliti wapiga kura kuwa kutotokeleza majukumu yao. Soko linanuka uvundo kutokana na maji machafu ya taka. Wanachojua viongozi ni

kukusanya kodi (uk2)

hawatekelezi majukumu yao ya kusafisha soko

- Udhalimu/ukatili
- Viongozi kutumia vitisho na kuwanyang'anya wafanyabiashara kilicho chao (sudi anasema katika uk 3)
- Vijana watano waliokuwa wakifanya maandamano wanauawa na wachuuzi sokoni wanaumia uk 16
- Chuki za kikabila
- Vijikaratasi vinaenezwa kuwatia woga watu kutoka kabila fulani. Wanaambiwa kuhama (uk.51-52)

Unafiki

- Majoka anasema kuwa wanasagamoyo wasiruhusu watu wachache waliojazwa kasumba za kiloloni kuwarejesha katika utumwa. Pia anadai kuwa hatuwezi kukubali kutawaliwa tena yeye anatenda mambo yayo hayo anaokashifu.
- Ubadhirifu
- Serikali inakopa pesa nyingi na kuziweka katika miradi isiyofaa (pesa inakopeshwa na k utumiwa katika mradi wa kuchonga kinyago cha hayati Marala Bin Ngao
- Unyakuzi wa ardhi ya umma
- Ardhi ya soko inanyakuliwa na majoka anajenga hoteli ya kifahari katika ardhi hiyo na kuwagawia wendani wake kama vile kenga baadhi ya sehemu ya ardhi hiyo
- Matumizi mabaya ya mamlaka

Kenga anamshauri majoka kutumia uwezo wake kuharamisha maandamano na kuwaamuru maafisa wa polisi watumie nguvu zaidi kuwatawanya waandamanaji (uku 34)

- Dawa za kulevya na pombe haramu

Tunu anasema kuwa juzi walizika watu waliokufa kutokana na pombe haramu. Wengine wamegeuka kuwa vipofu (ku 63

- Umaskini umekidhiri katika jamii hii wafanyabiashara katika soko la sagamoyo ni watu wenye elimu na talanta kochokocho kama vile Sudi. Wangali wanaishi katika umaskini licha ya bidii zao. Boza anasema kijirununu cha pesa nane.. maskini akipata (uk 7
- Vijana wanatumiwa kumvamia Tunu na wapinzani wengineo (zozote (alama 20)

- Tamaa, Majoka ana tamaa ya mali ya umma kwa sababu analifunga soko la chapakazi ili ajenge hoteli ya kifahari. Vilevile yuko na tama ya wake za wengine m.f Ashua
- Uozo, Mamapima anapewa kibali na serikali ya majoka kuwauzia watu pombe haramu inayowaua na kuwafanya vipofu. Vilevile majoka yuko na kampuni kubwa ya uzalishaji sumu ya nyoka barani (dawa za kulevya) ambayo inauzwa katika shule ya majoka na majoka academy
- Ubarakala: Kuna vibaraka ambao wanamshauri Majoka isivyofaa m.f. Kenga anamshauri Majoka kulipiza kisasi kwa Ashua.
- Tenga Utawala: Majoka anawatenga wasiomuunga mkono k.v. Tunu na Sudi na kuwaleta karibu wanaoukubali ungozo wake m.f. ni mama pima na Ngurumo na pia Kenga.

- Matumizi ya vyombo vya dola: Polisi wanatumika kuwatawanya wananchi kutumia vitoza machozi. Hali hii inwafanya wanasagamoyo kufa na wengine kuwa walemavu.
- Kuotkuwa na uhuru wa vyombo vya habari: Majoka anasema Sagamoyo kitabaki kituo kimoja tu Sauti ya Mashujaa.
- Hali ngumu ya maisha: Wananchi wanoishi katika mazingira machafu, Kombe anasema wamegeuza soko kuwa uwanja wa kemikali na taka. Wanasagamoyo wengine hawana hata chakula.
- Ukosefu wa uwajibikaji: mama pima anawauzia watu pombe haramu licha ya kuwa ni kinyume cha sheria. Pombe hiyo inawaua watu na kuwapofusha vilevile mama pima anamgawia Ngurumo uroda ili amsaidie kupata kandarasi ya kuoka keki ya uhuru.

(1 x 20 =20)

3. <u>KIGOGO</u>

a)-maneno ya Tunu

-anamwabia majoka

-ofisini mwa majoka

-Ashua alikuwa gerezani

b) Sifa za Tunu

- Mwanamapiduzi
- Msomi
- Mtetezi wa haki
- Jazili
- Mzalendo
- Mwajibikaji
- Mzindushi
- Mwenye mhawalaka mwema

c) Thibitisha kwa kutoa mifano kuwa Maisha ya Majoka yametawaliwa na dhuluma.

- Dhuluma ni kitendo cha kumnyima mtu haki au stahiki yake; ni uonevu, ni tendo lisilo la haki. Majoka alidhihirisha dhuluma maishani mwake binafsi na katika uongozi mwake.
- Serikali yake hutoza wanabiashara kodi lakini wanafanyia kazi katika mazingira machafu. Uvundo umekithiri. Sudi anasema. “Ni jukumu lao kuhakikisha soko ni safi si kukusanya kodi pekee….. (uk 3).
- Bali na kulipa kodi isiowaletea huduma yoyote wafanyakazi wa soko wanalalamika kuwa wanadaiwa pesa zaidi. Kombe asema kuwa ni lazima wpate chakula na pia wawape wenye nchi kitu kidogo.
- Shua asema mahali wanapofanya kazi wanadaiwa kitu kikubwa au kitu chote.
- Utawala wake unawanahangaisha wafanyakazi, hawafanyi kazi kwa amani Ashua asema “…na kuhangaishwa na wenye nguvu ndiyo hewa tunayopopumua…” (uk2). Sudi anathibitisha hilo anapolalamika kwamba, “si

haki kuchukua kilicho chetu na kututishatisha"(uk3).

- Anadhulumu raia kwa kutumia raslimali za Sagomoyo kujinufaisha pamoja na wachache, wanaomunguka. Wao ndio hula ile keki kubwa, huku raia wakitaabika. Sudi anamwambia Boza, "Hapo basi – kijikeki. Kwa nini wewe upate kidogo? Sagamoyo ni kwenu, shrehe ni zenu.. na keki kubwa ni ya kina nani"(uk 14)
- Ni dhuluma pia kwa serikali ya majoka kufunga soko la Chapakazi mahali ambapo watu wengi hufanya biashara ili kupata chakula chao cha kila siku.
- Katika kiwanda chake wafanya kazi wanapujwa. Soko la Chapalazi lilipofungwa bei ya chakula kwenye kioski cha kampuni ya Majoka and Majoka ikapanda maradufu. Wafanyakazi hawawezi kugharimia chakula. Hii ni dhuluma dhidi ya wafanyakazi. Majoka kuendelea kujitajirisha huku wafanyakazi wake wakiumia (uk 17)
- Maandamano yanayokumba jimbo la Sogamoyo si walimu, si wauguzi, si wafanyakazi wa kampuni, si wafanyakazi wa soko ni ithibati tosha kuwa watu wanadhulumiwa.
- Ni dhuluma pia kuwaua watu.
- Alimuua Jabali kuwa mshindani katika siasa.
- Wale vijana watano wa Majoka and Majoka Company waliuawa wakidai haki yao kwenye maandamano.
- Tunu alikuwa auawe kwa kukashifu vitendo vyake vya kidhalimu.
- Kingi alionywa kuwa angevunjwavunjwa na chatu kwa kukaidi amri ya Majoka ya kuwapiga watu risasi.
- Majoka anawaua hata washirika wake wa karibu akihofia kuwa wangetoa siri zake. Kwa mfano Ngurumo aliuawa ilhali alikuwa mfuasi wake sugu. Chopi alipangiwa kuuawa pia kwa kijua 'mengi'. Hii ni dhuluma iliozidi. Majoka anasema anaona ziwa kubwa ajabu lililofurika damu… kuna kilio cha ndani kwa ndani na machozi mengi humo yasiyoonekana… (uk 73) na kwamba mikono yake ilikuwa imefungwa nanga humo damuni. (uk 73).
- Serikali yake imewahini wananchi raha, wanaishi kwa hofu. Heshima anakiri kwamba yeye na Tunu wake wanaishi kwa hofu nyingi. Wanaogopa kwamba wanaweza kuvamiwa wakati wowote hasa akitilia maanani kuwa mwanawe nusura auawe. Tunu anapopiga nduru kwa kuota mamake anafikiri wameshambuliwa.
- Isitoshe serikali ya Majoka inawahangaisha watu kuwatupia vijikaratasi vya kuwashurutisha wahame Sagamoyo si kwao. Siti anasema, "Jana walitutupia vijikraratasi… Tuhame Sagamoyo si kwetu" (Uk 52-53).

- Anaamuru polisi kusambaratisha kikatili maandamano raia ambao hawakuwa na hatia. Walikuwa wakidai haki yao tu.
- Anwawadhulumu raia waliochagua kwa kutowapa huduma muhimu kama vile hospitali, barabara, maji safi, vyoo, nguvu za umeme, elimu na hata ajira kwa vijana waliokamilisha masomo. Viogozi wasiowajibika hawatilii maanani mahitaji ya umma.

4. **HADITHI FUPI.**

Kwa kurejelea hadithi ya *Mapenzi ya Kifaurongo* onyesha jinsi jamii imegawika kitabaka kuegemea

(a) Uchumi

(b) Kazi
(c) Elimu

- Tabaka ni kundi la watu katika jamii linalojitofautisha na kundi jingine kwa misingi ya kiuchumi, kielimu, kikazi n.k. katika hadithi hii matabaka haya yamedhihirika.

(a) Kiuchumi, kuna tabaka la juu matajiri na la chini la maskini. Watu wenye fedha nyingi wanaweza kununua magari makubwa ya kibinafsi, kujenga majumba ya ghorofa, kununua matatu na mabasi.

- Matajiri wanaweza kuwapeleka watoto wao shule za mikoa na kitaifa maana wanau wezo wa kulipa karo ya huko.
- Watoto wa matajiri wakifuzu kwenda chuo kikuu wanahahikisha wanaishi maisha ya kifahari. Mavazi yao ya kutoka nchi za nje wamenunuliwa simu za bei ghali, vipakatalishi na Ipad
- Wazazi hawa ni msaada kwa watoto wao, wanawapa pesa za kutosha za matumizi chembilecho Penina, babake humtumia elfu tano kila wiki.
- Watoto wa matajiri hawasumbuki hata baada ya kufuzu vyuoni na kukosa kazi. Penina analipiwa kodi na wazazi wake na nyumbani mwake mna runinga na kochi. Bila shaka amenunuliwa na wazazi wake.
- Utajiri wa wazazi ndio unawafanya baadhi ya wanafunzi wa chuo cha kivukoni kutokuwa makini sana. Masomo yakiwa magumu, wengine wanahiari kuyaacha. Wanajua wanaweza ungana na wazazi wao katika biashara zinazowaletea mapato makubwa, kwa mfano magari ya uchukuzi na nyumba za kupanga.
- Shakila anatafutiwa kazi na mamake kwa sababu ana cheo kikubwa kazini mwake. Ni mkurugenzi mkuu.
- Tabaka la maskini linawakilishwa na Dennis na wazazi wake. Dennis mara nyingi anabaki kutamani/kumezea mate magari makubwa yanayoendeshwa na wenye pesa.
- Dennis anakiri kuwa "kwetu tunapigania mikono ielekee vinywani." (uk 20) Haya ndio maisha amezoea"Dennis, hata chuoni anakosa chakula, anakosa pesa za kununua na anakosa kwa kukopa,asema, pesa zangu zimekwisha na sina kwingine ninakoweza kukopa kwa"(uk 18.)
- Maisha ya watu maskini ni ya hadhi ya chini; ya kunywa uji mweupe bila sukri, mavazi ya bei ya chini yakilinganishwa nay a matajiri ambayo ni ya kutoka nchi za nje.
- Chumba cha Dennis kinaonyesha anatoka katika tabaka la chini. Hakina vitu vya thamani. Kuna kijiredio ambacho kinaimba kwa sauti ya chini, shuka za kitandani ni

kuu kuu zimechanikachanika n.k. hakika kuna utengano wa wazi kati ya maskini na matajiri.

- Watoto kutoka jamii maskini wanasomea shule za hadhi ya chini, shule za vijijini. Watoto kama vile Dennis huishi wakiwazia umaskini wao katika jamii uliowakosha nafasi ya kusomaa katika shule za kifahari.
- Tabaka la maskini hufikiri kuwa elimu ni njia moja ya kuwanasua kutoka umaskini. Dennis anasoma kwa bidii ili awe daktari, mhadhiri, mtangazaji au mwandishi msifika.
- Anatamani kuwa ataweza kununua gari kubwa na hata kuwasaidia wazazi wake. Anawaza moyoni hivi, "Maskini nitawalipaje wazazi wangu wema wlionitendea? Nani atawafidia nguvu na jasho lao…uk 25. Kwa hivyo ni jambo la kutamausha mno Dennis anaposaka kazi kwingi na anakosa. Miaka mitatu

baada ya kufuzu chuoni na bado alikuwa akifanya 'tarmacking' yaani kutafuta kazi.

- Watoto kutoka jamii maskini hawapati msaada wa kupata ajira kutoka wazazi. Maasa wazazi hawajulikani na hawana uwezo. Hii ndio sababu Shakila anapata kazi katika kampuni ambamo mamake anafanya kazi naye Dennis anakosa.

5. **LAZIMA: SHAIRI**

d) i) Kujitahadhari na vyote vinavyong`ara sababu zitawadhuru
ii) Kujiepusha na zinaa
iii) Wasiandame baa.
iv) Wasifikirie wanaovalia kinadhifu na kujipondoa ndio wazuri na kuwaandama.
v) Wasiandame/ wasipapie anasa
vi) Kumcha Jalia
vii) Kuvumilia na kujikaza zozote 4 x 1 = 4

e) I) Tabaini – si hayati si mamati ub 1
ii) Msemo- makaa kujipalia ub 2
kaza kamba.
iii) Methali - si mlamgo nyumba nzuri…ub 4
iv) Tashbihi- wamepita ja umeme ub 5
kufa kama nyani ub 6 Zozote 2 x 1 = 2
c) Mathnawi – migao miwili kila mshororo.
ii) Ukara – vina vya ndani vinatofautiana lakini vya nje vinafanana kila ubeti. ( 2 x 1= 2)
d i) Tabdila - huno - huo ubeti 1
ii) Inkisari – mkamba - mkaamba ubeti 1
juta – kujuta ubeti 1
alo – aliye ubeti 8
ngia – ingia ndani
iii) utohozi - sitoria ub 5
iv) Lahaja -hino – hiyo ubeti 1
v) kuboronga sarufi – makaa kujipalia
Madhara kukadiria zozote 2 x 1= 2
e) Ingawa vitu vitaonekana bora na kuvutia machoni.
ii) Dunia ina udhaifu na maovu mengi.
iii) Vijana ninawasarifu / nawasihi iwapo mtanisikia.

iv) Tahadhari na vyote vinavyong`ara kwani vinaweza kukudhuru. 4 x 1= 4
i) Toni ya ushairi- mshairi anawashauri vijana dhidi ya kutotahadhari na ya dunia. 1x 1= alama 1
j) Nafsi neni – mshauri/ mzazi/ mhenga alama 1
Nafsi pokezi – vijana alama 1
k) i) Balagha – wawapi leo madume, anasa walopapia?
Umuhimu – kuibua hisia za nafsi nenewa kuhusu kupapia anasa na raha.
ii) Bora/ zuri (alama 2)

**FASIHI SIMULIZI**

6. Miviga ni sherehe za kitamaduni ambazo hufanywa na jamii yoyote katika kipindi maalumu cha mwaka. *(1x2=alama2)*

b) Sifa za miviga

- ✓ Miviga huandamana na matendo Fulani k.m kucheza ngoma, kupioga magoti

- ✓ Huongozwa na watu mahususi k.m kuna wanaongoza kafara
- ✓ Huandamana na utoaji mawaidha/ulumbi
- ✓ Maleba huvaliwa na wanaohusika
- ✓ Hufanyiwa katika mazingira maalum
- ✓ Huambatana /hufungamna na utamaduni wa jamii husika
- ✓ Hufanya katika kipindi/wakati maalum
- ✓ Huwa na kutolewa kafara
- ✓ Sadaka hutolewa
- ✓ Kuna kula viapo – wahusika huweka ahadi kutenda wema *(zozote 5x1=alama5)*

c) Udhaifu

- ✓ Husababisha kudorora kwa maendeleo
- ✓ Huleta utengano kati ya jamii/majirani
- ✓ Huasi mabadiliko ya kiwakati (nyingine zimepitwa na wakati)
- ✓ Madhara yaweza kutokea hasa vifaa butu vinapotumika
- ✓ Huleta utengano wa kijinsia, kumtukuza mwanaume na kudunisha mwanamke k.m jando na unyango *(zozote 3x1=alama3)*

d) Umuhimu wa ngomezi

- ✓ Ni njia ya kuwasiliana katika jamii husika
- ✓ Hudumisha usiri wa jamii husika
- ✓ Hutumiwa kutangaza matangazo muhimu kuhusu shughuli maalum
- ✓ Huendeleza utamaduni wa jamii
- ✓ Huisaidia jamii kuionea fahari historia yao
- ✓ Hutahadharisha kuhusu matokeo ya dharura
- ✓ Hudhihirisha ufundi wa kisanaa (kutumia zana Fulani za muziki)
- ✓ Hutekeleza majukumu ya maandishi katika jamii zisizojua kuandika
- ✓ Huburudisha *(zozote 6x1 = alama 6)*

e) Vizingiti

- ✓ Mwingiliano wa makabila tofauti hauruhusu tena matumizi ya ngomezi
- ✓ Maendeleo ya teknolojia hayaruhusu ngomezi k.m barua, simu
- ✓ Watu wamekuwa wabinmfsi – hawawezi kuitika ngoma ikipigwa
- ✓ Ukosefu wa usalama – watu kushambiliwa wakiitikia wito wa ngomezi

*(zozote 2x1=alama 2)*

# MARANDA HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)
## Mwongozo wa Kusahihisha

**Miundo ya hatuba: ifuate utaratibu wa insha ya hotuba ambao ni:**

(i) kichwa kiwepo katika insha hii. Kichwa hiki kiandikwe kwa herufi kubwa na kipigiwe mstari

(ii) Utangulizi wa hotuba uzingatie itifaki.Anza kuwatambua waliopo kwa kuwataja kulingana na vyeo (hadhi) vyao

(iii) Mwili wa hotuba:zungumzia suluhisho la tatizo la umaskini

(iv) Kuwe na hitimisho:neno au maneno ya kuonyesha shukrani

(v) Nafsi ya kwanza(umoja)izingatiwe(msemo halisi)

**Baadhi ya hoja za kuzingatia ni:**

(i) Kuwepo na njia za kuwasaidia maskini kuanzisha amali za kuzalisha mali
(ii) Kuwepo na mashairika au benki ambazo zinashughulikia maskini kwa mikopo na misaada Mingineyo
(iii) Kupunguza bei za bidhaa za pembejeo za ukulima ambao ni tegemeo kubwa la watu wengi
(iv) Kuhakikisha kuwa pato lakitaifa limesambazwa vizuri ili kuyafikia maeneo mengi
(v) Misaada ya kifedha kwa watu wasiokuwa na uwezo wa kiuchumi
(vi) kuhakikisha kuwa huduma za kimsingi kama maji ya umwagiliaji na miundo msingi Imeboreshwa
(vii) Kuwaelimisha wengi ili kuwapa msingi mzuri wa kujiendeleza kiuchumi
(viii) Kuhimiza uwekezaji katika maeneo ya mashambani

**2 Changamoto zinazowakumba vijana**

(i) magonjwa sugu mathalani ukimwi
(ii) Ujana (ushababi)
(iii) Shinikizo la hirimu (shinikizo-rika)
(iv) Kuibuka kwa lugha ya vijana isiyoeleweka na wazazi wao,basi kukosa maongozi bora
(v) uchumi kudorora
(vi) Athari za utandawazi
(vii) Uigaji wa tamaduni za kigeni
(viii) Umaskini uliokithiri
(ix) Ukosefu wa ajira
(x) Dawa za kulevya

3. Kisa kidhihirishe maana ya methali kuwa kosa linastahili kurekebishwa likiwa dogo. Kosa likiwa Kubwa huenda liserekebike

**Mambo ya kuzingatia**

(a) Kisa kinafaa kuwa katika wakati uliopita
(b) Anza kwa chako kwa maneno yote yaliyodokezwa
(c) Mahali pa matukio patajwe

(d) Baadhi ya matukio ni:
- (i) Moto
- (ii) wizi
- (iii) Ugaidi
- (iv) Baharini/majini
- (v) Ajali barabarani

# MARANDA HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha
## Mwongozo wa Kusahihisha

***a)Kueleza msimamo wa Mugambi kuhusu kumpa mwanawe urithi***
(alama 2)

- Hakufurahishwa na kitendo cha mwanawe kudai urithi kwa kuwa alikuwa ma umri mdogo

Alitaka mwamawe akamilihe masomo kwanza,ajijengee msingi bora wa maisha yake ya kesho

Na hata kupata mali yake mwenyewe

b)kutaja sababu kuu iliyomfanya Tom kutekeleza vitendo vya kinyama
( alama 1)

-Matumizi ya dawa zakulevya

***c.)kueleza athari tano za watoto kutowatii wazazi wao kwa mujibu wa (alama 5)***

***Taarifa hii***

(i) ukosefu wa amani katika familia
(ii) Watoto kuacha masomo kutokana na utukutu na wengine kutohudhuria sule ili wawalinde wazazi wao
(iii) Watoto kujitosa katika matumizi ya dawa za kulevya
(iv) Kuhatarishwa kwa maisha ya wazazi na yale ya watoto watiifu;Tom alimjeruhi Abdallah kwa upanga kwenye kisigino huku akimpiga mamake teke kifuani akaanguka chini
(v) Laana, mamake Tom alimlaani
(vi) Uhalibifu wa mali;Tom alivivunjavunja kenyekenye vyombo vya mamake
(vii) Upyaro ambapo watoto watukutu hawatusi wazazi wao

***d.)Sababu iliyomfanya Tom aliepuka mkono mrefu wa serikali?*** (alama 1)

– Aliweza kuwahonga askari madhali alikuwa na fedha nyingi alizopata kutokana na Ulanguzi wa dawa za kulevya ;hali iliyomfanya kutochukuliwa hatua za kisheria

***e.)Kufafanua wasifu wa Tom kulingana na taarifa hii*** ( alama 3)

-Katili –Alimrushia nduguye upanga na kumjeruhi kisigino alimpiga mamake teke la ubavuni,akaanguka chini

-Mwenye mapuuza /mkaidi-Alipuuza mawaidha ya ndugu zake na hata ya baba yake

- Mpyaro- Alikuwa akiwarushia wazazi wake cheche za matusi
- Mjinga –anakataa kusoma huku akidai kuwa hawezi kuendelea kusoma elimu ya wakoloni
- Mwenya majuto-anajua vitendo vya kinyama alivyokuwa aliwatendea watu wa aila yake

***f.) kueleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumiwa katika taarifa*** (alama 3)

iv. Sudi - Bahati njema/ngekewa/jaala/suudi/saada
v. Kuzunguka mbuyu-kuhonga/kutoa rushwa
vi. Kuwamamamnua- Kuwatenganisha

(c) Bila kubadilisha maana asilia ,fupisha aya tatu za kwanza.(Maneno 50-50)(alama 5,1 utiririko)

**Matayarisho**

- Dhuluma kwa wanawake ni hali ya tangu jadi
- Elimu ya jadi alimwandaa mwanamke kuwa kama chombo cha kumtumikia mwanaume
- Taasubi ya kiume imechangia pakubwa kudhulumiwa kwa mwanamke
- Demokrasia ya jadi ilimfungia mwanamke nje hakuruhusiwa kushirika katika shughuli za kisiasa na utawala
- Mwanamke alichukuliwa kama msihiri na mganga
- Wanawake hawakupewa fursa ya kupata elimu
- Mwanamke alipojitokeza na kusema jambo la busara alipuuzwa na hata kutukanwa hadharani

(d) Kwa kurejelea aya tatu za mwisho ,pambanua hoja muhimu zinazogusiwa na mwandishi
(maneno 70-80) (alama 8,1 utiririko)

**Matayarisho**

- Kumezuka mwamko mpya kutokana na elimu ya kisasa
- Wanawake wanajihami na kujiendeleza katika ulimwengu uliotawaliwa na wanaume
- Wanawake wamekeuka misingi ya utamaduni na kung'oa asasi za jamii zilizowanyanyasa
- Mazimio mengi yamepitishwa na umoja wa mataifa juu ya kuondolewa kwa ubaguzi dhidi ya wanawake
- Wanawake wameonyesha vipaji katika nyanja mbalimbali za maisha
- Wanawake wamejikakamua katika kutekeleza kajukumu ya kuyaongoza naisha yao na ya wengine
- Wadumishaji wadhuluma dhidi ya wanawake hawana budi kusalimu amri
- Wanawake wapewe haki sawa na wanaume
- Itikadi na mila za jadi zimeendeleza kuwa kikwazo kikubwa kwa ukuaji wa hadhi ya wanawake

**MATUMIZI YA LUGHA** **(Alama 40)**

***a.)Andika sauti zenye sifa zifuatazo:***
(alama 2)

v. Kikwamizo sighuna cha kaakaa gumu-/sh/
vi. Kipasuo kwamizo cha kaakaa gumu-/ch/
vii. Irabu ya nyuma ,wastani -/o/
viii. Nazali ya kaakaa laini-/ng'/

***b) Weka shadda katika neno lifuatalo ili itoe maana mbili tofauti*** (alama 2)

Wa<u>la</u>kini- doa,kasoro,dosari,ila
Wala<u>ki</u>ni –kiunganishi "lakini"

c) Tunga sentensi moja ukitumia nomino katika ngeli ya U-YA pamoja na kivumishi kiashiria kisisitizi cha karibu (2 marks)

-Ugonjwa uu huu utamfisha
- magonjwa yaya haya yatawafisha

***d)Onyesha mofimu katika neno:*** (alama 3)

a…………… li……………..ye…………. m……. ch……….. …. a
Nafsi/ngeli wakati kirejeshi yambwa mzizi kiishio

***e) Kanusha sentensi ifuatayo*** (alama 1)

Ukimpiga utashtakiwa na kuchkuliwa hatua kali

-Usipompiga hutashtakiwa wala kuchukuliwa hatua

***f)Andika sentensi ifuatayo kulingana na maagizo .*** (alama 1)

Mwanafunzi huyo alipita kwa vile alisoma kwa bidii

Anza kwa nomino ya kitenzi jina

-kupita kwa mwanafunzi huyo kulitokana na kusoma kwake kwa bidii

***g)Changanua sentensi ifuatayo kwa kielelezo cha mishale*** (alama 3)

Mama na nyanya walinunuliwa jozi za viatu na baba

S → KN +KT
KN → N+U+N
N → Mama
U → na
N → nyanya
KT → T+N+H+N+H+N
T → walinunuliwa
N → jozi
H → za
N → viatu
H → na
N → baba

***h) Andika sentensi ifuatayo kwa wingi***

Nikimuuzia ua hili ataweza kuifanya harusi yake iwe ya kupendeza (alama 2)

-Tukiwauzia maua haya,yataweza kuzifanya harusi zao ziwe za kupendeza

***j) Andika sentensi ifuatayo katika usemi wa taarifa:*** (alama 3)

" mito yetu imechafuka mno;itabiditushirikiane wakubwa kwa wadogo ,wamaume kwa wanawake ili tuisafishe''.Waziri wa mazingira alituhimiza

- Waziri wa mazingira alituhimiza kuwa ingebidi tushirikiana wakubwa kwa wadogo,wanaume Kwa wanawake ili tuisafishe mito yetu ambayo ilikuwa imechafuka mno

***k) Eleza matumizi ya 'ku' katika sentensi ifuatayo*** (alama 2)

Hukumwelewa alivyoeleza namna ya kuwalisha mifugo

- Hukumwelewa-Kikanushi cha wakati uliopita
- Kuwalisha-Kiambishi cha ngeli ya KU-KU

***l) Andika sentensi ifuatayo katika ukubwa*** (alama 2)

Mtoto aliwaua nyoka kwa kupiga vichwa

-Toto liliyoua majoka kwa kuyapiga majichwani

-Jitoto liliyaua majijoka kwa kuyapiga majichwani

***m) Bainisha aina za shamirisho katika sentensi ifuatayo*** (alama 3)

Baba yake alivamiwa na wezi waliomvunjia mlango kwa chuma

- Baba yake –Kitondo
- Mlango- Kipozi
- Chuma- ala

n) ***Kwa kutunga sentensi eleza matumizi mawili ya mkato***
(alama 2)

i. Kupumua katika sentensi ndefu
ii. Kutenganisha katika orodha
iii. Kuandika anwani
iv. Hutumia baada ya jina la mtu
Titus, mbona umechelewa
Hutumiwa katika usemi halisi

***o)Eleza maana mbili za sentensi hii:*** (alama 2)

Mamake Juma na Maria walitutembelea

- Maana ya kwanza walituzuru/walikuja kwetu
- Walitembea badala yetu au kwa niaba
- Mwanamke mmoja ambaye ana watoto wawili (Juma na Maria) alitutembelea
- Wanawake wawili ambao ni mamake Juma na mwingine mamake Mariamu walitutembelea

***p) Tunga sentensi sahihi ukitumia kitenzi 'la' katika kauli ya kutendwa***
(alama 2)

- Chakula kimeliwa na mtoto

***q) Andika kinyume cha sentensi*** (alama 1)

Watoto wameombwa waanike nguo

- Watoto wameamrishwa/wamelazimishwa
- Wameshurutishwa waanue nguo

r) ***Bainisha aina za virai vilivyopigiwa mistari*** (alama 2)

Ubaguzi wa kijinsia umekashifiwa na
Viongozi wenye msimamo thabiti mno

- wa kijinsia-kirai kihusishi
- Viogozi wenye msihamo thabiti mno-kirai nomino

***s) Ainisha vishazi katika sentensi ifuatayo*** (alama 2)

Angalilima kwa bidii angalivuna mavuno tele

- Angalilima kwa bidii-Kishazi tegemezi
- Angalivuna mavuno tele-Kishazi huru

***t)Tunga sentensi zenye vivumishi vya pekee vya kuonyesha dhana zifuatazo***
(alama 2)

(i)Umilikisho- Sentensi iwe na matumizi sahihi ya "enye'
(ii)kutobagua- Sentensi iwe na matumizi ya 'o-ote'

(u) Bumba ni kwa nyuki Kishazi/mtungo ni kwa samak Msafara (alama1)
ni kwa siafu

**ISIMUJAMII (ALAMA 10)**

(c) ***Eleza sifa tano za lugha rasmi*** (alama 5)

i. Biashara-Kiswahili kilifanywa lugha ya biashara pwani na bara
ii. Dini-Kiswahili kilitumika kusambaza dini za Uislamu na Ukristo
iii. Vyombo vya habari kama magazeti ya Kiswahili yalizuka nyakati za ukoloni
iv. Siasa-wahusika wengi katika vita vya ukombozi nchini

Kenyawalitumia Kiswahili

v. Elimu-wamishenari walitumia Kiswahili,kufundisha,kuandika,kusoma,kuhesabu na kazi mbalimbali
vi. Utawala wa kikoloni hesa sera ya lugha ya wajerumani ilisisitiza matumizi ya Kiswahili
vii. Utafiti-Steere na kraft walifanya utafiti wa kina kuhusu Kiswahili na hata kuandika vitabu

***(d) Eleza mambo matano yaliyochangia katika maenezi ya Kiswahili katika (alama 5)***
***Afrika Mashariki kabla ya uhuru***

i. Hutumika katika shughuli rasmi za kielimu mikutanoni bungeni
ii. Aghalabu huwa lugha inayosemwa nchini na nje ya nchi
iii. Inaweza kuwa lugha mojawapo ya wenyeji au ya kigeni
iv. Huwa imesanifishwa
v. Huwa ni lugha yenye historia ndefu ya kimaandishi
vi. Huwa na msambao mkubwa

# MARANDA HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

**USHAIRI**

1.

(a)

i. Wasiwadharau walimu kwa kuwa ni muhimu kwao
ii. Waamke mapema ili wadurusu
iii. Wajiunge na makundi wanapodurusu
iv. Watumie karatasi za mitihani iliyopita kufanya marudio
v. Waepuke kelele darasani
vi. Wazingatie yaliyomo kwenye mtaala
vii. Wajihusishe katika michezo ili wapate nishati ta kudurusu
viii. Wasiogope mtihani wa kitaifa bali wamakinike na kuukabili ( 5x1)

(b)

i. Lina beti kumi
ii. Kila ubeti una mishororo mine
iii. Kila mshororo una vipande viwili-ukwapi na utao
iv. Lina kibwagizo- kwa bidii durusuni,mtihani mfaulu
v. Lina mizani kumi na sita kwa kila mshororo
vi. Lina vina vya kati na vya mwisho vinavyobadilikabadilika kutoka mmoja hadimwingine (4x1=4)

(c) (i) **Mazida**

Mtambueni-Mtambue

Mtihanini- mtihani
Makundini- makundi
Awalini-awali
Nguvuni- nguvu
Mkapotezani- mkapoteza
Mfahamuni- mfahamua

(ii) **<u>Inkisari</u>**
Kitaka- mkitaka
Sielekeze- usielekeze
Mlofunzwa-Mliyofunzwa
Lilo-lililo
Iliopita-iliyopita

Yalo- yaliyo
Ulo -ulio
Yafwateni- yafuateni
Kwauliza- Kuwauliza

(iii) Tabdila
Muweze-mweze
Muepukeni-mwepukeni

(iv) <u>Kuboronga sarufi</u>
Kwa bidii durusuni-durusuni kwa bidii
Wa kitaifa ukija- Ukija wa kitaifa
Watii nao walimu- walimu nao watii
Kufanukiwa kitaka-kitaka kufanikiwa
Ni upuzi msiseme- msiseme ni upuzi
Kuwauliza mwahitajika- mwahitajika kuwauliza

(d) Uhuishi/tashihisi:neneni na vitabuni,vitakuja walipani

(e) Toni ya kushauri ambapo nafsineni anawashauri wanafunzi
Wajitayarishe vyema ili wafaulu mtihani

(f) Nafsineno anawashauri wanafunzi wawatii walimu wao na wasije wakawadhihaki
Kuwa wao ni muhimu kwao
Anaendelea kuwahimiza kuwa wawaulize walimu wao maswali yaliyowawia vigumu na pia
Wajitahidi katika marudio yao ili waweze kufaulu mtihani

(g) Dhikaka-Kejeli
Kaditama- Mwisho /tamati

2. (a) **Kueleza muktadha wa dondoo**

i. Ni mawazo yanayompitikia Ridhaa anapokumbuka maneno ya marehemu mwanawe Annatila(Tila)
ii. Mjadala wenyewe unahusu mafanikio baada ya uhuru
iii. Ridhaa yumo nyumbani kwake akitazama masazo ya aila yake;ambayo ni majivu
iv. Hii ni baada ya kuuawa kwa familia yake kinyama ma mzee kedi alipoliteketeza jumba lake La kifahari

(b) **Kutaja mbinu ya lugha inayojitokeza kaitika dondoo**

a. Balagha:Pana matumizi ya swali isilohitaji jibu
b. Jazanda:Watoto wa miaka hamsini kumaanisha kuwa bado waafrika wangaliwanatawaliwa na wakoloni kwa njia isiyo ya moja kwa moja:sifa za ukoloni zingali barani afrika
c. Kinya:Waafrika wanaendelea kuwategemea wakoloni baada ya kupata uhuru

(c) **Maudhui ya ukoloni mamboleo**

(i) Baada ya miaka hamsini ya uhuru ,tumebaki kuwa wategemezi wa wakoloni hao hao waliotupa uhuru

(ii) Baada ya miaka hamsini ya uhuru,mataifa mengi ya kiafrika hayajakuwa kiuchumi lakini Yamebaki kuwa wategemezi wa hao hao wakoloni ambao walitupa uhuru

(iii) Wakoloni walipoondoka Afrika .walowezi(settlers) na waafrika wenye uwezo walimiliki mshamba yaliyokuwa ya wakoloni na kufanya waafrika kuwa masquota katika vituo vya usuli wao

(iv) Waliokuwa wakoloni ndio wanaoamua waafrika watakuza nini katika ardhi yao

(v) Waafrika wanendelea kuwatengemea wakoloni kwa lishe na ajira ambayo ni ya Kujungujiko

(vi) Waafika wanakuza mazao madogo ambayo huenda kumfaidi huyo mkoloni aliyetupa uhuru.Hatujaweza kujisagia kahawa yetu ingawa mbegu ni zetu,kunachoka kulikuza lao lenyewe kisha tunawapelekea waliokuwa wakoloni walisage na kutuuzi kwa bei ya juu

(vii) Mwaafrika aliridhi umilikaji wa ardhi kwa kutumia hatimiliki kutoka kwa mzungu hali ambayo aliwafanya wengi ambao hawakuwa na uwezo wa kununua mashamba kuwategemea wenye uwezo

(viii) Ubinafsi wa mzungu ulirithiwa na mwaafrika kutoka kwa wakoloni.Tunaelezwa kuwa watoto waliosoma pamoja na Ridhaa walimwita mfuatamvua pia hawakutaka kucheza naye kwa madai kuwa alijunga na shule yao ili awashinde katika mitihani yao,wanamsingizia wizi wa kalamu.Hali hii ni kama ilivyokuwa wakati wa ukoloni ambapo wakoloni walikuwa na ubinafsi wa hali ya juu

(ix) kupitia kwa maneno ya Tila kwa babake,tunaelezwa kuwa machimbo yam awe ya ujenzi
Vito na hazina za mafuta zimepewa kampuni za kibnafsi ambazo ni za kigeni.huku nchini Uchimbaji madini unahifadhiwa na wageni ambapo fedha zinazotokana na rasilimali hii Zinaishia kwenye mifuko ya wageni kufaidi nchi zao

(x) Kampuni za kigeni zimewapa wenyeji(waafrika) ajira ambayo mshahara wake ni mdogo Sana <mkia wa mbuzi>

(xi) Msimulizi anatueleza kuwa vijana wanauwa kwa mitutu ya bunduki wanapojaribu kujikomboa kutokana na ukoloni wa mwaafrika yaani uongozi wa kikatili unaondelezwa Viongozi wa Africa

(xii) Ukoloni mamboleao unaendelezwa na wazungu ambao wanawaajiri waafrika na kuwapa Mshahara wa kijungujiko ilihali wao wana chuma mamilioni kutokana na waajira hao

(xiii) Ukoloni mamboleo unadhirika kupitia kwa mahindi yaliotolewa bure ilikuwapunguzia makali ya kutotesheleza kwa chakula ambako kunaing'ata nchi

(xiv) Wana wa viongozi huenda kusomea ngambo kwa kuiona elimu ya humu kama isiyo wahakikishia mstakabali mwena wa raia wake

3 (a) **Maudhui ya utu katika riwaya ya chozi la heri**

Dkt.Ridhaa anaonekana kujawa na utu kwa kudhamini masomo ya wapwa wawili wa mzee kedi

Ridaa alijenga kituo cha afya cha mwanzo mpya ili kunusuru maisha ya binadamu waliokuwa wakiangamia kwa kukosa huduma bora za afya

Mwangeka na Apondi walikubali kumchukua umu na kuwa motto wao wa kupanga

Kiriri aliyekuwa mwajiri wa kangata alionyesha utu kwa kumwacha kangata afaidi ardfhi yake kiasi cha kuchukuliwa kuwa wanatoka mbari moja na kangata

Neema anaonyesha kujawa na utu kwa kitendo cha kumwokota motto Immaculata aliyekuwa Ametupwa jaalani akampekeka pamoja na mwanapolisi wakampeleka katika kituo cha watoto cha Benefacto

Mtawa Gizarina wa kituo cha kituo cha benefactor alikuwa na utu kwa kuwa alijitoa kuwapokea watoto mbali mbali waliohitaji msaada wa malezi

Mtawa pacha aliyemhudumia zohali,baada ya kupata mimba na kuteswa na wazazi wake,alimtafutia shule ili aendelee na masomo aliyokuwa ameachishwa

Mashirika ya kidini yalitoa misaada kwa waadhiriwa wa majanga mbali mbali katika jamii.Wakristo nawaisilamu waliungana pamoja kutoa msaada katika kambi za waliotimuliwa kutoka kwao

Shirika la jeshi la wajana wa kristo lilidhihirisha utu lilipoamua kujenga makao ya watoto yatima

Watoto waliotupwa na wazazi wao na wenye wazazi wahitaji.Chanda chema alipata msaada kupitia kwa shirika hili

Shirika la kidini la lakikisho la itaki na utulivu linadhihirisha utu kwa kuwasaidia watoto kupata elimu bora.chanda chema anasaidika kuendelea na masomo yake kupitia shirika hili

Tulia alimsaidia Kaizari kufunganya na kumsindikiza hadi njia panda.Alimkumbatia na kumwabia Kuwa mwenyezi mungu ndiye hupanga na nguvu na mamlaka kutoka kwake.

Katika hospitali aliyofanya kazi Selume,kuna mgonjwa aliyepelekwa na wasamaria wema Katika hospitali baada ya kuumizwa katika mgogoro wa kupigiana ardhi katika eneo la Tamuchungu.

(b) **<u>Maudhui ya uozo wa maadili katika jamii ya choza la heri</u>**

- Ubakaji-Lime na mwanaheri walibakwa na mabarobaro watano mbele ya macho ya wazazi wao
- Ulaguzi wa dawa za kulevya-Dick anaifanya kazi ya kusafirisha dawa za kulevya kutoka nchi Moja hadi nyingine
- Uporaji na wizi-vurugu za baada ya uchaguzi alipochacha,vijana walivunja maduka ya waarabu.wahindi na hata waafrika wenzao
- Mauaji-kendi anaichoma nyumba ya Ridhaa ambapo aila ya Righaa inachomeka
- Unyakuzi wa ardhi-watu wamejinyakulia maelfu kwa maelfu ya ekari wakajenga
- Viwanda na maduka ya kibiashara kuwaacha wenyeji bila hata makazi
- Uendelezaji wa biashara haramu-Bi.kanagara walishirikiana na sauna
- Katika kutekeleza biashara ya kuwauza watoto
- Kuavya minba-Baada ya sauna kubakwa na baba yake wa kambo(bwana maya) mamake Sauna Kuavya mimba hiyo
- Kutupwa kwa watoto wachanga-Neema anamwokota motto katika jaala na kumpeleka katika Makazi ya watoto ya benefactor
- Mapenzi ya baba na bintiye (Sauna)
- Ukabila- huu unajitokeza baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya mwanamke ambapo majirani
- Waliwagueuka wenzao waliokuwa wametoka kwa kabila tofauti
- Matumizi ya pombe haramu –Vijana wanasomea shahada za uzamili,wanajihusisha na unywaji wa pombe haramu na kufariki.
- Ukeketaji wa watoto wa kike –Tauma anaelezea kuwa asingepashwa tohara asingeolewa
- Ndoa za mapema-Pete anaozwa kwa mzee fungo kama mke wake wane
- Ufisadi-katika mtaa wa tononokeni ,kuna watu waliojenga majumba yao katika
  maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya ujenzi wa barabara
- Uuzaji wa mahindi yaliyoharibika-Lunga alipigwa kalamu baada ya kugundua mahindi
  yaliyokuwa yametoka ughaibuni yalikuwa hatari kwa usalama ,hata wa panya
- Kuajiriwa kwa watoto wadogo ambao hat vifua havijapanuka watoto walinyakuliwa na kupelekwa sehemu mbali mbali nchini kufanya kazi
- Kutupwa kwa taka karibu na nyumba za watu-katika mtaa wa mabanda wa somber

Anakoishi Bw.makiwa taka linamwagwa katikati mwa msongamano wa kibanda

Kutoka kwa waishipo waheshimiwa.

"Nimekuja kuwakombao…."

4 (a) <u>Kueleza muktadha wa dondoo hili</u>

Maneno haya yanasenwa na tunu,anamwabia ngurumo.wamo mangweni kwa mamapima

Asiya.Tunu anamwambia ngurumo maneno haya baada ya ngurumo kidai kuwa sudi na
Tunu hawakuwa na nidhamu kwa kuwa walikuwa wameenda kuzua fujo baani mwa asiya.
Tunu na sudi walikuwa wameenda kuwaalika akina Ngurumo kwenye mkutano ambao
Ungefanyika kwenye langu kuu la soko la chapakazi ,siku ya kuadhimisha miaka sitini za uhuru

(b) Kuthibitisha kuwa msemewa na wenzake walistahili kukombolewa kwa kutumia hoja kumi na Mbili

(i)**Uharibifu wa mali ya umma:**Viongozi wa sagamoyo wanatumia mali ya umma vibaya

(ii)**Ufisadi:**Viongozi wanakosa kuwapa wanasagamoyo huduma hata baada ya kukusanya kodi kutoka kwao

4

(iii) **Unyakuzi wa ardhi:**Majoka anapanga kunyakua soko la chapakazi

(iv) **Uharibifu wa uchafuzi wa mazingira:**kupitia kwa kombe ,tunapata kuna uchafuzi wa mazingiraLimegeuzwa uwanja wa kumwagia kemikali na taka

(v) **Mauaji**:watu wengi wanoupiga uongozi wa majoka wanauawa kinyama

(vi) **Ukosefu wa kazi:**wanasagamoyo walihitaji kukombolewa kutoka kwa janga la ukosefu wa Kazi

(vii) **Matumizi ya dawa za kulevya:**wanasagamoyo walihitaji kukombolewa kutokana na Matumizi ya mihadarati inayowafanya baadhi yao kubadhiri pesa na hata kuaga dunia

(viii) **Ubabadume:**wanasagamoyo walistahili kukombolewa kutoka kwa mfumo wa ubabadume ambapo wanaume wanajiona bora kuliko wanawake

(ix) **Ufuska/usherati:**Tunamuona majoka kama kiongozi akiwa na jicho la nje.ambapo anajaribu Kumshawishi Ashua wajihusishe na mapenzi

(x) **Tamaa**:kutokana na tama,majoka na Kenya wanapania kunyakua ardhi ya soko la chapakazi

(xi) **Ukoloni**- mamboleo:Serikali ya sagamoyo inategemea mikopo kutoka kwa nchi za kimagharibi na mashariki

(xii) **Umaskini**:umaskini unawafanya wanasaganoyo kuishi maisha duni

(xiii) **Utabaka:**Jamii ya sagamoyo ina matabaka mawili pale ambapo kuna walalahoi na matajiri

(xiv) **Anasa**:Tunawaona ngurumo na walevi wenzake wakijihusisha na anasa kule kwa Mamapima ambapo wanabugia pombe haramu

(c) Kueleza umuhimu wa msemwa kwa kutumia hoja nne

Msemwa ni ngurumo.baadhi ya umuhimu wake ni:

(i) Ni kielezo cha vijana waliopotoka kimaadili.Anajihusisha na mapenzi

Asiya aliyekuwa mke wa Boza ili Asiya apate kandarasi ya uokaji keki.

(ii) Anaendeleza maadhui ya ukatili.Kupitia kwake tunaona namna viongozi wa kiimla wanavyotumia vikaragosi wao kutekeleza mauaji wa wapinzani wao.

(iii) Kupitia kwake tunapata sifa ya asiya kama mfusuka kwa kuwa anashiriki mapenzi naye

(iv) Ametumiwa kama kielelezo cha vijana wanaoacha shule na kujiingiza katika matumizi ya dawa za kulevya.Baadaye dawa hizi za kulevya huwaangamiza vijana hawa.

**<u>Tamthilia ya "Kigogo" ni kioo cha uhalisi wamaisha ya jamii za kiafrika. Thibitisha</u>**

**5**.<u>Majibu</u>

Kioo ni kifaa ambacho watu hutumia kutazama sura zao.Watu wakiona sura zao zina kasoro hiyo kabla hawajatokea mbele za watu.Tamthilia ya kigogo inatumika kama kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika kwa sababu imemulika sura za jamii hizo.

Tamthilia hiyo imeweza kuonyesha kasoro mbalimbali zilizomo katika jamii hizo.

Kasoro hizo ni pamoja na:

1) Uongozi mbaya.-huu ni uongozi ambao hautilii maanani maslahi ya wananchi wote.
2) Mauji ya watu –kuna mauaji ya watu wasio na hatia kama vile Jabali.
3) Usaliti-limesalitiwa na viongozi walioko madarakani kwa vile wanashughulikia mahitaji yao.
4) Ulipaji wa vizazi –Anamtia Ashau nguvuni ili alipe kisasi kwa sudi ambaye hataki kumchongea kinyoga
5) Suara la Migogoro-kuna migogoro baina ya kati ya kundi la Tunu dhidi ya kundi la utawala.
6) Ubinafsi na ukiritimba-Hii ni hali ya mtu kujali mambo yake tu bila kufikiria mambo ya wengine.
7) Ukoloni wa mamboleo-Unajitokeza kwa mambo yafuatayo,kwanza kutegemea misaada kutoka nchi za kigeni ni kugeni ni kuendeleza ukoloni wa mambo leo.
8) Athari za ulevi na dawa za kulevya-limejaa vijana wenye uraibu wa kulewa pombe haramu kama vile Ngurumo na walevi wenzake.
9) Matumizi ya vikaragozi-Vijana walevi wanataka kumpigia Majoka kura hawamtaki mtu mwingine.
10) Ufisadi-vikaragozi wengine kama Kenga anatoa ushauri mbaya kwa majoka ili kujinufahisha.
11) Matumizi mambaya ya vyombo ya dola-askari jela kama chopi ni mpyaro na katili.
12) Unyakuzi wa ardhi-Majoka ananyakua uwanja wa soko la chapakazi ili ajenge hoteli ya kifahari
13) Kuangamiza wapinzani-Jabali aliuawa kwa hila za majoka ili asimpinge.
14) Tenga tawala-Ngurumo anarejelewa na chopi kama 'mtu wetu'

15) Elimu duni- wanafunzi wanatumia dawa za kulevya na wamekuwa wadhaifu.

16) Utawala wa kiimla –Majoka anatawala kwa kutumia mabavu.

17) Ulevi-Ngurumo na mtu wa1 na wa 11 ambao wameathirika mno na ulevi; hawana akili razina

18) Matabaka-kuna vngogo wenye mali mingi na wanalala hoi wasio na mali mfano;Vinyago hula makombo ya keki ya uhuru.

19) Ukosefu wa uajibikaji-kuna njaa kutoka na wafungwa kwa soko,watoto wa sudi wameteseka na njaa.

20) Viongozi wanafuja mali ya umma-Kenga anamrumbuni Sudi kwa fedha nyingi.

21) Hakuna huduma za afya-Mandhari ya soko ni chafu na Sudi anasema kuwa watu wanasumbuliwa na aina nyingi za ndwele.

22) Uharibifu wa mazingira –anaruhusu ukataji wa miti.

6 a) **Haya ni maneno ya Penina**

Penina anazungumza na Dennis

Wako katika chumba cha Dennis katika chuo kikuu

Penina anataka kuanzisha mahusiano ya kimapenzi na Dennis ambaye ni wa tabaka la chini

b)Pengo linalorejelewa ni kupata mpenzi anayeweza kuwa mchumba,penina amekosa mpenzi wake.Mwanzoni Dennis hukubaliana na jambo hii kwa sababu ya tofauti za kitabaka lakini baadaye anashawishika na penina anakubali.

c)Ithibiti za kuwepo kwa athari za kitabaka mahusiano ya kimapenzi kati ya penina na Dennis;

i)Chuoni hakuna maingiliano ya moja kwa moja kati ya wanafunzi wa tabaka la juu na lile la chini.Hii inamaanisha kuwa pia ni vigumu kuwa na mahusiano ya kima.penzi baina ya wanafunzi wanaotokana na matabaka tofauti.

ii)Dennis anamueleza penina kuwa itakuwa vigumu kuanzisha mahusiano ya kimapenzi kutokana tofautizao za kitabaka

iii)Penina anakubali kuwa ni ukweli kuwa tofauti za kitabaka ni tatizo katika mahusiano ya kimapenz lakini wanafaa kupinga hali hiyo.

iv)Wazazi wa Dennis na Penina wanatashwishi na mapenzi yao kwa sababu ya tofauti za kitabaka.

v)Penina anasema kuwa hawezi kuolewa na mwanaume asiye na mshahara mkubwa ;hii ni kusema kuwa lazima mumewe awe tajiri.

vi)Mapenzi baina ya Dennis na Penina yanatamanika kwa sababu ya tofauti za kitabaka.Dennis ameshindwa kupata kazi ya mshahara mkubwa ili aweze kkatika tabaka la juu.

vii)Penina anamshauri Dennis kuwa atafute mpenzi mwingine maskini kama yeye aliyezoea uchochole

viii)Wazazi wa Penina walimwonya Penina dhidi ya kuchumbiwa na Dennis kwa kuwa wao ni wa matabaka tofauti

d)Hulka za Penina

i)Mwenye dharau,Dennis anasema kuwa Penina anamdharau na kumwona kama kinyaa au matapishi.

ii)Mwenye kiburi,Penina alimfukuza Dennis kutoka nyumbani kwa kiburi mno.
iii)Mkali,Penina alimjibu Dennis kwa ukali wakati Dennis anapouliza kuhusu chakula.
iv)Mdadisi
v)Ni mtambuzi
vi)Mnafiki
vii)Mwernye tama

7)a) **Maudhui yanayoendelezwa kipitia muhusika kidawa:**
i) Ndoa;anakubali kuolewa na Dida hata baada ya kutoa masharti ya kisasi ambayo antarajia kuwa Dida angezingatia.
ii) Mapenzi;anampenda Dida kwa hivyo anakubali kuacha kazi yake shuleni ili mapenzi yao yasimbaratike kutokana na wivu wa Dida.
iii) Bidii;anafanya kazi mbalimbali kwa wakati moja ili aweze kuyakidhi mahitaji ya familia yake licha ya kuwa Dadi hapendezwi na hali hii
iv) Nafasi ya mwanamke;ameonyesha mwanamke kama mwenye mapenzi kwa mumewe na pia mwenye bidii.Anaonyesha bidii kwa kufanya kazi kadhaa na kukubali kuacha kazi hizo ili kulinda ndoa yake.
v) Usasa-anaamini kuwa katika ndoa za kisasi ,mwanamke na mwanaume wana nafasi na majukumu sawa kwenye familia zao.
vi) Elimu; amesoma madarasa kumi na mawili;pia pia anafanya kazi ya umetroni shuleni
vii) Ajira; kidawa anafanya kazi ya umetroni shuleni ambapo anawalinda wanafunzi wa kike bwenini, pia anauza nguo na viatu.
viii) Uaminifu;yeye ni mwaminifu katika ndoa yake licha ya kuwamumewe anashuku kuwa ana mahusiano ya kimapenzi na mwalimu mkuu.
ix) Mabadiliko;annamini katika mtindo tofauti wa maisha kati ya mke na mume tofauti na ilivyokuwa kitambo,mwanamke na mwanaume wanafaa kushirikiana katika ndoa.
x) Utamaduni;anamwarifu Dadi kuwa aende ampose kwao ili amwoe ,haya ni kuwa mujibu wa utamaduni.

b)**Maudhui yanayoendelea kupitia mhusika Dadi.**
i) Wivu;kutokana na hisia za wivu,Dadi anafikiria kuwa mkewe kidawa ana mahusiano ya mapenzi na mwalimu mkuu,anafanya uchunguzi kuhusu jambo hili.
ii)Taasabi ya kiume ;Dadi anaamini kuwa nyumbani kuna kazi za mwanaume na zile za wanawake,mwanaume hafai kufanya kazi za jikoni.
iii)Mapenzi;Dadi alimtafuta kidawa kuwa mkewe wa ndoa ingawa kidawa alikuwa amewakataa wanaume wengine kadhaa.
iv)Ndoa;anafaulu kumshawishi kidawa kuwa mkewe wa ndoa ingawa kidawa alikuwa amewakataa wanaume wengine kadhaa.
v)Elimu;Dadi anaamini kuwa ingawa hakusoma sana shuleni yeye si mjinga hivyo ana uwezo wa kutambua mambo mbalimbali.
vi)Ajira;Dadi anafanya kazi ya uchuuzi wa samaki kwa vile hakusoma sana
vii)Ujanja;anapoelekea shuleni,anafanya ujanja wa kupitia kwa mwalimu mkuu ili abainishe iwapo yupo nyumbani au la.
viii)Utamaduni;anaamini kuwa kuna kazi za wanawake na wanume nyumbani

kwa mujibu wa utamaduni wa kiafrika.
ix)Uasherati;anashuku kuwa kidawa ana mahusiano ya kimapenzi na mwalimu mkuu hili ni tendo la kiusherati.
x)Nafasi ya mwanamke;Dadi anaamini kuwa majukumu ya mwanamke ni kutekeleza kazi ya jikoni.

8.a) **Mawaidha**

a) Mawaidha hutolewa katika miktadha rasmi kama vile jandoni,harusi,kwenye mazishi,darasani na kanisa.

b) Katika jamii nyingi,wazee na watu walio na vyeo vikubwa na waliochukuliwa kuwa na hekima ndio waliopewa jukumu la kuwatolea vijana mawaidha.

c ) Mwenye kutoa mawaidha huliewa jambo jambo analousia kwa undani

d) Mwenye kutoa mawaidha hutumia ligha inayoathiri hisia za wanausiwa,kama vile methali

e) Mawaidha hulingana na vipera vingine vya fasihi simulizi kwa mfano,methali hufumbata mawaidha,pia utambaji ngano,miviga kama vile jando na harusi huandamana na utoaji wa mawaidha.

f) Maudhui katika mawaidha ni mapana.Huwezi kugusia masuala kama vile dini,uongozi,ujasiri,amali,elimu na taaluma.

g) Mawaidha yanatolewa katika miktadha rasmi huwa na muundo maalumu wenye sehemu tatu;

i) Utangulizi-katika sehemu hii anayetoa mawaidha huanza kwa kauli ya kuvuta makini ya hadhira.

ii) Mwili-Mawaidha huwasilishwa na kusisitizwa kwa kutumia kauli sisitizi pamoja na tamathali za usemi kama vili methali.

iii) Hitimisho-Mwasishaji huonyesha msimamo wake kuhusiana na suala analousia.

c) -Kuelekeza
-Huelimisha
-Huadilisha
-Hutambulisha jamii

d ) i) Kuwauliza maswali
ii) Kuimba wimbo pamoja na hadhina
iii) Kuwaomba wakriri tena jambo alilosema
iv) Huwashirikisha katika kupiga makofi au kuigiza wahusika

e) Nyimbo hutumiwa kuwasilisha ujumbe,mzito katika hadithi,
-Hutenganisha matukio yanoyojumnisha hadithi
-Husisimua hadhira katika utambaji
-Hurefusha hadithi
-Ni kipumuo.Hupunguza hadhaira uchovu au huzuni
-Huipa hadidhi toni Fulani,kwa mfano wimbo wa huzuni huipa hadithi toni ya huzuni
-Huendeleza hadithi
-Huangazia maadili katika hadithi

-Huburudisha
-Husisimua hadhira na kuiondolea ukinaifu wa masimulizi makavu.

# SUNSHINE SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)
## Mwongozo wa Kusahihisha

**INSHA YA WASIFU**

1. Swali la lazima
   Huu ni utungo amilifu
   Mtahimiwa azingatie
   (i) Mwaka wa kuzaliwa na alikozaliwa nchi, gatuzi, eneo bunge
   (ii) Wazazi wake watambuliwe na nchango wa katika kumfadhili iwapo kuna watu wengine
   Waliofadhili watambuliwe
   (iii) Elimu yake katika viwango vyote
   (iv) Kazi au taaluma anayozingatia
   (v) Tajiriba yake na umaarufu wake
   (vi) Tuzo ambazo amepata na machapisho ambayo amechapisha
   (vii) Changamoto zake katika maisha.
   (viii) Mchango wake katika kufaidi jamii
   (ix) Ndoto zake

Mtahiniwa azingatie mambo Chanya pekee. Asiingilie maisha yake ya kibnafsi

2 Hii ni insha ya mjadala.Pawe na hoja za kuunga mkono na kupinga

***Faida ya mitandao ya kijamii***

(i) Kupasha taarifa kwa muda mfupi iwezekanavyo
(ii) Burudani-sinema,vichekesho
(iii) Ni nyenzo ya kuelimisha kuhusu masuala tofauti katika jamii kwa vile hufikia watu wengi iwezekanavyo
(iv) Huunganisha watu bila kuzingatia asili yao,matabaka yao au hata umri wao
(v) Hutumiwa kufanya biashara kwa kutangaza na kuagiza bidha
(vi) Huunda nafasi za kazi kwwa vijana na hili kupelekea
(vii) Nchi kupata ushuru unaolipwa kupitia kwa biashara za mitandao
(viii) Huwezesha maingiliano ambapo baadhi ya watu hupata wachumba,wapenzi na marafiki
(ix) Hurahisisha mawasiliano duniani kwa kufanya dunia kuwa kama kijiji kimoja
(x) Huimarisha utafiti kwa muda mfupi

***Hasara za Mitandao ya kijamii***

(i) Wahalifu kupora mali ya watu kupitia kwa mitandao
(ii) Husambaratisha familia-wahusika hutumia muda mwingi kwa mitandao
(iii) Hueneza picha chafu kwa urahisi
(iv) Inaweza kutumiwa kuingilia maisha ya watu binafsi kwa kufichua siri zao
(v) Vijana huzembea wanapotumia muda mwingi kwa mitandao
(vi) Hutumiwa kuchochea kwa muda mfupi wezekanavyo
(vii) Hugharamia pesa nyingi zinazoweza kutumiwa kuboresha maisha kwa namna nyingine

3. **Hii ni Insha ya methali**

Ukiona vyombo vya bahari vikielea vimeundwa kisayansi

Tunapoviana vitu au mambo ya watu yamefanikiwa tukumbuke wamevifanyia kazi. Huhimiza juhudi maishani.

Mwanafunzi atunge kisa kitakachodhihirisha pande mbili za methali

4. ***Insha ya Mdokezo***

(i) Lazima mtahiniwa amalizie kwa maneno aliyopewa
(ii) Mtahiniwa asiongezee neno lolote baada ya mdokezo na asipachike neno lolote katika mdokezo
(iii) Anakili kimalizo jinsi kilivyo
(iv) Akikosa kunakili kimalizo asituzwe kwa vile amejitungia swali
(v) Kisa kidhihitishe namna mtoto wa Kiume alivyotelekezwa
    (a) Mtoto wa kiume kudekezwa hivyo kupotoka
    (b) Kuaminiwa ni dume hivyo kujingiza katika maovu kama vile uhalifu, matumizi ya dawa za kulevya na ulevi
    (c) Watoto wa kiume kwa kutelekezwa hupatana na vifo inavyotokana na ulevi athari za dawa za kulenvya,kupigwa risasi,kupigwa kitutu
    (d) Mara nyingi watoto wa kiume hatimaye huwa korokoroni
    (e) Watoto wa kiume kuwehuka

# SUNSHINE SECONDARY SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha
## Mwongozo wa Kusahihisha

**UFAHAMU:** Alama 15

(a) Umma kunyamaza na kukosa kutetea haki zao
(b) Alianza kuwathamini watoto wake walemavu
(c) Kutengwa hata na wazazi wao na kuonekana kama masimbi na mashate
(d) Ukombozi haupatikani kwa siku moja bali utachukua muda na ulihitaji uvumilivu
(e)(i) wajihadhari na hasira
(ii) Waepuke matumaini yaloyozidi uhalisia
(iii) Waepuka ulevi wa ushindi
(iv) Wapate elimu ya kujielewa hao ni kina nani
(f) (i) Wachache
(ii) Mfumo wa kujilimbikizia kila kitu
(iii) kumtoa mamlakani

**UFUPISHO:** **Alama 15**

(a) i) visa vya watu kupatikana na pesa bandia
ii) polisi kunasa bilioni 32 Kiambu
iii) Pesa zilikuwa dola,pauni na za Kenya
iv) Zilikuwa kwa masanduku 20 ya mabati
v) Washukiwa wafikishwa mahakamani
vi) Pesa zingine bandia kupatikana ndani ya benki ya Barclays
vii) Kuwepo kwa pesa hizi ni ishara kuna watu walio na viwanda vya kutengeneza pesa
viii) Wananchi wanazitumia bila taarifa

(b) (i) Matokeo ya pesa bandia ni kuporomoka kwa uchumi
(ii) Hili lilifanyika mwaka 1992
(iii) Ni hatari kusambaa kwa pesa bandia hasa Kenya inapokumbwa na madeni mengi
(iv) Pesa zikisambaa hupoteza dhamani yake
(v) Bidhaa na huduma kuwa ghali
(vi) Wahuni wachache wakiruhusiwa tutakuwa tumeidhinisha kuporomoka kwa uchumi
(vii) Polisi wana wajibu wa kuchunguza hilo

**MATUMIZI YA LUGHA**

(a) Mtahini akadirie sentensi tofauti
Ajabu!mtoto mzuri ameweza kusoma vizuri

(b) (i)Tamko la neno
(ii)Mama,baba

(c) 41– Kikwamizo
– mdomo na neno
–Ni sauti hafifu

101 – Sehemu ya ulimi – nyuma
-Mkao wa mdomo –viringwa
Mwinuko wa ulimi -Kali

(d) Kindumbwendumbwe

(e) Mtahini akadirie sentensi tofauti
Walikaa kimya
Kimya kingi hushangaza
Walikimya

(f ) (i) Mwishoni mwa tanakali za sauti
(ii) Huonyesha hisia tofauti
(iii)Kutoa amri ,ombi au rai

(g)Kuonyesha ukubwa
Kuonyesha dharau
Kiambishi kinachorejelea mtendaji
Kuunda nomino ili kuonyesha mazoea
(i) Jipaka hilo limekunywa maziwa
(ii) Jizee hilo linaudhi
(iii) Atajisomea
(iv) Msomaji msikilizaji

(h)

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| S | | | | | |
| S1 | | | U | S2 | |
| KN | KT | | | KN | KT |
| N | T | N | | N | T |
| mwanasiasa | anahutubuwananchi | | huku | O | wakimshangilia |

(i)Wao ndio wakulima bora watakaotuzwa na makatibu wakuu wa kilimo

(j) Mtahini akadirie
Utepe ule ule

(k) LI-LI-LO-PIK-W-A
LI – Mofimu ya kipatanishi ngeli
Li – Mofimu ya wakati
Lo- Mofimu ya urejeshi "o"
PIK- Mofimu ya mzizi
W- Mofimu ya mnyambuliko
A – Mofimu ya kiishio

(l) Mama aliita Sara mara mbili kwa hasira

(m) Japo wageni walikuwa wengi –Kishazitegemezi waliweza kuwatumbuiza-kishazi huru

(n) Kipaka/kijipaka kilirukia kifupa/kijifupa
Kilichorushiwa kwa kidirisha /kijidirisha

(o) Ukifanya kazi kwa bidii utafanikiwa

(p)Mfuatano wa matendo

(q) Aliwafunza vizuri

**ISIMUJAMII :** Alama 10

(a)(i) Uhusiano :Hutegemea kama ni wa kirafiki rasmi,kama vile mama na mtoto, mtoto na mwalimu
Hivyo ligha huwa tofauti

ii) Malezi :Malezi aliyopewa mtu huathili lugha zinayotumia :kuna wale waliofunzwa lugha ya adabu wengine hawakufunzwa,wengine wakaruhusiwa kijieleza vizuri huku wengine wakidhibitiwa

(b) (i) Ni chombo cha mawasiliano
(ii) Ni kitambulisho cha taifa
(iii) Kuunganisha wananchi
(iv) Huleta umoja wa kitaifa
(v)Kuendeleza utamaduni na mila za taifa hilo

( c) (i) Lugha ya upole
(ii) Lugha ya kihoji
(iv) Ishara za kisayansi hutumiwa
(iv) Kuna matumizi ya ndimi mseto
(v) Kuna lugha agizi
(vi) Msamiati maalum hutumiwa
(lazima mtahini atolee mifano)

# SUNSHINE SECONDARY SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

**1.SEHEMU A: Fasihi Simulizi**

(a) Miviga ni nini (alama 2)

Ni sherehe za kitamaduni ambazo hufanywa na jamii yoyote katika kipindi maalum cha mwaka

(b) Sifa za Miviga

(i) Huandamana na matendo,yanafuata utaratibu maalum
(ii) Huongozwa na watu mahususi
(iii) Kuna utoaji wa mawaidha
(iv) Maleba maalum huvaliwa na wahusika
(v) Hufanyika mahali sherehe inapofanywa
(vi) Huambatana na utamaduni wa jamii husika

(zozote 5)

(c) Hasara za Miviga

(i) Baadhi ya miviga imepitwa na wakati
(ii) Baadhi ya miviga inakinzana na malengo ya kitaifa
(iii) Hujaza watu hofu inapohusisha kafara za binadamu na ushirikina
(iv) Baadhi hughalimu kiasi kikubwa cha pesa

( zozote 3)

(d) Changamoto za mtafiti wa miviga

(i) Gharama ya utafiti
(ii) Baadhi ya wanajamii huhisi kana kwamba wanapelelezwa
(iii) Wahojiwa huenda wakadai kulipwa
(vi) Huenda mtafiti akabiliane na vizingiti vya kidini
(v) Kupotea kwa vifaa vya kuhifadhia data
(vi) Tafsiri za data iwapo Miviga iliwasilishwa kwa lugha ya jamii
(vii) Mtafiti huenda asiwe na wakati wa kutosha
(viii) Vikwazo kutoka kwa watawaha akosapo idhini ya kufanya hivyo

**Kigogo: Maudhui**

**ELIMU**

(i) Huzindua kwani waliolimika wanaelewa siasa za Sagamoyo na kutetea haki za wanyonge – Tunu na Sudi na Ashua

(ii) Huadilisha kwani wale wote waloelimika hawakubali kushiriki katika maovu-sudi anakataa hongo ya kisiasa kati yake na ngao junior

(iii) Elimu hii haibagui kwa misingi ya kijinsia wanawake na wanaume wanapata nafasi ya elimu hii

(vi) Elimu hii ni muhimu kwani walioelimika wanaitumia kwa manufaa yao kujitegemea na zaidi Kufaidi jamii-tunu,sudi na ashua

(v) Waliopata elimu wana msimamo dhabiti na hawawezi kushawishika japo wana matatizo ya kifedha-sudi alikataa hongo ya kenga naye Ashua aka kataa kazi ya majoka,tunu akakataa ndoa ya kisiasa

(vi) Elimu hii imedunishwa inapotumiwa kama soko la kulangua dawa za kulevya

badala ya kupitisha maarifa

(vii) Wanaoshindwa kufanikiwa katika elimu hii hutafuta vijisababu vya kila aina-Ngurumo analaumu mwalimu na historia

(viii) Waliopata elimu hii wanafanya kazi duni kama Ashua kuchuuza maembe

(ix) Elimu ya sagamoyo si bora kwani baadhi ya wahusika wanaisaka elimu hii ng'ambo – Tunu na Ngao junior

(x) Baadhi ya wahusika wanaidunishwa – Husda anasema heri elimu yake ya msingi (zozote 10)

**UJANA**

(i) Ujana ni umri wa kufanya kazi.Ashua,Tunu na Sudi ndio umri mwafaka wa kusaka elimu-vijana ndio wanaotafuta elimu-Ashua,Ngurumo,Tunu na Sudi

(ii) Umri huu vijana huanzisha familia-Ashua na Sudi,Tunu anashawishiwa aolewe

(iii) Vijana ndio wanaotetea haki za wanyonge kama vile Tunu an Sudi wanamkabili Majeka kwa sababu ya haki za wanyonge

(v) Wengine hata wanalipia kwa damu yao wanapoandamana na kuuwawa –vijana watano

(v) Huu ndio umri wa kuchukua uongozi-Tunu anachukua uongozi mwishoni

(vi) Vijana huhamasisha wananchi kuhusu haki zao-Tunu ,Sudi, na Siti wanaelekea kikao cha walevi kuwazindua na kuwahamasisha

(vii) Huu ndio unri ambapo baadhi ya vijana hushiriki katika uhalifu-Ngurumo kushambulia Tunu wakiwa na wahuni wengine na huenda pia walihusika katika mauaji ya Jabari

(viii) Vijana wawa hawa hushiriki ulevi na hili hutumiwa na Majoka ili wasielewe siasa za sagamoyo

(ix) Wengine hutumia dawa za kulevya zinazosababisha vifo-ngao junior

(x) Baadhi ya vijana wana jicho la je-Ngurumo kuingilia ndoa ya Boza na Asiya (zozote 10)

**MVUNJA NCHI NI MWANANCHI**

(i) Majoka- Alilangua dawa za kulevya katika shule ya majeko academy
Alipora mali ya umma (soko la chapakazi)

Aliruhusu uuzaji wa pombe haramu
Ukataji miti
Alifunga soko la chapakazi na kuharibu uchumi wa sagamoyo –kwa jumbe alikuwa kiongozi mbaya

(ii) Kenga- Alimshauri majoka vibaya afunge soko la chapakazi ili naye apate sehemu kaitika kiwanja cha soko hilo

(iii) Boza – Alikuwa kikaragosi cha Majoka aliyemuunga mkono bila kutathmini viongozi wake, Alikula makombo ya keki na kuunga mkono hata kufungwa kwa soko

(iv) Ngurumo – Alishiriki uhalifu kwa kumshambulia Tunu wakiwa na wahuni wa kulipwa
Hii ni namna ya kuvunja nchi kwani Tunu alikuwa mtetezi wa haki za umma

(v) Kombe:- Hana msimamo wa kisiasa hivyo hawezi kutegemewa katika ukombozi

(vi) Asiya (mama pima) Alivunja nchi yake kwa kuuzia wananchi kama vile

Ngurumo na walevi wengine pombe haramu aliyodhuru afya yao.

(vii) Askari – Kuua vijana watano wakati wa maandamano ni kuvunja nchi kwani vijana hao walikuwa wakitetea haki yao

(viii) Wananchi wanavunja nchi yao kwa kuteua viongozi wabaya kama vile Majoka

(ix) Mtu wa I & ii walivunja nchi yao kwa kushiliki ulevi na kutumia dawa za kulevya

(x) Ashua alivunja nchi yake kwa kuamini propaganda kuwa Sudi alikuwa na Tuna walikuwa mapenzi nje ya ndoa kando na juhudi za kupigania haki za wanyonge.akiwa korokoroni alimzomea Sudi

(xi) Walevi pale kwa mama pima walishiriki ulevi badala ya kufanya kazi ya ujenzi wa taifa (zozote 10 x 2) = 20

(xii) Chopi na Ngao Junior walishiriki katika matumizi ya dawa za kulevya

## SEHEMU E: USHAIRI

4

(a) Dhamira ya mtunzi kuhimiza binadamu asifuate maovu hasa yanayohusiana na kudhulumu wanyonge bali afuate maadili na atetee wanyonge (alama 2)

(b) Ainisha bahari
Mpangilio wa maneno –kikwamba
Vipande vya mishororo-Mathnawi
Idadi ya mishoro - tarbia (alama 3)

(b) Urudiaji
Usambamba – moyo wanambia –huu ni urudiaji wa kifungu (alama 2)

(d)(i) Beti saba
(ii) Mishororo minne kwa kila ubeti
(iii) Migao/vipande viwili kwa kila mishororo
(iv) Vina vya kila ubeti ni tofauti
(v) Shairi lina kibwagizo-moyo wanambia woga ndio mwanzo wa maafa
(zozote 4)

(e) Ubeti wa tano kwa lugha ya nathari (alama 4)
Epuka tabia za wizi na hata usitamani bali ukashifu vitendo vya aina hiyo kwani ukiogopa
Huenda maafa yapatikane.

(f) Uhuru wa kishairi ( alama2)
(i) Inkisari-neno wanambia limefupishwa kutoka kwa neno unaniambia
(ii) Kuboronga sarufi-kuwa mwizi usiote badala ya usiotee ukiwa mwizi

## USHAIRI (SWALI LA 4)

(g)(i) Dikteta :Mtu anayeongoza kiimla
(ii) Kasuku:anayezungumza bila vitendo
(iii) Mnyonyaji-Anayetesa na kudhulumu wengine

## USHAIRI SWALI LA 5

5(a) Anwani mwafaka-nabaki tupu,mimi mtupu
(b) Taswira mwono
(c) Anakashifu tabia ya kudhulumu wanaozalisha mali lakini wanabaki maskini
(d) Shairi huru-Halijazingatia kanuni za arydhi/utunzi
(e) Toni – unyonge
(f) Kinaya – kuangazia dhamira kuu.
(g) Mistari mishata-ujumbe hueleweka katika mshororo unaofuata mfano-ni mimi tumbo kubwa
(h) Kuonyesha namna wanaozalisha mali wanavyoteseka
(i) Mzalishaji mali/mtu wa kawaida/kibarua

**HADITHI FUPI**

6(i) Muktadha

Haya ni maneno ya babake Sara akimzomea Sara iwapo angelipoti kuwa amebakwa kama yanavyotokea katika mawazo ya Sara
(alama 4)

(ii) Sifa mbili na umuhimu wa babake Sara

(a) Mkali – Hukemea watoto wake wanapokosea kama Sara anavyodhihirisha katika mawazo yake
(b) Ana mapenzi ya dhati-alipojua bintiye ana mimba anagharamia matibabu bila kulalamika
(c) Ni msiri-alipojuzwa kuhusu mimba ya Sara hakumfichulia
(d) Mwajibikaji- Alipeleka bintiye Sara shule na alipojifungua aliendelea kumtunza (zozote 2)

**UMUHIMU**

(a) Ni kielelezo cha wazazi wakali wanaogofyawatoto wao hadi hawawezi(watoto) kuwafichulia siri hata kama zinaathiri maisha yako
(b) Ni kielelezo cha wazazi wanaokabiliana na athari za vitendo viovu kupitia kwa watoto wao-Inabidi atunze bintiye mjamzito baada ya kitendo cha ubakaji (zozote 6x2)

**UBAKAJI**

(iii)(a) Wanawake hubakwa kwa sababu za kimaumbile
- Sara anasema alibakwa kwa sababu ni Mnyonge kimaumbile

(b) Ubakaji utokeapo mwanamke huathirika zaidi sara anapata mimba ambayo hakutaka

(c) Ubakaji utokeapo mwanamke hulaumiwa kama Sara anavyolaumiwa na babake na walimu Wake

(d) Wanawake wanapobakwa huvunjiwa unanajike utu na kuharibiwa maisha kama Sara Anavyohisi

(e) Wanawake hukosa namna ya kukabiliana na tatizo hili hivyo hujilaumu nao wabakaji huendelea kutekeleza vitendo hivyo

(f) Kwa vile sheria mara nyingi hukosa kuadhibu wabakaji kwa wakati ufaao,wananchi huchukua sheria mkononi kushambulia wabakaji kama lilivyouliwa bakaji lile kwa vua la mawe.

**Anwani-Chozi la Heri**

(i) Ridhaa kutengwa shuleni na wenzake na kuitwa mfuata mvua,baadaye wanamkubali baada ya ushauri
(ii) Kaizali kupona donda lililosababishwa na kuona binti zake wakibakwa
(iii) Ridhaa kupatana na Mwangeka na kuliliana chozi la heri
(iv) Siku mwangeka alipomwoa Apondi alimwaga chozi la Heri
(v) Dick/umu na mwaliko walipopatana .walilia chozi la heri
(vi) Mwanaheri anatokwa na chozi la heri anaposimulia wenzake yaliyompata –kutoweka kwa mamake
(vii) Neema anapokumbatia mwanawe wa kupanga anatokwa na chozi la heri
(viii) Ridhaa anatokwa na chozi la heri anapoitwa bubuu na mjukuu badala ya babu
(ix) Ridhaa anatokwa na chozi la heri kwa kuona Mwangeka na Apendi wakioana
(x) Chozi la heri linamtoka mwangeka aliposimuliwa na babake sababu ya kutozika mabaki ya aila yake

**TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

7.Nafasi ya mwanamke

Ndoto ya mashaka

(i) Mwanamke hulazimishwa kwa ndoa kama alivyofanyiwa Waridi.
(ii) Hapangi uzazi
(iii) Anapokabiliwa na shida kaitika ndoa hujitorokea na kumwacha mume akiwa pweke
(iv) Mlezi –Bi kidebe,hukabiliwa jukumu la ulezi
(v) Hujitegemea kwa vibarua vidogo –kidebe

**Masharti ya kisasa**

(i) Mwanamke ana uhuru wa kijiteulia mume kidawa alijiteulia Dadi
(ii) Anashiriki katika maamuzi muhimu ya ndoa, anampa Dadi masharti ya kumsaidia
(iii) Anapanga idadi ya watoto atakaopata –Kidawa alipanga kupata mmoja

(iv) Hufanya biashara za kando kukidhi mahitaji ya familia alichuuza bidhaa
(v) Ana Uhuru wa kutangamana na yeyote apendaye
(vi) Bado anadhibitiwa na mume kwani mwishowe anaamua kuacha kazi
(vii Ana uhuu wa kuvaa anachotaka na kijipamba

**Mapenzi ya kifaurongo**

(i) Mwamanke ni mnafiki-Penina anadanganya Dennis anampenda hata kama ni maskini lakini nia yake ilikuwa kujihusisha naye kimapenzi
(ii) Anasawiriwa kama mpenda mali-Penina amamfukuza Dennis alipokaa sana bila kupata mali
(iii) Mwanamke anasawiriwa kama mjenzi wa taifa mamake Shakila ni mkurungezi wa kampuni

(iv) Mwanamke ameng'amgana na wanaume kusaka elimu ya juu .Penina na wasichana wengine kama Shakila
(v) Baadhi ya wanawake huona kuwa ufanisi wao utatokana na maisha ya ndoa-msichana mmoja waliyesoma na Dennis alisema kuwa angeelewa aepukane na adha ya masomo

**Shogake dada ana ndevu**

1. Mwanamke anasawariwa kama Mbeya-mama Safia anakiri kushiriki umbeya akimsengenya Mkadi
2. Mwanamke anapojihusisha na mapenzi ya kiholela athari hasi humpata-Safia kupata mimba asiyohitajji
3. Mwanamke kufanya kazi zote za nyumbani Safia husaidia mamake kazi zote za nyumbani
4 Mwanamke amepotoka kimaadili-Safia anaingiza kimwana kwa nyumba yao na kujihusisha kimapenzi
5. Mwanamke ni katili Safia ana avya mimba na kuangamia

# BAHATI GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)
## Mwongozo wa Kusahihisha

**1. Hii ni barua rasmi.**
**Ihusishe mambo yafuatayo:**
a) Iwe na anwani mbili: Ya mwandishi na ya mwandikiwa.
b) Tarehe chini ya anwani ya mwandishi.
c) Mtajo: Kwa Waziri,
d) Kichwa: MINTI: YAH: KUH:
e) Mwili/Kiini /maudhui
f) Hitimisho: Wako mwaminifu, sahihi na Jina.

Usahihishaji ulenge masuala muhimu yafuatayo:
a) Muundo /sura ya barua rasmi:

i) Anwani mbili
ii) Tarehe
iii) Mtajo
iv) Kichwa
v) Mwili
vi) Hitimisho

b) Maudhui; yaliyomo, majibu ya swali. Yafuatayo yanaweza kushughulikiwa kwa ufafanuzi.

i. Misimamo mikali ya kidini/ukengeushi wa kidini(radicalization)
ii. Ufisadi mipakani unaowaruhusu magaidi kupenya
iii. Ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana wadogo
iv. Kulipiza kisasi
v. Tamaa ya pesa
vi. Ukengeushi wa kimaadili
vii. Kutamauka maishani

Maudhui matano yanaweza kushughulikiwa kikamilifu.

**2. Hii ni insha ya mjadala wazi.**

a) Mtahiniwa anaweza kuchukua mkondo wowote kati ya hii mitatu.

i) Akubaliane na usemi huo, hivyo ashughulikie athari mbaya pekee za utandawazi kwa vijana. Hapa ashughulikie kwa kina hoja tano.

ii) Apinge usemi huo; hivyo ashughulikie athari nzuri- manufaa ya utandawazi katika maisha ya vijana. Lazima ashughulikie hoja zisizopungua tano.

iii) Ashughulike pande zote mbili; atoe hoja na kutetea uzuri wa utandawazi na hoja za kutetea ubaya wa utandawazi, kisha atoe msimamo wake kulingana na uzito wa hoja.

b) Hoja zifuatazo zinaweza kushughulikiwa:

i) Mkengeuko wa maadili.
ii) Mataifa makubwa/ yaliyoendelea kutawala machanga, hivyo kudunisha maisha ya vijana wake.
iii) Mataifa makubwa kuyanyonya na kuyafyonza mataifa machanga hivyo kusababisha umasikini miongoni mwa vijana.
iv) Kurahisisha mawasiliano kati ya mataifa mbalimbali hivyo kuimarisha biashara miongoni mwa vijana
v) Kurahisisha usafirishaji wa watu, bidhaa na habari kati ya vijana kutoka mataifa mbalimbali.
vi) Kupanuka kwa fursa za ajira miongoni mwa vijana
vii) Kusababisha kuenea kwa kasi mabadiliko ya kila aina ulimwenguni kama vile kiuchumi, kisiasa na kijamii.
viii) Kupujua tamaduni za kiafrika miongoni mwa vijana.
ix) Kuathiri mahusiano kati ya jamaa na marafiki.
x) Umeeneza ubinafsi miongoni mwa wanajamii hususan vijana

c) Mtahiniwa ajadili hoja zake kikamilifu kiaya kwa kutoa mifano.

**3. Hii ni insha ya methali.**

Mtahiniwa abuni kisa kinachoafiki maana ya methali.
Maudhui yalenge mtu anayedhaniwa alivyo na kumbe ni kinyume.

a) Pande zote mbili za methali zishughulikiwe kikamilifu.
b) Methali aliyopewa inaweza kuwa kichwa/anwani ya insha ya mtahiniwa.
c) Si lazima mtahiniwa atoe maana ya methali na matumizi yake.

**4. Hii ni insha ya mdokezo tamati.**
a) Mtahiniwa ahitimishe insha yake kwa maneno aliyopewa bila kuzidisha wala kupunguza.
b) Mtahiniwa abuni kisa kitakachooana na hitimisho alilopewa.
c) Anaweza kutumia mbinu rejeshi ili kuvyaza kisa kitakachoafikiana na hitimisho alilopewa

**MWONGOZO WA KUDUMU**
**UTANGULIZI.**
Karatasi hii imedhamiria kutathmini uwezo wa mtahiniwa wa kuwasiliana na msomaji na kuwasilisha ujumbe kimaandishi,akizingatia mada aliyopewa. Mawasiliano haya yatategemea ukwasi wa lugha ya mtahiniwa, kwa mfano, kutunga sentensi sahihi zenye mtiririko mzuri kimawazo, lugha ya kuvutia na yenye mawazo asilia, ubunifu mwingi na hati nadhifu. Kwa kutegemea maagizo ya swali lenyewe na umahiri wa lugha, ni lazima

kutilia mkazo mtindo, mada na uwezo wa mtahiniwa kufuata maagizo vilivyo. Mtahini lazima aisome insha yote huku akizingatia sarufi, hijai, hoja, msamiati na mtindo ili aweze kuikadiria kwa kurejelea viwango mbalimbali vilivyopendekezwa. Viwango vyenyewe ni A, B, C na D kutegemea uwezo wa mtahiniwa.

**VIWANGO MBALIMBALI.**
**KIWANGO CHA D KWA JUMLA MAKI 01-05.**
i) Insha haieleweki kwa vyovyote vile ama uwezo wa mtahiniwa wa kutumia lugha ni hafifu sana, hivi kwamba mtahinilazima afikirie kile mtahiniwa anachojaribu kuwasilisha.
ii) Mtahiniwa hana uwezo wa kutumia maneno ya Kiswahili kwa njia inayofaa.
iii) Lugha imevurugika, uakifishaji haufai na insha ina makosa ya kila aina.
iv) Kujitungia swali na kulijibu.
v) Insha ya urefu wa robo ikadiriwe hapa.

**NGAZI MBALIMBALI ZA KIWANGO CHA D**.
D- (D YA CHINI) MAKI 01-02.
i) Insha haina mpangilio maalum na haieleweki kwa vyovyote vile.
ii) Kujitungia swali tofauti na kulijibu.
iii) Kuandika kwa lugha isiyo Kiswahili au kuchanganya ndimi.
iv) Kunakili swali au maswali na kuyakariri.
v) Kunakili swali au kichwa tu.
D WASTANI MAKI 03.
i) Mtiririko wa mawazo haupo.
ii) Mtahiniwa amepotoka kimaudhui.
iii) Matumizi ya lugha ni hafifu mno.
iv) Kuna makosa mengi ya kila aina.
D+ (D YA JUU) MAKI 04-05.

i) Insha ya aina hii hukuwa na makosa mengi ya kila aina, lakini unaweza kutambua kile ambacho mtahiniwa anajaribu kuwasilisha.
ii) Hoja hazikuelezwa kikamilifu/ mada haikukuzwa vilivyo.
iii) Mtahiniwa hana uhakika wa matumizi ya lugha.
iv) Mtahiniwa hujirudiarudia.
v) Insha itakayozingatia sura lakini ikose maudhui ikadiriwe hapa.

**KIWANGO CHA C KWA JUMLA MAKI 06-10**.
i) Mtahiniwa anajaribu kuishughulikia mada japo hakuikuza na kuiendeleza vilivyo.
ii) Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kwa njia isiyovutia
iii) Mtahiniwa anaakifisha sentensi vibaya.
iv) Mtiririko wa mawazo unaanza kujitokeza japo kwa njia hafifu.
v) Insha ina makosa mengi ya sarufi, ya msamiati na ya tahajia (hijai).
C- (C YA CHINI) MAKI 06-07.
i) Mtahiniwa ana shida ya kuwasilisha na kutiririsha mawazo yake.
ii) Mtahiniwa hana msamiati wa kutosha wala miundo ya sentensi ifaayo.

iii) Mtahiniwa anafanya makosa mengi ya sarufi, ya hijai na ya msamiati na insha yake haieleweki kwa urahisi.
C WASTANI MAKI 08.
i. Mtahiniwa anawasilisha ujumbe lakini kwa njia hafifu.

i) Dhana tofauti tofauti hazijitokezi wazi.
ii) Mtahiniwa hana ubunifu wa kutosha.
iii) Mtiririko wa mawazo ni hafifu na hana ufundi wa lugha unaofaa.
iv) Anajaribu kushughulikia mada aliyopewa.
v) Mtahiniwa ana shida ya uakifishaji.
vi) Mtahiniwa anafanya makosa mengi ya sarufi, ya hijai na ya msamiati lakini bado insha inaeleweka.

C+ (C YA JUU) MAKI 09-10.
i) Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri akizingatia mada lakini kwa njia isiyo na mvuto.
ii) Dhana tofauti tofauti zimejitokeza japo kwa njia hafifu.
iii) Kuna mtiririko wa mawazo japo hana ufundi wa lugha unaofaa.
iv) Misemo na methali zimetumika kwa njia hafifu.
v) Ana shida ya uakifishaji.
vi) Kuna makosa ya sarufi, ya msamiati na ya hijai yanayoathiri mtiririko wa mawazo.

**KIWANGO CHA B KWA JUMLA MAKI 11-15**
i) Mtahiniwa anaonyesha hali ya kuimudu lugha.
ii) Mtahiniwa anatumia miundo tofauti tofauti ya sentensi vizuri.
iii) Mtahiniwa ana uwezo wa kutumia lugha kwa ufasaha.
iv) Mada imekuzwa na kuendelezwa kikamilifu.
v) Insha ya urefu wa robo tatu ikadiriwe katika kiwango hiki.

**Ngazi mbalimbali za kiwango cha B.**

B- (B YA CHINI) MAKI 11-12
i) Mtahiniwa anawasilisha ujumbe vizuri kwa kueleza hoja tofauti tofauti akizingatia mada.
ii) Mtahiniwa ana mtiririko mzuri wa mawazo.
iii) Mtahiniwa anatumia mifano michache ya msamiati unaovutia.
iv) Makosa yanadhihirika kiasi.
B WASTANI MAKI 13
i) Mtahiniwa anadhihirisha hali ya kuimudu lugha.
ii) Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika akizingatia mada.
iii) Mtahiniwa anateua na kutumia mifano michache ya msamiati mwafaka.
iv) Sarufi yake ni nzuri.
v) Makosa ni machache/ kuna makosa machache.
B+ (B YA JUU) MAKI 14-15
I) Mawazo ya mtahiniwa yanadhihirika na anajieleza waziwazi.

ii) Mtahiniwa anawasilisha ujumbe kwa njia inayovutia na kwa urahisi akizingatia mada.
iii) Mtahiniwa ana mchanganyiko mzuri wa msamiati unaovutia.
iv) Sarufi yake ni nzuri.
v) Uakifishaji wa sentensi zake ni mzuri.
vi) Makosa ni machache ya hapa na pale.

**KIWANGO CHA A KWA JUMLA MAKI 16-20**
i) Mtahiniwa ana ubunifu wa mawazo yanayodhihirika na kutiririka akizingatia mada.
ii) Mtahiniwa anadhihirisha ujuzi wa lugha yenye mnato.
iii) Ana uwezo wa kutumia tamathali za usemi ili kutoa hisia zake kwa njia bora na kwa urahisi.
iv) Umbuji wake unadhihirisha ukomavu na ukakamavu wake kimawazo.
v) Insha ina urefu kamili.

**USAHIHISHAJI NA UTUNZAJI KWA JUMLA**.
Mtahini ni sharti aisome insha yote akizingatia vipengee muhimu. Vipengee hivi ni maudhui, msamiati, mtindo, sarufi na hijai.

**MAUDHUI**.
Maudhui ni hoja au mambo yanayozungumziwa, kuelezewa au kuhadithiwa kwa mujibu wa mada iliyoteuliwa. Maudhui ndio hasa uti wa mgongo wa insha yoyote ile. Ubunifu wa mtahiniwa hukisiwa kwa kutathmini uzito wa maudhui yake kulingana na mada teule.

**MSAMIATI**.
Msamiati ni jumla ya maneno yatumiwayo katika lugha husika. Mtahiniwa anatarajiwa kutumia msamiati unaooana na mada teule. Kutegea ukwasi wa lugha alionao, mtahiniwa anatarajiwa kuikuza mada kwa kuifinyanga lugha kiufundi. Ni muhimu kuelewa kwamba kutokana na maendeleo na ukuaji wa teknolojia na mawasiliano, maneno mapya yanaibuka kila uchao.

**MTINDO**.

Mtindo unahusu mambo yafuatayo:

- Mpangilio wa kazi kiaya.
- Mtiririko na mshikamano wa mawazo kiaya na katika insha nzima.
- Hati nzuri na inayosomeka kwa urahisi.
- Matumizi ya tamathali za usemi, kwa mfano methali, misemo, jazanda na kadhalika.
- Kuandika herufi vizuri kwa mfano Jj, Pp, Uu, Ww na kadhalika.
- Sura ya insha.
  Unadhifu wa kazi ya mtahiniwa.

**SARUFI**.

Sarufi ndio msingi wa lugha. Ufanisi wa mawasiliano hutegemea uwezo wa mtahiniwa wa kutunga sentensi sahihi zenye uwiano wa kisarufi. Mtahini ataonyesha makosa yote ya sarufi yaliyo katika insha anayosahihisha. Makosa ya sarufi huweza kutokea katika:

Matumizi ya alama za uakifishaji.

1. Kutumia herufi kubwa na ndogo mahali pasipofaa.

2. Matumizi yasiyofaa ya ngeli na viambishi, viunganishi, nyakati, hali, vihusiano na kadhalika.
3. Mpangilio wa maneno katika sentensi.
4. Mnyambuliko wa vitenzi na majina.
5. Kuacha neno linalohitajika au kuongeza neno lisilohitajika katika sentensi.
6. Matumizi ya herufi kubwa katika:

a. Mwanzo wa sentensi.

b. Majina ya pekee.

i. Majina ya mahali, miji, nchi, mataifa na kadhalika.

ii. Siku za juma, miezi n.k

iii. Mashirika, masomo,vitabu n.k

iv. Jina la mungu.

v. Majina ya kutambulisha hasa wanyama wa kufugwa, kwa mfano yale ya mbwa- Foksi, Jak, Popi, Simba,
Tomi na mengineyo.

**MAKOSA YA HIJAI/TAHAJIA**.

Haya ni makosa ya maendelezo. Mtahini anashauriwa asahihishe huku akiyaonyesha yanapotokea kwa mara ya kwanza tu.

Makosa ya tahajia huweza kutokea katika:

Kutenganisha neno kwa mfano ‗aliye kuwa'

Kuunganisha maneno kwa mfano ‗kwasababu'

Kukata silabi visivyo afikapo pambizoni kama vile ‗ngan - o'.

Kuandika herufi isiyofaa kwa mfano ‗ongesa' badala ya ‗ongeza'

Kuacha herufi katika neno kwa mfano ‗aliekuja' badala ya ‗aliyekuja'

Kuongeza herufi isiyohitajika kama vile ‗piya' badala ya ‗pia'

Kuacha alama inayotarajiwa katika herufi kama vile j i
Kukosa kuandika kistari cha kuendelezea neno afikiapo pambizoni au kukosa kukiandikia mahali pasipofaa.
Kuacha ritifaa au kuiandikia mahali pasipofaa, kwa mfano ngombe, ngom'be, n'gombe, ngo'mbe n.k
Kuandika maneno kwa kifupi kama vile k.v, k.m, v.v, n.k na kadhalika.
Kuandika tarakimu kwa mfano 27-08-2010.

**UKADIRIAJI WA UREFU WA INSHA.**
Maneno 9 katika kila mstari – ukurasa moja na nusu.
Maneno 8 katika kila mstari – ukurasa moja na robo tatu.
Maneno 7 katika kila mstari – kurasa mbili.
Maneno 6 katika kila mstari – kurasa mbili na nusu.
Maneno 5 katika kila mstari – ukurasa mbili na robo tatu.
Maneno 4 katika kila mstari – kurasa tatu na robo tatu.
Maneno 3 katika kila mstari – kurasa nne na nusu.

# BAHATI GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM – Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha
## Mwongozo wa Kusahihisha

**UFAHAMU**
1.Hatetereki anapoishiwa abadilishe wazo kuhusu shule ya ndoto lake.
2. Uamuzi wa kutohama kutoka shule hii hata baada ya kuona yaliyompata. 2 x 1 = 2

**B: Shule ya binafsi**
1. Alitunzwa kama kikembe.
2. Walimu waliomfunza walitamka kimombo kwa njia bora.

**Shule ya upili** Matamshi ya walimu yaliathiriwa na lugha ya asili. walimu wasiojali uelewa wa wanafunzi. Wasioshughulika wasipofanya kazi za ziada. zozote 3 x 1 = 3
**C: Mitaa walikoishi**
– Uamuzi wa kununua nyumba Karen.
– Kuruka hadi pwani.
– Mama yake kumiliki jumba katika shamba la ekari.
– tatu ufuoni. zozote 3 x 1 = 3

**D:**
– Mwanafunzi kukosa viatu.
– Chakula duni katika shule hii.
– Idadi ya wanafunzi katika darasa.
– Kushambuliwa na wadudu.

– Kuongozwa na mvulana wa alama . zozote 3 x 1 = 3

**E:**
– Uhuishi - Tumbo la gari.
– Misemo - Ragba ya mkanja.
– Takriri - Sikujua.
– Methali - Mgeni njoo mwenyeji apone. 2 x 1 = 2

**F:**
– Alimstahi - Heshimu.
– Kughairi - badilisha.
– Kunighasi - kunikasirisha. 3 x 1 = 3

Katika sehemu ya ufahamu adhibu ifuatavyo.

1 **1**/**2** x makosa 6 ya hijai = 3 **1**/**2** x makosa 6 ya sarufi = **3** Jumla **6**

**UFUPISHO**
a) i) Binadamu alipewa uwezo wa kumiliki kila kitu.

ii) Binadamu alipewa akili na maarifa ili kupanga mambo yake.
iii) Alipewa uwezo wa kuwasiliana na wenzake kwa kutumia lugha.
iv) Alipewa uwezo wa kufaidika kutokana na mazingira yake.
v) Alipewa uwezo wa kuza na kujaza dunia. (Yoyote 5x1=5)

b) i) Binadamu amekuwa dubwana linalojenga na kubomoa.

ii) Viwanda vinachafua maji na kuua viumbe muhimu kwa binadamu.
iii) Moshi kutoka viwandani umedhuru ukanda wa ozone na joto kuzidi duniani.
iv) Idadi ya binadamu imeongezeka zaidi ya uwezo wake.
v) Maradhi na ufukara yamekuwa matatizo makubwa kwa binadamu.
vi) Binadamu anafyeka misitu yote.
vii) Binadamu amewafurusha na kuwaangamiza baadhi ya wanyama.
viii) Chemichemi za maji zimekauka na kuwa jangwa. (Zozote 8x1=8)

*tanbihi : alama 1 ituzwe kwa mtirirko katika kila swali*

**3. MATUMIZI YA LUGHA: (Alama 40)**
a) Taja sifa mbili bainifu za irabu/u/. (alama 2)
- irabu ya nyuma - Irabu mviringe/hutamkwa na mdomo ukiwa mviringo. 2x1=2
b) Tunga sentensi kwa kutumia kiwakilishi huru cha nafsi ya tatu umoja (alama 2)
mf :Yeye atasoma kidagaa kimemwozea. (1x2=2
c) Andika umoja wa sentensi zifuatazo (alama 2) .
-Akitaka nimsamehe aje aniombe radhi kwa aliyonifanyia. 1x1=1
- Lililosemekana ni kuwa lake limeharibiwa na binamuye. 1x1=1
d) Yakinisha. (alama2)
- Anaskia la mwadhini na lamteka maji msikitini. 1x2=2


e) Bainisha shamirisho kipozi na kitondo katika sentensi ifuatayo. (alama 2)
Kitendo-chakula
kipozi -mwanawe 2x1=2
f) Tunga sentensi moja yenye chagizo ya mahali na ya wakati. (alama 2)
-mfano: Walienda **uwanjani jana jioni** 1x2=2 (mahali wakati )
g) Onyesha mfumo wa sauti katika tungo: matumbwini. (alama 2)
K+KI+KKKI+KI (4x½=2).
h) Tambua vipashio vya sarufi ya Kiswahili (alama 3)
- Sauti - Silabi - Neno – Sentensi (zozote 3 x 1=3

i) Huku ukitoa mfano, eleza mantiki inayopatikana katika kauli ya kutendua. (alama 2)
- Vitenzi katika kauli hii huwa na maana ya kinyume k.m funga - fungua fukia-fukua kosa-kosoa 1x2=2

j) Taja matumizi manne ya kiambishi "ki" (alama 2)
- Hutumiwa kuonyesha udogo wa nomino k.m kibuzi.
- Hutumiwa kama kiambishi cha upatanisho wa kisarufi ngeli ya ki-vi.
- Hutumiwa kufananisha na vielezi vya namna mfano.
- Hutumika mwanzoni mwa majina ya lugha k.v Kiswahili.( ½x4=2)

k) Eleza maana mbili ya sentensi ifuatayo
(alama 2)
- Jambazi lilimwibia Okoth gari jipya.
- Jambazi liliiba gari likampa Okoth.
- Jambazi liliiba gari la Okoth. 2x1=2

i) Bainisha vishazi huru na vishazi tegemezi katika sentensi ifuatayo
(alama 2)
Nitaenda maktabani- Kishazi huru
ingawa ninaumwa na kichwa- Kishazi tegemezi
2x1=2
m) Andika katika kauli ya kutendesha (alama 1)
- Ile pombe aliyokunywa Chacha ilimlevya. 1x1=1
n) Changanua kwa kutumia mtindo wa kielelezo cha matawi. (alama 4)




Mtoto ambaye amefika ni ndugu yangu.
o) Andika kinyume cha sentensi ifuatayo. (Alama 2)
- Huzuni alikashifu nduguye aliyetawanya takataka zote. 1x2=2
p) Tumia neno "vibaya" kama:
i) Kivumishi
Vyombo vibaya vimetupwa (1x1=1)

ii) Kielezi
Aliimba wimbo huo vibaya. 1x1=1
q) Tunga sentensi yenye kihusishi cha 'a'- unganifu katika ngeli ya U-ZI. (alama 1)
Ukuta wa nyumba umebomoka. (1x1=1)
r) Mbwa wetu amekatwa mkia. Geuza katika hali ya ukubwa. (alama 2)

Jibwa letu limekatwa jikia/kia /Jijibwa letu limekatwa jikia. (1x2=2)

s) Tunga sentensi moja kutofautisha maana ya maneno haya. (alama 1)
Mkembe, mkebe
Sentensi iwe maana ya: mkebe- chombo cha bati kinachotumiwa kuweka vitu vidogo vidogo
mkembe - mtoto mdogo mwenye umri baina ya mwaka mmoja na miaka sita au kijana aliyebaleghe ambaye hajoa.

t) Tumia ngali kutunga sentensi ili kuleta maana ya: (alama 2)
i) tendo kuendelea :Wanafunzi wangali wanacheza uwanjani (1x1=1)
ii) Tendo kutoweza kufanyika kwa sababu ya wakati kupita: Mwalimu angalikuwa na pesa angalienda ulaya. (1x1=1)

**4. ISIMU JAMII**

a)– Kuwepo kwa lahaja nyingi- baadhi yazo hazingeeleweka na kila mtu.
– Kulikuwa na haja ya kuwa na hati sawa ya kuandika Kiswahili –Kul;ikuwa na hati nyingi kwa
mfano ,Kirumi , kilatini na kiarabu.
– Kulikuwa na haja ya kusawazisha maandishi ya kitaalamu katika kamusi.
– Haja ya kuwa na lugha moja ya mawasiliano na elimu –kutumika katika kamusi.
– Haja ya kuwa na lugha moja ya mawasiliano na elimu –kutumika katika mikutano, shuleni, vyuoni n.k (5x1=5)

b) Sajili ya mazishi /matanga /kilio masikitiko /msiba/ maombolezo/uzikaji.

**Sifa**

– Msamiati maalum kwa mfano makiwa marehemu.
– Lugha ya kufariji/liwaza
– Yenye matumaini
– Matumizi ya vihihisishi oh, wuui,
– Lugha ya kusitasita
– Huhusisha sana mambo ya kidini na Mungu na Imani za jamii.
– Ni lugha ya hasira.
– Kuchanganya ndimi
– Inaadaman na viziada lugha

– Matumizi ya sentensi fupi
– Matumizi ya sentensi ndefu
– Imesheheni sifa za m wendazake
– Matumizi ya lugha isiyozingatia kanuni za kisarufi. Zozote 5x1=5)

# BAHATI GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

**1. CHOZI LA HERI**

a) - maneno ya Ridhaa
- akimwambie mwanawe Mwangeka
- wamo kwenye nyumba yao iliyochomwa
- anamwelezea dhiki ambazo amepitia tangu ghasia za baada ya kutawazwa kwa kiongozi mpya kuzuka.

4x1=4

b) msemo/nahau-onja shubiri 1x2=2

c)
i) Kubomolewa kwa nyumba mtaani Tononokeni bila kufidiwa
ii) Kutapeliwa na raia wenzake fisadi wanaomuuzia ardhi katika eneo lililotengewa ujenzi wa barabara
iii) Kuchomekewa na nyumba-jengo lake la kibiashara linachomeka kutokana na hitilafu ya moto
iv) Kufiwa na familia yake katika moto, Mzee Kedi anafariki, hata nduguye Makaa anachomeka katika mkasa wa moto.
v) Kuitwa mfuata mvua akiwa shuleni kwa sababu ya kuwa mwanafunzi mlowezi katika eneo la msitu wa Heri
vi) Kutengwa mchezoni akiwa shuleni
vii) Kusimangwa na wanafunzi wenzake
viii) Kusingiziwa wizi wa kalamu
ix) Kubakwa kwa wapwake Lime na Mwanaheri wanapovamiwa na wahuni
x) Dadake Subira anavamiwa na wahuni na kukatwa kwa sime
xi) Kula mizizi-mwitu kwa kukosa chakula katika kambi ya wakimbizi
xii) Kuugua shinikizo la damu baada ya kupoteza aila yake. 7x2=14

Tanbihi: kuonja shubiri ni kukumbwa na dhiki.Mtahiniwa ajadili dhiki alizopitia Ridhaa maishani mwake.

**2. USHAIRI**

(a) Je, mashairi haya mawili ni ya aina gani.

A – huru – halijazingatia arudhi za utunzi wa ushairi.
B – tarbia – lina mishororo 4 katika kila ubeti.
- Kikwamba – neno 'dunia' laanzia kila mishororo.
- Mtiririko – vina vya kati na mwisho vina keketo.

- Mathnawi – kila mshororo una vipande viwili.
- Shairi la arudhi kwa sababu limezingatia arudhi za utunzi wa ushairi.
*Kutaja na kueleza.*(alama 2)

(b) Taja dhamira kuu katika kila shairi.

A - Kukashifu viongozi wanaouwatesa wafanyakazi.
- Kuangazia haki duni ya ufanyakazi mikononi mwa waajiri katili.

B - Kuangazia jinsi binadamu afaa kutahadhari na dunia inayo dhuru / angamiza. (Hoja 1x2 = 2) (c) Kulinganua mashairi haya kiumbo.

| A | B |
|---|---|
| (a) lina beti 4 | - lina beti 4 |
| (b) idadi ya mishoro kila ubeti ni tofauti | - kila ubeti una mishororo 4 |
| - vina vyatofautiana kwa kila ubeti | - vina vina keketo |
| - halina kibwagizo | - lina kibwagizo maalum |
| - mishororo haija gawika vipande vipande | - limegawika kuwili ukwapi na utao |
| - mizani yatofautiana kwa kila mshororo | - mizani ni sawa 8,8 |

*Tatu za kwanza – kila hoja lama 1 x 3 = 3*

(d) **Nafsinenewa katika mashairi haya mawili**.

A – Mwajiri katili anayewadhulumu wafanyakaziakijitajirisha kwa jasho lao.
B – binadamu asiyetahadhari na dunia. *Kila hoja alama 1 x 2*

(e) **Matumizi ya mbinu hizi za kimtindo katika shairi la A**.

(i) Kweli – kinzani - kilio kisichokuwa na machozi.
- barabara zisizokuwapo.

(ii) Mishata - utazame mlolongo wa
- watokwao na jasho kapakapa na - wanaotafunwa uhai na jua liso.
*Ya kwanza al. 1 x 2*

(f) Tabdila badala ya waichezee – kupata urari wa vina 'ye'

Kutaja na kueleza umuhimu – alama 1

(g)

| A | B |
|---|---|
| - Kazi inawala chenga | - dunia kama tapeli inahadaa |
| - Wanatafunwa uhai na jua | - dunia inampiku mwenye akili |
| | - dunia yapika majungu (alama 2) |

(h) Ubeti wa tatu katika shairi la A kwa lugha nathari.
Pia mchunguze maskini na mapato ya kazi yake duni, yasiyotosheleza mahitaji yake, na anayevalia nguo zilizochanika na zisizosetiri mwili usio na nguvu, na hulia bila kutokwa na machozi. (hoja zozte 4x1 = alama 4)

(i) Maana ya msamiati.

(i) Inampiku – inamshinda / inamweza
(ii) (ii) Makontena – shehena / mizigo mizito / makasha. (hoja 2x1 = alama 2)

**3. FASIHI SIMULIZI**

c) Mandhari ambapo pana watoto wachanga wanaocheza.
1x2=2
d) Fafanua mbinu ambazo utatumia kukusanyia data huku ukionyesha sababu za uteuzi wako.

(alama 18)

Kusikiliza-mtafiti anaweza kuwasikiliza Watoto wanapocheza na kusimulia visa vyao.
-Mtafiti atapata ujumbe asilia na halisi kwa sababu Watoto hawatatia chuku michezo yao
Kushiriki-mtafiti anaweza kujiunga na Watoto katika michezo yao na kujirekodia anachokibaini katika ushirika huo.
-mtafiti huja karibu na Watoto na kupata habari za kuaminika moja kwa moja.
Kurekodi-mtafiti anaweza kutumia vinasasauti, kanda za video, filamu au upigaji picha.
-mtafiti hupata habari za kutegemewa na anaweza kuzirejelea baadaye/kumbukumbu
Uchunzaji/kutazama-mtafiti anashuhudia kwa macho michezo ya Watoto inapoendelezwa.
-mbinu hii ni bora kwani utendaji hautaadhiriwa kwani wachezaji/washiriki hawatajua kuwa wanatazamwa.
Kutumia Hojaji-mtafiti anaweza kutayarisha hojaji ambayo ataipelekea mhojiwa ambaye anapaswa kuijaza.
-mbinu hii ni bora kwani mtafiti anaweza kuwafikia watoaji wengi wa habari kwa wakati mmoja.
Mahojiano-mtafiti anaweza kukabiliana ana kwa ana na waahusika anaonuia kupata maarifa kutoka kwao.
-mbinu hii inamwezesha mtafiti kupata ufafanuzi wa papo kwa hapo

**Zozote 6x3=18**

*Tan :Mtahini atoe mbinu, aifafanue kisha atoe sababu ilia pate alama 3 katika kila hoja.*

**ii)**

a) Ulumbi ni uhodari wa kutumia lugha kwa ufundi wa kipekee. 1x2=2
b) Sifa za mlumbi.
i. Hutumia lugha kwa njia inayovutia na kushawishi hadhira
ii. Mlumbi huwa jasiri- huwa mkakamavu.
iii. Hutumia chuku kwa ufanisi mkubwa.
iv. Anapaswa kutumia vipengele anuwai vya lugha kama vile ushairi, methali, nahau, taswira.
v. Hutumia lugha kutegemea muktadha na hadhira yake.
vi. Huwa na kipawa cha kuwa viongozi katika jamii. (,Zozote 4 x 2= 8)

c) Umuhimu wa Ngomezi.
i. Ni njia ya kupitisha ujumbe wa dharura katika jamii — vita.
ii. Ni kitambulisho cha jamii.
iii. Huhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii.
iv. Hukuza uzalendo – wanajamii huionea fahari mbinu hii ya kuwasiilana.
v. Hukuza ubunifu – jinsi wanajamii wanavyokabiliwa na aina tofautitofauti za ujumbe ndivyo wanavyojifunza mitindo mipya.
vi. Ni njia rahisi ya kuwasilisha ujumbe. 4x2=8
d) i. Toni katika rununu.

ii. Kamsa /milio kwenye magari/ving'ora ambulensi.
iii. Kengele shuleni
iv. Firimbi michezoni. (Zozote 2 x 1 = 2)

**4. KIGOGO**
a) -maneno ya Tunu
-akimwambia Sudi
-wakiwa barazani mwa nyumba ya Sudi
-wakizungumza kuhusu jinsi ya kuzitetea haki za wanasagamoyo
4x1=4
b- uwajibikaji-Tunu na Sudi wanawajibika kwa kujitolea katika kulinda haki za kimsingi za Wanasagamoyo na wanachukulia jambo hili kuwa jukumu lao
uzalendo-Tunu na Sudi ni wazalendo kwani wanataka kuiona Sagamoyo iliyo na ufanisi kwa wananchi wote.
2x2=4
e) Msemaji ni Tunu
i) Anaongoza maandamano Sagamoyo na kukiri kutolegeza msimamo wake hadi soko lifunguliwe
ii) Anapanga kuleta wachunguzi kutoka nje kuchunguza mauaji ya Jabali
iii) Anamkashifu Majoka kwa uongozi wake uliojaa mauaji
iv) Anahutubia wanahabari kuhusu hali halisi Sagamoyo kwa ujasiri
v) Anapigania usalama wa kila mtu Sagamoyo bila ubaguzi
vi) Anamsamehe Mamapima anapomwomba msamaha
vii) Anakataa kuolewa na mhuni Ngao Junior jambo linalomwezesha kuendeleza utetezi wa haki za wanasagamoyo.
Zozote 6x2=12
*Mwalimu akadirie majibu ya mwanafunzi yalingane na mafanikio ya Tunu.*
**ii)**
-Kwanza kuna migogoro kati ya wananchi na polisi. Polisi wanawapiga na kuwajeruhi wananchi wasio na hatia.
-Pili kuna migogoro kati ya polisi na viongozi wao. Viongozi wanawatisha polisi. Naye kingi mkuu wa wanapolisi anatishiwa kufutwa kazi.
-Kuna migogoro kati ya wananchi na viongozi wao.

Majoka anawatusi wancanchi waliojataa kuenda katika sherehe zilizoandaliwa katika

uwanja wa wazalendo.
-Kuna migogoro kati ya viongozi na vituo vya habari.
Majoka anafunga vituo vyote vya habari baada ya kupeperusha mbashara mgomo uliongozwa na tunu.
-Kuna migogoro kati ya viongozi na wapinzani wao.
Tunaona jinsi majoka anapinga kuvamiwa kwa tunu wakiwa na kenga.
Majoka pia anapanga mauaji ya jabali babake tunu.
-Kuna mgogoro unaozuka kati ya kiongozi na mshauri wake.
Kenga anapomgeuka majoka anaitwa kunguru.
- Migogoro ya kitabaka ambapo tabaka la juu linadhulumu watu wa tabaka la chini. Watu wa tabaka la juu wana maisha mazuri kama vile Majoka huku wa tabaka la chini wakimia kama akina Hashima. Jambo hili linaleta kutoelewana baina ya matabaka haya.
-Migogoro ya viongozi na wanachi. Viongozi wanaendeleza utawala wa kidhalimu, ni fisadi na hawajali raia jambo linalosababisha ktoelewana baina yao. Wanachi hata wanaanza harakati a kjikomboa mikononi mwao.
-Migogoro ya wanachi na askari. Askari na raia hawaelewani. Kila raia wanapogoma, askari wanafurusha na kuwatesa
-migogoro ya wafadhili na viongozi. Majoka hafurahishwi na wafadhili wanaosaidia akina Tunu na anawataka warudi kwao. Wafadhili hawa nao wanapinga utawala wa Majoka. 10x2=20
Migogoro ya viongozi na vyombo vya habari. Majoka anapendelea vituo vinavyoeneza propaganda na kupinga vinavyoelea ukweli wa mambo
migogoro baina ya watetezi wa haki na vibaraka. Akina Tunu na Sudi hawaelewani kabisa na vibaraka wa Majoka kama vile Ngurumo na Boza.

**5. HADITHI FUPI**
**i)**

a) Haya ni maneno ya Sasa
Akimwambia Mbura
Katika sherehe baada ya kula
Wanazungumzia ile hali ya matumbo yao kushiba ilhali wengine wanadhikika tu. 1x4=4

b) -Kula vibaya na vizuri-tunavyojua na tusivyovijua, hatujui vitokako na visikotoka
-magonjwa-sukari, presha,saratani,obesity, madonda ya tumbo
-vifo-kuuana kwa mabomu, risasi , kunyongana, kuuana kifikra, kimawazo, kunyang'anyana vinavyoonekana na visivyoonekana-haki, utu, heshima, uhuru
-lawama
3x2=6

c) i) Uwajibikaji
Beluwa anawajibika katika kazi yake anapomwagiza Sara kwenda hospitalini kupimwa akiwa na ujauzito wa miezi sita.

Sara anawajibika anapotunga mimba, ingawa alikuwa amebakwa, hakuavya mimba

ila aliamua kuilea.
Wazazi wa Sara wanapojua kuwa ana ujauzito, waliwajibika kwa mtunza vyema n ahata baada ya kujifungua wanamfanyia sherehe.
3x2=6

ii) Ukatili
Lile janadume bakaji lilikuwa na tabia ya kuwanajisi wasichana wadogo kama vile Sara
Sara alihofia kuwaeleza wazazi hali yake kwa kuhofia ukatili wa baba yake ambaye angemfurusha nyumbani iwapo angegundua ujauzito wa Sara.
Umati unampiga yule mbakaji kwa hasira hadi kifo 2x2=4

**ii)**

**TUMBO lisiloshiba**

(i) Viongozi kuweka vitego na vikwazo vya sheria ili watu wadogo wasiweze kutetea mali zao.
(ii) Kutowahusisha maskini katika maamuzi muhimu yanayoathiri maisha yao.
(iii) Kunyakua ardhi ya madongoporomoka ambapo watu maskini waliishi.
(iv) Kupanga njama za kuwapatia wanyonge visenti vichache ili waondoke madongoporomoka.
(v) Jitu la miraba mine kula chakula chote bila kubakishia wateja.
(vi) Wanamadongoporomoka kubomolewa vibanda vyao na mabuldoza.
(vii) Askari wa baraza kutimua watu waliokuwa wanabomolewa .
(viii) Jeshi la polisi kulinda askari wa baraza wakibomoa vibanda vya wanamadongoporomoka.
(ix) Askari kuwapiga virungu watu. 5x2=10

**SHIBE INATUMALIZA.**

(i) Mzee mambo kulipwa kwa vyeo viwili alivyovifanyia kazi.
(ii) Waajiriwa kwenda kazini na kukosa kufanya kazi.
(iii) Viongozi kuibia wananchi kwa kujipakulia mshahara
(iv) Waajiriwa wawili kufanya kazi moja – Sasa na Mbura ni mawaziri wa wizara moja.
(v) Mzee mambo kuandaa sherehe ya kuingiza watoto nasari kwa kutumia pesa za umma.
(vi) Mzee mambo kuandaa sherehe kwa kutumia rasimali za nchi- magari, vyakula.
(vii) Sasa na mbura kula vyakula vyao na vya wenzao. 5x2=10

# KABARAK HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

# Mwongozo wa Kusahihisha

1. Ni insha ya ilani:Majibu pia yanaweza kushirikisha tahadhari ya katibu kuhusu mambo ambayo yanaweza kuwatia ndani watu kwa mujibu wa sheria za baraza. Baadhi ya hoja ni
   1. Wakaazi hawaruhusiwi kufuga mifugo kama ng’ombe, mbuzi, kondoo, punda
   2. Kutolipa ada zinazotozwa na gatuzi
   3. Kufungua biashara pahala pasiporuhusiwa na bila leseni
   4. Uchafuzi wa mji kwa kutupa taka ovyo ovyo, kukojoa mitaani, maji taka.
   5. Ujenzi wa nyumba bila idhini ya wataalamu wa gatuzi
   6. Magari ya matatu kupitia katika maeneo yasiyoruhusiwa
   7. Biashara haramu
   8. Uuzaji wa bidhaa ghushi
   9. Kughushi Leseni

   **Matokeo ya Ukiukaji**
   Kufunguliwa mashtaka
   Kutozwa faini
   Kuny’ang’anywa leseni
   Magari kufungiwa kwa muda Fulani
   Muundo
   Anwani: Ilani kwa wakaazi wa mji……
   (Neno Ilani lazima lijitokezee) Tarehe
   Utangulizi: Atambue anayetoa Ilani
   Mwili: - Azungumzie maudhui na hatua zitakazochukuliwa.
   Uhimizo: ataje mtoaji wa ilani, na cheo chake

2. Jitihada za kumwinua mtoto wa kike zimepelekea kudhalilishwa kwa mtoto wa kiume. Jadili
   Hii ni insha ya mjadala
   1. Kimsingi insha hii ina sehemu mbili; mtoto wa kike na jinsi anainuliwa huku pia kukiwa na mtoto wa kiume na jinsi amedhalilishwa.
   2. Mtahiniwa aweza kuwa na hoja nyingi upande mmoja mradi kila upande uwe na angalau hoja tatu
   3. Mwisho yafaa mtahiniwa atoe msimamo wake kuhusu mjadala huu. Je yeye aunga upande gani?
   4. Amedhalilishwa kwa miaka na miaka
   5. Amedhalilishwa na utamaduni
   6. Anapigwa na waume na pia mabwana zao.
   7. Anafanyishwa kazi nyingi za nyumbani hususa za jikoni.
   8. Anaozwa mapema tena kwa wazee
   9. Anajisiwa, anabakwa, achafuliwa
   10. Anyimwa nafasi ya kupata elimu
   11. Anyimwa urithi wa wazaziwe na mumewe.
   12. Apashwa tohara ya lazima
   13. Arithiwa na shemejiwe mumewe aagapo

14. Apatapo mimba afukuzwa shuleni

**Jinsi mtoto wa kiume amedhalilishwa**

1. Miradi mingi na hela nyingi zimetengewa mtoto wa kike.
2. Mashirika mengi yamebuniwa kutetea mtoto wa kike na wanawake, mfano chama cha maendeleo ya wanawake.
3. Alama za wasichana kuingia vyuo vikuu zimeshushwa kiasi.
4. Shule za mabweni za wasichana nyingi ilhali mtoto wa kiume ameachwa kumezwa na magenge kama vile munguki na pombe haramu
5. Wakati jamii inamtetea mtoto wa kike ilhali mtoto wa kiume ameachwa ajiamulie hatima yake bila mtetezi wa moja kwa moja.

3. Mwanafunzi aandike insha ilete ukweli wa methali.
Mkasa uliosababishwa na maneno yaliyosemwa na mtu.

4. Mtahiniwa atumie nafsi ya kwanza.
Adhihirishe hali aliyojiingiza. (Lazima iwe mbaya. Aonyeshe jinsi alivyojuta.
(insha ina pande mbili)

# KABARAK HIGH SCHOOL

## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019

## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

## Mwongozo wa Kusahihisha

**SEHEMU A: UFAHAMU (Alama 15)**

1. Ajali hutokea bila kutarajia (ala. 2)
2. Hutokana na ajali wasiofikiria watu wengi kama vile kuteleza msalani.
Aidha wengine huteleza walipokanyaga vitu vyenye unyevu sakafuni.

Watu wazima na watotohulemazwa na ajali hizi.
(ala. 3)

3. (i) Watu wanapozama katika shughuli au kupata jazba ya kutenda kazi
(ii) Kuubeba mzigo wenye uzani usiokadiriwa.
(iii) Ukiwa umepanda juu ya kibao kuangika picha ukutani
(iv) Ajali kutokana na vifaa vya nyumbani k.v. visu, meko ya gasi, mashine zinazotumia umeme n.k.
(ala. 3)

4. (i) kukuza tabia na mazoea ya kuwa waangalifu nyumbani
(ii) Ni vizuri kupata ujuzi wa jinsi ya kutumia vifaa na kuhakikisha tunavirusha ipasavyo
(iii) Kuwepo kwa vifaa pamoja na uwezo wa kutoa huduma ya kwanza.

5. (i) Jazba - Msisimko/ msukumo / hamu kuu
(ii) Makasri - Majumba ya kifahari
(iii) Makovu - Alama / mabaki yatokayo na majeraha
(iv) Kuepua - Kutoa kitu mekoni

**SEHEMU B: MWONGOZO WA UFUPISHO**

a) Ujumbe wa aya 3 za kwanza:
- ✓ Ardhi ni mali ya taifa na inarithishwa vizazi
- ✓ Ndiyo chanzo cha riziki nan i dafina kubwa
- ✓ Awali ilifunikwa na miti na matawi
- ✓ Ilikuwa na rotuba
- ✓ Binadamu waliharibu mazingira kwa kufyeka
- ✓ Hili liliwaletea mavuno hafifu
- ✓ Matone ya mvua yalitawanya chembe za udongo
- ✓ Upepo ukachukua tabaka la juu la ardhi
- ✓ Hili likapoteza udongo wa rutuba
- ✓ Mazao hayakustawi
- ✓ Matokeo yakawa mmonyoko na maporomoko ya ardhi

(Hoja 8 x 1) (+ 1 ya mtiririko)

b) Masuala ya aya 2 za mwisho:
- ✓ Serikali inahimiza wakulima kupanda zaidi
- ✓ Watumie maarifa bora ya zaraa. Mfano: kunadhifu udongo, kutumia mbolea na kadhalika.
- ✓ Wasio wakulima serikali imefungua shule za mafundisho maalum ili waongeze maarifa na bidii kazini.
- ✓ Kule maelezo ya serikali yalikofuatwa barabara, kumekuwa na maongezeko ya mazao.
- ✓ Walakini kuna watu wanaopotosha wengine kuwa waasi amri za serikali kuhusu zaraa

(Hoja 5 x 1 + 1 ya mtiririko)

**SEHEMU C: MATUMIZI YA LUGHA**

(a) (i) /r/
(ala. 1)
(ii) /l/

(b) IKKI – Imba / imla
(ala. 1)
(c) Ya – Ik - a - yo
Ngeli kauli kiishio "o"rejeshi
(ala. 2)
(d) Taarifa - mama amefika
Amri - fungeni mlango! Mbili, moja au
Ombi - Tafadhali nisamehe sufuri
Swali - unatoka wapi! Lazima atoe mfano ili
Mshangao - Salaale! Umeiba apate alama 2 / 0
(ala. 2)
(e) Kijinga - namna mfanano
(ala. 2)
Haraka haraka - namna kikariri
(f) (i) Kijana aliyemzungumza na nyanyake - Kishazi tegemezi
(ii) Ameingia katika darasa lililochafuliwa na wanafunzi - Hura
(iii) Lililochafuliwa na wanafunzi Lazima atambue – Kishazi tegemezi cha kwanza ilia pate Alama
(ala. 2)
(g) S $^1/_2$ $\rightarrow$ KN $^1/_2$ (N + V + E + S) 1 + KT $^1/_2$ (T + E) $^1/_2$
(ala. 3)

(h) Mti - kipozi
Kisu - ala
Chagizo - jana asubuhi
(ala. 3)
(i) Karani alimwita Karanja ili amtume kwababu yake lakini alimwambia hakutaka kupita njia hiyo ya kwa babu yake (ala. 3)

(j) Ingieni - wingi
Darasani - mahali ndani
Niwape - nafsi
Ni - kitenzi kishirikishi kipungufu (ala. 2)
(k) (i) Ningalisoma kwa bidii ningalipita mtihani – hakuna ewezekano
(ii) Ningesoma kwa bidii ningepita mtihani - kuna uwezekano (ala. 2)
(l) Vijiti vya msonobali hutengeneza vijimeza vizuri (ala. 2)
(m) JI – MA kwa mfano Jicho - macho
JI – ME jiko - meko
Q - MA gari - magari
(ala. 3)
Zingi lazima atoe mfano.
(n) (i) Ataenda kwa mtu mwingine
(ii) Yeye ataenda labda alikozaliwa (ala. 3)
(iii) Nafsi ya tatu ('a')
(o) Mwanafunzi asoma / yuasoma darasani (ala. 1)
(p) (i) Nilitembea hadi sokoni - mahali
(ii) Nilifunza hadi jioni - wakati (ala. 2)
(q) Auguaye huhitaji daktari (ala. 2)
(r) Kivumishi - Mkomavu

Nomino - Ukomavu (ala. 2)

(s) (i) Kutoa maelezo ya ziada
(ii) Kuonyesha mabadiliko ya ghafla
(iii) Kuonyesha nani aliyesema maneno Fulani (ala. 2)

**SEHEMU D: ISIMUJAMII**

(a) (i) Tatizo la mawasiliano kutokana na wingi wa lahaja
(ii) Haja ya kuwepo kwa lugha moja ya mawasiliano
(iii) Haja ya kusawazisha maandishi ya kitaalamu
(iv) Kurahisisha shughuli za kidini
(v) Haja ya kuwepo kwa lugha moja inayofahamika na kila anayekifahamu Kiswahili
(vi) Haja ya kuondoa tofauti katika namna ya kuendeleza maneno kwa sababu hati tofauti zilifumiwa kuandikwa Kiswahili

(b) (i) Uzingatia ukweli wa mambo bila porojo au uzushi
(ii) Istilahi za taaluma husika hutumika; kila taaluma ina istilahi zake.
(iii) Lugha ya heshima / adabu
(iv) Lugha rasmi hutumika
(v) Lugha kavu
(vi) Lugha yenye mantiki – mtiririko unaofaa
(vii) Huelezea mambo bila mapendeleo au kuonyesha hisia za mzungumzaji

# KABARAK HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHA**

1. (a) Eleza muktadha wa dondoo hili
(ala. 4)
Msemaji - mawazo yake Dennis
Alikuwa anarejerea Shakila

Mahali - Katika afisi ya Shirika la kuchapisha magazeti
Tukio - Ni baada ya kumwona mamake Shakila (pandikizi la mama) akipita huku akisubiri kufanya mahojiano.

(b) Fafanua mbinu za lugha zilizotumiwa katika dondoo hili
(alama 6)
Chuku - Akanyagapo chini, ardhi inatetemeka.
Taswira - picha ya ardhi ikitetemeka
Msemo/ Nahau - kujitia hamnazo

Za kwanza 3 x 2 = 6
Kutaja - 1
Maelezo - 1

(c) Eleza madhila kumi yaliyompata Kabwela (alama 10)
- (i) Anakosa kazi katika shirika la magazeti
- (ai) Kuachwa na Penina
- (bi) Kukejeliwa na Daktari Mabonga
- (iv) Hapewi pesa za masurufu na wazazi
- (v) Kushindwa kujibu maswali wakati wa mahojiano – anaaibika
- (vi) Njaa – Anaamua kupika uji
- (vii) Hana nguo za kisasa/ simu/tarakilishi n.k.
- (viii) Anasumbuka kiakili kwa sababu ya hali /asili/umaskini
- (ix) Kufukuzwa na Penina
- (x) Shuka zake zimechanika

**SEHEMU B: CHOZI LA HERI**

2. "……………. Wanahofia kusema wasije wakavikata viganja vinanyowalisha …………….."

(a) Eleza Muktadha wa dondoo hili (alama 4)

Msemaji: Mwaliko
Msemwa: Mwangemi
Mahali: katika hoteli ya Majaliwa ambapo wote wawili walikuwa wameenda

Tukio: Wanaongea kuhusu ndugu zake Mwaliko, Umulkheri na Dickson, waliokuwa wametoroshwa na Auntie Sauna. Mwangemi anampa Mwaliko matumaini kuwa wako hai na bila shaka wangekutana. Mwaliko anashuku kukutana kwake na ndugu zake kwa kuwa polisi hawakuwajibika ipasavyo kuwafuata kutokana na kuhongwa na walaguzi wa watoto.

(b) Taja maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili.

Maudhui ya ufisadi

(c) Kwa kutumia hoja kumi, eleza namna maudhui uliyotaja hapo juu (1b) yanajitokeza riwayani (alama 10)
- (i) Viongozi wanawanunua raia ili wawapigie kura
- (ai) Hazima ya jitegemee inayotarajiwa kuwapa vijana mtaji wa kuanzisha biashara inaandamwa na ukabila na unasaba.
- (bi) Viongozi wananyakua maelfu ya maelfu ya ekari na kujenga viwanda na maduka ya bishara.
- (iv) Katika ukurasa wa 57 watu walilaghaiwa na kuuziwa shamba la wenyewe kwa njia za kifisadi
- (v) Majumba ya Ridhaa yalibomolewa kwa kisingizio kuwa yalinjengwa katika eneo lililotengewa ujenzi wa barabara mbadala. Barabara haikujengwa na shamba la Ridhaa kunyakuliwa.
- (vi) Katika uk 41 tunapata kuwa kuna tume za kupigana na ufisadi ambazo zinaundwaa, na jambo hili ni ishara kuwa kuna ufisadi unaoendelezwa.
- (vii) Pia katika uk 13, "Uchukuzi wa milungula pia ni aina ya ufisadi katika

serikali" "Wengine walionekana wakitoa milungula hadharani, wengine wakatishia kuishtaki, uizara husika kwa kile walichokiita ukiukaji wa haki za umiliki mali"

(viii) Wasimamizi wa hospitali wananyakua dawa na kuziuza kwenye maduka yao

(ix) Uongozi haumpi Shamsi kazi baada ya kuhitimu. Unamtaka atoe hongo.

(x) Bwana mabavu ananyakua shamba la kina Shamsi kiasili na kuwageuza vibarua kwenye shamba lao.

(xi) Familia ya bwana Kute inafisidi chakula cha msaada kwa kujigawa mara tatu kupata mara tatu zaidi ya posho waliyopata wengine.

(xii) Baada ya kutangazia raia kuwa msitu wa mamba ni marufuku, viongozi wanaendeleza ukataji wa miti na uchomaji wa makaa usiku.

(xiii) Baadhi ya viongozi wananyakua hata madhabahu kwenye mlima wa nasibu ili kujenga hoteli kubwa za kitalii

(xiv) Halmashauri ya elimu inawasaliti wanafunzi wanaotoka katika familia maskini kwa kuwapa mikopo wanafunzi kutoka familia zinazojiweza na kuwacha wanafunzi maskini wajifanyie vibarua ili kujilipia karo.

(d) Eleza sifa nne za mzungumzi (alama 4)

(i) Msomi - anasoma hadi chuo kikuu na kuhitimu kwa shahada ya isimu na lugha

(ai) Mdadisi - Anamuuliza Mwangemi kama anadhani kuwa ndugu zake Dick (Dickson) na Umulkheri (Umu) wako hai

(iii) Mwenye haya - Anacheka kwa haya Neema anapomuuliza kama alikuwa anataka kuwaletea mkaza mwana.

(iv) Mwenye Kumbukumbu - Anakumbuka kuwa dada yake Umulkheri (Umu) alimwambia kuwa mamke alimwacha akiwa na umri wa miaka mitano

(v) Mwenye shukrani - Anawashukuru wazazi wake Mwangemi na Neema ambao walijisabilia kumwelimisha licha ya kuwa hakuwa mwanao halisi.

(vi) Mwenye bidii - Anafanya kazi yake kwa bidii ya mchwa katika kampuni ya magazeti ya Tabora kama mhariri katika kitengo cha biashara. Tunaelezwa kuwa Mwaliko anaifanya kazi yake kwa bidii ya Mchwa.

(vii) Mwenye mapenzi ya dhati - Anawapenda wazazi wake, Mwangemi na Neema kwa dhati. Anamwambia Neema "Nitakwenda nawe mama"

**3. (a) Migogoro katika Chozi la Heri**

Migogoro ni hali ya kuwepo kwa mivutano/mikinzano/mfarakano baina ya wahusika katika kazi ya fasihi. K.m.

1. Mgogoro kati ya Mzee Kedi na familia ya Ridhaa wakati mzee Kedi anashiriki katika mauaji ya familia ya Ridhaa.

2. Mgogoro shuleni kati ya Ridhaa na wanafunzi wenzake wanapomwita "mfuata mvua"
3. Mgogoro wa kijnsia kati ya Mwekevu na Mgombea wa kiume. Mwekevu anarushiwa cheche za matumizi.
4. Mgogoro wa kijamii unajitokeza baada ya mkoloni kupuuza sera za mwafrika za umiliki wa ardhi.
5. Mgogoro katika familia yam zee Mwimo Msubili kwa sababu familia yake ilikuwa kubwa na hangeitosheleza kwa chakula.
6. Mgonjwa mmoja kwenye hospitali ya mwanzo mpya anapata majeraha mabaya baada ya kuvamiwa kwenye mzozo wa ardhi kule Tamuchungu.
7. Panatokea mgogoro kati ya baba na mama Pete. (uk 147)
8. Ridhaa anajipata katika hali ya mgogoro wa nafsi. (uk. 12) ……… baada ya muda wa mvutano wa hisis na mawazo.
9. Mgogoro wa kisiasa kuhusu ni nani atakayekuwa kiongozi wa jamii kati ya mwanamme na mwanamke (uk. 19)
10. Mgogoro kati ya raia na polisi wakiwa katika harakati za kudumisha amani (uk. 19)
11. Nyamvula anajikuta katika mgogoro wa nafsi yake wakati ambapo imani yake inakinzana na kazi ya mmewe ya kuwa mwanajeshi (uk.62)

(10 x 1= 10)

**(b) Uozo katika Chozi la Heri**

1. Kuvunjika kwa ndoa/ kuwacha waume k.m. Naomi, Subira.
2. Mapenzi kati ya baba mlezi na bintiye Sauna alipopachikwa mimba na babake.
3. Wanawake kuavya mimba. Mamake Sauna anamsaidia mwanawe kuavya mimba.
4. Wizi/uporaji wa mali. Nyumba na maduka yaliporwa wakati wa vita vya baada ya kutawazewa kwa kiongozi mpya.
5. Ukatili. Mabarobaro wanawavamia watu na kuwafanya unyama …. Uk 25 alikula mikato miwili ya sime akazirai kwa uchungu.
6. Uendelezaji wa biashara haramu km. ulanguzi wa watoto
7. Ubakaji. Lime na Mwanaheri walibakwa babayao akitazama
8. Ulanguzi wa dawa za kulevya. Dick anafanya kazi ya kusafirisha dawa za kulevya
9. Kutupwa kwa watoto wachanga, km. kitoto Nasibu
10. Matumizi ya pombe haramu - vijana wa vyuo vikuu wanabugia pombe na kufanya wengine kuaga dunia
11. Ukeketaji wa watoto wa kike
12. Mauaji. Watu kupigwa risasi na kuuawa kam kuku
13. Ndoa za mapema – Pete aliolewa akiwa mdogo.
14. Ukosefu wa malezi bora- Naomi na Subira kuwaacha watoto wao.
15. Ufisadi – watu kunyakua sehemu zilizotengewa ujenzi wa barabara.
16. Ubaguzi wa kikabila

(10 x 1 = 10)

**SEHEMU C: KIGOGO**

4. "Na mwamba ngoma huvuta wapi?

**(a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama 4)**

(i) Msemajio ni Kenga
(ii) Msemewa ni Majoka
(iii) Wako katika ofisi ya Majoka
(iv) Ni baada ya Majoka kumwelezea kuhusu habari gazetini kuhus umaarufu wa Tunu

(1 x 4 = 4)

**(b) Tambua tamathali mbili za semi zilizotumika katika muktadha huu (alama 2)**

(i) Methali – mwamba ngoma huvuta……
(ai) Swala la balagha - huvuta wapi?

(1 x 2 = 2)

**(c) Fafanua sifa sita za msemewa wa maneno haya**

Msemewa ni Majoka

(i) Ni katili – alishiriki katika mauaji ya Jabali
(ii) Ni mkware - Alikuwa amemuoa Husda lakini alitaka kujihusisha kimapenzi na Ashua
(iii) Ni mpyaro – aliwatukana wanasagamoyo wajinga
(iv) Ni fisadi – alinyakua mali ya uma kam vile soko la chapakazi
(v) Ni msaliti – Aliwasliti wanasagamoyo kwa kuwa walimchagua ilhali anajinufaisha yeye, pia anamsaliti Husda kimapenzi.
(vi) Ni mwenye dharau
(vii) Ni laghai
(viii) Ni dikteta
(ix) Ni mwoga (1 x 6 = 6)

**(d) Thibitisha ukweli kuwa kila mwamba ngoma huvuta kwake ukirejelea Tamthilia nzima ya Kigogo (alama 8)**

(i) Kenga anamfuata Majoka na uongozi dhalimu kwani ananufaika nao. Mfano ardhi
(ii) Ngurumo anaunga mkono uongozi thalimu wa Majoka ili aendelee kunufaika. Mfano pombe.
(iii) Mama pima anautetea uongozi wa Majoka kwa kuwa ananufaika nao, mfano. Kandarasi ya kuoka keki, kibali cha kuuza pombe haramu
(iv) Majoka ana ari ya kuwafurusha wafanyabiashara kutoka sokoni ili alinyakue kwa matumizi yake kibinafsi ya kujenga hoteli ya kifahari.
(v) Wafadhili wa kina Tunu wanatia habari chumvi kuhusu umaarufu wa Tunu.
(vi) Wanapolisi wanayafuata maagizo ya Majoka ya kuwashambulia wanasagamoyo ili walinde kazi yao.
(vii) Chopi anatekeleza uhuni wa Majoka ndiposa asije akamwaga unga wake. (Kufutwa kazi)
(viii) Husda anaolewa na Majoka kwa sababu ya utajiri wa Majoka.
(ix) Boza anajipendekeza kwa kenga ili apewe mradi wa kuchonga kinyago. Pia anasema mke wake ndiye aliyeioka keki

(8 x 1 = 8)

**5. KIGOGO**

Sumu ya nyoka husababisha madhara mengi kwa mhusika/ kiwemo kuua. Kuna mambo mengi yanayodhuru au kuwaua wananchi katika utawala wa

Majoka.

(i) Unyakuzi wa ardhi - majoka na mshairi wajifurahia eneo la soko la chapakazi ili ajenge hoteli iya kifahari
(ii) Kuamrisha askari kutawanya waandamanaji na kuasababisha kifo cha vijana watatu
(iii) Vitisho – wanaharakati wanaopinga utawala wa Majoka wanatishwa. Kuna vikaratasi vinavyorushwa katika makazi yao ili wahame (siti anamweleza mamake Tunu)
(iv) Kuangamiza wapinzani wake – Jabali aliuawa kwa njama za Majoka na chama chake bila kikasambarakati
(v) Ukosefu wa utu. Majoka hathamani utu/uhai wa mtu. Majoka anaamrisha watu wapigwe risasi bila kujali.
(vi) Tengatawala – uhasama unapandwa na viongozi ili kuwagaza wananchi mf. Sudi ana uhasama na Boza sababu wako katika mirengo tofauti ya kisiasa.
(vii) Kuzorota kwa maendeleo. Jimbo la Sagamoyo limetimiza miaka sitini ya uhuru lakini bado liko nyuma kimaendeleo.
(viii) Rushwa - Mamapima anatoa hongo ya uroda kwa Ngurumo ilia pate mradi wa kuoka keki ya uhuru.
(ix) Elimu mbovu – elimu inayotolewa katika shule za kifahari inawalemeza vijana badala ya kuwandaa wawe wazalendo Majoka and majoka academy.
(x) Utawala wa kiimla – majoka anataka aendelee kutawala ingawa urubani umemshinda na amekwisha zorotesha nchi.

(xi) Matabaka – Sumu ya nyoka iliyozagaa katika jimbo la Sagamoyo imesababisha kuwapo kwa matabaka. Mambwenyenye – majoka, Kenga - maskini - wananchi
(xii) Uvivu na ubwete – Majoka ni kiongozi ambaye hajali umuhimu wa kazi. Anatenga mwezi mmoja ya kupumzika katika kuadhimisha miaka 60 ya uhuru.
(xiii) Ukimtamba – Majoka ana rasilimali nyingi na miradi mingi mikubwa. Anamiliki Majoka and Majoka Company, Majoka and Majoka modern resort
(xiv) Ukoloni mamboleo. Jimbo la sagamoyo linaongozwa kwa mikono amabayo halipwa kwa muda mrefu. Halipwa kwa vizazi vya sasa na hata vyavyo
(xv) Ufujaji wa fedha za umma. "mikopo iliyochukuliwa haikutumika vizuri. Kenga anamweleza Sudi kuwa akikubali kuchonga kinyago cha marara bin Ngao angepata fedha za kubadilisha maisha yake.
(xvi) Kuwafunga raia bila sababu – mf. Ashua kutiwa mbarani ili iwe funzo kwa Sudi
(xvii) Kupanga njama ya kumwua Tunu.
(xviii) Kufunga soko la chapakazi ambayo ni tegemeo kwa raia wa sokomoko
(xix) Majoka anamwambia Kenga lazima chatu mmoja atolewe kafara (auawe)

(xx) Anapanga kutumia mamlaka kuzima uchunguzi wa Tunu kuhusu kifo

cha jabali

(xxi) Anafuja pesa za kusafisha soko la chapakazi

(xxii) Anatumia mamlaka yake kudhibiti vyombo vya habari

**SEHEMU YA D: USHAIRI**

**SHAIRI LA A**

1. **Eleza ujumbe wa mwandishi katika ubeti wa nne (alama 2)**
   Hatari ya wingu na umuhimu wa kujikinga
   Anasema tangazo haliwapiti, wahimizwa kujikinga na hatari (2 x 1 = 2)
2. **Onyesha ufundi wa kimuundo wa mwandishi katika utunzi wa shairi hili (alama 4)**
   i. Ametumia beti sita
   ii. Kila ubeti una mishororo mitatu
   iii. Vina vimepangwa kwa mtindo wa ukaraguni
   iv. Idadi ya vipande katika kila mshororo ni viwili
   v. Idadi ya mizani inatofautiana katika mishororo (4 x 1 = 4)
3. **Eleza namna jazanda imetumika katika utungo huu (alama 2)**
   i. Wingu - ni hatari iliyopo
   ii. Vungu - ni mikakati ya kujikinga kutokana na hatari yenyewe (2 x 1 = 2)
4. **Kwa kuzingztia idadi ya mishororo katika beti tambua aina ya ushairi huu (alama 1)**
   Tamthlitha – kila ubeti una mishororo mitatu (1 x 1 = 1)
5. **Tamthini ustadi wa mshairi katika matumizi ya idhini ya kishairi (alama 3)**
   i. Inkisari – yalo – yaliyo
   ii. Lahaja – wananti – wananchi
   iii. Tabdila – tafakali – tafakari (3 x 1 = 3)
6. **Litie shairi hili katika bahari tatu tofauti (alama 3)**
   i. Mathnawi – jina vipande viwili katika kila mshororo
   ii. Ukaraguni – vina vyake vinafanana kulingana na beti. Vinabadilika kutegemea ubeti
   iii. Tathlitha – lina mishororo mitatu kila ubeti (3 x 1= 4)
7. **Andika ubeti wane kwa lugha ya kwaida / tutumbi (alama 4)**
   Hampitwi na tangazo linalowahimiza mjikinge na hatari hii kwani ukiichezea kwa vile ina nguvu za kukuvuta na kukuua.
8. **Eleza sifa mmoja ya nafsi neni katika shairi hili (alama 1)**
   Mshawishi/ mwelekezi mwema
   Daima mwape kujiseti, mjitunze kujijari
   Vumilia kwalo vungu, nje kuna dhoruba

**SHAIRI LA B**

a) Maendeleo ya umma (1 x 1 = 1)

b) Ni shairi huru - halina mpangilio wa vina

Mahususi
Idadi ya mizani inabadilika
Mishororo haitoshani (aina alama 1)
(sabau alama1)

c) Kuonyesha ni mambo gani muhimu katika maendeleo ya umma kama vile kuheshimiana usawa na kumiliki vitu (alama 3)
d) Urudiaji wa maneno } Kusisitiza
Urudiaji muundo – mstari wa kwanza
Urudiaji wa silabi - Urari wa vina (3 x 2 = 6)
e) Jazanda tama ya fisi
Istiari - dola – shilingi (2 x 2 = 4)
f) Masikitiko – baada ya kuondoka mkoloni walidhani hali ingeimarika kutaja al. 1
Sababu al. 1
g) Ni msimulizi (1 x 1 = 1)

h) Vitu kubaki gulioni – kuviona madukani wanaoweza kununua ni matajiri pekee (ala. 1)
Msimulizi anarejelea maskini asiyejiweza kiuchumi na hawezi kumudu bei ya bidhaa madukani

**<u>SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI</u>**

8. **a) Sifa**
   1. Hutolewa na wazee maarufu walioteuliwa.
   2. Hufanywa mahali maalum k.v. pangoni, mwituni n.k.
   3. Huandamana na sala
   4. Huandamana na utoaji kafara k.v. kuchinja mbuzi, n.k
   5. Huandamana na maombi (Hoja 5 x 1 = 5)

**b) Tofauti**

| Maigizo yakawaida | Sanaa yamaonyesho |
|---|---|
| ✓ Mazingira ya kuzua/maalum | ✓ Hutumia mazingira halisi |
| ✓ Matukio ya kuiga | ✓ Matumio halisi/ ya kila siku |
| ✓ Huwa na wahusika na hadhira maalum | ✓ Washiriki na waigizaji walio pia hadhira |
| ✓ Matumizi ya ukumbi na jukwaa maalum | ✓ Hakuna haja ya ukumbi wala jukwaa |
| ✓ Hutumia maleba na vifaa vya kuzua mazingira maalum | ✓ Hakuna vifaa maalum bali huwa mazingira yenyewe |
| ✓ Hugawika katika maonyesho kutumia lugha kwa njia maalum | ✓ Muundo wake hufululuza au hayajagawika katika maonyesho |

| | |
|---|---|
| ✓ Wahusika hufanya mazoezi kabla ya igizo halisi | ✓ Hawahitaji kufanya mazoezi kwa nini matukio ya kila siku |
| ✓ Huwa na malipo | ✓ Hamna malipo |

(Hoja 5 x 2 = 10)

c) Miktadha ambamo ulumbi hutumika katika jamii
  i. Katika mijidala bungeni
  ii. Katika hotuba za kisiasa
  iii. Katika mahubiri maabadini
  iv. Katika mijadala shuleni
  v. Kortini
  vi. Katika shughuli za kijamii k.v. posa
  vii. Katika sala / dua
  viii. Katika maapizo
  ix. Katika malumbano ya utani
  x. Katika majigambo/ vivugo

d) (i) Miviga ni ibada au sherehe za kitamanduni ambazo kwa kawaida ufanywa kipindi Fulani cha mwaka. Sherehe hizi utaratibu wa sanaa za kimaonyesho.
Maapizo ni kauli za kuomba Mungu, miungu au mizimu kumwadhibu mtu Fulani au watu katika jamii kutokana na matendo yao maovu. (2 x 1 = 2)
(ii) Ngoma ni unenguaji wa viungo vya mwili kuambatana na midundo maalum ya ala za muziki au mahadha ya muziki wenyewe.
Ngomezi ni maigizo ya sanaa ya kuwasilisha ujumbe kwa kutumia ngoma

(2 x 1 = 2)

# ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)
## Mwongozo wa Kusahihisha

**1.Hii ni insha ya hotuba**

Muundo wa hotuba ufuatwe

(a) Kichwa – Kiandikwe kwa herufi kubwa na kipigiwe mstari

Kianzie kwa neno Hotuba….

(b) Utangulizi uwepo

(c) Mwili – Wenye hoja zinazofuatana kimantiki

(d) Hitimisho

Maudhui ya kuzingatiwa

**(a) <u>Madhara ya ufisadi</u>**

(i) Pesa za miradi mbalimbali ya maendeleo kubadhiriwa.

(ii) Wafadhili kukataa kuipa nchi mikopo na pesa za maendeleo.

(iii) Kiwango duni cha miradi inayotekelezwa

(iv) Kuwepo kwa wafanyikazi wasiohitimu kazini

(v) Uchumi wa nchi kudorora

(vi) Huduma muhimu kukosekana kwa wananchi

(vii) Migomo ya mara kwa mara

(viii) Baadhi ya maeneo ya nchi kutengwa kimaendeleo

(ix) Hatimiliki bandia kuwepo kwa wingi

(x) Kuzuka kwa biashara haramu

**(b) <u>Njia za kupambana na ufisadi</u>**

(i) Kuwaelimisha raia kuhusu madhara ya ufisadi

(ii) Jamii kuwajibika katika vita vya kupambana na ufisadi

(iii) Kuwepo kwa sheria kali ambazo zitawafunga wafisadi

(iv) Wafanyakazi wa serikali kutangaza mali wanayomiliki

(v) Kulipwa mishara bora kwa wafanyakazi ili wasiwe fisadi

(vi) Dini kufunza waumini maadili

(vii) Mali ya watu fisadi itwaliwe na serikali

(viii) Kampeni dhidi ya ufisadi kupamba moto.

(ix) Pesa za umma zikusanywe kwa njia ya kiteknolojia.

**2. Nafasi ya nyimbo za kitamanduni katika ufanisi wa jamii**

(i) Zilitumika kukuza vipawa vya uimbaji
(ii) Kuboresha umoja na ushirikiano katika jamii
(iii) Kama njia ya kuburudisha wanajamii
(iv) Kuwaepusha vijana katika fikra za kutenda maovu
(v) Zilitumika kufunza maadili katika jamii
(vi) Zilitumika kama kigezo cha kukuza lugha
(vii) Zilitumika kukashifu matendo hasi katika jamii
(viii) Katika sherehe hizi vijana waliweza kupata wachumba
(ix) Zilitumika kuendeleza na kufunza mila na tamaduni za jamii husika.

**3. Bahati ni chudi**

Chudi ni bidii

Maana ya methali hii ni kuwa ili kufanikiwa katika jambo Fulani ni sharti mtu afanyie jambo hilo bidii kubwa.

Methali hii hutumiwa kuwahimiza watu wazidishe bidii kazini mwao ili waweze kufanikiwa.

(i) Kisa lazima kioane na maana ya methali hii
(ii) Pande zote mbili za methali zidhihirike.

4. Msimulizi ajipate katika hali ambapo yuko kivyake. Kwa mfano amepotoka na baadaye anagundua wenzake hawajapotoka au anafanya bidii peke yake na wengine wanalaza damu.

Au anaunga au kupinga jambo fulani pekee na alidhani wako pamoja na wenzake.

Tan: Mtahini atumie nafsi ya kwanza

# ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha
## Mwongozo wa Kusahihisha

**SEHEMU A: UFAHAMU (Alama 15)**

**1.Kipe kifungu hiki anwani mwafaka (alama 1)**

Kutuza muda/wakati/ kuchelewa

**2.Taja watu walio na mazoea ya kuchelewa katika shughuli walizoalikwa (alama 3)**

(i) Waumini katika ibada
(ii) Waombolezaji kwa mazishi
(iii) Wanaohudhuria harusi na maharusi
(iv) Wateja wa benki
(v) Wanaohojiwa kwa kutafuta kazi
(vi) Wageni mashuhuri katika mikutano

6 x ½ = 3

**3. Taja sababu zinazofanya watu kushindwa kutimiza miadi (alama 4)**

(i) Uzembe
(ii) Kutowajibika /mapuuza / kisingizio
(iii) Kutojiandaa kwa ipasavyo / kutopanga
(iv) Kutekeleza mambo mengi kwa pamoja
(v) Kuharibika kwa vyombo vya usafiri
(vi) Kiburi 4 x 1 = 4

**4. Taja na ueleze njia nne zinazoweza kuondoa tatizo la kuchelewa (alama 4)**

(i) Kujitayarisha /kujiandaa mapema / mf. Kupanga mwenendo wa barabara
(ii) Kuwajibika katika kuzingatia wakati/ratiba
(iii) Kuweka sera za kuwaelimisha watu kuhusu umuhimu wa kuzingatia saa
(iv) Kuweka kanuni za kuwafungia nje wanaochelewa
(v) Wananchi wazinduliwe kuwa wana haki ya kufumukana muda wa shughuli unapokwisha

**5.Eleza maana ya maneno haya kama yalivyotumiwa katika taarifa (alama 3)**

(a) Ujima – Ushirikiano
(b) Miadi – ahadi ya kukutana kwa sababu maalum
(c) Pancha – mpasuko kwa gurudumu

**<u>SEHEMU B: UFUPISHO (Alama 15)</u>**

(a) Kila siku vyombo vya habari hueleza kuhusu mateso ya watoto
- Kuna vingine ambavyo havijaripotiwa
- Watoto huuawa na wavamizi vitani
- Kuna wazazi wanaowapiga watoto kinyama
- Kuwachoma
- Kuachwa bila chakula

(b) Kenya ni mojawapo ya nchi zilizotia sahihi mkataba wa kulinda haki za watoto
- Ina idara katika ofisi ya makamu wa rais inayoshughulikia maslahi ya watoto
- Serikali ilianzisha kampeni kabambe za kukomesha mateso dhidi ya watoto
- Watu wengi na hata watoto wenyewe hawajui haki zao
- Sheria ya watoto ilipitishwa ili kutetea haki za watoto katika nchi ya Kenya

- Watoto wanafaa kulindwa kutokana na ubaguzi/ kutunzwa na wazazi na kupewa elimu ya kiakademia na dini / kulindwa kiafya / kuheshimiwa katika jamii.
- Watoto wasinyanyaswe kiuchumi
- Watoto wenyewe wanapaswa kuwasaidia wazazi wao inapostahili.
- Watoto wanafaa kudumisha umoja wa jamii na kuendeleza maadili katika jamii

(alama 8 + 1 ya mtiririko)

**Adhabu**

- Adhibu kosa la sarufi litokeapo kwa mara ya kwanza hadi 6 x ½ = 3
- Adhibu kosa la hijai litokeapo kwa mara ya kwanza hadi 6 x ½ = 3

**SEHEMU C: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA (Alama 40)**

(a) Vipasuo (alama 2)
/dw/ /tw/ (2 x 1= 2)

(b) (i) KKK – blan – keti (alama 2)
(ii) K - Mlango, m – tu
(iii) IK - Al – hamisi
(iv) KIK - Mak - taba Dak – tari (2 x 1 = 2)

(c) Kilichonywewa (alama 3)

| Ki | - | li | - | cho | - | nyw | - | ew | - | a |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Ngeli ya KI -VI | | wakati uliopita | | kirejeshi | | mzizi | | kauli ya mnyambuliko | | kiishio |

(6 x ½ = 3)

(d) Unda nomino (alama 2)
(i) Madhara - kudhuru
(ii) Kitenzi - kitendo, tendo, mtendaji, utendaji, n.k. (2 x 1 = 2)

(e) Tambua virai vihisishi (alama 2)
Wengine wao waliegesha kando ya barabara iliyokarabatiwa na kampuni ya kichina

Kando ya barabara - RH

Na kampuni ya kichina - RH (2 x 1 = 2)



(f) i) Raia wakipatana maendeleo yataimarika (alama 2)
***Raia watakapopatana maendeleo yataimarika***
ii) Mkiwatesa watoto wenu mtashtakiwa
***Mwatesapo watoto wenu mtashtakiwa*** (2 x 1 = 2)

(g) Mtego ulimnasa ndovu huyo (alama 3)
***Jitego / Tego limelinasa jidovu / dovu hilo*** (6 x ½ = 3)

(h) Msichana amepigwa vibaya (alama 2)

***Msichana mbaya amepigwa*** (1 x 2 = 2)

***V***

(i) Yambwa tendwa - miche ya matunda (alama 4)
Yambwa tendewa - mwalimu mkuu
Yambwa ala - vijiti
Chagizo - nje ya nyumba yake (4 x 1 = 4)


(j) Vurumai (alama 2)
- ghasia, fujo, zogo, vurugu, kizaazaa,rangaito, kivangaito, tendabeluwa (2 x 1 = 2)

(k) (i) maana na (alama 2)
ii) au
iii) Sawa sawa na
iv) Kuandika tarehe
( Mwalimu akadirie mifano) (2 x 1 = 2)

(l) S - KN(N + V) + KT (T + E) (alama 4)

| KN | | KT | |
|---|---|---|---|
| Walimu | wote / | walikusanyika | ukumbini |
| N | V | T | E |

(4 x ½ = 2)




(4 x ½ = 2)

(m) **"Tungefika mapema tungekamilisha shughuli zote," Alikiri Kyalo (alama 2)**
Kyalo alikiri, "Tungefika mapema tungekamilisha shughuli zote." (1 x 2 = 2)

(n) i) **Alipokelewa mgeni** **(alama2)**
Mgeni alipokelewa kwa niaba yake
ii) **Alipokezwa mgeni**
Alitetewa mgeni ampokee (2 x 1 = 2)

(o) **Kinyume cha sentensi** **(alama 3)**
Vijana walikita kambi kabla ya machweo / mawio / magharibi (3 x 1 = 3)

(p) Asha hakuwapelekea wageni chakula wala hakuwanavya mikono (3 x 1 = 3)

**SEHEMU D: ISIMU JAMII (Alama 10)**

(a) **Sifa zozote tano za lugha ya itifaki**
**(alama 5)**
Itifaki ni lugha inayotumika katika shughuli za kiubalozi

1) Huwa ni lugha ya adabu hata palipo na uhasama
2) Hutaja vyeo na sifa za wahusika pamoja na nchi zao, mfano; Balozi au mjumbe wa Jamhuri fulani.
3) Hulazimu maamkizi au maneno machache ya utangulizi kwa mwenyeji
4) Huhusisha maneno sahili yaliyoteuliwa kwa uangalifu ili kufanikisha mawasiliano
5) Lugha ya wastani isiyo na mihemko kama furaha na ukali
6) Huhitaji matumizi mwafaka ya shadda, toni na vituo.
7) Hutegemea matumizi ya viziada lugha kama vile, tabasamu na miondoko.
8) Hutumia tasfida kuficha ukali ili kutochoma au kuzua uhasama.
9) Msamiati unaotumiwa hutegemea mada, mazingira na dhamira.

(zozote tano) (5 x 1 = 5)

(b) Hakiki sifa zozote tano za sajiliya kituo cha polisi
(alama 5)

1) Lugha yenye ukali. – lugha ya kuamrisha
2) Kuna maswali dadisi
3) Lugha ya sheria hutumika. Mfano; wakili
4) Lugha ya kunyenyekea
5) Lugha ya misimu. Mf; mguu wa kuku – bastola
6) Kuna kuchanganya na kubadilisha msimbo

(zozote tano) (5 x 1 = 5)

# ALLIANCE GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

1(a) maelezo ya mwandishi
- Anamrejelea Bwana Kimbaumbau
- Ni baada ya Sauna kukataa kushiriki mapenzi naye
- Wote wawili walikuwa Kazini

(4 x 1 = 4)

(d) Ubabedume/ Taasubi ya kiume (1 x 1 = 1)

(e)

(i) Jamaa za Kangata kupinga elimu ya mabinti zake

(ii) Kimbaumbau kumdhulumu Naomi anapokataa kujihusisha kimapenzi naye.

(iii) Mwimo Msubili kutotaka kukutana na mwanamke asubuhi kwa madai kuwa ni Mkosi.

(iv) Lime na Mwanaheri kunajisiwa na vijana wahuni.

(v) Bwana Maya anamdhulumu mamake Sauna kwa mapigo na matusi aulizapo swali lolote lile.

(vi) Kuuzwa kwa Pete kwa Fungo ili wazazi wake wapate pesa za kuwaelimisha ndugu zake watano wa kiume.

(vii) Pete anabakwa na mlevi anapolewa chakari

(viii) Mamake Zohari kuridhia kila asemalo mumewe na kushidwa kumtetea anapopata himila.

(ix) Mamake Mwangeke aliwahi kumwonya kulia kama msichana. Hii ni ishara kuwa jamii yamwona mwanamke kama mnyonge.

(x) Mwanzi anakataa kukubali matokeo ya uchaguzi madhali anashindwa na mwanamke, Mwekevu.

(xi) Wahafidhina kuamini kwamba mtoto wa kiume ndiye pekee anayestahili kuwa mrithi wa mali ya babake.

(xii) Ushindi wa Mwekevu unaonekana kama kutoheshimiwa kwa mwanaume.

(xiii) Mwekevu kusingiziwa wizi wa kura anapomshida Mwanzi.

(xiv) Kutishwa, kutusiwa na hata kutengwa kwa Mwekevu anapojitosa katika siasa zilizoaminiwa kuwa ni za wanaume

(xv) Fungo anamharibia Pete maisha anapomwoa kisha kumfukuza anapojifungua mtoto.

(xvi) Mwanamke kuonekana kama mnyonge anayestahili kulia akabiliwapo na vizingiti au changamoto maishani. Mwanaume hafai kulia

(alama 15 x 1 = 15) (zingatia hoja nyingine zozote sahihi)

2(a) maneno haya ni ya sauti ya mzee Kenga mawazoni mwa Majoka. Haya yanatendeka katika Ofisi ya Mzee Majoka wakati Husda na Ashua wanapigana. Majoka anakumbuka ushauri wa Kenga wa jinsi ya kumnasa Ashua kwa kusababisha fujo baina yake na Husda

(b) (i) Kumwaga kemikali na taka sokoni licha ya kuwa wananchi wanakaa na kufanyia biashara zao katika soko.

(ii) Kuwatumia wahuni kunyamazisha wapinzani. Mzee Kenga anakutana na Wahuni chini ya mbuyu ambao baadaye wanamwumiza Tunu.

(iii) Kuruhusu dawa za kulevya na wanafunzi ambao wanakuwa makabeji

(iv) Kuwaua wapinzani, kama vile vijana watano walioandamana

(v) Kuwatumia polisi kuwaua na kurushia waandamanaji risasi na vitoa machozi.

(vi) Kuwanyima wafanyakazi haki, kama vile walimu na wauguzi wanaongezewa asilimia ndogo ya mshahara kasha kupandisha kodi.

(vii) Utawala kuruhusu uuzaji wa pombe haramu kinyume na katiba, ambao umesababisha vifo na kufanya watu kuwa vipofu.

(viii) Kufungulia biashara ya ukataji miti ilhai watu wanategemea miti hiyo kuboresha mazingira.

(ix) Kufunga kituo cha runinga ya Mzalendo kwa kuonyesha mkutano wa Tunu na wapinzani wengine wa utawala.

(x) Utawala kutumia vyombo vya dola kuwafukuza watu wanaoenda sokoni na kuweka ulinzi mkali licha ya kuwa ulikuwa uwanja wa umma.

(xi) Kuwarushia wakazi vijikaratasi vyenye ujumbe hasimu wakitakikana wapahame mahali ambapo wamekuwa wakiishi kwa muda wote wa uhai wao.

(c) (i) Kenga anamshauri Majoka amwalike Ashua na Husda ili patashika itokee, naye Majoka apate jinsi atakavyolipiza kisasi kwa Sudi kwa kukataa kuchonga kinyago.

(ii) Anamshauri Majoka atangaze kuwa maandamano ni haramu kisha anawamuru maafisa wa polisi watumie nguvu zaidi dhidi ya umma unaondoa maandamano.

(iii) Majoka anakataa Suala la polisi kutumia nguvu zaidi lakini Kenga anamwambia "Acha moyo wa huruma….. Siasa na hisia haziivi kwenye chungu kimoja ndugu yangu.

(iv) Anakubali pendekezo la Majoka la kufunga Runinga ya Mzalendo kwa kupeperusha matangazo ya mkutano moja kwa moja.

(v) Kenga alihusika katika kupanga mauaji ya Jabali kwani Majoka anamsifu kwa kupanga hilo na hata wanapigishana Konzi

(vi) Anaibua pendekezo la kumuua Chopi kwa kutofuata maagizo ya kumuua Tunu akisema, "Nafikiri Chopi lazima aende safari."

(vii) Anamwambia Majoka kuwa si kweli kwamba watu watampigia Tunu kura na kusema, "Tunu hawezi kupigiwa hata!"

(viii) Anapendekea kukusanya kodi ya juu na kukataa kuitumia vyema na kwa njia halali k.v. kutoa taka.

3(a) **Fafanua mbinu nane anazotumia Majoka katika uongozi wake.**

a) Uvumi kwa mfano – Sudi na Ashua wanaiwinda roho ya Tunu

ai) Ahadi za uwongo – kutoa chakula kwa wasiojiweza

iii) Zawadi - keki za uhuru

iv) Vitisho - Akiwa chopi watamwaga unga

v) Mapendeleo - Tunu na Ashua walipewa kazi wakakataa. Ashua angekuwa mwalimu mkuu katika shule mojawapo za Majoka kama angekubali.

vi) Sela - Wanaompinga wanafungwa jela k.v. Sudi anasema amefungwa mara nyingi katika jela alikofungwa Ashua.

vii) polisi - polisi wanatawanya waandamanaji

viii) Mabavu - Madai ya kuwafukuza wafadhili wa wapinzani ili wavunje kambi zao Sagamoyo, Nguvu zaidi kutawanya waandamanji

ix) Kudhibiti vyombo vya dola - Majoka kutaka kufunga vituo vyote kibaki Sauti ya Mashujaa

x) Ulaghai - mf. Kuongeza mishahara ya walimu na wauguzi kisha kupandisha kodi.

xi) mavamizi - mf. Tunu kuvamiwa na kuvunjwa muundi

xii) Ulinzi - Majoka ana walinzi wengi. (10 x 1 = 10)

(b) Ishara

i) Kinyago cha kike kinachochongwa na Sudi na kukiita shujaa halisi wa Sagamoyo kinaashiria shujaa wa kike atakayelikomboa Jimbo la Sagamoyo dhidi ya uongozi dhalimu

(ai) Fimbo ya Kenga yenye kichwa cha Nyoka ni ishara ya jinsi alivyokuwa katili kwa raia. Kwa mfano, anamuua Jabali

(bi)Uchafu wa soko ya chapakazi ambao unamsababisha hata Mzee Kenga kuziba pua yake anapoenda huko ni ishara ya maovu yaliyokithiri jimboni Sagamoyo.

(iv) Kitendo cha Majoka kuzungumza na babu yake anapozirai ni ishara kuwa wafu walikuwa wakimwita madhali naye aliokuwa amewaua

(v) Majoka kuvaa mkufu shingoni wenye kidani cha umbo la swila ni ishara ya namna Majoka alivyokuwa hatari kwa maisha ya raia wa jimbo la Sagamoyo.

(vi) Kujaa kwa maziara jimboni Sagamoyo hadi hakuna nafasi ya kuwazika wafu wengine ni ishara ya mauaji yaliyokuwa yametekelezwa na Majoka.

(vii) Kilio na machozi mengi ndani ya ziwa lililofunika damu ni ishara ya raia waliouliwa na Majoka wanalilia haki yao.

(viii) Kutojaa kwa raia jinsi ilivyo kawaida katika mkutano wa kuadhinisha sherehe za uhuru pamoja na siku ya kuzaliwa kwa Majoka ni ishara ya raia kuasi Majoka kutokana na uongozi wake dhalimu.

(ix) Hali ya Majoka kujiona ndani ya ziwa lililofurika damu ni ishara ya mauaji mengi ya raia aliyokuwa akitekeleza katika uongozi wake.

(x) Damu ya Jabali anayoiona Majoka ikitiririka mikononi mwake akiwa amezirai ni ishara kuwa yeye ndiye aliyemuua Jabali

(Zingatia nyingine zozote sahihi alama 10 x 1 = 10)

**1 (a) Eleza muktadha wa maneno haya (alama 4)**

Haya ni maneno ya Jairo. Anahutubu katika sherehe ya kumuaga mwalimu Mosi ambaye alikuwa anastaafu kutoka kazi ya ualimu. Sherehe hii ilifanyika shuleni. Jairo anamkosoa mwalimu Mosi kumpatia matumaini ya uongo masomoni ilhali alijua hawakuwa na uwezo wa kimasomo badala ya kumruhusu aende ajaribu mbinu nyingine ya kujikimu kimaisha ili awe mtu wa maana katika jamii.

**(b) Onyesh vile kinaya kinavyojitokeza (alama 2)**

Jairo anamkosoa mwalimu kwa kumfunza na kumpa matumaini maishani badala ya kumwachilia mapema aende akaibe na kuua. Jairo analodokeza hapa ni kuwa ili mtu awe wa maana ni lazima aibe na aue.

**(c) "Kinaya kimetumika kwingine kwingi katika hadithi ya Mwalimu Mstaafu" Thibitisha (ala. 9)**

- Ni kinaya kwa Jairo kudai ili mtu awe wa maana, athaminiwe na kuitwa mhesimiwa na kuwa bingwa lazima aibe, apore au aue
- Ni kinaya kwa Jairo kuuona uelekezi na ushauri wa mwalimu wake kama upotoshi na upotezaji wa muda. Jairo anadai alipotezewa muda kwa kupatiwa matumaini ya uongo.
- Ni kinaya pia kwa mwalimu Mosi kutaka ahutubie mtu ambaye atamkosa badala ya kumsifu.
- Ni kinaya kwa Jairo kuona elimu haina manufaa yeyote ilhali wenzake walifaidi kutoka kwa elimu ya mwalimu wao.
- Ni kinaya kwa Jairo kumtoa bintiye na mkewe kama zawadi kwa mwalimu wake kama shukrani ya zawadi anazompa. Ni kinaya kwa mtu kubadili mkewe kama zawadi.
- Ni kinaya kwa Jairo kudai kuwa pombe ni kiliwazo cha kimawazo kinachomsahaulisha masibu ya maisha na kumkosoa mwalimu wake kwa kumwonya dhidi ya matumizi ya pombe.
- Ni kinaya kwa mkewe jairo kukubali kitendo cha mumewe Jairo kumtoa kama zawadi kwa familia nyingine. Anakubali kubadilishwa na mali.
- Ni kinaya kwa Jairo kudai kuwa ufuska ndio raha ya maisha na kuwa uaadilifu haufai. Anadai kuwa maisha ni bora bila nasaha za mwalimu.
- Ni kinaya kwa mkewe mwalimu Mosi, Sera kukubali na kumkaribisha mwanamke mwingine na watoto wake kwenye familia yake.

(hoja zozote 9)

**(d) Umuhimu wa msemaji katika hadithi (alama 5)**

- Ni kielelezo cha utovu wa nidhamu miongoni wa wanafunzi. Anakunywa pombe na hata kujihusisha katika ufuska.
- Kupitia kwake uwajibikaji wa mwalimu Mosi unajitokeza. Kama mwalimu

alimkanya kunywa pombe na hata ufuska.

- Anaendeleza maudhui ya umaskini katika hadithi.
- Anakuza sifa za wahusika wengine kama vile Mwalimu Mosi.
- Ametumiwa kudhihirisha ukweli wa methali "asante ya punda ni mateke."

2 (a) Masharti ya Kisasa

- Mwanaume humposa mwanamke. Dadi alienda nyumbani kwa Kidawa kumposa
- Mwanamke ndiye huamua wakati wa kuolewa na nani wa kumwoa. Kidawa alimchagua Dadi baada ya muda mrefu.
- Ndoa huandamana na masharti. Dadi alipewa masharti na Kidawa ili akubali kuolewa naye.
- Wanandoa hufanya kazi pamoja ili kukithi mahitaji ya nyumbani. Dadi anachunza samaki na Kidawa ni metroni
- Wanaume hawafurahi wake wao wanapotangamana na wanaume wengine. Kidawa anaposimama kuongea na wanaume, Dadi anadhika sana.
- Wanandoa husaidiana kazi za nyumbani, Dadi anasaidia kidawa kazi za nyumbani kama vile kuosha vyombo na kufagia.
- Wanandoa wanapanga uzazi, Dadi na Kidawa wanapanga kuwa na mtoto mmoja pekee.
- Mwanamke anaajiriwa. Kidawa aliajiriwa shuleni kama metroni.
- Mwanamke anajinunulia nguo na fashoni nyingine. Kidawa ananunua viatu na kanzu anayovalia kwenda kazini.
- Ndoa imekosa uaminifu. Dadi anashuku kuwa Kidawa ana mapenzi na mwalimu mkuu.
- Kiwango cha elimu si kikwazo katika ndoa. Kidawa anaolewa na Dadi licha ya kuwa ana kisomo cha juu kuliko Dadi.

- Mwanamke amekengeuka. Kidawa anapenda fashoni.
- Wote wawili. Mwanamke na mwanaume wanachangizana nyumbani.
- Kuna makubaliano ya kufanya mambo kwa pamoja. (13 x 1 = 13)

(b) Shibe inatumaliza

- Mzee Mambo hafanyi kazi wizarani ilhali analipwa mshahara mkubwa kuliko Sasa na Mbura wanaofanya kazi wizarani
- Mambo anatumia runinga ya taifa inayofaa kuufahamisha umma masuala ya taifa lao kwa maslahi yake. Anaitumia kupeperusha sherehe inauofahamika nyumbani kwake.
- Mambo anaifilisi serikali kwa kutumia pesa za serikali kugharamia sherehe

zake binafsi. DJ na wenzake wanalipwa mabilioni ya pesa za serikali kwa kusimamia sherehe hii.

- DJ anaipunja serikali kwa kutumia mtaji wa bohari kuu ya dawa za serikali kufungua duka lake la dawa.
- DJ anaifilisi serikali kwa kupokea huduma za maji, umeme na matibabu bure ilhali wananchi maskini wanazilipia.
- Wafanyakazi wa umma wanaibia serikali saa za kazi. Sasa na Mbura wanahudhuria sherehe zilizofanyika kwa Mambo siku nzima ilhali walipaswa kuwa kazini.
- Mzee Mambo anatumia magari ya serikali kwa maslahi yake binafsi. Kwa mfano, anayatumia kusomba maji, chakula, kuwaleta jamaa wa Mambo shereheni na mapambo.

(7 x 1 = 7)

3 (a) Shughuli za kiuchumi

(i) Ufugaji / wafugaji – Anayeimbiwa wimbo alipozaliwa fahali alichinjwa.

(ai) Ukulima / kilimo - Anaahidiwa shamba la migomba na maparachichi

(2 x 2 = 4) ( lazima mwanfunzi athibitishe)

**(b) Nani mwimbaji wa wimbo na anamwimbia nani? (alama 2)**

Mwimbaji – mjomba

Mwimbiwa – mpwa (mtoto wa dadake mwimbaji)

(2 x 1 = 2)

**(c) Huu ni wimbo wa aina gani? Thibitisha (alama 2)**

Nyisho – mpwake anatayarishiwa kukabiliana na kisu cha ngariba

Mwanafunzi lazima athibitishe (2 x 1 = 2)

**(d) Mwimbaji wa wimbo huu ana taasubi ya kiume – Thibitisha kauli hii (alama 2)**

- Anaona kuwa waoga ni akina mama
- Anasifu wanume wa mbari yao kuwa si waoga

- Akilia atachekwa na wasichana
- Anaambiwa kuwa ni "Ndume / mme" akabiliane na kisu (2 x 1 = 2)

**(e) Nyimbo zina wajibu gani katika jamii (alama 6)**

- Huwatayarisha wanapoenda kupashwa tohara
- Hukashifu woga na kuhimiza ujasiri
- Husawiri falsafa ya jamii. Wanaume hawaogopi.
- Huonyesha majukumu mapya ya wanaotiwa jandoni
- Huleta jamii pamoja
- Hukuza na kuendeleza tamaduni na desturi za jamii
- Hutumbuiza / huburudisha
- Hukosoa / kusahihisha maovu (6 x 1 = 6)

**(f) Ijapokuwa nyimbo ni nzuri zina ubaya wake. Thibitisha kauli hii (alama 4) (ubaya wa nyimbo)**

- Huweza kuibua hisia za ukabila na utabaka
- Hutumika kueneza propaganda. Hueneza uchochezi
- Kuna ukosefu wa maadili katika baadhi ya nyimbo. Baadhi huwa na matusi, vitendo vya ngono n.k.
- Nyimbo zinalevya/ pumbaza watu
- Husababisha uzembe
- Baadhi huwa ghali/huhitaji kiasi kingi cha pesa kununua au kutoa na kuzirekodi

(4 x 1 =4)

4 **(a) Taja na ueleze mikondo ya shairi hili (alama 4)**

- Tathlitha
- Mathnawi
- Msuko
- Ukara
- Sabilia

**(b) Eleza dhamira ya shairi hili (alama 2)**

Kuzindua /kuonyesha watu jinsi maisha ya ulimwengu yalivyo na misukosuko/ matatizo

**(c) Taja tamathali za usemi zilizotumiwa katika shairi hili (alama 2)**

Sitiari - papa, ndovu, samba, fisi dagaa – kusimamia watu
Tashbihi - kama dau baharini, mibuyu na mivute inatikiswa kama usufi na pamba

**(d) Eleza muundo wa shairi hili (alama 4)**

- Beti 8
- Kila ubeti una mishororo mitatu
- Kila mshororo una migao 2 ila kibwagizo (cha mmoja)
- Vina vya mwisho vinatiririka lakini vya kati haritiririki
- Shairi halina kibwagizo

**(e) Eleza ujumbe unaojitokeza katika ubeti wa 5 (alama 3)**

Mibuyu na mivute inasukwa kama pamba au usufi seuze migomba hii, viumbe tu hali gani

**(f) Onyesha matumizi ya idhini ya kishairi (alama 3)**

Tabdila - duniya, mgamba, hiyi, kiangaliya
Inkisari - la kwamba (kuamba – kusema)
Kuboronga sarufi – na kuvurugika myamba
- Limeshamiri tofani
- Kila mmoja lakumba
- Mibuyu… kama usufi na pamba inarushwa

**(g) Eleza maana ya maneno haya (alama 2**

Mdaduwa - mwenye kufanya sawa (kusawazisha)
Kutamba - Kusambaa

**5 (a) Hali ya mzungumziwa**

- Mcheshi
- Mwenye bidii
- Maskini (2 x 1 )

(b) Inkisari; babuze – babu zetu
Kuboronga sarufi; Aliye na kubwa hamu
Aliye na hamu kubwa (2 x2)

(c) Taswira sikivu, anasikiliza videge vya anga vinavyotumbuiza
Taswira mnuso; Rihi ya maua zikimletea
Taswira mguso; umande kumbusu miguuni (3 x 1)

(d) Maswali ya balagha hukuza maudhui ya unyanyasaji
Pia kunyimwa haki kwa binadamu maskini (2 x 1)

(e) Tashihisi - umande kumbusu miguuni
Kinaya - kuwa mrejelewa anafuraha ilhali anafanya kazi za sulubu (kulima)
Tashibihi - Tabasamu kama mtu aliye na kubwa hamu (3 x 1)

(f) Huruma - mateso mrejelewa anayoyapitia (1 x 2)

(g) Mchunguzi / mpita njia wa karibu na mrejelewa (1 x 1)

(h) Beti tatu
Mistari mishata
Mishororo haina mizani sawa
Hakuna urari wa vina (3 x 1)

# SACHO HIGH SCHOOL

## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019

## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)

**LAZIMA**

**Athari hasi**

i) Kutumia muda mwingi kwa mitandao.
ii) Kutazama picha na video za ponografia zinazowapotosha kimaadili.
iii) Kuiga tamaduni za kigeni.
iv) Huchochea uhalifu.
v) Kuingiliwa kwa maisha ya kibinafsi ya mhusika.
vi) Athari za kisaikolojia kutokana na wanayoyaona.
vii) Mahusiano mabaya.
viii) Kushuka kwa maadili ya jamii.

**Athari Chanya**

i) Kupata nafasi za kazi.
ii) Kupata wafadhili
iii) Kuongezea maarifa
iv) Kuwezesha utafiti
v) Kujenga mahusiano mazuri
vi) Ni njia ya kuunganisha aila.
vii) Ni njia ya kupata burudani.

*Mwanafunzi anaweza kuegemea upande wowote ule au achanganye hoja kutoka pande zote.*

**2.** **Kupofuka**

i) Maradhi tofauti hasa ya maini
ii) Kufilisika
iii) Kusambaratika kwa ndoa
iv) Vifo
v) Uhalifu
vi) Ulofa
vii) Kutamauka
viii) Kudorora kwa uchumi wa nchi kwa vile vijana hawafanyi kazi.
ix) Kutekeleza majukumu ya unyumba.
x) Huleta migogoro katika familia.

**3.** i) Mwanafunzi atunge kisa kitakachodhihirisha maana ya methali.
ii) Atunge kisa kitakachoonyesha mtu/mhusika fulani aliyepotoka kitabia kisha akawaathiri wenzake anaoingiliana nao.

**4.** Mwanafunzi asimulie kisa kuhusu mtu ambaye hawajaonana kwa muda. Matukio yaonyeshe mseto wa hisia labda kutokana na tendo zuri au baya lililofanywa.

# SACHO HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha
## Mwongozo wa Kusahihisha

**A. UFAHAMU**

1. Kwa kuwa mfano mbaya ambao Bwana Tenge anajihusisha na mapenzi ya kiholela mbele ya watoto. *2x1=2*
2. i) Ajira ya watoto
   ii) Dhiki za kisaikolojia – Tenge afanyapo mapenzi mbele ya watoto.
   iii) Makazi duni – chumba kidogo. *3x1=3*
3. i) Kuhamishwa bila kujali maslahi ya watoto wao.
   ii) Vyumba vidogo sana.
   iii) Umaskini *3x1=3*
4. i) Mvumilivu
   ii) Mnyonge
   iii) Mlezi mwema
   iv) Mwenye utu *3x1=3*
5. Ndoa ina changamoto ya kukosa uaminifu ambapo Tenge aliwaleta wanawake wengine ndani ya nyumba mkewe alipoenda mashambani.
6. i) Danguro – Nyumba inayotumiwa na Malaya kufanyia uasherati. *1x1=1*
   ii) Kisaikolojia – inayohusiana na akili ya binadamu. *1x1=1*

**B. UFUPISHO**

a) i) Ripoti za uhalifu wa pesa za umma katika serikali za kaunti ni za kusikitisha.
   ii) Mabilioni ya pesa hufujwa katika serikali kuu.
   iii) Wananchi wanakosewa mtindo huu ukiendelea katika serikali za kaunti.
   iv) Katiba mpya ilipopitishwa wakenya walidhani ingewatatulia matatizo yao.
   v) Miaka tisa baadaye kuna mafanikio ingawa yanaweza kuboreshwa.
   vi) Magavana hubuni nafasi za kazi na kupatia marafiki zao.
   vii) Wananchi wameanza kufa moyo kuhusiana na ugatuzi.
   viii) Changamoto za ugatuzi ni ulafi wa viongozi wachache.
   ix) Wakosoaji wa ugatuzi huchochea wananchi wasichangie maendeleo katika kaunti zao.

***(alama 8, 1 ya mtiririko)***

b) i) Juhudi za maendeleo haziwezi kufanikishwa bila ushirikiano.
   ii) Ni jukumu la viongozi kuonyesha nia ya kutumia mamlaka kwa manufaa ya raia.
   iii) Tume ya maadili ya kupambana na ufisadi inafanya kazi nzuri ya kuwashtaki magavana waliofuja mali ya umma.
   iv) Asasi zote na washika dau wasifumbie macho maovu.
   v) Nchi inatawaliwa kwa misingi ya kisheria hivyo viongozi wasihurumiwe.
   vi) Adhabu kali pekee zitakomesha uongozi mbaya.

***(alama 7, 1 ya mtiririko)***



a –

b –



**C. SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**

a) i) /e/
- Irabu ya mbele
- Irabu ya tandazwa
- Hutamkiwa ulimi ukiwa wastani. 2 x ½ = 1

ii) /ch/
- Kipasuo - kwamizo
- Ni ya kaakaa gumu
- Ni sauti sighuna/halifu 2 x ½ = 1

b) i) Kalamu, kitabu, kijiko, darasa n.k 1 x 1 = 1
ii) Umma, amwa, embe, imba.. n.k 1 x 1 = 1

c) i) mwanafu'nzi
ii) Al'hamisi

d) i) Kuonyesha habari za ziada.
*Mfano: Madereva (wa lori) wamepewa leseni.*
ii) Kuonyesha maneno yasiokuwa na umuhimu katika sentensi.
*Mfano: Nikienda Mombasa (ninavyotarajia) nitanunua nazi.*
iii) Kuandika nambari au herufi.
*Mfano: (1) (a) (ii)* 1 x 1 = 1
iv) - Kuonyesha sauti ya ving'ongo
*Mfano: Ng'ombe, Ng'oa*
- Kuonyesha tarakimu au herufi iliyodondoshwa
*'57 , n'taondoka* 1 x 1 = 1

e) i) A – WA 1 x 1 = 1
ii) I – ZI 1 x 1 = 1

f) Madege hayo yana majoya mengi. 2 x 1 = 2

g) M – li – ye – m – [pik] – i – a 6 x ½ = 3

*Nafsi wakati kirejeshi kitendwa kauli kiishio*

h) Mwanafunzi atumie kielezi cha idadi
*Mfano: mara moja, mara kadha, tena* 1 x 1 = 1

i) Ingawa alitia bidii masomoni, alifeli mtihani.
kishazi tegemezi kishazi huru 1 x 1 = 1

j) (alama 3)

| S | | | | |
|---|---|---|---|---|
| KN | | | KT | |
| N | V | S | T | N |
| Mvua | kubwa | inayonyesha | itasababisha | mafuriko |

*Ukurasa* 2

k) Mama huyo alijengewa nyumba kwa matofali na Kirwa. 2 x 1 = 2

l) Walimu hawatakuwa wakifunza. 2 x 1 = 2

m) "Nitawatembelea wazazi wetu leo jioni," Muliwa alimwambia Farida. 4 x ½ = 2

n) i) tokwa na pumzi kwa nguvu kama vile baada ya kukimbia au kufanya kazi ya sulubu.
ii) Kibanda aghalabu cha turubali kinachotumiwa na wasafiri wanaokwenda kuishi mahali pasipo majumba
iii) Tua, pumzika 2 x 1 = 2

*Mwanafunzi sharti atunge sentensi moja pekee.*

o) Walale!

p) Mama alijitua kikapu mgongoni baada ya kuepua chungu mekoni. 2 x 1 = 2

q) huo tata – RV (kirai vumishi)
jana jioni – RE (kirai elezi) 2 x 1 = 2

r) Nafsi (ya kwanza)
Kiunganishi
Wakati uliopo
Kihusishi cha 'a' unganifu
Upatanisho wa kisarufi wa ngeli mbalimbali
Mfano: Machungwa hayo nayo ni ya Tanzania. 3 x 1 = 3
*Mwanafunzi sharti atunge sentensi moja itakayodhihirisha matumizi matatu tofauti.*

s) i) Pakata
ii) Chomoa

t) i) Mama huyo alijifungua mtoto msichana.
ii) Mtoto ameenda kujisaidia/pembeni/haja/msalani.

**D. ISIMUJAMII**

a) Hospitalini/Zahanatini 1 x 2 = 2

b) i) Sentensi fupi fupi.
ii) Kuchanganya ndimi mfano: chest, pain relievers
iii) Lugha haizingatii kanuni za kisarufi mfano: niko poa
iv) Lugha ni ya udadisi
v) Msamiati maalum mfano: Pain relievers
vi) Lugha ya unyenyekevu hasa kwa upande wa mgonjwa mfano: Asante sana, nashukuru
vii) Lugha ya matumaini mfano: utakuwa sawa.
viii) Lugha ya majibizano – Kibiko na Cheupe.

# SACHO HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

**RIWAYA: CHOZI LA HERI**

**1. Riwaya ya Chozi la Heri inayasawiri matatizo ya wanajamii. Jadili.**

a) Kupoteza jamaa – Familia ya Ridhaa inateketea ndani ya nyumba yake kutokana na
ghasia za kikabila.

b) Ubakaji – Lime na Mwanaheri wanabakwa na genge la vijana ambao wanawavamia nyumbani.
c) Tamaa ya mali – Wafanyabiashara katika jumba la kupangisha la Ridhaa wanawafungia wateja wao ndani wakati wa mkasa wa moto ili wasipate mali.
d) Tatizo la makazi – Watu wanatolewa katika msitu wa Mamba kwa kulazimishwa japo walipewa hatimiliki na serikali.
e) Ulanguzi wa dawa za kulevya – Dick anapelekwa kwa Buda ambapo analazimishwa kufanya kazi ya ulanguzi wa dawa za kulevya.
f) Ukosefu wa maadili – Fumba anamringa Rehema mwanafunzi wake wa Kidato cha Tatu.
- Bwana Maya anamdhulumu kimapenzi Sauna, mwanawe wa kambo.
g) Kudhulumiwa na vyomba vya Dola – Askari, wakiwemo wale wa 'Penda Sugu Ujute', wanatumia vitoza machozi na hatimaye kuwapiga risasi vijana na kuwaua.
h) Tatizo la malezi – Naomi, Annette and Subira wanawasaliti wanao na waume zao wanapoamua kuwaacha na kwenda kwingineko.
i) Ulanguzi wa watoto – Bi. Kangara anamtafutia Sauna ajira ya kuwateka nyara watoto wa watu na kuwauza.
j) Tatizo la huduma za matibabu – Matajiri wanawadhulumu maskini wasiojiweza kwani wananyakua dawa zilizotengwa kwa ajili yao.

k) Kujichukulia sheria mikononi – Wanajamii wanaonyesha ukatili wanapompiga Lemi kisha kumteketeza kwa kisingizio cha kuiba simu.
l) Ukosefu wa ajira – Vijana wanaohitimu kutoka vyiuoni hawapati nafasi za kazi au zinatolewa kwa mapendeleo.
m) Ufisadi – Watu wanaogombea nafasi za uongozi huwahonga wananchi kwa hela na vitu vinginevyo ili wapigiwe kura mfano: Papa.
n) Ndoa za mapema – Pete anaozwa akiwa mchanga sana na wajomba zake. Anaozwa kwa Fungo kama mke wa nne.
o) Ukeketaji wa wanawake – Tuama anaelezea jinsi yeye na wenzake walivyopashwa tohara ili wasikose waume. Hata hivyo, wasichana wengi huishia kuvuja damu nyingi na hata kufa.
p) Ukosefu wa kazi – Shamsi anaeleza jinsi nafasi za kazi hutolewa kwa mapendeleo hivyo wengi huishia kuwa maskini hasa walio na shahada mbalimbali,

q) Pombe haramu – Shamsi anasema kuwa wengi hufa na kupofuka kutokana na unywaji wa ndengelua iliyotiwa vijasumu ili iive haraka.
r) Uavyaji – Sauna anaavishwa mimba na mamake ili asiiletee familia yake fedheha.
- Pete alijaribu kuavya mtoto wake wa pili bila kufanikiwa.
s) Mimba za mapema – Zohali alipata mimba akiwa kidato cha pili.

- Rehema aliringwa na mwalimu wake Fumba akiwa angali shuleni.

t) Umaskini – Ni kutokana na ukata ambapo wananchi wanaenda kuchota mafuta kutoka kwa lori lililobingiria ili wayauze kwa watu wenye magari ya kibinafsi.

20 x 1 = 20

## TAMTHILIA: KIGOGO

**2.a**) Maneno haya ni ya Ngurumo kwa Tunu huko mangweni alipowaambia Ngurumo na Mama Pima kuwa ilikuwa kinyume cha sheria kuuza pombe haramu.

*4 x 1 = 4*

**b**. i) Ngurumo – alishiriki ulevi pale Mangweni.

ii) Babedume – Alimdharau mwanamke anaposema kuwa heri ampe paka kura wala sio mwanamke.

iii) Mkware – alijihusisha kimapenzi na mama Pima ilhali ni mke wa Boza

iv) Mhalifu/mhuni – alitumiwa na Majoka kutekeleza uhalifu wa kisiasa kama vile kuwashambulia wapinzani wake (Majoka) *Zozote 3 x 1 = 3*

**c**. i) Kielelezo cha namna elimu inavyopevua mhusika kimawazo na hata kumpa ujasiri – alimkabili Majoka.

ii) Ametumiwa kuonyesha kuwa wanawake wana uwezo wa kuchukua nafasi za uongozi iwapo watakuwa jasiri.

iii) Ni kielelezo cha wanawake walio na msimamo dhabiti – alikataa njama za Majoka.

iv) Ni kielelezo cha wanawake wasiodhamini mali – Japo Ngao Junior alikuwa na mali, alikataa kuolewa naye. *Zozote 3 x 1 = 3*

**d.** i) Ni kinyume cha sheria kuuza pombe haramu ilhali Majoka ameruhusu.

ii) Majoka ametoa kibali cha ukataji miti.

iii) Haki ya kuandamana kukiukwa vijana watano wanapouawa.

vi) Kituo cha runinga ya Mzalendo kutishiwa kufungwa.

v) Majoka kuamrisha Kingi afurushe maandamano ya umma.

vi) Wapinzani kushambuliwa na hata kuuliwa. Mfano: Jabali na Tunu.

vii) Haki ya wafanyabiashara kukiukwa na kuwafungia soko.

viii) Dawa za kulevya kulanguliwa shule.

ix) Ashua kutiwa mbaroni bila hatia.

x) Unyakuzi wa ardhi ya umma.

xi) Wanasagamoyo kutozwa kodi ya juu zaidi.

xii) Walimu na madktari kuongezwa mishahara kisha kodi kupandishwa.

xiii) Watu wa jamii ya kina Kombe kutishiwa kuhama Sagamoyo.

*Zozote 10 x 1 = 10*

**3a**) (i) Badala ya wanafunzi kupata maarifa shuleni, huishia kuwa makabeji kutokana na matumizi ya dawa za kulevya.

(ii) Wahusika kama Majoka hutumia shule kama soko ya kulangua dawa za

kulevya.

(iii) Elimu hii ni duni kwani walioelimika hawapati kazi za kuwawezesha kujitegemea.
(iv) Walioelimika wanatumia elimu kujifaidi badala ya kuwa wategemezi – Sudi.
(v) Wanatumia elimu hiyo kuikomboa jamii – Sudi na Tunu.
(vi) Elimu hii si bora hivyo basi baadhi ya wahusika wanaisaka ng'ambo – Ngao Junior.
(vii) Wanaoshindwa kupata elimu huwa na vijisababu vya kila aina, mfano: Ngurumo kumlaumu mwalimu wa Historia.
(viii) Elimu hii inawapa wahusika maadili – Wote walioelimika wana maadili, kama vile, Sudi, Tunu na Ashua wakilinganishwa na Husda, Boza na Ngurumo.
(ix) Baadhi ya wahusika hudunisha elimu – Husda anasema heri yeye wa kisomo cha msingi.
(x) Elimu hii inawapa wahusika msimamo dhabiti – walioelimika hawashawishiki rahisi – Sudi na Tunu.
(xi) Inawapa wake na waume nafasi sawa wala haibagui kwa misingi ya jinsia – Sudi, Ashua, Tunu. *Zozote 10 x 1 = 10*

**b**) (i) Wanaharakati kama Tunu na Sudi waliwazindua wananchi – Tunu na Sudi wanaelekea Mangweni kuwahamasisha kuhusu uongozi mbaya.
(ii) Maandamano – Vijana waliandamana wakitetea haki zao – baadhi waliuawa.
(iii) Mitandao ya kijamii – ilitumiwa na wanaharakati kuchochea umma dhidi ya Majoka hadi Kenga anakiri kuwa haipendi mitandao ya kijamii (uk. 33)
(iv) Vyomba vya habari – Runinga ya Mzalendo inapeperusha maandamano ya wana Sagamoyo moja kwa moja (uk. 37); watu kutoa maoni kwa gazeti (uk. 33)
(v) Migomo – Walimu na wauguzi waligoma wakitaka nyongeza ya mishahara.
(vi) Wananchi walisusia sherehe ya Majoka.
(vii) Wananchi walishirikiana na kumwaga pombe haramu.
(viii) Sheria – Kingi alingatia katiba kulinda haki za wananchi.
(ix) Jumuiya ya mataifa – Tunu alileta wachunguzi kutoka nje kuchunguza kifo cha Jabali upya.
(x) Umoja wa wananchi – walishirikiana pamoja ili kumwondoa Majoka.

*(Zozote 10 x 1 = 10)*

**SEHEMU C: HADITHI FUPI – TUMBO LISILOSHIBA NA HADITHI NYINGINE**

**4**. **a**) Sauti ya ndani ya Dadi akiikejeli kauli ya mke wa mwalimu mkuu baada ya kupitia nyumbani mwa mwalimu mkuu. Mke wa mwalimu akamwambia Dadi kwamba mumewe alikuwa ameenda kazini, kazi zimemzidi na hivyo ameenda kuzipunguza.

*(Zozote 4 x 1 = 4)*

**b**) Litifati – Mwalimu mkuu ana kazi nyingi na lazima aende usiku usiku kuzipunguza.
Uradidi/Takriri – usiku usiku
– Leo ni leo
Mdokezo – Lkini leo ni leo…. *(Zozote 2 x 2)*

**c**) i) Dadi alifika bwenini.
ii) Dadi aliwaza vile angeipanda paipu iliyotoka chini mpaka juu karibu na dirisha la mwalimu mkuu.
iii) Dadi alianza kupanda ile paipu.
iv) Hapo juu aliishika na kuing'ang'ania ile paipu kisha akapeleka kichwa chake upande wa kushoto wa lile dirisha.
v) Kidawa aliingia ofisini mwa mwalimu mkuu.
vi) Mwalimu mkuu alimwambia Kidawa aketi kitini.
vii) Kidawa alisema hataki kuketi na kusema kwamba alitaka kuacha kazi.
viii) Mwalimu mkuu akamuuliza kama alikuwa amefikiri hayo kwa vile maisha yalikuwa magumu.
ix) Kidawa alisema kwamba mume wake hakumwamini na alimfikiria kuwa na jicho la nje.
x) Kelele zikapigwa huko nje na Kidawa na mwalimu mkuu wakazisikia.
xi) Dadi akaanguka chini kama kole ya nazi.
xii) Mwalimu mkuu na kidawa wakateremka chini mbio.
xiii) Njiani wakakutana na walinzi wawili na wasichana waliokuwa wakitoka kwenye vyumba vyao.
xiv) Kundi kubwa la watu lilikuwa limezunguka mtu fulani aliyekuwa amelala kwenye kokoto huku kapoteza fahamu.
xv) Kidawa alipopiga tochi alimkuta mumewe Dadi damu imemwenea kichani.
xvi) Mwalimu mkuu alikwenda kupiga simu kuita ambulensi. *(Zozote 6 x 2 = 12)*

**5. a**) **Tumbo lisiloshiba**
i) Jitu lenye tumbo linakula chakula chote katika mkahawa wa Mzee Mago bila kuwajali wateja wengine.
ii) Jitu lenye tumbo linarejea Madongoporomoka na mabuldoza kubomoa vibanda vya wakaazi.
iii) Wanamadongoporomoka wananyanyaswa kisheria kwani hawapati haki kwa kuwapata wanasheria waaminifu ni adimu kama haki yenyewe.
iv) Wakubwa wa jiji wako tayari kuichukua ardhi ya wakazi wa Madongoporomoka kwa ajili ya upanuzi wa jiji bila kujali watakakohamia. *(4 x 1 = 4)*

**b**) **Shibe inatumaliza**
i) DJ anamiliki duka kubwa la dawa ambalo mtaji wake ni bohari ya dawa za serikali. Wananchi wanakosa dawa katika hospitali za umma.
ii) DJ anapata maji, umeme, matibabu na huduma zote za kimsingi na serikali ilhali wananchi waliojawa na dhiki na ufukara wakilazimika kuzilipia.

iii) Baadhi ya viongozi kama Mzee Mambo wanapewa mishahara mikubwa na serikali kwa kufika kazini wala sio kufanya kazi huku wananchi wengi wakiishi maisha ya ufukara.

iv) Viongozi wengi hutumia raslimali za nchi kwa manufaa ya kibinafsi badala ya kufaidi umma. Mzee mambo kwa mfano, anatumia vyombo vya habari kupeperusha sherehe aliyoandalia wanawe yanayoathiri wananchi. *(4 x 1 = 4)*

**c) Mame Bakari**

i) Sara anabakwa na janadume katili alipokuwa akirudi darasa la ziada 'twisheni' na kuhimili.

ii) Wasichana wa shule wanaoambulia uja uzito hufukuzwa shule – kulingana na mawazo ya sara.

iii) Sara anaona akinyanyaswa na jamaa zake, majirani na wanafunzi wenziwe kwa kutengwa kama mgonjwa wa ukoma.

iv) Sara anawaza jinsi babake angemfukuza nyumbani kwa kuwa mja mzito akiwa angali shuleni.

v) Majirani wa Sara walimtesa kisaikolojia kwa kumsemasema baada ya kugundua kuwa ni mja mzito. *(Zozote 4 x 1 = 4*

**d) Kidege**

i) Mose ambaye anapinga kuchukuliwa kwa samaki wa kidimbwi cha bustani ya Ilala, anajipata akibanwa na mbawa za ndege wawili wakubwa.

ii) Samaki wa kidimbwi cha Ilala wanaliwa na ndege wakubwa.

iii) Videge vilikuwa vikinyanyaswa na midege kiasi cha kushirikiana ili kuiangamiza. Hii inaonyesha jinsi viongozi wanaotawala katika jamii (midege) huwanyanyasa wananchi walio chini yao (videge)

iv) Mose anapoipa midege iliombana chakula ili imwachilie aende zake, midege hiyo inakula chakula lakini haimwachilii huru kamwe.

**e) Tulipokutana Tena**

i) Bogoa anatenganishwa na jamaa zake anapopelekwa kwenda kuishi na Bi. Sinai.

ii) Bogoa anafanyizwa kazi nyingi na ngumu na Bi. Sinai kama vile, kumenya vitunguu maji, vitunguu thomu na malimau, kukuna nazi, kupara na kutoa matumbo ya samaki, kudondoa mchele miongoni mwa kazi nyingine

iii) Bogoa ananyanyaswa na Bi. Sinai anapoamshwa mapema kuliko wengine ili kuchoma mandazi ya kuuza shuleni.

iv) Bogoa ananyimwa elimu na Bi. Sinai.

v) Bi. Sinai ananyima Bogoa haki ya kupewa lishe bora kwani hulazimika kula makoko na makombo yaliyobaki baada ya watu kushiba.
vi) Bogoa ananyanyaswa na Bi. Sinai anapochomwa viganja vya mikono kwa moto anapounguza mandazi aliyokuwa akichoma. *(Zozote 4 x 1 = 4)*

**USHAIRI**

**6. (a)** Kijana/Dagaa *1 x 2 = 2*

**(b)** i) Mpangilio wa beti
ii) Vipande vya mishororo
iii) Urari wa vina
iv) Urari wa mizani
v) Urari wa mishororo *4 x 1 = 4*

**(c)** i) Lahaja mfano: Magego
ii) Kuboronga sarufi mfano: na wake udogo – na udogo wake

iii) Inkisari mfano: wafaa – unafaa *3 x 1 =*

**(d)** i) Ukawafi
ii) Mtiririko
iii) Tathlitha/utatu *3 x 1 = 3*

**(e)** Kijana ninakupa nasaha kwamba ukubwa ni jaa na ni vizuri utie bidii kabisa kazini. Ni vyema kuchimbua mihogo ili upate riziki.

**(f)** Sitiari – Jikaze kimbogo
Msemo – kuwa taa
Takriri – dagaa
Methali – ukubwa ni jaa *Zozote 2 x 1 = 2*

**(g)** Ya kuhimiza/
Ya matumaini *1 x 2 = 2*

**7. (a)** Shairi huru – i) Vina havifanani
ii) Anatumia mashata mfano: katu, eti
iii) Lina umbo la paa la nyumba
iv) Matumizi ya alama za kuakifisha
v) Idadi ya mishororo haitoshani kwa beti
*Kutaja – 1*

**(b)** i) Kupigwa
ii) Anahamishwa
iii) Anatishwa kwa bunduki
iv) Kuletewa hatimiliki bandia *4 x 1 = 4*

**(c)** Huzuni/ujasiri *1* x 2 *= 2*

**(d)** i) Shairi la beti saba
ii) Lina umbo la paa la nyumba/Pembe tatu/Piramidi

iii) Vina havifanani
iv) Idadi ya mishororo hailingani *3 x 1 =*

**(e)** Usambamba ni urudiaji wa kirai au sentensi.
Mfano: Siondoki
Niondoke hapa kwangu! *2 x 1 = 2*

**(f)** Mshairi anasema kamwe hawezi kuondoka kwake na anawashauri watu wanaomnyang'anya shamba watazame chini ya mti ule waache kaburi la babu zake.
*4 x 1 = 4*

**(g)** Inkisari – sendi - siendi
nende – niende
Kuboronga sarufi – Yangu mimi ni ardhi hii – Ardhi hii ni yangu mimi.
*1 x 1 = 1*

**(h)** i) Karatasi – Hatimiliki
ii) Nimesaki – Nimebaki *2 x 1 = 2*

**SEHEMU YA E: FASIHI SIMULIZI**

**8. (a)** Ngomezi ni aina ya fasihi ambayo huwasilishwa kwa kutumia milio ya ngoma badala ya midomo. *1 x 2 = 2*

**(b)** i) Kila mdumdo wa ngoma huwakilisha kauli mahususi kwa lugha ya jamii ambamo ngomezi imezuka.
ii) Ngomezi hutegemea mapigo, wizani na upatano unaotokana na ngoma inayopigwa kuwasitisha ujumbe.
iii) Fasiri/maana hujikita na kutokana na jamii husika. Jamii ndiyo huyapa mapigo ya ngoma zake.
iv) Kila mpigo wa ngoma hufuata mtindo wa kishairi. Kila mpigo huwakilisha silabi au mizani katika lugha tamkwa. *4 x 2 = 8*

**(c)** i) Ni nyenzo ya kupitisha ujumbe wa dharura kuhusu matukio ya dharura kama vile vita.
ii) Ni kitambulisho cha jamii. Huonyesha ufundi wa jamii wa kutumia vyombo vya muziki.
iii) Huhifadhi na huendeleza utamaduni wa jamii kutoka kizazi hadi kingine.
iii) Ni nyenzo ya kukuza uzalendo. Wanajamii hufunzwa kuionea fahari mbinu hii yao ya kuwasiliana.
v) Hukuza ubunifu. Jinsi wanajamii wanavyokabiliwa na aina tofauti za ujumbe ndivyo wanavyojifunza mitindo mipya ya kuwasilisha ujumbe kwa ngoma, hivyo kuimarisha ubunifu.

vi) Ni njia rahisi ya kuwasilisha ujumbe bila kutegemea sauti ya mtu.

*Zozote 5 x 1 = 5*

(d) i) Kutoelewa mapigo mbalimbali yanayowakilisha jumbe tofauti hivyo kutoweza kupata data kamili.

ii) Gharama ya utafiti – Huenda gharama ikawa kubwa kiasi cha kushindwa kuimudu iwapo itamlazimu mtafiti kusafiri ili kukusanya data.

iii) Kupitwa na wakati ambao ngomezi inatekelezwa. Huenda mtafiti akaenda kukusanya data wakati ambao hamna jambo la kulazimu upigaji wa ngoma kwa ajili ya kuwakilisha ujumbe.

iv) Matatizo ya mawasiliano na uchukuzi – Ikiwa mkusanyaji analazimika kwenda mbali kukusanya habari hasa sehemu kame, itakuwa vigumu kufika huko kwa sababu ya ukosefu wa vyombo vya usafiri kama vile, magari.

v) Wanajamii wengine kukataa kutoa habari hasa iwapo watashuku kwamba mtafiti anawapeleleza.

vi) Ukosefu wa usalama – huenda mkusanyaji akavamiwa iwapo baadhi ya wanajamii wanaotafitiwa si karimu.

vii) Kikwazo cha lugha – Iwapo mtafiti anazungumza lugha tofauti na jamii anayotafiti, huenda akashindwa kuwasiliana nao na hivyo kuhitajika mkalimani ili kumtafsiria.

*Zozote 5 x 1 = 5*

# FRIENDS SCHOOL KAMUSINGA
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)
## Mwongozo wa Kusahihisha

**1.** Hii ni insha ya mahojiano
- insha hii iwe na Mada / Kichwa
- huwa na wahusika zaidi ya mmoja
- ujumbe utatolewa kulingana na mahojiano husika
- maudhui hutokana na maswali na majibu ya washiriki
- mhoji ni mwanahabari (mwanafunzi)
- mhojiwa ni waziri wa kilimo
- sura ya mahojiano (mtindo wa tamthilia) maswali na majibu
- majina mhojiwa na mhoji au vyeo vyao viandikwe upande wa kushoto wa karatasi
- asipozingatia sura ya mahojiano atolewe alama nne (-4S)
- mwanafunzi ajihusishe kama mhusika, asipojihusisha aondolewe alama mbili

**Mahojiano**
Athari za baa la njaa
- vifo vya binadamu / watu
- vifo vya mifugo
- shule kufungwa kutokana na ukosefu wa chakula
- maradhi mbalimbali yamezuka k.m. utapia mlo
- kuhama kwa jamii kutafuta chakula
- pato kubwa la kitaifa linatumiwa kushughulikia njaa
- kudumaa kwa maendeleo ya wananchi na kitaifa
- wanasiasa matajiri kujinufaisha wakitumia fursa hii

**Hatua zinazochukuliwa kukabiliana na baa la njaa**
- serikali kutangaza baa la njaa kama janga la kitaifa
- kubuniwa kwa wizara ya mipango maalum inayoshughulikia tatizo hili miongoni mwa mengine
- misaada ya chakula kwa wahasiriwa kutoka kwa serikali na wahisani wengine
- serikali inawahimiza wafugaji kuuza mifugo wao ili kuepuka ukosefu wa nyasi na maji
- serikali inanunua mifugo kutoka kwa wakulima walioathiriwa na njaa
- pia inawahimiza wananchi kupanda mimea inayoweza kuhimili ukame k.v. mihogo, mtama n.k.
- wakulima kupewa mbegu za kupanda bila malipo
- wakulima wanahimizwa kupanda mimea inayochukua muda mfupi kukomaa katika sehemu zinazopata mvua chache

- serikali inajenga mabwawa ya maji ili kukusanya maji wakati wa mvua ambapo wakulima wataweza kunyunyizia mimea yao maji wakati wa kiangazi
- serikali kutenga mabilioni ya pesa ili kuwezesha shirika la nafaka chini (NCPB) kununua na kuhifadhi mazao kutoka kwa maeneo yanayojitosheleza kwa mvua

**2.** <u>Madhara ya ufisadi</u>
- vifo kutokana na ajali barabarani
- kutotibiwa bila hongo katika hospitali za umma
- kutupiliwa mbali kwa matokeo ya mitihani
- kushuka kwa viwango vya elimu
- watu kufutwa kazi kutokana na ufisadi
- familia kuteseka baada ya kufutwa kazi kwa mmoja wao aliyeshiriki ufisadi
- uharibifu wa mazingira
- kufungwa jela kwa wahusika
- viongozi kupoteza nyadhifa zao
- kudidimiza haki ya wananchi
- huleta fedheha kwa familia

**Suluhu**
- kuhamasisha wananchi kuhusu athari za ufisadi kupitia vyombo vya mawasiliano
- serikali kuwashika wahusika na kuwashtaki

- kuwafuta na kuwasimamisha wafanyikazi wa umma wanaohusika katika ufisadi
- raia kutoa ripoti kwa serikali kuhusu wanaohusika
- kuundwa tume ya kuwachunguza, kuwahoji na kutafuta ukweli kuhusu watuhumiwa
- kuundwa kwa chama cha kukabiliana na ufisadi
- sera kutaifisha mali au mashamba yaliyonyakuliwa na kurudisha kuwa mali ya umma

3. **Insha ya methali**

Mtahiniwa aandike kisa kinachooana na methali hii

Mwanafunzi azingatie sehemu mbili za methali hii

**Maana ya methali**

Malezi ya kudekeza watoto huleta majuto kwa mzazi baadaye

Mzazi akimbembeleza mtoto na kumdekeza bila kumwelekeza vyema, akiwa na tabia mbaya na kuelekea kuasi na kumtia aibu mzazi atataabika mwenyewe

4. **Hii ni insha ya mdokezo**

- Lazima mtahiniwa amalize kwa maneno aliyopewa, asipomaliza kwa maneno hayo ataadhibiwa kimtindo
- Kisa kisisimue ajabu

Mtahiniwa aonyeshe hali ya huzuni (kutendeka kwa jambo la kuhuzunisha)

# FRIENDS SCHOOL KAMUSINGA
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha
## Mwongozo wa Kusahihisha

1. a) - wizi wa mali ya umma
- vyeo na madaraka kutolewa hivi hivi tu
- uuzaji wa stakabadhi za serikali
- kuiba dawa
- kuhonga ili kupata nafasi za kusoma
- kuhonga au kutumia undugu ili kupata kazi
- kutowajibika kikazi
- kuiba dawa

*zozote 4 x 1 = 4*

b) - kufilisisha serikali
- kunyima wagonjwa matibabu
- kuzorotesha maendeleo na huduma muhimu
- kuelimisha watu wasiohitimu na kuacha walio werevu
- kupandisha vyeo watu wasiostahili
- kazi kufanywa vibaya bila uajibikaji

***zozote 2 x 1 = 2***

c) - kuunda tume na kamati za kuchunguza visa vya ufisadi
- kurudisha mali iliyoibiwa
- kuwashtaki uhalifu

***3 x 1 = 3***

d) - uhaba wa kazi
- uozo wa maadili katika jamii
- kuongezeka kwa umaskini
- tamaa ya anasa na starehe
- uongozi mbaya wa kitaifa
- kukosa huruma na uajibikaji

- kukosa uzalendo ***zozote 2 x 1 = 2***

e) hongo / chai / kadhongo / kuzunguka mbuyu

f) i) kuenea kwa jambo au habari
ii) walioumizwa / waliodhuriwa
iii) ona wivu

***1 x 3 = 3***

**2.** a) Fupisha aya tatu za mwanzo (maneno 70)

**Jibu**

***Rasimu ya kwanza***

- tatizo la njaa limekuwepo kwa muda mrefu na limekithiri
- wananchi wengi hutegemea kilimo
- kilimo hutegemea mvua isiyotabirika
- bidhaa za ukulima zimekuwa ghali
- sehemu kubwa ya ardhi ni kame na haiwezi kutumika kwa kilimo
- mazao yanahifadhiwa vibaya
- kuna vita vya kikabila
- mazao ya wakulima hununuliwa kwa bei ya chini
- kutozuia mmomonyoko wa udondo
- serikali inakosa sera mwafaka
- kuna shida ya kutegemea misaada ya chakula

***Jibu kamili***

Tatizo la njaa limekuwepo kwa muda mrefu na limekithiri kwa kuwa wananchi wengi hutegemea kilimo ambacho pia hutegemea mvua isiyotabirika. Bidhaa za ukulima zimekuwa ghali na sehemu kubwa ya ardhi ni kame na haiwezi kutumika kwa kilimo. Mazao ya wakulima hununuliwa kwa bei ya chini na mmomonyoko wa udongo hauzuiwi ipasavyo. Serikali haina sera mwafaka na kuna shida ya kutegemea misaada ya chakula (maneno 72)

<u>Maelezo</u>

Zingatia hoja zote muhimu na uandike jibu lako kwa kuzingatia upatanisho wa

kisarufi na maendelezo sahihi ya maneno.

b) Fupisha aya mbili za mwisho (maneno 60)

**Jibu**
***Rasimu ya kwanza***

- tatizo la njaa linaweza kutatuliwa kwa kuwaelimisha wakulima kuhusu mbinu bora za ukulima
- kuwapa wakulima mbegu zitakazohimili kiangazi
- ukulima wa kunyunyizia mimea maji uzingatiwe
- mazao yahifadhiwe vizuri
- ardhi isiyotumiwa itolewe kwa kilimo
- wakulima waelimishwe kuhusu umuhimu wa kuzuia mmomonyoko wa udongo na jinsi ya kufanya hivyo
- mazao yanunuliwe kwa bei nafuu
- serikali iwe na sera mwafaka za kukabiliana na tatizo hili

***Jibu kamili***
Tatizo la njaa linaweza kutatuliwa kwa kuwaelimisha wakulima kuhusu mbinu bora za ukulima, kuwapa wakulima mbegu zinazohimili kiangaza kwa kuzingatia ukulima wa kunyunyizia mimea maji. Pia, mazao yahifadhiwe vizuri, ardhi isiyotumika itolewe kwa kilimo na wakulima waelimishwe kuhusu umuhimu na jinsi ya kuzuia mmomonyoko wa udongo. Isitoshe, mazao yanunuliwe kwa bei nafuu na serikali iwe na sera mwafaka za kukabiliana na tatizo hili. (maneno 63)
***6 x 1 = 6 + 1 (mtiririko) = 7***

***<u>Maelezo</u>***
Zingatia hoja zote muhimu na uandike jibu lako kwa kuzingatia upatanisho wa kisarufi, uakifishaji na maendelezo sanifu ya maneno. Hakikisha umetumia lugha ya nathari (ya mtiririko)

**3. MATUMIZI YA LUGHA**

a) i) |d| ghuna
ii) |t| sighuna ***alama 2***

b) i) mbwa, mbweha, kinywa
ii) oa, ua ***alama 2***

c) Chaka hili halizai ua jeusi ***alama 2***

d) D<u>a</u>da a<u>liinu</u>ka na a<u>kaketi</u> <u>nje</u> <u>ya</u> nyumba. ***alama 2***

e) Ijapokuwa ni mgonjwa - kishazi tegemezi
tutamwandalia karamu leo - kishazi huru ***alama 2***

f) <u>Ki</u>toto - kuonyesha udogo
<u>Ki</u>jinga - kuonyesha kielezi ***alama 2***

g) i) Mahali <u>mle</u> mnavutia - (kivumishi)
ii) <u>Mle</u> mnapendeza (kiwakilishi)
iii) Ingieni <u>mle</u> chumbani au ingieni chumbani <u>mle</u> (kielezi)

h) Jiti lililokuwa limebebwa na jivulana lilivunjika ***alama 2***

i) Nyumba - shamirisho kipozi
Atieno - shamirisho kitondo

matofali - shamirisho ala

k) Chagizo ni neno au maneno ambayo hueleza zaidi kuhusu kitendo
Mkulima hodari zaidi atatuzwa kwa bidii yake

i) Kuandika tarehe
Neno ambalo halijakamilika
Kuunga maneno na kujenga neno moja
Kugawa kuonyesha silabi za neno
***Mwalimu atathmini sentensi***

m) "Kuna umuhimu kuwatii wazazi wenu" Mwalimu aliwasisitizia wanafunzi"
"Hili litaongeza siku zenu duniani"

n) Mfano: Sisi twala chakula
Watoto wacheza

***Mwalimu atathmini jibu la mwanafunzi***

o) walikuwa - vitenzi vishirikishi vikamilifu
wangali

walikuwa wangali
Tn t t
pia ni vitenzi sambamba

p) Wachezaji wachezao kwa bidii ndio wafauluo maishani

q) Jiwa

r) Wadudu wanaotusumbua hapa kwetu nyumbani watamalizwa na dawa niliyonunua

**ISIMUJAMII**

a) Hii ni sajili ya michezo ***alama 2***

b) Sifa za sajili ya michezo
- lugha changamfu / ucheshi
- lugha isiyozingatia sarufi
- vijalizo - maelezo ya ziada kuhusu mambo yalivyokuwa uwanjani
- lugha ya kijazanda
- matumizi ya msamiati wa kimachachari : lugha yenye ladha / mvuto
- matumizi ya istilahi- maneno maalum ya kimichezo k.m. kupenya, viunzi
- kuchanganya lugha
- lugha ya wasifu - kutaja sifa za wachezaji
- matumizi ya lugha ya kasi
- matumizi ya chuku
- taharuki ya michezo
- matumizi ya takriri
- matumizi ya sentensi fupifupi
- lugha ya moja kwa moja
- matumizi ya sentensi zisizokamilika ***alama 8***

# FRIENDS SCHOOL KAMUSINGA
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

**1.** a) Pindu - kifungu katika mshororo wa mwisho wa ubeti kuanza ubeti mpya
*1 x 2 = 2*

b) - kuonyesha kuwa mja hana nguvu
- amekumbwa na masaibu
- Mungu amtoea katika giza
- Mungu ampe maisha mema

*3 x 1 = 3*

c) - beti tano
- tarbia - mishororo minne katika kila ubeti
- vina vya kati na vya mwisho - vinabadilika katika kila ubeti
- idadi ya mizani 8, 8 = 16 (kila mshororo)
- kibwagizo - hakuna - kuna kiitikio na kimailizio
- mishororo ina vipande viwili

*zozote 4 x 1 = 4*

d) Inkisari
- nondolea
- zilonifunga
- mazida - mfano - muokozi

Kuboronga sarufi - igeuze yangu nia
Tabdila - Afia
*kutaja - 1*
*mfano - 1*
*zozote 2 x 2 = 4*

e) Kiumbe wako nimeteseka mno. Naomba unipe afueni na unirehemu. Ninaomba nikikusudia. Wewe ndiwe muumba unayeweza kunipa niyahitajiyo

*4 x 1 = 4*

f) i) Nimeteseka au ni taabani
ii) Nimulikie, niletee nuru
iii) nichangamke au nistarehe moyoni

*1 x 3*

**2.** "Vipi binadamu anavyoweza kuyazoa maji yaliyomwagika?"

a) i) Haya ni maneno ya Mwanaheri
ii) Akimwambia Kairu na Umu
iii) Walikuwa katika shule ya Tangamano
iv) Ni baada ya kukutana na kuanza kusimuliana kuhusu yaliyowafika hadi wakakutana pale *alama 4*

b) Swali balagha - vipi, binadamu anavyoweza kuyazoa maji yaliyomwagika ? *alama 2*

c) Sifa tatu za msemaji (Mwanaheri)

i) Mwenye mawazo mapevu. Mama yake angetafuta suluhu kwa mgogoro kati yake na wakwe zake badala ya kujiua
ii) Mwenye busara - anaamini kuwa hakuna haja ya kushughulikia mambo ambayo hawezi kuyabadilisha
iii) Mwenye bidii - anatia bidii shuleni. Anafuata ushauri wa mwalimu Dhahabu kwamba elimu itamletea mabadiliko

d) **Hakiki jinsi binadamu alivyomwagikiwa na maji katika riwaya**
i) Lunga kumwagikiwa na maji pale anapoachwa na mkewe Naomi
ii) Umu na nduguye wanamwagikiwa na maji kwa kuachwa mayatima wakati Lunga anapoaga
iii) Ridhaa anamwagikikwa na maji wakati anapoipoteza aila yake yote isipokuwa Mwangeka
iv) Mwangeka anamwagikiwa na maji kufuatia kifo cha mkewe na mtoto wake
v) Zohali anamwagikiwa na maji pale anapotungwa mimba katika umri wa ujana na kupelekea afukuzwe shuleni na kuteswa na wazazi
vi) Waafrika wanamwagikiwa na maji pale wanapokatazwa na wakoloni kulima mazao yaletayo fedha huku ikiwalazimu kufanya vibarua kwao
vii) Baadhi ya vijana wa rika la Tuama wanakufa baada ya kupashwa tohara
viii) Hospitali inamwagikiwa na maji pale Selume analalamikia ukosefu wa mwangaza, ukosefu wa glavu na deni kutokana na usimamizi duni
ix) Wakaazi wa msitu wa mamba wanaharibikiwa pale wanapofurushwa huku vyakula walivyolima vikiibiwa na viongozi
x) Vijana barobaro wanaotumiwa na wanasiasa kuandamana wanamwagikiwa wa maji pale wanapomiminiwa risasi vifuani wa walinzi huku wakiuawa
xi) Kitoto kinachookotwa na Neema kilimwagikiwa na maji pale kilitupwa na mama mzazi badala ya kukilea
xii) Ridhaa anasimulia mwanawe Mwangeka vile walivyobomolewa nyumba zao kwenye mtaa wa Zari, hawakupewa fidia yoyote nao wale waliowauzia viwanja hivi waliingia mitini
xiii) Lunga kufutwa kazi na mkurugenzi kwa kupinga mradi wa ununuzi mahindi

*zozote 11 x 1 = 11*

3. **Fafanua changamoto zinazoikabili jinsia ya kike katika riwaya ya Chozi la Heri**

i) Matusi na vitisho - Bwana Maya alipoulizwa maswali na mkewe alimpiga makonde, kumpa vitisho na matusi. Aidha, anaselea kumwuliza sababu za kuhusiana ngono na bintiye Sauna

ii) Kubakwa - Sauna anababakwa na babake wa kambo Bwana Maya. Mamake naye anamsaidia kuavya mimba hiyo

iii) Ndoa za mapema - Pete baada ya kupashwa tohara anaozwa kwa mzee Fungo kwa lazima. Nyanyake anajaribu kumtetea lakini hakufaulu

iv) Kukatizwa elimu - kiu yake Pete ya kuendelea kusoma inakatizwa baada ya ndoa ya lazima kwake bwana Fungo

v) Waume zao kukosa uaminifu katika ndoa - Mfano Bwana Tenge anashiriki ngono na wanawake wengi wakati Bi Kimai yuko kijijini

vi) Uongozi / ushindi wake kudunishwa - ushindi wake Mwekevu unadhalilishwa na mpinzani wake kuandaa maandamano ili kupinga kuchaguliwa kwake

vii) Kutelekezwa - mfano ni Chandachema anayeondoka kwa jirani yake baada ya kulalamikia vitu vidogo vidogo kuonyesha kutoridhika kuishi naye. Aidha Zohali anatelekezwa na wazazi wake na kuishia kuwa ombaomba mjini

viii) Mazingira duni ya kazi - Subira anafanya kazi katika mazingira duni yasiyo na nguvu za umeme pia kukosa vifaa muhimu vya kufanyia kazi

ix) Kufukuzwa shuleni - Zohali anafukuzwa shuleni baada ya kupata mimba

x) Tamaa ya maisha ya juu - mfano ni Sally mpenziwe Billy anayemtaliki kwa kujengewa chumba kama tundu la ndege. Aidha Naomi mkewe Lunga anamtaliki kwa kuona uduni wa maisha yao baada ya Lunga kufutwa kazi

xi) Kujitia kitanzi - Subira baada ya kumtoroka mumewe anakunywa sumu kwenye chumba huku amejifungia

xii) Utasa - Neema, mkewe Mwangemi anakosa mtoto hivyo kumpanga Mwaliko

xiii) Ujane - Rachael Apondi ni mjane wa Mandu. Hivyo anaposwa na Mwangeka baadaye

xiv) Kifo - Lilly Nyamvula, Anatila, Becky na mkewe Ridhaa wanaangamia katika mkasa wa moto kwenye jumba kubwa lake Ridhaa baada ya ghasia za uchaguzi kuzuka

xv) Simango la wanafamilia - jamaa zake Kaizari hawakukoma kumwita Subira mwizi wa mali yake mumewe na jamaa zake. Hivyo anamtaliki Kaizari.

xvi) Umaskini - Umaskini wake Chandachema unamfanya kufanya kazi duni. Aidha, kutokana na umaskini wake Sauna, unamfanya ashiriki biashara mbovu ya utekaji nyara kwa watoto na kuwa kijakazi

xvii) Taasubi ya kiume - Jinsia ya kiume inalenga kudhibiti mwanamke kwa njia zifuatazo :

xviii) Kumposa mapema - Pete kwa Fungo

xix) Kumbaka mwanamke mfano: Maya kwa Sauna

xx) Kutodhamini ushindi wa mwanamke - mfano ushindi wake Mwekevu kudhalilishwa

xxi) Kupata watoto nje ya doa - mfano ni Kairu anazaliwa nje ya ndoa na babake ni tajiri

xxii) Kushiriki ngono nje ya ndoa - Bwana Tenge anashiriki ngono na wake wengi wakati mkewe yuko mashambani

xxiii) Walimu kushiriki ngono na wanafunzi wa kike - mfano mwalimu Fumba kwake

Rehema na kumzaa Chandachema

xxiv) Mwanamume mmoja mpita njia kumsimanga Neema aache kujishughulisha na kile kitoto kwenye biwi kwani wamepata wengi pale

xxv) Askari kumuuliza Umu maswali yenye kuudhi kwenye kituo cha polisi

xxvi) Mzee Fungo kutoonekana akijishughulisha naye Pete baada ya kurudi kwa mke wa kwanza. Anampa uhuru wa kuondoka. Anamwita 'Mwanakwenda'

xxvii) Kaango kumuoa Akelo Kiriri pindi tu anapokamilisha masomo yake ya kidato cha nne

xxviii) Bi Kangara na mumewe kufanya biadhara haramu ya kuwateka nyara mabinti na kuwapeleka ndanguroni

xxix) Biashara duni - baadhi kama vile Sauna wanafanya biashara duni ya utekaji nyara na ujakazi. Aidha, Chandachema anachuna majani chai ili kulipa karo na mahitaji ya kimsingi. Aidha, Pete anashiriki ukahaba jijini

*zozote 20 x 1 = 20*

**4.** a) **<u>Eleza muktadha wa kauli hiii</u>**

i) Haya ni manno ya Kenga

ii) Akimwambia Majoka

iii) Wakiwa ofisini mwa Majoka

iv) Ni baada ya Majoka kusoma habari gazetini zinazoonyesha umaarufu wake Tunu wa kupigiwa kura

*4 x1 = 4*

b) Jazanda - "Ukitaka kumfurusha ndege kata mti" (kuwaua wanaompinga Majoka)

Taswira - kutaja 1 mfano *2 x 1 = 2*

c) **<u>Onyesha jinsi wahusika kadha walivyofurushwa kama ndege</u>**

- Majoka anampangia Jabali kifo ambaye ni kiongozi wa upinzani kwa kupinga utawala wake potovu
- Majoka anadhihirisha uuzaji wa sumu ya nyoka kwa wanafunzi wa shule jambo linalosababisha wawe makabeji
- Tunu aliponea pale Mzee Marara alitaka kumbaka katika umri mdogo
- Mama Pima anawauzia vijana pombe haramu inayosababisha vifo na upofu
- Sudi anafurushwa pale mkewe anafungiwa na Majoka. Sudi anapitia wakati mgumu kwani watoto wake wanakosa mlezi na kuwapeleka kwao Tunu. Ashua anaumizwa na walinzi
- Ngao Junior kwa matumizi ya sumu ya nyoka anazirai na kukata roho katika uwanja wa ndege
- Majoka anaifanya familia yake Tunu kuwa na wakati mgumu wa kupata bima ya kugharamia kifo cha babake kilichotokea kwenye kampuni yake ya Majoka na Majoka Company
- Ngurumo anafurushwa pale anaponyongwa na Chatu akitoka ulevini
- baadhi ya waandamanaji wanauawa na wengine kujeruhiwa wanapotetea haki zao
- familia ya Hashima wanarushiwa karatasi za kuamrishwa wahame Sagamoyo. Wanafahamishwa kuwa Sagamoyo si kwao
- Majoka anaidhinisha ukataji wa miti unaosambabisha ukame
- Majoka anafurushwa kama ndege pale watetezi wa haki wanapindua uongozi wake
- wasomi wanafurushwa pale wanakosa kazi hata baada ya kuhitimu. Wanaishia kufanya kazi duni

*zozote 12 x 1 = 12*

**5.** - Mauaji ya kiholela - Jabali
- vitisho kwa wananchi - Chopi
- unyanyasaji wa wananchi - kutozwa kodi kupita kiasi
- unyakuzi wa ardhi ya umma - soko la Chapakazi
- kutiwa jela bila sababu - Ashua
- kugawanya watu kwa matabaka - matajiri na maskini
- kukatika juhudi za ukombozi - Tunu
- viongozi wanaendeleza ufisadi
- viongozi kutumia propaganda
- matumizi ya vyombo vya dola kukandamiza wananchi
- kuendeleza biashara haramu (kutoa kibali) kwa Mama pima
- uongozi wa kiimla
- viongozi hawataki kutoka uongozini
- kukosa ajira - Ashua alikuwa amesomea ualimu
- viongozi kutumia vyeo vyao kuendeleza biashara haramu kama vile dawa za kulevya
- viongozi kuomba ufadhili kutoka nchi za magharibi kufadhili miradi isiyofaa - uchongaji wa vinyago
- uchafuzi wa mazingira - ukataji wa miti
- viongozi kutumia mamlaka yao kuharibu ndoa za watu - ndoa ya Sudi na Ashua
- viongozi hawachukui hatua kwa wanaoleta vurugu
- viongozi kuzawadi vikaragosi wanaounga mkono uongozi mbaya
- ubadhirifu

*zozote 20 x 1 = 20*

**6.** a) **Mapenzi ya kifaurongo**

i) Ndoa iliyotarajiwa ya Dennis na Penina ilitawaliwa na unafiki. Penina anamjia Dennis na wazo la kuwa wapenzi bila kuzingatia hali duni ya familia yake. Dennis anapokosa ajira anamfukuza
ii) Inatawaliwa na kuhimiliana
iii) Imetawaliwa na kukata tamaa - Penina anakata tamaa baada ya Dennis kukosa kazi
iv) Imezingirwa na utabaka wa kiasili
v) Mapenzi hukua, huugua na hufa*5 x 1 = 5*

**Masharti ya kisasa**

Ndoa ya Dadi na Kidawa

i) Ndoa inayodhibitiwa na masharti
ii) Ndoa ya kugawana majukumu
iii) Ndoa ya kupanga uzazi
iv) Ndoa inayoruhusu mwanamke kufanya kazi. Kidawa anafanya kazi ya umetroni usiku na kuuza bidhaa mtaani
v) Baadhi ya watu huingilia ndoa za wenzao kama njia ya kuona mapenzi yamevunjika baina ya wanandoa husika *5 x 1 = 5*

**Mtihani wa maisha**

- wazazi wa Samuel ni wenye mapenzi wanaonyesha mapenzi kwa mtoto huyu wao kwa kumpeleka shuleni akajipatie elimu
- Samuel anaonyesha mapenzi kwa Nina. Kwa muda amekuwa mpenziwe
- Nina anaamini kuwa mwanaume huyu ni bingwa kutokana na kudanganywa alikodanganywa na mwanaume huyu
- mamake Samuel ana mapenzi ya dhati kwake, baada ya Samuel kujaribu kujitoa uhai mamake anamsihi waende nyumbani "Twende zetu nyuumani mwanangu."

*zozote 4 x 1 = 4*

**Ndoto ya Mashaka**

i. Kuna ndoa ya Mashaka na Waridi
ii. Kuna ndoa ya mtumwa na mumewe mzee Rubeya
iii. Tatizo la kwanza ni ndoa ya kulazimishwa. Mashaka na Waridi walitoka kwenye matabaka mawili tofauti
iv. Waridi - tabaka la kitajiri
v. Mashaka - tabaka la maskini
vi. Kuna kutohusisha wanawake katika ndoa. Mamake Waridi hakuhusishwa katika harusi
vii. Ndoa inakumbwa na tatizo la malazi bora - upendo, kujikubali, ukosefu wa taasubi ya kiume
viii. Kuna changamoto zinazojitokeza baada ya kifo cha mmoja. Mashaka anawachwa yatima
ix. Kuna utengano katika ndoa. Waridi anatengana na mumewe kutokana na hali ngumu ya kiuchumi

*zozote 6 x 1 = 6*

**7.** a) Maneno haya yanasemwa na Mbura
- alikuwa anazungumza na Sasa
- walikuwa kwenye sherehe iliyoandaliwa na mzee Mambo
- walikuwa wanazungumza kuhusu 'kula kwao'

*4 x 1 = 4*

b) **Sifa za Mbura**
- ni mzalendo - anafanya kazi kwa bidii katika wizara yake kama njia ya kuonyesha uzalendo
- mwenye tamaa - anajaza sahani kwa chakula na kukila chote
- mwenye utu - anataka wananchi wale kwa niaba ya viongozi kama vile wao wamekuwa wakila kwa niaba yao
- ni fisadi - amepokea kazi kwa afisi ya serikali kwa njia isiyo halali
- mzembe - baada ya kula sahani tatu za vyakula kwenye sherehe analala usingizi mzito badala ya kwenda kazini
- mletezi wa haki - mvumilivu
  - mpyoro
  - msema kweli

*zozote 6 x 1 = 6*

c) **<u>Jinsi viongozi walivyo wabadhirifu</u>**
- hulipwa mishahara mikubwa sana na serikali jambo linalochangia ubadhirifu wa mali ya umma
- sherehe kubwa za viongozi wa kiserikali huchangia pakubwa ubadhirifu
- viongozi hutumia raslimali za nchi kwa manufaa yao ya kibinafsi - magari ya serikali
- raslimali zilizotumiwa katika kuvinunua vyakula na vinywaji vingetumika katika kuendeleza asasi tofauti za kijamii
- DJ na wenzake wanapata mabilioni ya fedha kutokana na kuwatumbuiza wageni katika kama hizi
- viongozi wanawachukua baadhi ya watu wao wa karibu na kufanya juu chini kuona kwamba wanajifaidi na mali na raslimali za wananchi pasipo kuzitolea jasho kamwe
- upeperushaji wa matangazo katika vyombo vya habari ya sherehe za kiongozi binafsi ni njia ya kuendeleza ubadhirifu wa raslimali za umma
- Mbura ana Sasa wanaendeleza ubadhirifu pale wanapoamua kuchukua vyakula kupita kiasi katika sherehe za mzee Mambo
- kuwaajiri viongozi wawili wenye nyadhifa sawa katika sekta tofauti za umma
- vibaraka na vikaragosi kupewa mali ambayo ingewafaidi wananchi

*zozote 10 x 1 = 10*

**8.** a) **Miviga ni sherehe maalum za kitamaduni zinazoambatanishwa na nyimbo na ngoma** ***2 x 1 = 2***

b) **<u>Sifa za miviga</u>**
- huambatana na utamaduni
- huongozwa na watu maalum
- hufanywa mahali maalum - mwituni
- hufanywa kwa utaratibu maalum
- kuna kula kiapo
- hufanywa wakati maalum - kutawazwa viongozi, harusi, mazishi
- huambatana na mawaidha
- kuna kutolewa kafara

*zozote 6 x 2 = 12*
*kutaja - 1, kueleza - 1*

c) - Huburudisha
- huelimisha
- huelekeza
- hukuza mila na desturi
- huhifadhi historia ya jamii
- hutambulisha jamii
- huandaa wanajamii kukabiliana na hali ngumu
- njia ya kupitisha maadili kutoka kizazi kimoja hadi kingine
- huonyesha imani za kidini za kijamii
- huonyesha matarajio ya wanajamii

*zozote 6 x 1 = 6*

# NAIROBI SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)
## Mwongozo wa Kusahihisha

1. **Ni insha ya kiuamilifu**
   Sura ya mahojiano izingatiwe ifuatavyo:
   -Kichwa- iandikwe kwa herufi kubwa na ipigiwe mstari
   -Kuwe na wakuuliza maswali
   -Anayejibu maswali
   -Masolugha na vitendo vionyeshwe kwa mabano
   -Mtiririko unaofaa uzingatiwe
   -Tumia nukta pacha kutenganisha majina na semi zawahusika

   **Vyanzo vya malalamishi**
   - ✓ Baadhi ya wawaniaji kuwahonga wapiga kura
   - ✓ Vifaa vyakielektroniki vilivyofeli
   - ✓ Baadhi ya wawaniaji kutumia raslimali za umma kuchapa kampeni
   - ✓ Wapiga kura kuchukua muda mwingi kwenye foleni
   - ✓ Muda mchache wakuchapa kampeni
   - ✓ Baadhi ya maafisa kukosa uaminifu na kuegemea mrengo Fulani wakisiasa

   **Suluhu**
   - ✓ Wanaowahonga wapiga kura wahukumiwe
   - ✓ Vifaa vichunguzwe vizuri kabla ya zoezi kama hilo kufanyika
   - ✓ Wanaotumia raslimali za umma kuchapa kampeni wachukuliwe hatua kali kisheria
   - ✓ Vituo vya kupigia kura viongezwe
   - ✓ Muda wa kampeni uongezwe
   - ✓ Maafisa wanaoegemea mirengo ya kisiasa waajiriwe
   - ❖ Hoja zisipungue sita
   - ❖ Mwanafunzi aliye na hoja chini ya sita asituzwe zaidi ya alama kumi
   - ❖ Sehemu zote mbili za swali zishughulikiwe yaani, vyanzo na suluhu. Mwanafunzi akishughulikia sehemu moja asituzwe zaidi ya alama kumi.
   - ❖ Sura izingatiwe. Isipo, mwanafunzi aondolewe alama mbili za sura baada ya utuzaji.

2.
   - ✓ Ni insha ya kufuata mkondo mmoja.
   - ✓ Mwanafunzi atoe hoja zake aya baaada aya na zifafanunuliwe vizuri.

- ✓ Hoja zisipungue sita, iwapo zitapungua mwanafunzi asipate zaidi ya alama 10
- ✓ Mwanafunzi ajikite nchini, asipojikita apate bakshsishi alama 2

**Namnayakuimarishausalama**

- ❖ Kuwaajiri walinda usalama
- ❖ Mfumo wanyumba kumi
- ❖ Kuwe kataa mijini
- ❖ Wahalifu washikwe nakuchukuliwa hatua kisheria

- ❖ Askari zaidi kupewa mafunzo kuhusu usalama
- ❖ Vijana wanaoshiriki wapewe kazi

**3. Mkokoto wajembe si bure yao**

- ✓ Mkokoto ni alama iliyoachwa na kitu kilicho burutwa
- ✓ Maana- mtu anayeshinda akilima au akifanya kazi ya kulima japo polepole hakosi kuambulia patupu
- ✓ Matumizi- methali hii hutumiwa kutunasihi tujibidiishe kufanya kazi hata kama ni kwa hatua za polepole hatimaye tutafanikiwa
- ✓ Katika insha hii lazima mwanafunzi apeane maana ya methali. Asimulie tu kisa kinachodhihirisha maana ya methali
- ✓ Sehemu zote mbili za methali zizingatiwe na mwanafunzi asipo, asipewe zaidi ya nusu alama zilizotengewa swali
- ✓ Baadhi ya visa ni kama vile: mtu aliyejibidiisha kufanya kazi hata kama ilikuwa ya polepole na mwishowe akafanikiwa.

4.

- ✓ Ni mdokezo wa kutamatisha
- ✓ Mwanafunzi ahahakikishe ametamatisha kwa maneno aliyopewa. Asipo,
- ✓ Katika insha msimulizi aweze kusimulia kuhusu kijana/vijana ambaye alijiingiza au waliingizwa na vijana wengine kwa mambo maovu kama vile:
  -Madawa ya kulevya
  -Wizi
  -Kundiharamu
- ✓ Na akaathirika vibaya na ndiposa watu walioshuhudia athari hiyo kwa kijana au vijana hao wanakubaliana kuwa vijana washirikishwe kwa ujenzi wa kitaifa kwa labda kupewa kazi.

# Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha
# Mwongozo wa Kusahihisha

## 1. UFAHAMU

a) Kadiria – mfano: kuhamia mjini

Kichwa kihusiane na taarifa
1×1=1

b) Mvulana 1×1=1

c) Katika kupumzika kwake aliwasaidia wazazi wako kuchunga ng'ombe na mbuzi ili apate kuwa vichakani peke yake
2×1=2

d) Ulimfanya aimbe kwa sauti ya juu au kimya kimya na pengine kusinzia na kuota ndoto za hamu yake
2×1=2

e) –Angekosa fursa ya kupumzika mwituni

-Kutengana na mifugo wao ambao kwa muda mrefu alifanya urafiki nao
2×1=2

f) Alijitolea kusoma hadi ukomo wa masomo
2×1=2

g) i) kuwa na haki ya jambo/nastahili
1×1=1

ii) kupelekwa kwa maombi ya kutaka kuoa
1×1=1

iii) mwisho 1×1=1

## 2. UFUPISHO


a)

- ✓ maradhi ya kipindupindu yameripotiwa sehemu mbalimbali
- ✓ watu zaidi ya sita wameripotiwa kufariki na wengine kulazwa hospitalini
- ✓ maradhi yana changiwa na maji ama chakula chenye vidudu vya kolera
- ✓ mtu huharisha maji maji na kutapika

- ✓ si mara ya kwanza Kenya kuyashuhudia
- ✓ visa vingi viliripotiwa kati ya Desemba 2014 huku kukiwa na vifo vingi nchini
- ✓ chama cha madaktari cha sema mkurupuko wa kipindupindu ni ishara ya kasoro kwa mfumo wamatibabu
  Hoja 7×1=7

b)

- ✓ wanaohusika na afya ya umma kushughulika mapema
- ✓ wachunguze kiafya wanaopika kando ya barabara na vibanda
- ✓ wananchi wachukue hatua mapema
- ✓ wanaouza mboga wazioshe kwa maji safi
- ✓ wanaoendesha biashara ya maji wauze maji safi
- ✓ wanaonyesha ishara ya kipindupindu watafute tiba mapema
  Hoja 5×1=5




**3.SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA**

a) i) -Mahali pa kutamkia
-Namna ya kutamka
-Mtetemeko wa nyuzi za sauti
2×1=2

ii) /sh/ nikikwamizo ilhali /ch/ nikipasuo kikwamizo 1×1=1

b) Kadiria mradi sentensi hiyo iwe sahihi naiulize swali/taarifa/rai/kuamrisha/mshangao 2×1=2

c) ‘ala - zana
a’la-kihisishi cha mshangao
2×1=2

d) Kundi la sauti amabazo nitofauti na hutamkwa kama sauti moja. Mfanokadiria :

<u>ndi</u>zi
<u>nga</u>mia
je<u>ngw</u>a

2×1=2

e) ni – nafs iya kwanza umoja
-m- mtendwa
-a- kiendelezi
-ye- kirejeshi 4× ½ =2

f) Debe- LI-Ya 1×1=1
Mtaimbo- U-I 1×1=1
g) Mgonjwa anaskia na kusema lolote
1×2=2

h) Maji panya hayo yalinaswa mitegoni na maji nyama makubwa maji domoni

1×2=2

i) i) watalii huvutiwa na wanyama wa pori
1×1=1
ii) wadudu walivamia viota vya ndege 1×1=1

j) Daktari aliuliza, "Je, kuna jamaa wako yeyote ambaye anaugua ugonjwa huu?" 6× ½ =3
k) enyewe katika sentensi sahihi 1×2=2

l)

| S | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| $S_1$ | | | | U | $S_2$ | |
| KN | KT | | | | KN | KT |
| N | T | W | T | | W | T |
| Waswahili | husema | chema | chajiuza | ø | kibaya | chajitembeza |

m) Amani inatishiwa kuangamizwa hivi karibu ni kwa ongezeko la visa vya uhalifu. 1×2=2
n) Kadiria mfano: juu ya meza
karibu na kiti
kando ya barabara 1×2=2
o) Tangu awasili kutoka marekani- Ṡ.tegemezi
amewasaidia mayatima wengi- Ṡ. Huru
2×1=2
p) – baada ya ufafanuzi mrefu

- kutenganisha vishazi
- kuandika tarehe
-katika usemi halisi
-kutenga maneno yaliyonukuliwa
-katika barua baada ya mtajo/salamu
-hutumiwa baada ya kuhisishi
-katika ushairi kuonyesha vipande
-kuandika tarakimu 2×1=2

q) Mwanamwali- shamirisho kitondo
nyusi- shamirisho kipozi
wanja- ala
taratibu- chagizo zozote 2×1=2

r) Mfa maji haachi kutapatapa
1×1=1

**4. <u>ISIMU JAMII</u>**

a)
- ✓ Kuwepo kwa idadi ndogo ya wazungumzaji
- ✓ Ndoa za mseto ambapo lugha moja husahaulika
- ✓ Mielekeo hasiya watu kupendelea lugha moja na kudharau nyingine
- ✓ Sera za lugha katika taasisi na nchi kwa kupendelea lugha moja
- ✓ Uhamiaji ya watu mjini na kuacha kutumia lugha yao ya kwanza
- ✓ Athari ya elimu ya kisasa kwasababu taaluma hutekelezwa kwa lugha moja dhidi ya nyingine zozote 3×1=3

b)
- ✓ Humsaidia msemaji kutambua makosa yanayojitokeza wakati lugha inazungumzwa
- ✓ Hudhihirisha sifa na utamaduni wa watu
- ✓ Husaidia kuthibiti tabia na mienendo ya watu
- ✓ Huwafunza watu kaida za lugha
- ✓ Humsadia mzungumzaji kutumia lugha kwa ufasaha
- ✓ Hufunza jinsi ya kuwasiliana
- ✓ Huwasidia watu kuelewa sajili za lugha
- ✓ Humsadia mzungumzaji kutumia lugha kwa ufasaha zozote 4×1

c)
- ✓ Kuchanganya msimbo
- ✓ Kuna utohozi wamisamiati

- ✓ Msamiati wa kandanda
- ✓ Kauli fupifupi
- ✓ Kupiga chuku
- ✓ Maelezo yanayojenga taswira
- ✓ Lugha isiyo rasmi
- ✓ Kukatiza na kauli zozote 3×1=3

# NAIROBI SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

**1."Lakini itakuwaje historical injustice, nawe Ridhaa, hapo ulipo sicho kitovu chako?"**

***a. Eleza muktadha wa dondoo***

Hayo ni maneno ya Ridhaa yaliyokuwa yakimpitia mawazoni baada ya kumjibu Tila. Walikuwa kwa jengo au gofu la Ridhaa.Hii ni baada ya Ridhaa kukubali maneno ya Tila ya hapo awali. Inadhihirika kuwa amekubali kuwa yeye ni mgeni,si mwenyeji.

***b.Eleza tamathali mbili za lugha zilizotumika kwenye dondoo hili(alama4)***

Swali la balagha-...hapouliposichokitovuchako?
Kuchanganya ndimi-historical injustice.
Jazanda/ istiari- kitovu
Uzungumzi nafsia/monolojia

***c.Fafanua umuhimu wa msemaji wa maneno haya(alama6)***

Msemaji wa Maneno haya ni Ridhaa.
Umuhimu wake.

Ridhaa ametumiwa na mwandishi kutuonyesha adhari ya ukabila.
Ridhaa ni kielelezo cha watu wasiobagua watu wengine hakujali wanakijiji wenzake ni wa ukoo gani bali yeye alitekeleza miradi ya maendeleo ilikuwafaidi wote.
Ridhaa ametumiwa kuuonyesha udhalimu wa watu kwa kuhadithia namna majumba yake yalivobomolewa na kuchomwa pamoja na kuangamizwa kwa familia yake.
Ridhaa ni kielelezo cha watu waliosoma na kuneemeka.
Ametumika kukuza wahusika kama vile Tila
Kielelezo cha watu wenye bidi maishani
Ametumika kukuza maudhui ya utu na udhanaishi

***d.Ni mambo gani yaliyowakumba wale ambao kitovu(Alama6)***

Jibu walichomewa nyumba zao kwa mfano Ridhaa alichomewa jumba lake la kifahari.
Watu wao waliuwawa kwa mfano familia ya Ridhaa ilichomwa na Bwana Kedi jirani yao. Walikimbia na kutorokea msituni.
Watoto wao walibakwa kwa mfano mabinti zake Kaizari walibakwa na vijana wenzao.
Walitoroka na kuacha makwao wakawa maskwota au wakimbizi wa ndani kwa ndani.
Kuvunjika kwa ndoa kama vile Subira
Kuzorota kwa afya ugonjwa wa kipindupindu na kisukari

**HADITHI FUPI. TUMBO LISILOSHIBA**

**2. " Usiteketeze umati kama kuni zinavyoteketeza moto. Rudi,rudi kwa Mola wako."**

a) Msemaji wa maneno haya ni Mkumbukwa. Anamweleza Mkubwa. Walikuwa kwake Mkubwa. Baada ya Mkumbukwa kuiasi biashara ya mihandarati na kumwosia Mkubwa.

b) Msemewa ni Mkubwa. Ana sifa hizi.

I. **Mwenye bidii**- alikuwa akishughulisha na kazi ya kuuza pweza wa kukaanga na baadaye akauza kipande cha ardhi ili kuingia uongozini.
ii. **Mwenye utani**- anamtania utingo kuwa huwa haogi jambo lililomfanya utingo kukimia kwa kuchekwa na abiria.
iii. **Ni mtambuzi-** aliweza kuelewa maana ya unga japo hakuwahi tu kuona vituko vyake.
iv. **Mwenye utu**- alimpigapiga kijana mbwia unga aliyekuwa ameinama kama kwamba anarukuu na kumuuliza iwapo anaumwa.
v. **Mwenye tama ya mali**- alipotanabahi namna viongozi wanavyotajirika kwa kuuza unga , maneno 'unga na utajiri' yalimkaa moyoni kiasi chake kukosa usingizi usiku huo.

I. **Ni maskini**- alikuwa akifanya biashara ya kuuza pweza iliyokuwa na kipato kidogo . vilevile kabla ya kupata uongozi, alikuwa na suruali na shati kipande papa
ii. **Ni mfisadi**- baada ya kutia na kutoa, aliamua kufanya biashara haramu ya kuuza dawa za kulevya biashara ambayo huonekana kama ya kishetani. Vile vile alitoa kiasi kikubwa cha pesa ili kuwashawishi wapiga kura kumpendelea na ndipo akaupata ushindi.
iii. **Mwenye msimamo dhabiti**- baada ya kuyatia moyoni maneno aliyopewa na kijana Yule kuhusu utajiri na unga aliamua kutaufuta kwa udi na uvumba na ndipo akamwendea rafikiye kwa jina Mkumbukwa ili ajitome kwenye siasa apate pasipoti ya kidiplomasia.
iv. **Ni msiri**- mwanzoni hakumweleza Mkumbukwa sababu yake kuutafuta uongozi.
v. **Mwenye wasiwasi-** aliogopa kuwa huenda kisomo chake kingemzuia kupata uongozi

c) **Tashbihi-** Usiteketeze umati kama kuni zinavyoteketeza moto
**takriri/uradidi-** rudi rudi

d) ***mambo aliyoyatenda***

Amevitenda vitendo vingi viovu kama vile ;

i. kuuza dawa za kulevya ambayo ni biashara haramu.
ii. Kutoa hongo ili apate uongozi.
iii. Kumtapeli rafiki yake Mkumbukwa na kumuingiza katika uuzaji wa dawa za kulevya.
iv. Kutumia pasipoti ya kidiplomasia vibaya.
v. Kuwaharibu vijana kwa kuwauzia dawa za kulevya

***3. Huku ukirejelea hadithin ya Tumbo lisiloshiba na Shibe inatumaliza, fafanua maudhui ya ukiukaji wa haki***

**Tumbo Lisiloshiba.**

i. Viongozi kuweka vitego na vikwazo vya sheria ili watu wadogo wasiweze kutetea mali zao.
ii. Kutowahusisha maskini katika maamuzi muhimu yanayoathiri maisha yao.
iii. Kunyakua ardhi ya madongoporomoka ambapo watu maskini waliishi.
iv. Kupanga njama za kuwapatia wanyonge visenti vichache ili waondoke madongoporomoka. 188
v. Jitu la miraba mine kula chakula chote bila kubakishia wateja.
vi. Wanamadongoporomoka kubomolewa vibanda vyao na mabuldoza.
vii. Askari wa baraza kutimua watu waliokuwa wanabomolewa .
viii. Jeshi la polisi kulinda askari wa baraza wakibomoa vibanda vya wanamadongoporomoka.
ix. Askari kuwapiga virungu watu.
x. Kueneza zisizo za ukweli
xi. Mawakili kuwalaghai watu wanaodai haki

**Shibe Inatumaliza.**

i. Mzee mambo kulipwa kwa vyeo viwili alivyovifanyia kazi.
ii. Waajiriwa kwenda kazini na kukosa kufanya kazi.
iii. Viongozi kuibia wananchi kwa kujipakulia mshahara

iv. Waajiriwa wawili kufanya kazi moja – Sasa na Mbura ni mawaziri wa wizara moja.
v. Mzee mambo kuandaa sherehe ya kuingiza watoto nasari kwa kutumia pesa za umma.
vi. Mzee mambo kuandaa sherehe kwa kutumia rasimali za nchi- magari, vyakula.
vii. Sasa na mbura kula vyakula vyao na vya wenzao.
viii. Serikali kutafuta mbinu yoyote ile ili kupuja mali ya umma
ix. Wananchi hawana chakula ilihali viongozi wanakula chakula kingi
x. Propaganda- kulazimishwa kufuata sharia za serikali
xi. DJ wa hiyo sherehe kuuziwa na kuuza dawa za raia za hospitali
xii. (20x1=20)

<u>**SEHEMU YA C: TAMTHLIA KIGOGO**</u>

**4. "Oooh bebi, miaka yaenda mbio sana, nayo sura yako inachujuka……"**

***a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)***

i. Ni wimbo wa Kabaka anaouimba Ngurumo.

ii. Anamwimbia Tunu

iii. Wako Mangweni, mahala pa ulevi.

iv. Alikuwa anamdhihaki Tunu na wanaharakati wengine kuwatembelea ili kuwahamasisha kuhusu utawala dhalimu wa Majoka na kuwa ni vyema waupinge.

Hoja zozote 4 x 1 = 4

***b) Mhusika anayehusishwa na wimbo huu ana msimano gani wa kimapindjuzi? (alama 8)***

i. Ana msimano thabiti. Tunu anasimama kidete bila uoga kupambana na udhalimu wa utawala wa Majoka.

ii. Ni mfano bora wa watu wa jamii; kuwajibika na kuchukua jukumu la kuikomboa jamii inayokandamizwa.

iii. Anafanikiwa kushawishi wananchi wasihudhurie sherehe za uhuru na badala yake wakusanyike katika eneo la soko la Chapakazi ili wadai uhuru wa kweli

iv. Mateso ya kupigwa na kudhulumiwa na utawala havikatizi ari yake katika kuleta mapinduzi.

v. Baadaye kutokana na jitihada zake pamoja na wanaharakati wengine, uongozi wa Majoka unaondolewa na soko linafunguliwa tena.

vi. Anakataa kuozwa kwa lazima.

vii. Jasiri hamwogopi Majoka .

viii. Mwanaharakati wa kimapinduzi.

Hoja zozote 8 x 1 = alama 8

***c) Taja sifa zozote NANE za mhusika huyu (alama 8)***

i. Jasiri na mkakamavu.

ii. Mwenye busara.

iii. Mwenye msimamo thabiti.

iv. Ni mzalendo mwenye mapenzi ya dhati kwa nchi yake.

v. Mshawishi.

vi. Mwajibikaji.

vii. Msomi.

viii. Mwenye utu /mkarimju.

ix. King'ang'anizi – aling'ang'ania kudai haki mpaka akaangusha utawala wa Majoka.

x. Mzalendo

xi. Mtetezi

Za kwanza 8 x 1 = Alama 8

***5. Tamthilia ya 'Kigogo' ni kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika.Thibitisha.alama 20***

Kioo ni kifaa ambacho watu hutumia kutazama sura zao. Watu wakiona sura zao zina kasoro fulani hulazimika kurekebisha kasoro hiyo kabla hawajatokea mbele za watu.

Tamthilia ya Kigogo inatumika kama kioo cha uhalisia wa maisha ya jamii nyingi za kiafrika kwa sababu imemulika sura za jamii hizo.

Tamthilia hiyo imeweza kuonyesha kasoro mbalimbali zilizomo katika jamii hizo. Kasoro hizo ni pamoja na:

1. Uongozi mbaya – huu ni uongozi ambo hautilii maanani maslahi ya wananchi wote. Uongozi wa Majoka haujali haki za raia, hauheshimu katiba wala kujali uhuru wa vyombo vya habari.

2. Mauaji ya watu – Katika jimbo la Sagamoyo kuna mauaji ya watu wasio na hatia. Majoka anahusika katika mauaji ya mpinzani wa kiasiasa Jabali. Majoka anapanga njama za kumuua Tunu, kisha Chopi, kuna mauaji ya waandamanaji n.k

3. Usaliti –jimbo la Sagagamoyo limesalitiwa na viongozi walioko madarakani. Badala ya kushughulikia matatizo ya wananchi, wanashughulikia mahitaji yao. Kuna usaliti pia wa ndoa. Mamapima anamsaliti mumewe kwa kushiriki uroda ili apate mradi wa kuoka keki ya uhuru. Hii ni kasoro ambayo inajidhihirisha.

4. Ulipaji wa visasi – kiongozi wa Sagamoyo anaongoza kwa visasi. Anamtia Ashua nguvuni ili alipe kisasi kwa Sudi ambaye hataki kumchongea kinyago.

Aidha, ana kisasi kwa Sudi kwa kuwa ameoa mrembo hurulaini ambaye Majoka alimpenda. Kasoro hii inajibainisha katika uhalisia wa jamii nyingi za Kiafrika.

5. Suala la migogoro – tamthilia hii imebainisha kuwapo kwa migogoro anuwai katika jimbo la Sagamoyo. Kuna mgogoro kati ya kundi la Tunu dhidi ua kundi la watawala. Mgogoro huu unachochewa na kitendo cha Tunu kuongoza Wanasagamoyo kudai haki zao. Suala hili linasawirika katika jamii nyingi za Kiafriaka.

6. Ubinafsi na ukiritimba – Hii ni hali ya mtu kujali mambo yake tu bil kufikiria mambo ya mwingine. Utawal wa Majoka ni wa kibinafsi na ukiritimba. Wanafunga Soko la Chapakazi kwa manufaa binafsi.

7. Ukoloni mamboleo – Ukoloni mamboleo unajitokeza katika mambo yafuatayo. Kwanza, kutegemea misaada kutoka nchi za kigeni ni kuendeleza ukoloni mamboleo. Utawala wa Majoka unapokea mkopo kutoka mataifa ya kigeni. Mkopo huo unatakiwa kulipwa kwa miaka mia moja.

8. Athari za ulevi na dawa za kulevya – jimbo la Sagamoyo limejaa vijana wenye uraibu wa kulewa pombe haramu. Ngurumo na walevi wenzake wanaonekana kuraibu pombe haramu inayouzwa na Mamapima Mangweni. Aidha, wanafunzi katika shule za Majoka and Majoka Academy wna uraibu wakutumia dawa za kulevya.

9. Matumizi ya vikaragosi – vijana walevi wanazugwa akili kuhusu Majoka. Wanataka kumpigia kura na hawataki mtu mwingine. Kura yangu simpi mtu mwingine kama si Majoka heri nimpe paka wake

10. Ufisadi – Ngurumo anadai kuwa watu wa kigogo hupitia pale wakawarushia kitu (wanapewa vijisenti) Vikaragosi wengine kama Kenga anaota ushauri mbaya kwa Majoka ili kujunufaisha. Anafaidi kutokana na kufungwa kwa soko la Chapakazi kwa kutengewa kiwanja. Hoja zingine ni pamoja na

11. Matumizi mambaya ya vyombo vya dola – askari jela kama Chopi ni mpyaro na katili

12. Unyakuzi wa ardhi- Majoka ananyakua uwanja wa soko la Chapakazi ili ajenge hoteli ya kifahari.

13. Kuangamiza wapinzani – Jabali aliuawa kwa hila za Majoka ili asimpinge, aidha chama chake cha Mwenge kikafifia pia.

14. Tenga tawala – Majoka amegawanya watu ili awatawale kwa urahisi. Ngurumo anarejelewa na Chopi kama mtu wetu.

15. Elimu duni – Wanafunzi wanatumia dawa za kulevya na wamekuwa dhaifu – makabeji.

16. Utawala wa kiimla – Majoka anatawala kwa kutumia mabavu.

17. Ulevi – Kule Mangweni kuna vijana kama Ngurumo na mtu wa I na wa II ambo wameathirika mno kwa ulevi; hawana akili razini.

18. Matabaka – Kuna vigogo wenye mali nyingi na walalahoi wasio na mali mfano wachonga vinyago hula makombo ya keki ya uhuru.

19. Ukosefu wa uajibikaji – kuna njaa – kutokana na kufungwa kwa soko watoto wa Sudi wanateseka kwa njaa.

20. Viongozi wanafuja mali ya umma – Kenga anamrubuni Sudi kwa fedha nyingi.

21. Hakuna huduma za afya – Mandhari ya soko ni machafu na Sudi anasema kuwa watu wanasumbuliwa na aina nyingi za ndwele.

22. Uharibifu wa mazingira.

Hoja zozote 20 x 1 = 20

**SEHEMU D: USHAIRI**

**6.** a) Malalamiko /kuonyesha shida /jinsi maskini wanavyodhulumiwa nao wanaojiweza
2x1=2

b) Nafsi neni anadhamiria kuomba wasidhulumiwe nao wanaojiweza
Anadhamiria kutaja /kuangazia shida wanazopitia.

c) Maisha yetu yamekuwa na taabu nyingi.
-Matajiri wanapatikana kila sehemu.
-Vyakula vizuri havipatikani maana matajiri wamevichukua kwa pesa zao.
- Wanaoeleweka, tafadhali tutetee maana matajiri wametukalia vibaya.
1x4=4

d) Inkisari. Tu, ubeti 2. mshororo3 badala ya tuko.
utohozi. lodi (load), ubeti 7, mshororoi.
Mazida .elifeni (elifu) ,ubeti 7, mshororo 3. lx2=2

e)
i) madhnawi- lina vipande viwili(ukwapi na utao)
ii) Ukara ,vina vya ndani vinahadilikabadilika lakini vya nje havibadiliki vinabaki ‘ni’

2x2=4

f) Matajiri
Maskini

Kadiri/wastani (2x3=6)

**SEHEMU E: FASIHI SIMULIZI**

**7.** a)
i) Ngano ni masimulizi yanayotumia wahusika wasiokuwa binadamu. (1)
ii) Visasili ni hadithi zinazoelezea kwa nini viumbe fulani huwa na tabia au maumbile

fulani na Visakale ni masimulizi yanayohusu mashujaa wajamii fulani. (4)

iii) huleta utangarnano wajamii.

- Hukuza lugha.
- Huadilisha jamii.
- Chanzo cha kuheshimiwa.
- Hudumisha tamaduni zinazofaa katika jamii.
- Msingi wa kuteua viongozi bora.
- Hupatanisha maadui.

b)

i) **Umuhimu wa vitendawili**

- Huburudisha na kustarehesha.
- Hufikirisha.
- Huelimisha.
- Huonya.
- Huliwaza.
- Hukuza lugha.
- Hufunza adabu.
- Hukuza ushirikiano.

1x3=3

ii) **Hutaja/huuliza swali na kutoa jawabu**

-Hutumia majina ya mazingira.

-Hutoa onyo /tahadhari.

- Uhusisha watu wengi /makundi ya watu. 1 x 3=3

iii) hutaja /huuliza swali na kutoa jawabu

Hutumia majina ya mazingira.

Hutoa onyo/tahadhari

Uhusisha watu wengi/ makundi ya watu.

iv) Angurumapo simba mcheza nani?

Kiongozi akiamuru, hakuna wa kuuliza au kupinga. 2x 1=2

# MOI GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 1 (Insha)
## Mwongozo wa Kusahihisha

1. **SWALI LA LAZIMA**

Hii ni insha ya kiuamilifu.

Haya ni maandishi ya mtu binafsi kuhusu sifa zake maishani (mambo mazuri ya kumjengea sifa)

**Ya kuzingatiwa katika uandishi wa insha ya aina hii**:-

a) Mada-Hufafanua anayetajwa katika tawasifu hiyo.
b) Nafsi- Huendelezwa katika nafsi ya kwanza.
c) Hujikita katika ujumbe kuhusu mtu binafsi yaani-
   i) Mwaka na mahali pa kuzaliwa
   ii) Aila/familia yake
   iii) Hali yake ya ndoa
   iv) Kiwango chake cha elimu-chuo kikuu,shule ya upili,ya msingi na ya vidudu.
   v) Mtahiniwa ajikite katika kutoa mambo yake mema kama vile vitendo na mafanikio yake ili aonekane kama **kielelezo katika jamii**.
   vi) Vyeti na tuzo zote alizopata mhusika hutajwa.
   vii) Ni vyema mtahiniwa aonyeshe tajriba yake katika kazi mbalimbali hasa katika nyanja ya kidiplomasia.
   viii) Ni vyema aangazie juhudi zake maishani kwa mfano amekuwa akijihusisha na shughuli zipi na amefaulu vipi katika kazi hizo.
   ix) Katika kujijenga, ni vyema ataje vipaji vyake mbalimbali hasa vinavyohusiana na kazi ya ubalozi/uhusiano mwema kati ya mataifa mbalimbali.
   x) Risala ya rais wa nchi yake pia iandikwe katika wasifu huu kama njia ya kumalizia tawasifu yake.

**Tanbihi**-Kazi hii ipangwe kiaya na mawazo yafululuize.
Akizingatia yoyote yale ambayo yanaonyesha kwamba anaweza kuifanya kazi hiyo,atakuwa amejibu swali.

2. ***Utumizi wa afyuni[mihadarati} katika taasisi za masomo nchini ni suala ambalo ni muhala kutatuliwa. Jadili.***

**KUUNGA MKONO**

- Sheria hafifu inayowaruhusu wauzaji na watumiaji mihadarati kuendelea na shughuli zao.
- Kuporomoka kwa maadili ya kijamii na kushindwa kwa wazazi kuwathibiti watoto wao kwa kutowapa mawaidha.
- Vyombo vya habari vinachangia pakubwa katika kiwashawishi vijana kutumia mihadarati (runinga, redio, mtandao).
- Ukosefu wa wataalamu wa kutoa nasaha na mwelekeo kwa wanafunzi shuleni.
- Upungufu wa vielezo bora/mifano katika jamii kwani kuna watu wengi wanaotumia mihadarati katika jamii.
- Idadi kubwa ya wanafunzi ikilinganishwa na idadi ya walimu shuleni.
- Ufisadi: wanaowauzia vijana mihadarati hutumia hongo kufanikisha maovu haya, aidha mihadarati huingizwa nchini na matajiri wenye ushawishi.
- Baadhi ya majirani wa shule hudhani na hata kutumia njia hii kujipatia riziki.
- Shinikizo za wenzi huwasukuma vijana kutumia mihadarati.

**KUPINGA**

- Kutunga sheria kali zitakazowazuia watumiaji na wauzaji wa mihadarati.
- Kuwashauri wazazi kuwa mstari wa mbele kuwazungumzia na kuwashauri watoto wao.
- Kuthibiti vyombo vya habari ili kupunguza matumizi ya mihadarati.
- Kuwaajiri na kuongeza wataalamu wa ushauri shuleni na vijijini.
- Serikali ikabiliane na ufisadi katika viwango vyote, ukiwemo unaoruhusu uagizaji wa mihadarati na 'mabwenyenye' walio na ushawishi.
- Kuwaelimisha watu kuhusu njia halali, au mbadala za kujipatia riziki k.m. kilimo, biashara na kilimo biashara n.k.
- Wanafunzi washauriwe kujisimamia kimawazo na kuepuka shinikizo za wenzi./marika
- Vijana kupewa nasaha kuhusu athari za utumizi wa dawa hizi za kulevya.
- Walimu kuhimizwa kuwa karibu na wanafunzi ili kutambua wale wanaoenda upogo.

**TANBIHI**

- Mtahiniwa anaweza kuwa na hoja nyingi za kuunga mkono na moja au zaidi za kupinga.
- Mtahiniwa anaweza kuwa na hoja nyingi za kupinga na moja au zaidi za kuunga.
- Mtahiniwa atoe msimamo wake.
- Katika hali zote mtahiniwa asiwe na chini ya hoja nane.
- Anayekosa kushughulikia pande zote mbili asipite alama 10.
- Mtahiniwa anaweza kutoa hoja sawa pande zote almradi atoe msimamo.
- Hakiki hoja zingine za mtahiniwa.

3. ***Andika kisa kitakachodhihirisha maana ya methali: Mwenye kovu usidhani kapoa.***

Msimulizi asimulie kisa kitakachoonyesha ukweli wa methali hii.

Maana – Mtu ambaye amewahi kuwa mbaya hata akionekana kubadili mwenendo huenda akarudia maovu yake.

Mtahiniwa aonyeshe:

a) Makosa mhusika aliyofanya.

b) Jinsi makosa hayo yalimfanya kubadili mwenendo wake.

c) Kurudia makosa yale au mengine mabaya zaidi.

Kisa ndicho muhimu si utangulizi.

Sehemu ya pili ya methali yaweza kuwa ya sentensi moja au kirai kimoja – ikubalike kuwa mtahiniwa amezingatia mada.

4. ***Andika kisa kitakachomalizikia kwa: ... hivyo ndivyo ukurasa mpya katika kitabu cha maisha yangu ulivyofunguka.***

Mtahiniwa asimulie kisa kitakachoonyesha mabadiliko yalivyotokea katika maisha yake. Mabadiliko haya yaweza kuwa mazuri au mabaya.

Mtahiniwa atumie wakati uliopita; aonyeshe matukio yaliyomfikisha katika mabadiliko haya.

Kisa kioane na mdokezo aliopewa.

# MOI GIRLS HIGH SCHOOL

## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019

## Kiswahili Karatasi ya 2 - Lugha

## Mwongozo wa Kusahihisha

**Ufahamu**.

1. Wajibu wa kaunti / kazi ya kaunti. 1x1=1
2. (i)kutoa huduma za afya kwa umma kama kujenga hospitali na vifaa.
   ii)kusimamia maswala ya uchukuzi pamoja na ukarabati wa barabara.
   iii) kusimamia nyenzo za uzalishaji mali kama kilimo, uvuvi, ufugaji na ukuzaji

wa mimea.

(3x1= 3) zozote 2x1 = 2

3.(i) kubuni sheria za barabarani pamoja na kukarabati barabara

i) kutoa huduma muhimu za afya
ii) kuimarisha usalama
iii) kudhibiti matumizi ya dawa za kulevya 3x1=3

4. Kuunda sheria za kuzipa kaunti uwezo wa kuendeleza shughuli zake. (1x2=2)

5. (i) ufisadi

ii) uhaba wa fedha za kuendesha miradi ya maendeleo
iii) Majukumu ya kaunti kuingiliwa na serikali kuu
(iv) Ukosefu wa wataalamu waliohitimu katika nyanja mbalimbali. ( 3x1=3)

6. i) kubuni nafasi za kazi

ii) kufufua na kuanzisha viwanda vya uzalishaji bidhaa

(iii) kuimarisha miundo msingi (2x1= 2)

7. a) kubeba mizigo na kusafirisha abiria

b) ugavi wa mamlaka na rasilmali. (2x1=2)

**B. UFUPISHO**

a.) Majibu

i) Serikali kuwasilisha bajeti
ii) Kueleza jinsi mabilioni yalivyotumiwa
iii) Serikali ya Kenyatta kusema itatumia shilingi 1.6 trilioni kwa maendeleo
iv) Makadirio kuwasilishwa na kiongozi wa walio wengi bungeni
v) Kukosa kueleza jinsi ya kupata kitita hicho
vi) Kenya kudaiwa shilingi 1.8 trilioni na wafadhili
vii) kutolaumu wale wasioelewa ukubwa wa deni hilo
viii) Kugawanya deni hili kwa wakenya wote
ix) kila Mkenya kudaiwa shilingi 45,000

x) Rais Kenyatta kuridhi deni kutoka kwa Rais mstaa Kibaki
xi) Deni kumkosesha usingizi rais
xii) Kutafuta njia ya kulipa bila kuathiri uchumi

Zozote 8x1= 8

Mtiririko 2

b.) Majibu

i) Serikali kutenga fedha nyingi kuwalipa wafanyikazi
ii) KRA kutokusanya kiwango kinachohitajika
iii) Ukusanyaji wa ushuru kukatizwa na hofu wakati wa uchaguzi
iv) Serikali za kaunti kupendekeza kutumia mabilioni ambayo hawana

Zozote 4x1= 4

Mtiririko alama 1

**C. MATUMIZI YA LUGHA**

a) i)

Hewa haibanwi

Midomo huviringwa al 2*1

ii) silabi ikamilikayo kwa konsonanti km maktaba-mak

al maelezo 1, mf 1

b)i) u hupotea ukuta-kuta
ii) wingi huanza kwa nd ulimi- ndimi
iii) umoja w wingi ny waya –nyaya
iv) wingi mb ubavu-mbavu
v) umoja u wingi ny ufa-nyufa

za kwanza 2*1

c)i) sehemu ya neno ambayo huambikwa kabla au baada ya mzizi wa neno. al 1
ii) hu-m-f-ish-a
hu-hali ya mazoea
m-nafsi mtendwa/ kitendwa
f- mzizi
ish- kaulitendesha
a-kiishio

al ½*6=3

d) Yule mrefu sana ameanguka vibaya sana. al 2
e) Asha alisema kuwa hangeenda shuleni siku iliyofuata/ ambayo ingefuata. al 2
f) Kuku huku kunaudhi. al 2

g)sima-ugali zima-kamilifu/achisha taa/moto kuwaka
dada-ndugu wa kike tata-sumbua/sumbufu/ shida al 2

h) kwa niaba ya
kumchukua
kumwona / nia/ kusudi za kwanza 2x1

i) kurefuka
werevu al 2x1
j) Alikuwa akisoma al 2
k) Tukiwalipa pesa zao,watatuamini tena nyakati zijazo. al 2
l) "Labeka!" Maria alimjibu mamake. Nisubiri hadi Alhamisi. al 1/3*9=3
m) i) ulikuwa-kisaidizi
ii) ukifunga-kikuu
iii) ulikuwa ukifunga- sambamba
iv) u-kishirikishi kipungufu zozote 4x1

n) Nguo zichafukazo ndizo zifuliwazo. al 2
0)i) wakati
ii) mahali al 2
p) mama mzee-kirai nomino
alikuwa anatabasamu – kirai tenzi al 2
q) lishwa
nyweshwa/nywishwa

al 1

**D. ISIMU-JAMII**

(a) Ni mfumo wa sauti/ni chombo cha mawasiliano ya binadamu ambacho hutumia ishara na sauti nasibu zilizo na mpangilio maalum. (alama 1)

(b)

i. Lugha zote ni sawa – hakuna lugha iliyo bora kushinda zingine.
ii. Lugha hubadilika kutegemea mazingira, aina ya tukio, wakati na matumizi ya lugha hiyo.
iii. Lugha ina uwezo wa kukua mfano Kiswahili kimebuni msamiati TEKNOHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano).
iv. Lugha huweza kufa ikiwa msamiati wake umepotea.
v. Kila lugha ina sifa zake. (zozote 4 x 1 = alama 4)

(c)

i. Lugha ya heshima.
ii. Lugha ya upole.
iii. Matumizi ya maneno/msamiati maalum mfano Amina, Bwana asifiwe, Jehova n.k.
iv. Lugha iliyojaa ushawishi.
v. Lugha ya vitisho – mfano Usipotubu utaishia motoni.
vi. Kuchanganya ndimi.
vii. Ukalimani.
viii. Kurejelea vitabu vutakatifu. Mfano Bibilia.
ix. Nyimbo za kusifu.
x. Huandamana na ishara. –kupiga magoti, kufanya alama ya msalaba (zozote 5 x 1 = alama 5)

# MOI GIRLS HIGH SCHOOL
## K.C.S.E TRIAL AND PRACTICE EXAM - Julai 2019
## Kiswahili Karatasi ya 3 - Fasihi
## Mwongozo wa Kusahihisha

1. **4.Fafanuo ufaofu wa anwani *Chozi la Heri*** **(alama 20)**

**Jibu**

Mwandishi anatueleza kuwa Ridhaa alipoenda shuleni siku
Ya kwanza alitengwa na wenzake kwani hawakutaka ashiriki michezo yao. Kijana mmoja mchokozi alimwita 'mfuata mvua' Ridhaa
alikuja kuwashinda katika mitihani yote. Ridhaa alifululiza nyumbani na kujitupa mchangani na kulia kwa kite na shake.

Mamake alimliwaza na kumhakikishia kumwona
mwalimu keshoye. Tangu siku hii, huu ukawa ndio mwanzo wa maisha
ya heri kwa Ridhaa kwani baada ya mwalimu Kuzungumza na wanafunzi umuhimu wa kuishi pamoja kwa mshikamano, Ridhaa alipaa kwenye anga ya

elimu hadi kufikia kilele cha elimu na kuhitimu kama daktari.

Ridhaa alipotoka kwenye Msitu wa Mamba alijiona nafuu kwani wapwa zake-Lime na Mwanaheri walikuwa wamepata matibabu. Dadake Subira alitibiwa akapona. Mwamu wake Kaizari amepona donda lililosababishwa na kuwatazama mabinti zake wakitendewa ukaini(kubakwa) na vijana wenzao. Ridhaa anajua kuwa Kaizari ni afadhali kwa sababu hakuna aliyemtenga na mmoja kati ya jamaa zake. Ridhaa anapomfikiria Kaizari anajiambia heri nusu shari kuliko shari kamili.

Ridhaa aliposikia sauti ya kike ikitangaza, tangazo lile lilimrudisha katika mandhari yake ya sasa. Alijaribu kuangaza macho yake aone anakoenda lakini macho yalijaa uzito wa machozi ambayo alikuwa ameyaacha yamchome na kutiririka yatakavyo.

Wakati Ridhaa alimkazia macho Mwangeka-waka Mwangeka alikuwa akijiuliza iwapo babake amekuwa mwehu kwa kukosa kushirikiana na majirani kuchimba kaburi kuyazika majivumatone mazito ya machozi yalitunga machoni mwake Mwangeka. Akayaacha yamdondoke na kumcharaza yatakavyo.
Uvuguvugu uliotokana na mwanguko wa machozi haya uliulainisha moyo wake, ukampa amani kidogo. Moyo wake ukajaa utulivu sasa kwa kujua kuwa wino wa Mungu haufutiki.

Wakati Ridhaa_ alikuwa- akimsimulia Mwangeka msiba uliyomwandama tangu siku alipoondoka kwenda kuweka amani Mashariki ya Kati Ridhaa alisita akajipagusa kijasho
kilichoku- wa kimetunga kipajini mwake kisha akatoa kitambaa mfukoni na kuyafuta machozi yaliyokuwa yameanza kumpofusha. Uk 48 Mwangeka alipokuwa ameketi mkabala

na kidimbwi cha kuogelea mawazo yake yalikuwa kule mbali alikoanzia. Akawa anakumbuka changamoto za ukuaji wake. Akawakumbuka wana wake. Alipomkumbuka Annatila(Tila) mwili ulimzizima kidogo akatabasamu kisha tone moto la chozi likamdondoka. Katika Msitu wa Simba kulikuwa na maelfu watu waliogura makwao. Kati ya familia zilizoguria humu ni familia ya Bwana Kangata. Kwa Kangata na mkewe Ndarine, hapa palikuwa afadhali kwani hawakuwa na pa kwenda kwa kuwa hata kule walikokuwa wakiishi awali hakukuwa kwao. Uk 57 Wakati Dick walikutana kisadfa na Umu katika uwanja wa ndege, walikumbatiana kwa furaha. Machozi yaliwadondoka wote wawili na wakawa wanalia kimyakimya. Walijua fika kuwa jaala ilikuwa imewakutanisha na kwamba hawatawahi kutengana tena. Maisha sasa yalianza kuwa ya heri kwao. Baada ya miaka kumi ya kuuza dawa za kulevya, Dick alifaulu hatimaye kujinasua kutoka kwa kucha za mwajiri wake. Alianza biashara yake mwenyewe ya kuuza vifaa vya umeme 189 :111 p Sasa akaanza kujitegemea kwa kuwa amejiajiri.
Alikuwa ameu fungua ukurasa mpya katika maisha yake. Maisha yake sasa ni ya heri.

Wakati Neema na Mwangemi walikabidhiwa mtoto wao wa kupanga na Mtawa Annastacia, Mwaliko alimkumbatia Neema na kumwita mama na kumwahidi kuwa ataenda naye. Neema alidondokwa na chozi la furaha na kumkumbatia Mwaliko kwa

mapenzi ya mama mzazi. Hili lilikuwa ni chozi la heri kwa Neema.
(mwanafunzi aongezee hoja) (Hoja zozote 20 x 1 = 20)

**SEHEMU YA B**

**Tamthilia – Kigogo**

2 (a) (Dondoo)

Mnenaji : Kenga
Mnenewa Majoka
Mahali Ofisini mwa majoka
Mada (kuhusu) Jinsi/mbinu za kuwazima
Wapinzani na hasa kiongozi wao ambaye ni tunu aliyeongoza maandamano
(4 x 1=4)

(b) Mbinu nyingine walizotumia

- Mauaji – wapinzani kama jabali waliuawa
- Vishawishi/tuzo – Ashua na Tunu walikuwa wanapewa ajira ili kushawishika wakakataa
- Kutumia vikaragosi kama Kenga (mshauri mkuu, askari nk)
- Kutoa ajira kwa misingi ya mapendeleo
- Km Asiye na mradi wa keki Kenga alikuwa binamu wa Majoka
- Mikopo kutoka nje fedha ambazo zinafujwa kwa manufaa ya Majoka na wenzake kama vile Kenga zinatumiwa kupata uungwaji mkono
- Polisi – pollisi wana tumika kuwatawanya waandamaji
- Uchochezi – wapinzani wanatupiwa vijikaratasi vya kuwataka wahame.
- Hofu – Hashima anaishi kwa hofu
- Hii inawafanya watu kuwa wanyenyekevu na kumuabudu majoka
- Ukiritimba – lengo la majoka ni kuwa na Chama Kimoja cha kisiasa, kituo cha runinga na kampuni kutajwa kwa jina lake tu.
- Vyombo vya habari kituo; sauti ya mashujaa kinaendeleza shughuli zao majoka anatumia redio kutngaza katungwa kwa soko, watu kuchezewa nyinbo za uzalendo bandia.
- Kuidhinisha shughuli haramu – upikaji wa pombe, ukataji wa miti
- Unasaba uongozi wa kurithishwa kifamilia.
- Matumizi ya msimbo – Majoka na Kenga wanatumia lugha ya kitamathali/msimbo wanaofahamu wao tu. Km ‘Kuvunja miguu’ ‘kuvunjwa vunjwa na chatu’ kupangiwa safari (kuuawa)
- Kuficha siri – chopi anapashindwa kumuua Tunu kwa jama wanapanga kumuua ili kufanikisha kadhia hiyo.
- Propaganda km. Eti Jabali alifariki katika ajali wavamizi wa Tunu wanasema Ashua na Sudi ndio walikuwa wakiwinda roho yake
- Jela – ilitumiwa kulipiza kisasi na kuwatisha wazalendo km Ashua

3. **Athari ya tamaa na ubinafsi**

(i) Umaskini – unyakuzi wa soko la chapakazi wanasaga moyo wanashindwa ukimu mahitaji yao. Km. Ashua – anakuwa wa kuombaomba.

(ii) Ari ya mapinduzi. Tamaa na ubinafsi wa watawala vinawakasirisha wenzake: Tunu na Sudi kuazisha harakati za kuung’oa mamlakani uongozi wa majoka.

(iii) Uchafuzi wa mazingira. Tamaa ya wanaviwanda inawasukuma kutupa

kemikali kwenye mitaro ya maji. Kutupa taka na kemikali kwa njia ipasavyo kunge Matokeo ya taka hizi ni uchafuzi wa mazingira, kuenea kwa maradhi sugu na uvundo unaokirihi.

(iv) Utabaka – kutokana na tamaa ya majoka ya kutaka kuwa na mali nyingi, anaendeleza ukiritimba. Anamiliki viwanda, makapuni, shule za kifahari na hata maeneo ya kujiburudisha. Kitendo hiki kinasababisha utabaka katika jimbo la Sagamoyo. Kuna matajiri na mafukara kama vile walevi.

(v) Matumizi mabaya ya vyombo vya dola. Kutokana na tamaa ya kutaka kusalia mamlakani, Majoka anatumia vyombo vya dola kama polisi na jela kutekeleza unyama. Kwa mfano vijana watano na wachuuzi walioandamana wanapoteza wao.

(vi) Ukame-Hashima anaeleza kuwa msimu wa kulima mchele ulikuwa mbaya. Maziwa na mito ilikuwa imekauka jambo hili linachangiwa zaidi na hatua ya majoka ya kuruhusu ukataji wa miti.

(vii) Kuathirika kisaikolojia - Tamaa na ubinafsi wa majoka unamfanya kutekeleza ukatili ambao unaifanya nafsi yake kumhukumu na kumsuta kupitia mazungumzo yake na Babu ndotoni. Masimango haya yanamfanya kuhangaika na kukosa amani moyoni wake.

(viii) Unyanyasaji – Tamaa na ubinafsi wa viongozi vinawasukuma kukusanya kodi kubwa na hata kushiriki ufisadi kutoka kwa wachuuzi kama vile Ashua na Kombe jambo linalofanya maisha kuwawia magumu mno.

(ix) Tamaa ya kukopa kopa fedha katika mataifa ya nje kunaachia jamii mzigo wa kulipa madeni hayo.

(x) Tamaa na uubinafsi wa wafuasi wa Majoka kama vile Boza na ngurumo vinawafanya kufumbia macho uozo wa Kigogo Majoka. Wanapendezwa na uongozi wake.

Ngurumo anaapa kutompa mtu mwingine kura isipokuwa Majoka tu. Anadai kuwa yuko radhi kumpa paka wa Majoka kura kuliko kumpa mwanamke sampuli ya Tunu.

Tabia hii inasababisha hali ya maisha ya Wanasagamoyo kuwa mbaya Zaidi.

4. (a) Haya ni maelezo ya mwandishi

Akirejelea Mose aliyetazama samaki waliopewa ulinzi wa lazima.. videge kama nzige vilijaa kote hewani (uk 93)

Katika bustani ya Ilala mipumuo inayorejelewa ni ule uwezo unaowakilishwa na midege

(i) Wenye uwezo katika muktadha huu wanawakilishwa na midege ambayo inatamalaki himaya ya videge na kuviathiri. Midege inaelezwa kama iliyo na nguvu kubwa katika kupora, kuua, kuvamia na kuangamiza.

(ii) Midege ina sifa za kutisha; mwewe si mwewe, tai si tai. Katika ndoto yake, Mose anaona ulafi mkubwa. Tabaka lenye nguvu linahusishwa

na wanajamii wenye nguvu na uwezo wa kubwakura kama tai na mwewe.

(iii) Midege ina midomo mikubwa kama upanga na imekenue huku ikihema. Hapa tabaka kadamizi linasawiriwa kama lililotayari kumeza na kuvaia chochote kinachokimilikiwa na walalahoi.

(iv) Mose anapoangalia angani anaona dege kubwa lililoonekana kama lile lililopenda kula vifaranga na videge vidogovidogo. Hawa ni matajiri wakubwa wanaongamiza na kula jasho la wasio na uwezo.

(v) Mashing marefu ya midege ni uwezo tabaka kandamizi wa kuona an kufikia hata kile kidogo walich nacho maskini.

(vi) Macho yanayomulika kwa mwangaza mkali ni uwezo wa tabaka kandamizi wa kuona mali na raslimali za jamii na kuzipora. Macho haya makali pia yanatumika kama ishara ya vitisho na nguvu za kifedha walizonazo waporaji hawa.

(vii) Kelele na milio ya midege hii inaashiria vitisho na maangamizi yanayokuja na ukandamizaji wa tabaka kandamizi. Matajiri hutibua hali ya utulivu wanayokuwa nayo wenye uwezo mdogo.

(viii) Midege inawasiliana na kujadiliana kwa lugha ya binadamu. Tabaka kandamizi linatumia lugha kama nguvu kutawala tabaka la chin. Midege inatumia lugha kukubaliana na kuvifumba macho videge kuwa inajenga jamiii bali inaibomoa.

(ix) Midege inaruka kila mahali na kukanyaga maua. Tabaka dhalimu linatumia nguvu na uwezo wake kuyaharibu mazingira.

(x) Midege mingine inabeba matonge ya samaki na kunyang'anyana na kuharibu mazingira nguvu za tabaka twala zinatumika kuvamia, kuua nan a kuyaharibu mazingira.

(xi) Kitendo cha midege kuwategea samaki kidimbwini n ishara ya tamaa ya matajiri kuparamia raslimali za maskini.

5. (a) Mifano kumi ya Jazanda katika 'shibe inatumaliza'

(i) 'sasa' na 'mbura' – kusasambura (kumaliza kila kitu kuto kila kitu, kupora mali yote.

(ii) sherehe – mipango isiyo na maana ya kufilisi mali ya umma

(iii) mchele wa mbeya – Bidhaa za kigeni na zenye manufaa makubwa

(vi) mchele wa mbeya – Bidhaa za humu nchini na zenye manufaa makubwa

(v) Njaa uroho/uchi wa kupora mali ya umma serikalini

(vi) Kupakua vyakula – kupora mali ya umma

(vii) Shibe – unyakuzi wa mali kwa wingi zaidi

(viii) Kivuli (Mzee mambo) – mtu asiye na maana kama kivuli chake

(ix) Vyetu vyao – mali ya umma mali ya wananchi

(x) Kioo cha taifa wasapu fesibuku, kalamu na karatasi = Hadharani (uporaji wa mali ya umma unafanywa kila mtu akijua lakini hakuna hatua inachukuliwa)

( wimbo wa sijali lawama = Hii ni tabia yatakriban viongozi watu. Tabia ya kutojali wanayofanya au lawama kutoka kwa wananchi. Ni kana kwamba wao wanaoimba wimbo moja.

Mtahini ahakik majibi yoyote (10 x 1=10)

(b) Athari za ubakaji wanapitia mengi katika jamii ya hadithi hii. Thibitisha

kauli hii kwa mujibu wa hadithi hii.

(i) Msongo wa kimawazo. Waathiriwa wa ubakaji wanasumbuka kimawaza hasa. Wanapokumbuka dhuluma na unyama waliofanywa. Sara na machozi anapokumbuka alivyobakwa na kutamani ingekuwa ndoto.

(ii) Kuhujumiwa na ndoto na taswira ya kitendo cha kubakwa. Sara anapata picha chafu ambayo inamganda akili hata akijaribu kuipuuza. Picha ya mbakaji wa Sara bado iko akilini mwake.

(iii) Aibu Sara anakashifika baada ya kulazwa chali na kuvuliwa nguo zote "… akajikuta akiwa amelala chali, amekashifika, uchi si uchi," uk.47

(iv) Kutengwa na kubaguliwa, misuto na kashfa. Sara anatarajia laana na misubuko kutoka kwa kila mtu – wa karibu na wa mbali.

(v) Kukashifiwa na wazazi. Sara anawaza kuwa nyumbani babake atamchinja au kumfukuwa.

(vi) Lawama kutoka kwa wazazi. Sara anawaza kuwa babake atamlaumu kwa kukosa kusema habari ya kubakwa kwake kwa wakati ufaao. Sara anaona atalaumiwa yeye.

(vii) Kutoaminika, Sara hatarajii kuaminika na babake. "Nani akubake wewe?" uk.48

(viii) Kutengwa na kufukuzwa nyumbani. Sara anawaza kuwa nguo zake zitakunjwakunjwa na kutupwa nje na kuambiwa nyumba aione paa. Uk.48

(ix) Jamii kumwona anayebakwa kama mwenye kosa. Sara anahisi kuwa mjomba,kakake na hata mamake watamwona yeye kama shetani. Kosa ni la mwanamke si la mwanamume.

(x) Kufukuzwa shule, Sara anaona kuwa hakutakuwa na linguine ila kufukuzwa shule. Uk 49.

(xi) Kukashifiwa na kuaibishwa na walimu. Sara anaona kuwa mwalimu mkuu atamzomea na kumwambia shule ni ya wasichana si ya kina mama. "Hatufundishi wanawake hapa,tunafundisha wasichana. Uk. 49.

(xii) Kutengwa kukosa wa kumfariji. Wngi wanatarajiwa kumwambaa Sara kama mgonjwa wa ukoma. Uk.49

(xiii) Kujiwa na fikra mbaya kama kujiua. Sara anajiwa na mawazo mengi anapokuwa akitathmini mstakabali wa maisha yake. Wazo la kujiua, wazo la kutoa mimba kukabiliana na uhalisia na kuibeba mimba yake. Sara yuko kwenye njia panda.

MAJIBU

(a) Ndege
(b) Mke nyumbani/mchumba
(c) Ukara – vina vya kati kubadilika vya kati vina tiririka
Masthawi – vipanda viwili
Tarbia – mshororo minne
(d) Mishororo mine
- Vipande viwili – ukwapi na tuao

- Mizani 16 katika kila mshororo
- Vina ri, ni
- ri, ni
- ri, ni
- ni,wa

(e) Tabdila – muruwa na hishima
- Inkisari-ataka badala ya anataka
- Kuboronga sarufi – kama anavyo kubwa hasara-kama anavyo hasara kubwa

(f) Mke mwema mwenye heshima nzuri ya kusifu, hata akifungwa atadhamini makao ana furahi kuishi kule. Mke anayeishi nyunbani amezidiwa nguvu

(g) Anashauri kuwa wake wanaishi katika ndoa ni wachache/wengi wana tama

(h) (i) atahama
(ii) maneno

7. (a) mkulima ambaye ni nguzo ya Afrika ni kama mtumwa
Anateseka, ana huzuni na hana matumaini
Baadaye matumaini yanaweza kwisha
Kuna siku ambapo atafahamu haki yake
Wanamtesa wataadhwa alama 4

(b) (i) Tashbihi
kama kuni
kama bahari

(ii) kweli kinzani : mtumwa wa watumwa waliyoridhiya

(iii) Tashhisi

Pumzi zilizozima taa za Afrika
Amekita jembe lake akilisujudia alama 4

(c) Beti tano
Mishororo haitoshani
Shairi huru
Vina vya nje vipo alama 3

(a) Mshangao masikitiko kuwa aliye nguzo yla Afrika ni mtumwa wa watumwa
(b) (i) wakati atakapozinduka na kuidai haki yake
(ii) kutuliza hasira na matakwa/matatizo yake hata kama ni kidogo (alama 2)
(c) (i) umbo
(ii) uliokauka
(iii) kumwigisha /kumkopesha

**FASIHI SIMULIZI**

8. (a) kipera cha ngoma alama 2

(b) Dhima ya Ngoma

- Kuburudisha
- Ni kitambulisho cha jamii
- Kuhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii husika
- Huleta utangamano katika jamii
- Helimisha
- Hukuza uzalendo

(iii) Udhaifu wa mahojiano kama mbinu ya ukusanyaji wa data

- Mahojiano yanahitaji stadi za mawasiliano za kiwango cha juu
- Urasmi unaotokana no vikao vya mahojiano huenda ukatatiza mawasiliano kati ya mhojiwa
- Ukosefu wa muda wa kutosha wa mshojiano
- Mhojiwa huenda asimwamini mtafiti
- Mahojiano ni njia ghali ya kutafiti kutokana na gharama ya usafiri kwenda nyanjani
- Matatizo ya kutafsiri ikiwa data imeandikwa kwa lugha tofauti huenda yakaathiri mahojiano.

(alama 10)

*LATEST HIGH SCHOOL NOTES*
*0714497530* (Mr Isaboke)
Maths form 1-4
English form 1-4
kiswahili form 1-4
chemistry form 1--4
Biology form 1-4
Physics form 1--4
Agriculture form 1--4
Business form 1--4
Cre form 1--4
History form 1--4
Computer form 1--4
Geography form 1--4
Homescience f1--4
I.R.E studies f1-4
French notes
Setbooks guides
Primary school notes
KCSE Topicals
*CPA* tuitioning
Updated *CPA,CIFA ATD* KASNEB notes
Updated *CPS,CICT,ATD* KASNEB Notes
Updated *ICT,IT,ACCA,CFA* notes
Forex trading guidance
*CCTV* installation &Networking services
Online services
*_All the materials are in soft copy and we'll updated
Text /call or WhatsApp *0714497530 to get your copy_*
* +254714497530 (Mr Isaboke)*